

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

### **MKUTANO WA KUMI NA SITA**

---

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 27 Julai, 2009)**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### **DUA**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita anayeuliza swali la kwanza, karibuni tena baada ya mapumziko ya *weekend*, nadhani mna nguvu ya kutosha kwa ajili ya shughuli za wiki hii ya mwisho ya Bunge hili la 16. Swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linauliza na Mheshimiwa Shoka, kwa niaba yake Mheshimiwa Khalifa.

Na.281

### **Kiwanja kwa Ajili ya Kujenga Ofisi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

**MHE KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (K.n.y. MHE. SHOKA KHAMIS JUMA)** aliliza:-

Kwa kuwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI inakabiliwa na changamoto ya ufynywa wa Ofisi; na kwa kuwa Tume hiyo imepata fedha kutoka DANIDA kwa ajili ya kujenga jengo la Ofisi lakini inakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa kiwanja:-

Je, Serikali itasaidia vipi Tume hiyo kupata kiwanja cha kujenga Ofisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la kiwanja cha kujenga Ofisi za *TACAIDS* limepatiwa ufumbuzi na ofisi yangu imewaonesha Maafisa wa DANIDA kiwanja hicho Ijumaa tarehe 17 Julai, 2009. Kiwanja hicho kipo Mtaa wa Luthuli Na. 73, Dar es Salaam ama kwa lugha nyingine Makutano ya Mtaa wa Samora na Luthuli.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa jambo hili ni kitu kinachohitajika sana, je, anaweza kuliambia Bunge hili matarajio ya ujenzi huo utamalizika lini ili tatizo hili liweze kuondoka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa vile fedha ziko, kiwanja kimepatikana sasa michoro inaandaliwa. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba katika muda usiozidi miezi 24 jengo hili litakuwa limekamilika.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa inafahamika kwamba Makao Makuu ya Nchi ni Dodoma, hivi kuna sababu gani za msingi msiwaambie hizi Taasisi ambazo zinataka kujenga Makao Makuu yake zije kujenga Dodoma ili kuhamisisha mji wa Dodoma, ili ndiyo uwe Makao Makuu sawasawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kuna sababu za msingi kwa kweli za kujenga Makao Makuu ya TACAIDS hasa kwa vile chombo hiki ndicho kinahifadhi nyaraka zote kuhusu masuala la UKIMWI nchini kwetu lakini pia ni chombo ambacho kinawakutanisha wafadhili mbalimbali wa UKIMWI na mahala kwa kuwapata watu hawa ni Dar es Salaam. Lakini napenda kusema hapa pia kiwanja nilichotoja awali kilikuwa kimepangiwa kujengwa ofisi za kudumu za Waziri Mkuu. Kwa hiyo, ni ishara kwamba kama Serikali imeanza kubadilisha madhumuni ya baadhi ya viwanja basi naamini ofisi za Serikali zitakuja kuhamia Dodoma baadaye.

Na. 282

### **Mikopo ya Vijana Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mikopo ya vijana Bukombe inayotokana na 10% ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya haijawahi kutolewa kwa vijana tangu mwaka 2005:-

Je, Serikali inawaambia nini vijana wa Bukombe ambao wamejikuta wakitafuta mikopo ambayo haipatikani?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mikopo ya vijana inayotokana na asilimia kumi ya mapato ya Halmashauri kutoka vyanzo vyake (*own source*), haijawahi kutolewa kwa vijana wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe tangu mwaka 2005. Hata hivyo, kwa kutambua umuhimu wa kukwawezesha Vijana, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa vipindi tofauti imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe jumla ya shilingi milioni 13.1. Fedha hizo zimetumika kwa kutoa mikopo kwa vikundi zaidi ya 30 vya vijana vinavyoendesha shughuli za uzalishaji mali. Changamoto kubwa iliyopo kwa vijana ni kutorejeshwa mikopo wanayopewa kwa wakati. Kwa mfano, kwa mikopo iliyotolewa kwa vikundi 30 vya vijana mwaka 2003 ya kiasi cha shilingi 3,089,000/=; marejesho ni asilimia ishirini na sita tu sawa na shilingi 800,000/=.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimewahi kutoa mawelezo hapa Bungeni wakati nikijibu maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kuchangia katika Mfuko huo ulikuwa ni Halmashauri kutoa asilimia kumi ya mapato yake kwa mwaka wa kwanza (*base year*). Baada ya hapo, Mfuko huu unakuwa wa mzunguko (*revolving fund*). Kwa takwimu za mwaka 2003 (kwa maana ya *base year*), Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ilikusanya kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya shilingi milioni 453.8. Asilimia kumi ya mapato hayo ni shilingi milioni 45.38 ambayo hazijatolewa na Halmashauri. Ninaiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kutekeleza maelekezo ya Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Vijana japo kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa wito kwa Halmashauri zote nchini kukendelea kufuatilia marejesho kutoka kwa vikundi vinavyokopeshwa. Hii itawezesha Mfuko kuwa endelevu. Wanaokopeshwa wanapaswa kuelewa umuhimu wa kurejesha mikopo yao kwa mujibu wa mikataba ili wengine waweze kukopeshwa. Pia, kwa kushirikiana na *SIDO*, Halmashauri ziwe na utaratibu wa kutoa mafunzo mafupi yatakayotolewa kwa walengwa juu ya namna bora ya uendeshaji wa miradi husika. Aidha, zijiwekee utaratibu mzuri wa kuwafuatilia wakopaji ili kubaini mapema matatizo yaliyopo katika utekelezaji wa miradi yao, kuwapa ushauri na kuhakikisha kwamba wanarejesha mikopo hiyo.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu walionyipatia na kukikiri kwamba kweli hawajawahi kutoa mikopo hiyo lakini naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Halmashauri, vyanzo vingi vimeshafutwa na kupunguzwa kwa ajili ya kuondoa kero kwa wananchi, kwa hiyo, kusababisha hata mapato kwenye Halmashauri yapungue. Je, Serikali Kuu inasema nini kuwasaidia vijana hawa walioko Majimboni na Wilayani kwetu ili waendee kupata mikopo hii na hatimaye kuboresha maisha yao tofauti na hii mikopo kama ya shilingi milioni tatu ambayo haiwasaidii kitu?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Luhahula kwamba kuna vyanzo vya mapato ambavyo vimefutwa vilivyoonekana kwamba ni kero kwa wananchi. Lakini nataka nimwambie rafiki yangu kwamba mimi ninavyokumbuka kwa *records* zetu na utaratibu tunaoujua, vile vyanzo ambavyo tuliona kwamba ni kero kwa wananchi, vyanzo hivi Serikali iliamua kwamba Serikali itafidia na fidia hiyo itarudi mpaka kwenye *level* ya kijiji. Kwa hiyo, kuna kiasi ambacho Serikali inarejesha tena kule baada ya kuwa zimefutwa zile kodi ambazo zimeonekana kuwa ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumza hapa, ni kwamba kinachotakiwa kufanyika hapa kwenye *own source* yao ambayo nimeeleza humu ndani kwamba kwa mwaka ule ambao nimeutaja hapa walipata kiasi cha shilingi 400 na ushehe, asimilia hiyo inayozungumzwa hapa ni kwamba Halmashauri ya Wilaya Bukombe ilitakiwa itenge shilingi milioni 45 kwa ajili ya vijana ambao wanazungumzwa hapa. Ndicho ninachokiagiza hapa na ninachosema kwa Wilaya zote katika nchi hii kwamba ni lazima watekeleze maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukichukua hotuba aliyoitoe Mheshimiwa Ngwilizi kwa mwaka 2001/2002, mle ndani inasisitiza na kutoa maelekezo kwamba hivi vikundi lazima vipate hizo hela kutokana na *own source*. Tunamwomba Mheshimiwa Luhahula, aende, tutashirikiana naye, tutamsaidia kusukuma jambo hili ili hizi hela ziweze kupatikana na vijana waweze

kusaidiwa kwa sababu tulisema kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana. (Makofi)

**MHE. MGANA I MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja moja la nyongeza.

Kwa kuwa huu Mfuko ulianzishwa kwa nia njema sana; na kwa kuwa ni Halmashauri chache zinatekeleza maagizo ya Serikali, je, Serikali iko tayari kufuatilia kwa undani Mfuko huu kwa Wilaya zote ili vijana na akina mama wote wa Vijijini waweze kufaidika na Mfuko huu?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, anachokieleza Mheshimiwa Msindai hapa ni sahihi kabisa. Ninayo *document* na hotuba ambayo aliitoa Mheshimiwa Ngwilizi, inakiri tatizo hilo. Tatizo kubwa ambalo limejitokeza katika Mfuko huu ni kwamba hata wale ambao wamefuata maelekezo ya Serikali na kutenga asilimia kumi, vile vikundi vinapopokea zile hela havirudishi tena ili vikundi zaidi viweze kukopeshwa. Kwa hiyo, mimi nakubaliana naye kabisa na nichukue nafasi hii kwa ajili ya *records* za Bunge lako hili, kumshukuru Mheshimiwa Mgana Msindai wakati alipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya LAAC, amesimama imara kuhakikisha kwamba anazisimamia Halmashauri kuhakikisha wanapeleka katika Mfuko ule kama inavyoelekezwa. Natambua sasa hivi ni Makamu Mwenyekiti na anaendelea na jitihada hizo. Ushauri anaoutoa hapa sisi kama Serikali tunaupokea na tutaufanyia kazi. Ni sahihi kabisa.

Na. 283

### **Utekelezaji wa Maagizo ya Serikali**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, maagizo ya Serikali ya ngazi za juu kuhusu operesheni mbalimbali kama vile zoezi la kuhamisha mifugo hutekelezwa na wahusika wa ngazi za chini kinyume na maagizo ya awali na hivyo kusababisha udhalimu na unyinyasaji mkubwa wa wananchi:-

(a) Je, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utawala Bora, huwa inahusishwaje na utekelezaji wa maagizo hayo?

(b) Kama inahusishwa; je, ni kwa nini matatizo hayo hutokea ambayo yanaambatana na ukiukwaji wa haki za binadamu na ukosefu wa utawala bora?

(c) Kama Ofisi hiyo haihusishwi; je, Ofisi hiyo ina kazi ngapi katika nchi yetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Serikali katika uendeshaji wa shughuli zake, ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa shughuli hizo zinafanyika kwa misingi ya Utawala Bora unaozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Kwa hiyo, maagizo ya Serikali yanayotolewa na ngazi mbalimbali, yanapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia misingi ya Sheria, Kanuni na

Taratibu inayoambatana na maagizo hayo na kutokiuka haki za binadamu. Utekelezaji wa maagizo ambao unaambatana na udhalimu na unyanyasaji, ni ukiukwaji wa maadili ya kazi na ni kosa ambalo likibainika, mhusika huchukuliwa hatua za kinidhamu ama za kisheria kwa kutegemea uzito wa kosa lililotendwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nyingine, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kazi yake ni kujenga Utawala Bora nchini kwa kusimamia, kuratibu na kuhakikisha kuwa Serikali na Taasisi zake zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo hayajakidhi haja, kwanza swali langu la (a) halijapatiwa majibu. Niliuliza Wizara hii ya Ofisi ya Rais Utawala Bora, inahusishwaje kwenye utekelezaji wa maagizo ya Serikali?

Kwa kuwa matatizo ya ukiukwaji wa haki za binadamu na ukosefu wa utawala bora, ni tatizo sugu kwa maeneo mengi na hasa Vijijini. Tumekuwa tunashuhudia na Wabunge wamekuwa wakiyapata malalamiko haya sana kwa sababu ndiyo jirani na wananchi na mengine tumekuwa tunayaleta hapa kwa Waheshimiwa Mawaziri hayafuatiliwi kwa kupewa uzito wake na wananchi wanakuwa wameteseka sana mpaka Wabunge wagundue wananchi wanakuwa wamenyanyasika kwa kiasi kukubwa. Je, Serikali inaweka utaratibu gani maeneo yote kuhakikisha kwamba viongozi wanaowanyanyasa wananchi, wanaokiuka utawala bora, matatizo yanagundulika mapema kabla ya wananchi hawajateseka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, ina Ofisi katika kila Mkoa na katika kila Wilaya. Ziko ofisi za TAKUKURU, ziko ofisi za Usalama wa Taifa, kukiwa na zoezi lolote la kitaifa, taasisi hizi mbili zinashirikishwa ipasavyo. Kwa hiyo, ofisi ya Utawala Bora isionekane kama haina kazi. Ina kazi kama kawaida na ina mikondo yake mpaka katika ngazi ya chini.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusu ukosefu wa utawala bora, Serikali ina mikono kuanzia ngazi ya juu ya Kitaifa mpaka ngazi ya kijiji. Kwa hiyo, utawala bora unatakiwa kutekelezwa kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa, kote huku kuna mikondo yake ya Serikali. Kwa hiyo, utawala bora unatakiwa uanzie huko na unatekelezwa ipasavyo. Pale ambapo utawala bora unakiukwa, ile mikono ya Serikali inafanya kazi zake kama kawaida. Ziko Mahakama kwa ajili ya kutekeleza utawala bora. Ziko Ofisi za Vijiji kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo, ziko ofisi za Kata kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, Serikali sehemu zote hizo inatekeleza utawala bora. Kama Mheshimiwa Mbunge ana tatizo *specific*, naomba tuwasiliane, tuone kama tatizo hili halikutekelezwa ipasavyo au halikushughulikiwa, tulishughulikie.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi uya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anakiri Ofisi ya Utawala Bora katika ngazi za Wilaya na Mikoa inawakilishwa na watu wa Usalama wa Taifa na watu wa TAKUKURU na kwa kuwa katika oparesheni ya mifugo kila wanaotuhumiwa kujitwalia mifugo hiyo iliyokuwa imeporwa ni pamoja na watu hawa ambao ni watumishi katika Ofisi ya Utawala Bora, je, Waziri atakiri kwamba Ofisi hiyo ya Utawala Bora kwa namna moja ama nyingine kutokana na vitendo hivyo vya kinyama, itakuwa ni miongoni mwa wahalifu walioshiriki katika zoezi hilo la kiharamia lililowafanya Watanzania hao kuonekana kuwa wakimbizi katika nchi yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa zoezi la kuhamisha mifugo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, halikuwa zoezi la kiharamia. Lilikuwa ni zoezi halali na la Kitaifa, tatizo ni utekelezaji mbaya. Zoezi lenyewe si baya bali utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Ole-Sendeka, ana ushahidi kwamba zoezi hili aliyehusika kulivuruga au aliyekiuka haki za binadamu ni pamoja na wale ndugu zetu wa TAKUKURU au Usalama wa Taifa, ni vyema akauleta ili tuushughulikie. Lakini Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri imeshafanya kazi yake, imeshaleta ripoti, tutabaini wapi na watu gani wamekiuka utawala bora ili tuweze kuchukua hatua za Kisheria.

Na. 284

### **Ubomoaji wa Nyumba za Wananchi**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y MHE. FATMA M. MAGHIMBI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne, iliahidi maisha bora kwa kila Mtanzania na moja kati ya vielelezo vya maisha bora ni kujenga nyumba ya kuishi lakini hapo hapo kuna ubomoaji holela wa nyumba hizo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kubomoa nyumba hizo ni kukwamisha maisha bora ya Mtanzania?

(b) Kwa kuwa, Serikali huwa inaona wakati Watanzania wanapojenga nyumba hizo; je, Serikali haiwezi kubaini harufu ya rushwa kutoka Ofisi ya Mipango Miji ama wakati wa kujenga au kubomoa nyumba hizo?

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haibomoi nyumba za wananchi kwa lengo la kukwamisha juhudi zao za kujitea maendeleo ya kiuchumi na kijamii, bali ni kwa lengo la kuendeleza huduma za msingi za makazi, ziwe bora na endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo majukumu ya msingi kwa wananchi wake. Moja ya majukumu hayo, ni kusimamia upangaji wa Miji kwa kuzingatia viwango na masharti yaliyomo katika Sheria ya Mipango Miji, kwani kila mtu akiachiwa ajenge nyumba mijini kwa jinsi anavyotaka yeye, kungekuwa na vurugu kubwa na miji isingekalika. Aidha, Serikali huweza kubomoa nyumba za watu kutokana na sababu mbalimbali zikiwa ni pamoja na:-

(i) Watu wanapovamia na kujenga katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi maalum kama vile shule, zahanati, maeneo ya wazi na kadhalika;

(ii) Watu wanaojenga ndani ya maeneo ya akiba ya barabara (*road reserve*);

(iii) Watu wanaojenga nyumba bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za mipangomiji; na

(iv) Pale Serikali inapopitisha miundombinu kama barabara, reli, nguzo za umeme, au inapojenga majengo kwa ajili ya huduma za jamii kama shule, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ubomoaji wa nyumba za wananchi hasa kwenye maeneo panapojengwa miradi ya Serikali kwa manufaa na maslahi ya umma, sharti uthamini ufanyike na fidia ya mali husika ilipwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwisha kubaini udhaifu unaojitokeza katika Halmashauri za Miji na Wilaya unaosababisha wananchi kuvunja Sheria za Mipango Miji na kanuni zake kwa kujenga nyumba maeneo yasiyostahili. Udhaifu huo ni pamoja na uhaba wa watalaam wa sekta ya ardhi, udhaifu katika kusimamia Sheria za Mipango ya Miji, pia upungufu wa uadilifu kwa baadhi ya watalaam wa sekta hii. Katika kukabiliana na matatizo hayo, Bunge limetunga Sheria ya Kusimamia Maadili ya Maafisa Mipango Miji Na. 7 ya mwaka 2007, kwa lengo la kuwabana na kuwawajibisha Maafisa Mipango Miji wasiofuata maadili ya kazi zao. Aidha, Halmashauri mbalimbali chini ya Wizara ya TAMISEMI, zinachukua hatua za kuajiri wataalamu wa kutosha kusimamia majukumu haya.

Mwisho, napenda kutoa wito kwa wananchi na hasa wakazi wa mijini kwamba wanapoanzisha ujenzi wa nyumba, ni lazima wazingatie Sheria za Mipango Miji ili kuepuka suala la bomoabomoa. Kila mtu akizingatia Sheria za Mipango Miji, suala la bomoabomoa litakwisha.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa inaonekana kwamba zoezi hili la bomoabomoa linafanywa kiholela, maana wananchi wanajenga halafu Serikali inabomoa wakati ipo, je, Serikali inayo sera au dira inayoonesha kwamba miji ipi itabomolewa na lini ili wananchi wasianze kujenga na wasipate hasara ya bure?

La pili, kwa kuwa Watanzania wengi hawana pesa za kujenga nyumba kwa *cash*, ni lini Serikali itatoa mikopo kwa Watanzania ambao wanataka kujenga, ili nao wawe na nyumba nzuri na waishi maisha bora?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza. Kama nilivyojibu katika majibu ya awali kwamba iko Sheria ya Mipango Miji, namba 7 inayoongoza taratibu za kujenga nyumba mijini na hii ni kwa miji yote Tanzania Bara. Ndiyo maana nikatoa wito kwamba kila anayejenga akifuata Sheria hii, suala hili la bomoabomoa litakwisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo, kama nilivyoieleza kwenye hotuba yangu ya bajeti kwamba ile Sheria ambayo Bunge lilipitisha mwaka jana, Sheria ya Mikopo ya Nyumba tayari Kanuni zake zimeshakamilika na tayari imeanza kutumika kuanzia tarehe 1 Mei, 2009 na Mabenki yote sasa hivi yanajiandaa kuanza kutoa mikopo ya nyumba.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri; je,

Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba ujenzi holela unasababishwa na miji yetu mingi kukosa *master plan* na Wizara yake inasemaje kuhusu kusaidia miji ile ambayo haina *master plan*?

**SPIKA:** Kama vile Mpwapwa, sio? (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ujenzi holela katika miji yetu ni kweli upo. Karibu asilimia 70 ya miji yetu inakabiliwa na ujenzi holela na tatizo kubwa si *master plan*, tatizo kubwa ni upimaji wa viwanja hata pale ambapo michoro, upimaji wa viwanja katika miji yetu unakwenda taratibu mno na katika miji mingine unapita hata mwaka mmoja au miaka miwili Halmashauri ya Mji haijapima viwanja. Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote, wapime viwanja ili wananchi waweze kujenga kwa mujibu wa mpangilio wa viwanja vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, najua katika Halmashauri nyingi, wanalo tatizo la fedha lakini tunawashauri kwamba sasa hivi viwanja vikishapimwa, vinauzwa, kwa hiyo, wakikopa, wapakima viwanja, watakapowauzia wananchi viwanja vile, watarejsha ile mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ile Miji ambayo haina *Master Plan*, Wizara yangu iko tayari kusaidiana nao ili kuandaa *Master Plan* kwa sababu jukumu la kuandaa *Master Plan*, ni la Halmashauri yenyewe na Wizara yangu iko tayari kusaidiana nao kiutalaam.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa, majukumu ya Wizara hii na hiyo Mipango Miji, inaonyesha udhaifu ulioko Serikalini na kwa kuwa viwanja vipya vinapotolewa, *infrastructure* hakuna, ndiyo inayosababisha ujenzi holela. Je, lini Wizara yako itakuwa tayari inapotoa viwanja vipya kama kula Kibada, wataweka *infrastructure* kabisa na wataweka aina ya ramani na majengo yanayotakiwa kama nchi nyingine zinavyofanya?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nikubaliane naye kwamba katika viwanja tunavyopima sasa hivi, miundombinu kwa maana ya barabara, maji na umeme vinachelewa sana kufika na hili ni tatizo ambalo tunalishughulikia kwa kukaa na Wizara zinazohusika ili tuwe na utaratibu kwamba wanapopima viwanja, mtu wa maji, mtu wa barabara na mtu wa umeme vile vile afike.

Mheshimiwa Spika, lakini hii kuchelewa kwa umeme na maji kama viwanja vingekuwepo bado watu tu wangejenga katika mpangilio mzuri, maji na umeme vikawafuata. Sema tatizo letu kubwa kabisa upimaji wa viwanja, ni mdogo sana na hili ndilo linalosababisha ujenzi holela mijini. Narudia tena kwamba ili miji yetu iende sawa sawa, Halmashauri zote za Miji, kila mwaka lazima wapime viwanja vya kutosha ili Watanzania wajenge ndani ya mpangilio mzuri wakati huo huo tukihamasisha wenzetu wa miundombinu ya maji, barabara na umeme na wenyewe waongeze kasi.

Na. 285

**Kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Afya Hospitali ya Wilaya ya Lushoto**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO (K.n.y. MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA)** aliuliza:-



Kwa kuwa, kumekuwa na idadi kubwa ya wakazi wa Wilaya ya Lushoto na kuna mahitaji makubwa ya Wataalam wa afya:-

Je, serikali itaanzisha lini Chuo cha Manesi, Wakunga na Watumishi wengine wa Afya katika hospitali ya Wilaya ya Lushoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba nichukue nafasi hii, niwape pole sana wananchi wa Mkoa wa Tanga, kwa ajali mbaya sana ya basi ambayo imetokea Wilaya ya Korogwe na kupoteza maisha ya abiria wengi. Vile vile niwape pole sana wale majeruhi. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, lakini vile vile wale majeruhi awape kupona haraka.

**SPIKA:** Imetokea lini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Jana!

**SPIKA:** Looh, pole sana!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wilaya ya Lushoto inakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa Wataalam wa Afya. Hata hivyo, tatizo hili ni la nchi nzima ambapo wastani wa upungufu wa watumishi Kitaifa ni aslimia 62.

Mheshimiwa Spika, zipo jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kukabiliana na tatizo hili. kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), pamoja na mikakati mingine, upo mkakati mahususi wa kuongeza idadi ya wataalam wa afya nchini kwa kutekeleza yafuatavyo:-

- Kuongeza idadi ya udahili wanafunzi kwenye vyuo vya afya;
- Kupanua Vyuo vya Afya vilivyopo kwa kuvifanyia ukarabati, kuongeza Walimu, vyumba vya kufundishia na vifaa vya kujifunzia;
- Kufufua Vyuo vya Afya ambavyo vilikuwa vimefungwa;
- Kupitia mitaala kwa nia ya kupunguza muda wa mafunzo kwa kozi za Wauguzi na Matabibu kutoka miaka mitatu hadi miwili bila kuathiri kiwango cha taaluma;
- Kurejesha kozi za Matabibu Wasaidizi na Wauguzi Wasaidizi; na
- Kulegeza masharti na ajira kwa watumishi wa afya ili kuwawezesha kupangiwa kazi moja kwa moja kutoka vyuoni.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango niliyoitaja hapo, utasaidia kwa kiwango kikubwa, upatikanaji wa wataalam wa afya katika soko la ajira. Hata hivyo, pamoja na

upungufu wa watumishi uliopo katika soko la ajira, imebainika kuwa baadhi ya Halmashauri haziweki makisio ya watumishi hao kulingana na mahitaji halisi na hivyo kusababisha upungufu wa watumishi usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, nashauri Halmashauri zote, wanapoandaa makisio ya bajeti, wahakikishe kwamba wanakasimia watumishi wa afya kulingana na mahitaji na kuwasilisha Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kibali cha ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyo vyote vya kufundishia taaluma za afya vinavyomilikiwa na Serikali, mashirika ya dini na sekta binafsi hapa nchini ni vya Kitaifa. Wanafunzi hupangwa kujiunga na chuo chochote nchini kwa aina ya mafunzo wanayoomba ili mradi wana sifa zinazohitajika kujiunga na mafunzo husika.

Aidha, baada ya kuhitimu, wanachuo hupangiwa kazi mahali popote nchini kulingaana na mahitaji. Hivyo, wanafunzi toka Wilaya ya Lushoto, wanaweza kujiunga na vyyo vyovyote vilivyopo nchini na vilevile kufanya kazi mahali popote nchini. Kwa maana hiyo, Wilaya ya Lushoto inaweza kupata wataalam wa afya zaidi bila hata kuwa na Chuo cha Afya Wilayani ili mradi wazingatie ushauri nilioutoa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Lushoto, Jimbo la Bumbuli, kuna Chuo cha Matabibu kinachomilikiwa na Kanisa la Kilutheri. Chuo kinaendeshwa kwa ubia na Serikali. Kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha chuo kingine cha afya katika Wilaya ya Lushoto.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa amesema kwamba kuna Chuo cha Matabibu katika Hospitali ya Bumbuli, je, kwa nini Serikali haiweki kitengo cha mafunzo cha Wauguzi Wasaidizi kwa sababu Hospitali ya Bumbuli ina miundombinu inayoweza kutosheleza?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, pale kwenye Chuo cha Bumbuli tunafundisha Matabibu, lakini ni kwamba unapongeza Chuo kufundisha taaluma nyingine inamaana uongeze vile vile rasilimali watu, lakini vile vile na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema tu kwamba Mkoa wa Tanga umebahatika kuwa na Vyyo vya Ukunga. Korogwe tunacho Chuo cha Wakunga pale ambacho kinaitwa *School of Public Health Nurse*. Wilaya ya Muheza kuna Chuo cha Wauguzi lakini vile vile Tanga bado tena kuna Chuo cha Wauguzi.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa, kwa Mkoa wa Tanga na Lushoto, badala ya kutaka kuongeza ili kuhakikisha kwamba tunaongeza rasilimali, bado wana uwezo wakajiunga katika Vyyo hivi nilivyovitaja katika Wilaya ambazo ziko ndani ya Mkoa wa Tanga, lakini vile vile wana nafasi pia ya kwenda kuomba na kujifunza katika Mikoa mingine.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda kuuliza swali lifuatalo:-

Hivi sasa Wizara ya Afya imetangaza na ilitutangazia hapa Bungeni kwamba ina mpango wa kuwa na Zahanati kila Kijiji na kama tunavyojua tuna maelfu ya Vijiji katika nchi hii. Mimi nina hakika wananchi watakapoambiwa kujenga, watachukua muda mfupi sana kuzijenga hizo Zahanati, je, Serikali ina mpango gani wa ku-*train* watumishi ili Zahanati hizo baadaye zisiwe *White Elephant* katika Vijiji vyetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mpango wa MMAM kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tuna mpango wa kuweka Zahanati katika kila Kijiji na Vituo vya Afya katika kila Kata. Kama nilivyosema nilipokuwa naeleza katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba Serikali imepanga mikakati ya kuongeza udahili wa Wanachuo. Nataka niseme tu kwa kufanya ulinganisho, idadi ya waliodahiliwa imeongezeka kwa mfano, mwaka 2005/2006 tulikuwa tumedahili wanafunzi

1,013 lakini kwa mwaka 2008/2009 waliodahiliwa walikuwa ni 3,831 kwa maana hiyo, hii inaonyesha ni jinsi gani idadi ya wafanyakazi itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile naomba tu niseme, ili kuonyesha kwamba wataalam wanaongezeka, idadi ya wataalam waliopangwa kufanya kazi katika Sekta ya Afya imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Kuanzia Januari 2006 hadi kufikia Machi 2009, kuna jumla ya waajiriwa 11,709 waliopangiwa kwenye vituo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali kwa kweli kwa kutumia mpango huu, idadi itaongezeka na mpaka mpango wa miaka 10 utakapomalizika, tutahakikisha kwamba sehemu zote zitafikiwa. Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii niwaombe wananchi waendeleo kujenga na Serikali itaendelea kuleta wafanyakazi.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa sasa hivi Mabwana Afya Wasaidizi (*Health Assistants*) wanataka kujiendeleza lakini sasa hivi naona kama Serikali haina mpango nao, kwa nini sasa Serikali isiwe na mpango ili waweze kujiendeleza?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali haitaki kuwaendeleza Mabwana Afya Wasaidizi (*Health Assistants*). Kwanza, katika mpango wetu wa MMAM, Mabwana Afya wanapelekwa shuleni na wanasoma, kwa hiyo, tunatoa Mabwana Afya ambao ni wapya. Lakini vile vile wale ambao wako kazini, kuna utaratibu ambao tumeuweka kwamba, wale ambao wanataka kujiendeleza wanajiendeleza kwa njia ya masafa na sasa hivi tumeanzisha kitengo na tunao watu ambao wanajiendeleza kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge, kama ana Mabwana Afya wake kutoka Kigoma hawafanyi hivyo basi waende Halmashauri ili waweze kujiandikisha wawasiliane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wataweza kupata ule udahili ili waweze kusoma kwa masafa na si lazima waingie darasani.

Na. 286

### **Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia –Kichonda**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna kero kubwa ya maji katika kijiji cha Kichonda Wilayani Liwale na kwamba juhudi za kupata maji kupitia miradi mbalimbali ikiwemo *TASAF* hazijazaa matunda; na kwa kuwa, kijiji hicho kipo katika mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni:-

(a) Je, ni lini mradi huo wa maji wa Benki ya Dunia utanza Wilayani Liwale?

(b) Kwa kuwa, miradi ya awali kama ya *TASAF* haikufanikiwa kijijini hapo; je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuongeza utafiti wa ziada ili mradi wa Benki ya Dunia uweze kuwaondolea wananchi wa Kichonda kero ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Liwale kwamba, mchakato wa kumpata Mtalaam Mshauri wa kufanya usanifu wa mradi wa maji kwenye Vijiji 10 katika Jimbo la Liwale umekamilika. Tayari Benki ya Dunia imekwishatoa kibali na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imesaini mkataba na kampuni inayoitwa *Don Consult Ltd.in Association with Relief to Development Society (REDESO)*, tarehe 21/05/2009. Mtaalam Mshauri huyo alianza kazi tarehe 29/06/2009 katika Vijiji 10 vya Nahoro, Ngumbu, Kiangara, Kipule, Mpigamiti, Likombora, Makata, Namihu, Kichonda na Barikwa/Chimbuko.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mashirika ya *TASAF*, *JICA* na hata *DDCA*, yamefanya kazi kubwa ya utafiti wa maji chini ya ardhi lakini kwa bahati mbaya visima vilivyochimbwa katika Kijiji cha Kichonda havikuwa na maji. Katika utekelezaji wa programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inayoendelea katika nchi nzima Kijiji cha Kichonda kinatarajiwa kupata maji ya kutosha kutoka katika Kijiji cha Mbuli ambacho kimeonekana kuwa na maji mengi chini ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kazi sasa imeanza, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya Liwale, Mtaalam Mshauri na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba, wananchi wa Kijiji Kichonda nao wanapata maji ya uhakika kutoka kwenye vyanzo vya maji mbadala.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa nina imani na Wizara hiyo vizuri sana na kwa kuwa mradi wa *World Bank* utachukua muda mrefu, ni hatua gani za dharura ambazo zitaweza kuchukuliwa angalau tuweze kupata maji haraka iwezekanavyo kwa kipindi ambacho tunasubiri mradi wa *World Bank* kutekelezeka?.

Swali la pili, kwa kuwa kijiji cha Kichonda tunazalisha karibu mazao ya aina zote na kwa vile kuna wanyamapori wengi, kwa hiyo, kuna ukweli kwamba maji yapo karibu, je, ni kweli kwamba Serikali inashindwa kupata maji katika kijiji cha Kichonda, hatuna wataalam ambao wangeweza kufanya kazi hiyo vizuri zaidi ili Kijiji cha Kichonda tukaweza kupata maji badala ya kutegemea Mbuli ambayo iko umbali wa kilomita saba kutoka Kichonda?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua za dharura nilisema kwamba, *TASAF*, *JICA* na *DDCA* walifanya kazi ya kutosha kutafiti visima katika Halmashauri ile na hasa katika hicho kijiji lakini maji hayakuwa mengi ya kutosha. Lakini hata hivyo *TASAF* tayari ilikwishatenga tena shilingi karibia milioni sita (6,000,000) kwa ajili ya kuendelea na utafiti wa maji chini ya ardhi na mradi huo utaendelea tena kutekelezwa katika mwaka huu wa 2009/2010 na Serikali tutaendelea kufuatilia kuangalia kwamba, ni wapi ambapo maji yanaweza kupatikana na tuwasaidie wananchi wale wa Kichonda kama hatua za dharura.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wataalamu wa kupima maji chini ya ardhi, mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kigwalilo kwamba, wataalam wapo katika Wizara yangu ya Maji na Umwagiliaji na kwanza nimpe pole kwamba hata mchakato ulivyokuwa umechelewa

huko nyuma, tumegundua kwamba mojawapo ya sababu ilitokana na wao kufiwa na Mhandisi wao wa Maji. Naomba nimpe pole kwa hilo lakini nimhakikishie kwamba Wizara itaendelea kutuma wataalam kutoka Wizarani kwenda kuziba pengo hilo angalau ili shughuli hizi ziweze kuedelea na hivi sasa nimeamua kwamba, nitawaagiza Wataalam wa Rasilimali za Maji kwenda kushirikiana na Wahandisi hawa walioko pale pamoja na Mhandisi Mshauri ili kuangalia uwezekano wa kupatikana maji katika kijiji hicho ili tutatue tatizo hilo.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kweli Liwale kuna matatizo na kwa kuwa Liwale ni Mkoa wa Lindi kwa hiyo Wilaya zote za Mkoa wa Lindi zina matatizo ya maji hasa Nachingwea na Lindi Mjini. Lindi Mjini kwa miaka 30 kuna matatizo ya maji, je, Serikali itatusaidiaje?

**SPIKA:** Una maana hata Mchinga na Mtama pia? Majibu Meshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, uko utaratibu ambao unaendelea kutekelezwa kwa ajili ya miji ile ya Nachingwea, Masasi na hata Lindi labda tatizo tu ni kwamba angetenda apate maji sasa hivi. Lakini nataka nimhakikishie kwamba, mradi ule ambao tunautekeleza kwa ajili ya kupeleka maji katika Wilaya hizo, uko tayari kabisa unaendelea na hivi sasa wataalam wetu wametoka kule kwa ajili ya kuangalia kwamba ni hatua gani za dharura zitachukuliwa wakati mradi ule ukitekelezwa. Sasa kwa maelezo ya ziada kwamba tutafanya nini na ni hatua gani zimeamriwa zichukuliwe, nimkaribishe Mheshimiwa Mikidadi ofisini ili nimueleze kwa ufasaha zaidi.

Na.287

### **Serikali kusitisha kupeleka Form I Shule za Bweni**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

kwa vile Serikali imeamua kusitisha utaratibu wa kawaida wa kupeleka watoto wa *Form One (I)* Shule za Sekondari za Bweni kuanzia mwaka 2009, je, uamuzi huu una lengo gani na umezingatia athari za muda mfupi na muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijasitisha udahili wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza katika Shule za Bweni, bali imepunguza baadhi ya shule za bweni kwa wanafunzi hao kwa malengo yafuatayo:-

Moja, kuongeza nafasi za Kidato cha Tano ambazo zimekuwa chache sana, ikizingatiwa kuwa mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari nchini yameongeza idadi ya wahitimu wa Kidato cha Nne wenye ufaulu wa kutosheleza kudahiliwa kwa masomo ya Kidato cha Tano.

Pili, kutekeleza azma ya Serikali ya kupunguza gharama za uendeshaji wa shule za bweni bila kuathiri idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza. Idadi hii

haiathiriki baada ya wananchi kuhamasika kujenga shule za sekondari za kutwa katika kila Kata.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu, hauna athari kwani hautahusisha wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na shule zenye vipaji maalum, shule za watoto wenye mahitaji maalum na shule za michepuo ya ufundi na kilimo. Shule hizi zinaendelea kudahili watoto wa Kidato cha Kwanza kwa utaratibu wa kupanga wanafunzi kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu kwamba hatua hiyo haina athari na kwamba, wamepunguza tu udahili, nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anajua vile vile kwamba, shule za Kata zilizo pembezoni mwa nchi pamoja na Ludewa pengine hata Urambo, hazina Walimu wa kutosha au hawapo kabisa na kwa hiyo katika Wilaya hizo hawataweza kupeleka watoto mpaka Chuo Kikuu kwa sababu walikuwa wanapitia kwenye shule hizi za mabweni. Je, Mheshimiwa haoni kwamba, kitendo hiki cha kutunyima watu wa pembezoni kama Ludewa nafasi ya kuwa na wataalam kutoka maeneo hayo na wataalam hawa kuendelea kutoka kwenye maeneo machache hapa nchini ni kitendo cha ubaguzi na kinatunyima wananchi wengine haki zetu kama wananchi wa nchi hii?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, kitendo hiki ni ukwepaji wa Serikali kujenga shule za *High School* na kuwatupia mzigo wananchi waendeleo kujenga shule za *High School* licha ya kujenga shule za Kata, Zahanati, Vituo vya afya, kila kitu mzigo wanatupia wananchi, kwa nini Serikali haijengi shule hizi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya kupunguza kupeleka wanafunzi wa masomo ya kawaida kwenye shule za bweni zenye Kidato Tano na Sita, ni kupokea kwa haraka mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) ambapo wamekuwa wakifaulu kwa wingi na kwamba endapo tungelisubiri kujenga shule za Kidato cha Tano na Sita kwa mpango wa MMES II, tungechukua muda mrefu na hivyo tungewapoteza vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali haikwepi jukumu, dhamana iliyopewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mujibu wa Sera na Katiba ya nchi, tunaatambua wajibu wetu na shule hizo zitajengwa na katika hotuba ya Waziri mwaka uliopita wa 2008/2009 tulionyesha azma ya kujenga shule mbili za Sekondari za Kidato cha Tano kwa kila Wilaya naamini Mpango wa MMES II utakapoanza kutekelezwa, tutatimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, hatuwanyimi wanafunzi haki ya kwenda Vyuo Vikuu na ndiyo maana tumeona tufanye hivyo. Ingekuwa busara kusubiri tujenge ndipo waende. Wanafunzi wote watakaofaulu na kupata sifa za kwenda kwenye shule za vipaji maalum au wanafunzi wenye mahitaji maalum au wanafunzi wanaokwenda kwenye shule za ufundi, tutawapeleka.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba nimalizie kwa kusema, idadi ya wanafunzi ambao tumewapeleka kwenye shule za bweni ilibidi iingizwe kwenye mchakato wa bajeti ya mwaka huu kuepusha malalamiko na madai ya uhaba wa chakula, hatukuwa na njia nyingine ila kwenda kwenye uhalisia.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali.

Kwa kuwa wananchi wengi sana hapa nchini wanaendelea kiitikia ushauri wa Serikali wa kujenga hosteli katika shule za Kutwa, je, Serikali imejiandaa kiasi gani katika kuwasaidia wananchi hawa katika kuendesha hosteli hizo hasa kwa kuzingatia kwamba, kuendesha hosteli kuna gharama sana, hasa katika kupatikana kwa chakula, maji na umeme?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kwamba ujenzi wa hosteli ni gharama kubwa na ndiyo maana katika uamuzi wa kujenga shule za Sekondari katika kila Kata, tulitarajia shule zingejengwa karibu na makazi ya wananchi ili kuwapunguzia umbali na kuweza kuwapa utulivu na umakini kwa ajili ya kujifunza. Hata hivyo, kwa kuwa shule hizi hivi sasa zimeishagatuliwa kwenye Halmashauri na kwa kushirikiana na Mifuko mbalimbali ukiwemo wa *TASAF* bado Halmashauri na wananchi kwa ujumla, wanayo fursa ya kutumia Mifuko yao hiyo na fursa zilizopo kuweza kujijengea hosteli kwa faida ya watoto wao. Kwa hivi sasa, mambo yote yanayohusu ujenzi wa madarasa, maabara pamoja na hosteli, tumeishagatua, tunaomba maombi zaidi tuyaelekeze TAMISEMI.

Na. 288

### **Magenge ya Kutengeneza Barabara Vijijini**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mazao mengi ya chakula na ya biashara yanazalishwa Vijijini na hulipatia Taifa letu mapato makubwa; na kwa kuwa mtandao wa barabara za Vijijini ni muhimu sana kiuchumi, kuyalinda na kuboresha maisha ya Wakulima na Wafanyakazi wasiopungua asilimia 80 wanaoishi huko; na kwa kuwa, njia mojawapo ya kuongeza ajira kwa vijana wengi waishio Vijijini bila ajira, ni kurudisha haraka utaratibu wa zamani wa magenge ya kutengeneza barabara ili kuharakisha usafiri na usafirishaji wa mazao kwenye barabara kuu:-

Je, Serikali inaweza kuharakisha kuundwa kwa magenge ya kutengeneza barabara ili kuhakikisha kuwa kila mavuno makubwa yanayopatikana, yanafikishwa mapema kwenye masoko na kwenye maghala?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliondoa magenge yaliyokuwepo awali kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo ya barabara kuu baada ya kuanzisha sera ya kutumia Makandarasi kwa kazi hizo ili kuongeza ufanisi. Kwa mujibu wa Sheria Na. 13 ya Barabara ya mwaka 2007, magenge hayo hayaruhusiwi isipokuwa inaruhusu kuanzisha kambi kandokando ya barabara kuu kadri zinavyohitajika kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wasafiri, wasafirishaji pamoja na watumishi wa Wakala wa Barabara wanaosimamia Makandarasi wakati wanafanya kazi za matengenezo ya barabara. Hivyo, Serikali haina



mpango wa kurudisha utaratibu wa zamani wa kuwa na magenge ya kutengeneza barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa vijana kwenye ujenzi wa barabara, nawashauri washiriki katika kazi za matengenezo na ujenzi wa barabara kupitia kwa Makandarasi wanaopewa kazi hizo.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wakandarasi wengi nchini wanaotekeleza utengenezaji wa barabara zinazosimamiwa na *TANROADS*, barabara za udogo au changarawe, hawajengi mifereji ya kutoa maji ambayo husababisha barabara hizo baada ya mvua kunyesha kuharibika vibaya, je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha inawasimamia *TANROADS* nchi nzima kuhakikisha barabara za aina hiyo zinatengenezwa mifereji ili ziweze kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Lyamba kuwa ujenzi wa barabara bila kutoa msukumo katika ujenzi wa mitaro, ni kitu ambacho ni kigumu sana. Wataalamu wengi wanasema kwamba ili barabara idumu, ni lazima mitaro iliyoko pembeni isafishwe au izibuliwe maji, maji yaweze kupata mkondo wake wa kupita. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wale wote wanaosimamia barabara, tutawasihi na kuwasisitiza umuhimu wa kujenga mitaro uwepo na tumeona katika barabara ukitoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam maeneo ya Gairo, mitaro yote imezibuliwa na mingine wanaweka mawe na saruji. Hiyo ni hatua kubwa na hela kubwa imetengwa kwa ajili ya *maintenance* ya barabara zetu Mijini na Vijijini.

**SPIKA :** Nimekuona Mheshimiwa Ligallama kwa swali la nyongeza na la mwisho.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Kwa kuwa Wakandarasi wengi katika ujenzi wa barabara hasa hizi za *Regional Roads*, wanakuwa wanazifupisha kwa upana kutokana na kutokuwa kiwango maalumu, je, Serikali inafahamu hilo kwamba wengi wao wanazifupisha barabara hizi kwa upana wake ili kujipatia manufaa kwa ukandarasi wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, wakati wa kujenga barabara, mara nyingi kunakuwa na makubaliano baina ya mjenzi na yule anayetaka kujengewa na kama anayetaka kujengewa anakubali kujengewa kwa kupunguziwa, ni kwamba anakula hasara yeye. Ni mategemeo yangu kwamba wale wote wanaohusika na usimamizi wa ujenzi wa barabara, watakuwa makini kuona kwamba urefu na upana unaotakiwa ambao ndio pesa zinazolipwa yaani (*value for money*) inapatikana kwa barabara zile ambazo zinajengwa na wale wasimamizi wahakikishe kwamba barabara zote zinafuata ukubwa au upana ambao wamekubaliana katika mikataba yao.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, sasa kama kawaida ni matangazo nikianza na wageni.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Capteni John Chiligati na Mheshimiwa Juma Hassani Killimbah, ni Wazee Waasisi wa CCM toka Kata ya Shelui ambao kwa majina ni Mzee Maganga. Naomba Mzee Maganga tafadhali asimame na Mzee Juma Ramadhani, naona pia amekwishesimama na Sheikh Mohamed Yusuph, ahsante sana wazee wetu, karibuni sana kutoka Shelui, tunawashukuru kwa kuendelea kufuatilia harakati za siasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Viongozi wa Umoja wa Vijana wa CCM kutoka Sasagila Manyoni ambao ni Peter Mwaja Mwenyekiti wa Vijana, Magreth Ponda Kada wa CCM, ahsante sana karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni ishirini wa Mheshimiwa Fred Mpendazoe wa Kishapu, wakiongozwa na Ndugu Shija Ntelulu, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wageni wa Mheshimiwa Idd Azzani ambao ni Viongozi wa UWT, Jimbo la Kinondoni kutoka Kata kumi ambao ni Mwenyekiti na Makatibu wa Kata za Magomeni, Mzimuni, Kigogo, Lugumbi, Tandale, Kijitonyama, Makumbusho, Mwananyamala, Kinondoni, Hananasifu wakiongozwa na Kaimu Katibu UWT wa Wilaya ya Kinondoni Bi. Huba Issa. Karibuni sana, naona mnaushirikiano wa karibu na Mbunge wenu na hii ni faraja kubwa kwa sababu wakati huu Waheshimiwa Wabunge tumezongwazongwa hivi. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, nao ni Bwana Michael Mushi kutoka Shirika la Msaada, Serikali ya Marekani na Bwana Goodchance Marik, Mkurugenzi kutoka Shirika la Misaada la Serikali ya Marekani katika miradi ya *Health Policy Initiative (HPI)*, yule pale, karibu sana na hongera sana kwa kazi yenu nzuri katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge wa Ulanga, kwa maana ya Mashariki na Magharibi hususani Mheshimiwa Selina Ompeshi Kombani, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa wa Ulanga Magharibi. Wageni hao ni Waheshimiwa Madiwani na pia Watendaji kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga wakiongozwa na Bwana Salum Mdemba, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, wageni kutoka Ulanga tafadhali, ooh, wale pale, ahsante sana, tunawashukuru na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Oscar Mkasa, Mbunge wa Bihalamuro Magharibi ambao ni Bwana Robin Huus na mkewe, Sue Huus kutoka Canada. *Mr and Mrs Huus from Canada, we are happy to welcome you all and I believe you are friends of Tanzania, you are welcomed all the time, thanks very much and carry the message forward that Tanzania is a friendly country, thank you.* *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni hawa wa Ofisi tu, ni Bwana Reginald Miruko, Mhariri wa Gazeti la Mwannchi Jumapili, amefuatana na Ndugu Yahya Charahani ambaye ni Mhariri wa habari. Wanalitembelea Bunge. Wao leo hawakukaa kama Wanahabari, leo wamekuja kuangalia shughuli za Bunge, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunao pia wanafunzi arobaini na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi Mbwanga pengine watakuwa katika ukumbi wa *Basement*. Wanafunzi hamsini na Walimu, nadhani hivyo hivyo kutoka Sekondari ya Kikuyu Dodoma, nadhani hawakupata nafasi wako *basement*. *(Makofi)*

Pia wanafunzi thelathini na Walimu wao kutoka shule ya Morogoro Sekondari, nao nadhani wako *Basement, oh!* Wale pale, ahsante sana, karibuni sana vijana tunawatakia mema katika masomo yenu, nchi inahitaji wataalamu kama ninyi mkishahitimu.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Spika na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ni wanakwaya ishirini na sita kutoka kwaya ya *Victory Singers*, Urambo, wakiongozwa na Mlezi wao, Bwana Daudi Mnangala, naomba kwaya wasimame, viongozi wao ni Evarist Mbona, Makoko Chakupewa, Hezroni Michael na Tabitha David, karibuni sana ndugu zangu kutoka Urambo na nawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayofanya hasa katika kukemea maovu nchini, mambo ya Ukimwi na matatizo mengine. Ni kwaya nzuri sana na kazi mnayoifanya tunaithamini sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pamoja nao wapo, kundi la vijana sita la *Green Guard CCM* wakiongozwa Stephen Kilomo, wale pale. Mambo haya ndugu zangu Wabunge hasa wa Majimbo, usipokuwa na vijana wako wanakuzungukazunguka, inakuwa matatizo. Kwa hiyo, Stephen Kilomo, nawashukuru sana kwa huduma mnayonipa na bado mitihani mikubwa zaidi inakuja, karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna mtaalamu wa Ngoma ya asili ambaye ni mwanafunzi wa marehemu Mzee Mwinamila, yeye anatoka Kata ya Uyumbu, kule Urambo, ni Mzee Hassan Kiponda. Yule pale ahsante sana na karibu sana. Tungo zako za kuhimiza kilimo, tumezipenda sana. (*Makofi*)

Yupo pia mtaalamu wa Mashairi kule Urambo, anaitwa Amir Uledi, bwana Amir, naomba usimame, anatunga mashairi mazuri sana na nitamkutanisha pia na Mheshimiwa Mudhihr ili azidi kujimarisha katika taaluma hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Hatimaye kuna kikundi cha vijana saba ambao ni Kikundi Maalumu cha Hamasa cha Mbunge wa Urambo Mashariki, hawa wanaitwa kikundi cha Fagilia na kiongozi wao anaitwa Nicodemus Kilatu. Nico yule pale, wanafagilia ahsante sana, nimefarijika sana kwa ujio wenu, ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa ujumbe kwa wadogo zangu kama Simbachawene na wengine, hivyo ndivyo unavyojipanga katika Jimbo, nawashukuru sana wageni wangu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ameomba niwatangazie kwamba, wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala itakuwa na kikao leo saa saba mchana, ukumbi namba 219.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba leo saa saba mchana, Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, wakutane ukumbi namba 231 saa saba mchana.

Naona huo ndio mwisho wa matangazo kwa leo. Sasa namwita Katibu atuongoze kwa shughuli inayofuata, Oh! Samahani ndio taabu ya hivi vinavyoandikwa dakika ya mwisho, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila anaomba nimtambulishie mgeni wake Bwana Faraji Hussein Katalambula, mtunzi maarufu wa vitabu huyu. Ahsante Faraji. Bwana Faraji huyu tumesoma naye shule ya sekondari kwa hiyo na mimi nitafurahi tuonanae baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna tangazo limeponyoka hapa basi tutalitafutia wakati muafaka. Katibu!

## **KAULI YA WAZIRI**

### **Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa tamko la Serikali siku ya leo kuhusu uanzishwaji wa Benki ya Wanawake Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wazo la kuanzisha Benki ya Wanawake linatokana na ukweli kwamba wanawake ni kundi kubwa linalohitaji juhudi za makusudi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kujitelea maendeleo yao binafsi ya familia zao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Watanzania kwa sasa inakaribia milioni araobaini laki sita sitini na saba, mia saba tisini na nne. Kati ya hawa, wanawake ni 51% ambao ni takribani wanawake milioni ishirini laki sita tisini na sita, mia nane hamsini.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tunafahamu kuwa kundi hili kubwa la wanawake ndilo linalotoa mchango mkubwa katika uzalishaji mali na kuleta maendeleo ya uchumi nchini, lakini cha kusikitisha ni kwamba kundi hili kubwa ndilo lenye umasikini kubwa. Kwa hiyo, ili Taifa letu liendelee lazima lianze na kuwaendeleza wanawake. Kama sote tunavyofahamu kuwa kumuendeleza mwanamke ni kuendeleza familia na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuna vikwazo vingi katika kuwaendeleza wanawake ikiwa ni pamoja na desturi na mila potofu, Sheria zilizopitwa na wakati, mfumo dume unaokandamiza wanawake na kusababisha kuwa na wanawake wachache sana katika ngazi mbalimbali za uongozi na hivyo kukosa fursa ya kushiriki katika kupanga, kugawa na kumiliki rasilimali za nchi hii. Aidha, fursa ambazo zingeweza kuwapa wanawake uwezo wa kujiendeleza kiuchumi ni finyu na kwa kiasi kikubwa hazipo. Fursa hizi ni pamoja na kuwapa mikopo wanayohitaji wanawake ili kuendesha shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ndio maana katika maonyesho ya kibiasahara yaliyofanyika Dar es Salaam mnamo mwaka 1999, wanawake wajasiriamali walioshiriki katika maonyesho hayo kutoka Mikoa yote ya Tanzania, walimwomba Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Serikali isimamie uanzishaji wa Benki ya Wanawake, ambayo itajielekeza katika kuwapa mikopo wanawake wajasiriamali. Hatimaye Serikali ilitoa kibali cha kuanzisha Benki ya Wanawake mnamo Octoba mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, tamko hili la uanzishaji wa Benki ya Wanawake Tanzania ambalo limekuwa likisubiriwa kwa shauku kubwa na wanawake na umma kwa ujumla, ni moja ya mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Pamoja na kuwa walengwa wakuu ni wanawake, Benki hii imejipanga kutoa huduma kama Benki nyingine yoyote ya biashara.

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ya Benki hii, ni kuhamasisha na kukusanya amana kutoka kwa wateja na pia kutoa mikopo ikiwemo ya wajasiriamali wanaomiliki biashara ndogo, za kati na kubwa. Benki ya Wanawake Tanzania itatoa huduma kwa watu wote bila kujali jinsia, dini, kabila au hali ya kiuchumi, Benki itatoa huduma zingine

zikiwemo kuhamisha fedha, kubadilisha fedha za kigeni, huduma za kifedha pamoja na kutoa mikopo na ushauri wa masuala ya kibiashara na uzalishaji, hasa kwa biashara zinazomilikiwa na wanawake.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu ya Benki ni BENKI PEKEE KWA WOTE. Kauli mbiu hii, inatoa wito kwa umma wa Watanzania, wanawake na wanaume wenye uwezo na wasio na uwezo kununua hisa za Benki, mtu mmoja mmoja au vikundi zikiwemo SACCOS. Katika Mpango Mkakati wa Benki, Benki hii imejipanga kufungua matawi hadi kufikia Mikoa yote ili kuwa karibu na wajasiriamali wenye uwezo mdogo wanaotaka kujiendeleza kibishara na kwa uzalishaji mali. Hili linawezekana kwa sababu uongozi wa Benki unao watu ambao wanaguswa na mahitaji muhimu ya kiuchumi ya wanawake na pia ina watalaamu na Mameneja wenye uzoefu.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Benki hii usingewezekana bila ya kuungwa mkono na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ambaye wakati wote ameliunga mkono suala hili kwa hali na mali, hadi kuiwezesha Serikali kuchangia shilingi bilioni 2.1 za mtaji. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tunamshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa ushauri wake, tunamshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda (Mb), kwa maelekezo na msukumo wake akiwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tunamshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb) na wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa ushirikiano wao. Tunamshukuru Gavana wa Benki Kuu, Ndugu Benno Ndulu na watalaamu wa Benki Kuu waliotunga mkono katika masuala ya kitaalamu ya uanzishaji wa Benki. Aidha, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wote walionunua hisa za Benki za awali. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr Lucy Nkya (Mb), Katibu Mkuu, Bibi Mariamu Mwafisi, Mtaalamu Mwelekezi wa Benki, Bwana Altemius Milinga, Mratibu wa Benki, Bwana Ernest Chipata, Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu waliotangulia, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa ushauri wao. Namshukuru sana Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Benki, kwa kufanikisha uanzishaji wa Benki hii, natoa pia shukrani kwa Mheshimiwa Professor Peter Msolla (Mb), Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Uongozi wa Shirika la Posta Tanzania na Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Mheshimiwa Adam Kimbisa, kwa ushirikiano wao uliowezesha kupata jengo na nafasi ya maegesho ya magari.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamalizia, naomba nieleze kuwa, leo ni siku ya furaha na pengine ya kihistoria kwa wanawake na jamii yote ya Tanzania, kwa sababu hatimaye maandalizi ya kufungua Benki ya Wanawake sasa yamekamilika. Ninafurahi kulitangazia Bunge lako Tukufu na wananchi wote wa Tanzania kwamba kesho tarehe 28 Julai 2009 Benki ya Wanawake Tanzania inafungua milango yake na kuanza kutoa huduma za kibenki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tawi la kwanza la Benki ya Wanawake Tanzania ambalo linaanza kutoa huduma kesho, lipo katika jengo la Posta ya zamani, upande wa mtaa wa Mkwepe, jijini Dar es Salaam. Nafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Mkurugenzi

Mtendaji wa kwanza wa tawi hili, ni mwanamke mwenye uzoefu katika shughuli za Benki. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mtaje!

Mheshimiwa Spika, wajumbe wa Bodi ya Benki wanakuja kesho, mtawaona.

**SPIKA:** Jamani msimsumbue Waziri eeh! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kesho tutawatambulisha rasmi baadhi ya watendaji, wajumbe wa Bodi na wengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, natoa wito kwa wanawake wote wa Tanzania ambao Benki hii ni yao sasa washiriki mmoja mmoja na kwa makundi kununua hisa za Benki na kufungua akaunti zao kuanzia kesho, ili wamiliki Benki na kufaidi matunda yake. Aidha, natoa wito kwa wanaume wote wa Tanzania, wafanyabiashara, taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kununua hisa na kufungua akaunti ili kunufaika na huduma za benki na wakati huohuo kuwezesha Benki kuwa na mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa njema. Hiyo mimi nadhani hata sisi Wabunge tutapimwa wakati wa uchaguzi, swali moja litakuwa wewe unasema ni mtetezi wa haki za wanawake, je, una hisa katika Benki ya Wanawake? Kwa hiyo, mimi nitanunua hisa kesho na ninatumaini kwamba Waheshimiwa Wabunge watafuata mfano huo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Luhahula ambao karatasi imenikuta baadaye ni Bwana Elius Bhatikundulaga ambaye ni mjomba wake. Hii kwa Kisukuma maana yake havifunuliwi kwa hiyo sijui tena mambo makubwa hayo. Halafu ndugu Boniface Juvenile ambaye ni kutoka Jimboni kwake, Mheshimiwa Luhahula wale pale, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo naomba nimwite Mwenyekiti Jenista kwa muda ili niweze kushughulikia udhuru fulani unaonihusu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea kauli ya Serikali, kauli muhimu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Margaret Sitta, basi namimi kama mwanamke, naomba nimpongeze sana kwa juhudi hiyo na niwapongeze wanawake wote wa Tanzania. *(Makofi)*

## **HOJA ZA SERIKALI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, labda kwa faida ya Watanzania wote, baada ya kuahirisha shughuli za Bunge Ijumaa, leo tena Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, Waheshimiwa Wabunge bado wanayo nafasi ya kuendelea kuichangia. Hivyo baada ya shughuli zote za asubuhi, tunaendelea tena na michango mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa asubuhi hii ya leo ninaomba nianze na Mheshimiwa Festus

Limbu na Mheshimiwa Richard Ndasa atakuwa mchangiaji wetu wa pili Mheshimiwa Festus Limbu, tafadhali!

**MHE. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru sana wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Magu, kwa ushirikiano wanaonipa katika kuendeleza Jimbo na Wilaya yetu ya Magu. Lakini naomba uniruhusu nitumie fursa hii kutoa rambirambi kutokana na kifo cha Diwani wa Kata ya Magu Mjini, Mheshimiwa Lazaro Madata ambaye alifariki Ijumaa na ninaomba wananchi wa Kata ile na wananchi wa Jimbo langu, wawe na subira wakati wa tatizo hili ambalo limetumefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia masuala yanayohusu Jimbo langu halafu baadaye nitachangia masuala ya Kitaifa katika sekta hii. Katika Jimbo la Magu, Kata ya Kisesa, kuna kijiji kinaitwa Ihayabuyaga, kijiji hiki ni kikubwa kina Sekondari, kina maduka mengi na wananchi wengi wamejenga nyumba za kisasa lakini tatizo bado hatujapata umeme, naomba sana Waziri uweze kutusaidia kijiji cha Ihayabuyaga kiweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Ndagalu katika Jimbo la Magu, ni Tarafa pekee ambayo haina umeme, Tarafa zingine zote zina umeme, naishukuru sana Serikali kwa hilo. Tarafa hii ya Ndagalu, ina Kata kama nne ukianzia Kata ya Sukuma, Kata ya Ngh'aya, kata ya Nkungulu na Kata ya Sishani. Tarafa hii inachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwemo pamba, mahindi, mpunga, mtama, viazi, mhogo pamoja na mazao ya mifugo. Pia inaongoza katika kilimo cha pamba. Wilayani Magu, kuna wawekezaji wengi wametaka kuwekeza katika Tarafa hii hasa kwenye viwanda vya kuchambua pamba lakini wameshindwa kwa sababu ya kutokuwepo na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali kipindi cha nyuma kwamba kwa nini umeme usitoke Magu upite Vijiji vya Lumeji, Kitongo, Nkhaya, Nkungulu, Kabila na hatimaye uweze kufika Shishani? Mheshimiwa Waziri alijibu kwamba gharama ya kutoa umeme Magu ni takribani shilingi bilioni 3.7 kwa hiyo ikaonekana kwamba hizi ni fedha nyingi ambazo haziwezi kupatikana kwa mara moja, tukasema sawa. Lakini kama fedha ni kidogo angalau basi umeme ungeenda kwa awamu; utoke Magu uende mpaka Kabila, halafu kutoka Kabila kwenda Shishani baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukawa na *option* nyingine ya kutoa umeme Talo Sekondari katika Jimbo la Sumve kupitia Kadashi uende mpaka Maligisu halafu uende mpaka Kabila angalau kwa awamu hii ya kwanza twende hivyo, ukitoka Kadashi uende Nyanghanga na hatimaye uende Lumeji kama njia hiyo ya kutoka Magu ni ghali sana. Tulikuwa na mazungumzo na Waziri na tathimini imeshafanyika, ni matumaini yangu kwamba Waziri atafikiria ili kwenye bajeti hii umeme huo uweze kutoka Talo kwa kuanzia uende mpaka Kabila na baadaye utaendelea mpaka Mahaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chanzo kingine cha umeme kutoka Kasori *Ginnery* ambako ni mpakani mwa Wilaya ya Bariadi na Wilaya ya Magu, nilidhani *TANESCO* wangeweza kutumia pia umeme wa Kasori kuweza kuupeleka katika Vijiji vya Salama, Bugatu, Chandulu hadi Kabila. Kwa hiyo, naamini kwamba vyanzo vyote hivi kama chanzo cha kutoka Magu kwenda Mahaha kupitia Kabila ni ghali Waziri, naomba sana tuweze kutumia vyanzo vya Talo pamoja na Kasori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo kwa kweli limekuwa likinisumbua, katika sekta ya pamba kumekuwa na matatizo ya kusindika pamba kwa kutumia *diesel*. Gharama za kusindika pamba kwa kutumia *diesel* ni kubwa sana kiasi kwamba inachangia

katika kufanya bei ya mkulima iwe chini kwa sababu wazalishaji wanaotumia vinu vya *diesel* wanakuwa na gharama kubwa zaidi na kwa hiyo ushindani unakuwa siyo *fair*, kuna wale wenye *ginnery* za umeme gharama zao ziko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwekezaji mmoja anaitwa *Alliance Ginnery*, ameomba kwa muda mrefu apatiwe umeme lakini kila mara majibu ni yale yale kwamba Serikali haina pesa, hadi hapo itakapopata pesa waweze kupelekewa. Hawa *Alliance Ginnery* wamejitolea na kutafuta pesa zao takribani dola laki nane, wamejenga *line* kutoka Nyashimo pale Nyasho kupitia kwenye Vijiji vyote mpaka kwenye *ginnery* yao kwa makubaliano kwamba *TANESCO* wangewarudishia fedha zao dola laki nane. *TANESCO* wakasema hawawezi kurudisha isipokuwa wawekezaji wagharamie nusu ya gharama hiyo. *TANESCO* imeanza kuingia lini ubia na wawekezaji wakati hawa walikuwa wanaisaidia *TANESCO* kwa sababu ilikuwa haina pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba wamelipa nusu ya hiyo, lakini wamepata kigugumizi cha kumalizia hiyo nusu inayobaki, *Alliance* na *TANESCO* wanaingia ubia, kwa nini huyu bado analipa bili za umeme mpaka sasa? Ni mwaka umeisha toka *Alliance* amalize kufunga *line* hii, ameshalipa shilingi milioni 90 za umeme, ametafuta dola laki nane amepeleka umeme na bado analipia bili ya umeme. Namwomba sana Waziri amalize suala hili, kiwanda kile kinafanya vizuri sasa kwenye pamba na mimi kama Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba, nawapongeza sana *Alliance*, wasiendelee kubughudhiwa, warudishiwe fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie muda uliobaki kuzungumzia masuala ya Kitaifa yanayohusu umeme, nimemaliza mambo ya Jimbo. Watanzania hadi mwaka 2000, tulikuwa tunategemea zaidi kilimo na mazao ya viwandani kwa kupata fedha za kigeni lakini kuanzia mwaka 2001 kipofu akaona mwezi, tumeanza kupata mapato yatokanayo na madini yetu kwa wingi, tunamshukuru sana Mungu kwa utajiri huu ambao nchi nyingi hawana, tunauza kwa mwaka tani 40 za dhahabu na tani hizo kwa mwaka ni sawa na shilingi trilioni 1.3. Mapato haya yanatusaidiaje katika kuendeleza nchi yetu, katika kuweka misingi imara ya maendeleo ya nchi yetu, katika kuweka miundombinu ambayo tutajivuna kwamba tulikuwa na madini, baada ya kuwa tumbaki na mashimo katika miaka ijayo? Tunatumiaje utajiri wetu wa madini katika kuboresha huduma za jamii, kwenye afya, elimu, maji na barabara na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuuliza Mtanzania wa kawaida kwamba madini yametusaidia nini, mtu wa kawaida kule Magu umwuulize kwamba madini yamekusaidia nini katika kupunguza umaskini, katika kujenga misingi imara ya Taifa letu, anaweza kusema kwamba hajui kama kuna madini labda wale waliopo kule Geita waliozungukwa na migodi, hata kunakotoka dhahabu, barabara zimekuwa za shida, Shinyanga ambako Almasi imechimbwa kwa miaka mingi bado kuna vumbi, inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tani 40 za dhahabu ni kama shilingi trilioni 1.3, ukiangalia tunachopata kulingana na kitabu cha hotuba ya Waziri, mwaka 2007/2009, Taifa lilipata shilingi bilioni mia mbili arobaini na tisa. Katika shilingi trilioni 1.3 sisi tulipata shilingi bilioni mia mbili arobaini na tisa, tunachukua sehemu tu ya ile shilingi milioni mia tatu, ile shilingi trilioni moja inaenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, mwaka huu, ni afadhali kwani mwaka 2007/2008 mapato ya Serikali yameongezeka sana. Mwaka 2005/2006 ilikuwa shilingi bilioni 76 peke yake. Nashukuru Waziri na Wizara nzima kwa juhudi mlizofanya angalau tunapata



shilingi bilioni mia mbili arobaini na tisa ambazo zinatoka na *annual rents, royalties*, malipo ya maabara, ada za kijiolojia, ada za kuchambua madini na kodi mbalimbali. Hivi tunaridhika kwamba haya mapato tunayopata yanatosha? Mimi sikubaliani nalo na ninaona kwamba madini haya tumejisahau sana, tumbetwetea. Hata *structure* ya uchumi wetu tunashindwa kuubadilisha kwa kutumia madini, wenzetu Zambia walijisahau, shaba ile ilipo-*boom* hawakuitumia kujenga misingi ya uchumi yao, kuna nchi zinatumia rasilimali walizonazo kama mafuta ku-*transform* uchumi wao lakini sisi hatufanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti mwaka 1997, madini yalikuwa yanachangia asilimia 4.5 kwenye mauzo ya nchi za nje. Kilimo kilikuwa kinachangia asilimia 60, sasa hivi madini yanachangia asilimia 42 kutoka asilimia 4.5 mwaka 1997 mpaka asilimia 42. Kilimo sasa kinachangia asilimia 16 kutoka asilimia 60 maana yake ni kwamba pamoja na bei za mazao, kushuka kwenye masoko ya dunia, pamoja na bei za dhahabu kupanda lakini *structure* hii ya uchumi huwezi kuendelea nayo. Ukiwa na madini yanayokuingizia asilimia 42 ya fedha za nje, inabidi utumie mapato haya kubadilisha mfumo wa uchumi wako. Naomba sana kama nchi, tuamke tusijisahau, kipofu kaona mwezi madini haya yanakwisha na yatakapokwisha wananchi Watanzania, wajukuu wetu, vizazi vijavyo watauliza dhahabu yetu au madini yetu yalikwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitegemea Bunge hili lingejengwa na dhahabu, lakini limejengwa na mkopo! UDOM pia ingejengwa na dhahabu!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii, ili nami nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, lakini kama kawaida, naomba niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Ndassa Malima, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ni Mawaziri Vijana, wanachapa kazi vizuri sana nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina maombi yangu mawili kwa Wizara, kwanza naomba Wizara itumie busara, itatue mgogoro wa *IPTL* na *TANESCO*. Jambo la pili, naomba sana Wizara iendelee kufanya utaratibu wa kuondoa migogoro ya madini kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipendezi, kila siku Waheshimiwa Wabunge kutoka kwenye maeneo husika, wanalalamika lakini na wananchi inafikia mahali mpaka wanaandamana, Serikali yetu ni sikivu, itumie busara lakini pia itumie yale mapendekezo ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, tukifanya hivyo nina hakika tutakuwa tumeisaidia nchi kuondokana na migogoro ambayo inajirudia mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia niungane na Mheshimiwa Limbu hasa kwenye mradi wa umeme Vijijini, nimezungumza na Waziri, nimezungumza pia na Naibu Waziri

mimi na Mheshimiwa Limbu tukapendekeza na ninaomba hili mlichukue kwamba umeme utoke Taro Sekondari uende Ibindo, utoke Ibindo uende Kadashi kuna shule ya sekondari Marigisu, uende Nyashana kuna shule ya sekondari, utoke hapo uende Marigisu baada ya Marigisu uende Kabila, Jimbo la Mheshimiwa Limbu na gharama yake ni ndogo, tunaomba sana suala hili litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la ucheleweshaji wa miradi ya umeme hasa Vijijini. Katika Jimbo langu kulikuwa na mradi wa umeme Malya, umechukua zaidi ya miaka miwili, nashukuru sasa baada ya kupiga kelele mara kwa mara na baada ya kumwalika Mheshimiwa Naibu Waziri Malima na baada ya kuuliza swali humu Bungeni angalau sasa mradi huo unakwenda kwa kasi. Lakini ipo miradi mingi ya namna hiyo nchi nzima, sijui tatizo huwa ni nini lakini naomba sana, *TANESCO* nawaheshimu sana kwa utendaji wake lakini inawezekana tunashindwa kufanya hivyo labda kwa sababu ya kutokuweka kipaumbele, mnaweka vipaumbele vya vitu vingine ambavyo tunaweza kuviita kwamba ni matumizi mabaya ya fedha za *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 *TANESCO* ilikopa pesa kutoka kwenye mabanki yetu zaidi ya shilingi bilioni mia mbili themanini, nashukuru walizitumia vizuri lakini yapo matumizi mengine mabaya ambayo yakitajwa, Waheshimiwa Wabunge mtasikitika. Nyumba moja ilifanyiwa ukarabati kati ya nyumba saba, nyumba Na. 13, ipo Osterbay mtaa wa Toure na Cheza. Ukarakati wake ulitumia zaidi ya shilingi milioni mia sita, matumizi mabaya ya fedha za umma, halafu pesa hizi ni za mkopo, ambazo baadaye Watanzania watumiaji wa umeme watakuja wabebeshwe huo mzigo. Lakini zipo nyumba zingine sita ambazo ni nyumba Na. 89 ipo Guinea Road ukarakati wake ni shilingi milioni mia mbili hamsini, mia nne sitini na tatu, mia moja na arobaini, huo ni ukarakati siyo kujenga nyumba mpya. Ipo nyumba nyingine Na. 65 ipo Laibon Road, ukarakati peke yake tu ni shilingi milioni mia moja na tisini, mia na saba, mia nne na thelethini. Nyumba nyingine ni Na. 459 Mawenzi Road, ukarakati wake ni shilingi milioni mia moja na thelethini. Nyumba Na. 93 Guinea Road, ukarakati shilingi milioni themanini na nane, mia tano kumi na tano, mia nane na ishirini. Nyumba nyingine ni Na. 315 Toure Drive imegharimu shilingi milioni sabini na tisa na nyumba ya sita ni Na. 98 Uganda Line, shilingi milioni sabini na tatu na mia sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi yasemekana Bodi ya Wakurugenzi *TANESCO* haijui, ukarakati peke yake ukijumlisha unapata shilingi bilioni 1.4 pesa ambazo mngeweza kujenga nyumba zaidi ya ishirini. Naomba sana Waziri atuambie je, haya ndiyo matumizi mazuri ya pesa za umma? Mheshimiwa Rais kila siku anasema ni lazima tuwe na matumizi mazuri ya pesa zetu, leo umeme hakuna Vijijini lakini hizi pesa tulizokopa kutoka kwenye Benki zetu hizi, shilingi bilioni 280/- hivi tunazitumiaje? Kwa kujenga nyumba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Makao Makuu ya *TANESCO* zaidi ya wafanyakazi 500 wamerundikana lakini ukienda Mikoani na Wilayani wafanyakazi hakuna. Nguzo ikidondoka leo itachukua siku nne au tano ukiuliza, wafanyakazi hawatoshi. Ninaomba sana, hebu tuwe na utaratibu mzuri wa matumizi ya pesa. Lakini inapotokea namna hii kweli hili ni doa kubwa kwa *TANESCO*, kwa chomba ambacho wewe unakisimamia na baadaye utakaposimama, mimi napenda sana kwa kweli tupate majibu ya Serikali. Kama Bodi ya *TANESCO* matumizi haya ya shilingi 1.4 bilioni haijui, basi lipo tatizo kwenye Bodi ya *TANESCO* na *TANESCO* yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbaya zaidi, katika hiyo nyumba iliyokarakatiwa kwa zaidi ya shilingi milioni 600, yasemekana kwamba nyumba hiyo inafanyiwa utaratibu iuzwe kwa shilingi milioni 60 lakini imekarabatiwa kwa zaidi ya shilingi milioni 600

inatakiwa iuzwe kwa asilimia 10 ya shilingi milioni 60. Huu ni wizi mtupu na ni aibu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali suala hili, bahati nzuri nimetaja na namba ya nyumba kama si kweli waende waangalie. Nyumba zipo na zilikuwa zinakaliwa na Wakurugenzi wa *TANESCO*, waende waziangalie kama ni kweli Serikali iwanyooshee mikono wale ambao hawakufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *speed* ya upelekaji wa umeme Vijijini iwe kubwa, kwa sasa asilimia 12 ya umeme Vijijini kwa kweli haitufikishi mahali popote. Tunataka umeme Vijijini kunako watu wengi lakini umeme ni chachu ya maendeleo, ni maisha bora. Kama hatuna umeme kwenye Vijiji, tutabaki kupiga kelele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije nikagongewa kengele ya pili lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, ninyi ni wachapa kazi wazuri sana, naomba msimamie haya Waheshimiwa Wabunge wanayoyasema. Mheshimiwa Rais amewaamini pamoja na ujana wenu, chapeni kazi ili kusudi muondoe migogoro ambayo kila siku inajitokeza. Nimetaja *IPTL* lakini nimesema migogoro ya wachimbaji wadogo wadogo kwenye maeneo ya madini. Haiwezekani watu wakawa wanalialia tu kwenye nchi yao wanakuwa kama wakimbizi. Naomba sana Waziri haya ayachuke lakini lile la umeme Taro mpaka Kabila, naomba lipewe kipaumbele namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu asubuhi hii ya leo. Nami niungane na Wabunge wenzangu, kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika nchi yetu. Aidha, naomba niwapongeze kwa hotuba nzuri yenye kina ambayo imeandaliwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nianze kuchangia hotuba ya Waziri. Nianze na shukrani. Napenda niipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusambaza umeme Vijijini na nchini kote. Kazi nzuri hii ambayo inaendelea kufanyika na Serikali yetu na sisi wa Wilaya ya Kondo, tumenufaika. Katika miaka ya 1990 mradi unaoitwa Mradi wa Awamu ya Nne (*Electricity Four Project*), ulitekelezwa katika Wilaya ya Kondo na katika kutekeleza mradi huo, umeme ulivutwa kutoka Babati hadi Kondo na kupelekwa hadi Kibaya Kiteto. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba umeme katika Wilaya ya Kondo umefika hata katika Jimbo la Kondo Kusini umeme umeshafikishwa. Kwa hiyo, napenda nishukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwashukuru wapigakura wangu wa Tarafa ya Gioma na Mondo. Kwa nini nawashukuru? Wakati wa utekelezaji wa mradi huo, wananchi wangu walikuwa wastaarabu sana, wenyewe kule hawakudai fidia yoyote kuhusu mali. Maeneo ya mashamba waliyakabidhi bure kwa mategemeo kwamba pindi mradi utakapokamilika basi wao ndiyo watakuwa wanufaika wa kwanza. Lakini pia niwapongeze kwa kuwa walenzi wazuri wa mradi huu. Napenda nikuhakikishie kwamba tangu mradi huu umetekelezwa miaka kumi iliyopita hakuna hata pini moja iliyopotea katika mradi huo na mradi uko kama ulivyo hatuna matatizo. Kwa hiyo, niwapongeze sana wapigakura wangu hao wa Tarafa ya Goima na Mondo kwa uzalendo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba wakati wa utekelezaji wa mradi huo, ni vijiji vichache sana vimepewa umeme, vingi havijapata umeme mpaka leo. Niseme kwamba sehemu kubwa ya mradi uko katika Jimbo la Kondoa Kusini yaani eneo la kutoka Kondoa Mjini – Kibaya hado Kiteto, umeme unapita katika Jimbo langu la Kondoa Kusini lakini nasikitika kusema kwamba tangu miaka 10 iliyopita umeme uko pale haufanyiwi kazi, watu wanauangalia kwa macho. Sasa wananchi wangu wanauliza kwamba huu umeme uliletwa kwa makusudi gani na una faida gani? Nataka Serikali inijibu kwamba ulikuwa na faida ya maonesho au kwa ajili ya matumizi. Nikikutajia hapa Vijiji ambavyo viko karibu na njia ya umeme, utashangaa lakini kwa miaka kumi havijapata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi umeanzishwa kupitia MCC lakini Vijiji vilivyoteuliwa ni viwili/vitatu, lakini Vijiji vilivyopo katika njia ile ya umeme ni zaidi ya 30 na mradi wa umeme wa kupeleka kwenye Vijiji hivyo haifika hata shilingi milioni 30, ni karibu sana. Vingine viko kama kilomita moja kutoka njia ya umeme, kilomita tatu, sana sana kilomita nne, tano ndiyo viko mbali, lakini kila leo tukiomba umeme hatusikilizwi. Hivi mnataka wananchi waandamane ndiyo muanze kuwapa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema wapiga kura wangu ni wazalendo sana, wanalinda miundombinu hiyo mpaka leo miaka 10 wangukuwa siyo wastaarabu kwa kweli wangekwishaanza kuiharibu hiyo miundombinu lakini wamekuwa wastaarabu. Sasa kuwa mstaarabu ndiyo unaendelea kunyanyaswa na kutokuwa na huduma hiyo? Sasa naomba nitumie nafasi hii kusema kwamba wananchi wa Vijiji kama 30 hapa nitavitaja wavisikie, bado wanasota kusubiri umeme. Vijiji hivyo ni Kilemabalai, Sori, Paranga, Cheku, Waida, Pongai, Piho, Dalai, Tandala, Mirambo, Igunga, Ntakuja, Makamaka, Madaha, Churuku, Jinjo, Kinkima, Jangalo, Itolwa, Mlongia, Mapango, Mwailanje, Mwakisabe, Nkulari, Isusumya na Magasa. Hivi Vijiji viko karibu sana. Vijiji hivi ni 26, kwa kweli kama sidhani hata kama itafika shilingi milioni 300 ili kuvifikishia umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi waendee kupata moyo wa kuendelea kulinda miundombinu hii, naomba mnisaidie hivi Vijiji vipate umeme. Mimi nina Vijiji 90 katika Jimbo langu, kwa utaratibu huu wa kutoa Vijiji viwili viwili ama vitatu ina maana kwamba wananchi hawa watasubiri kwa miaka 45 hawajapata umeme. Hivi tunawasaidia nini? Umeme upo pale, siyo suala la kuleta umeme, umeme upo. Jambo hili ni sawa sawa na mtu unampelekea maji kwenye mlango wake halafu unafunga bomba kwamba asinywe maji. Hii mantiki sijaelewa bado, naomba Wizara na Serikali kwa kweli mtupe umeme kwa hivi Vijiji ambavyo vimebahatika kuwa karibu sana na njia ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipokuwa nakuja huku walikuwa wananiambia Mheshimiwa Mbunge ukienda iambie Serikali kwamba tumechoka kuangalia nyaya za umeme zikipitita juu ya vichwa vyetu. Kama hawataki kuteremsha umeme kwenye Vijiji vyetu, waondoe wapeleke sehemu nyingine, labda kuna wengine wanastahili zaidi kuliko sisi. Naomba hiyo aibu tuiondoe kwa sababu hatuna sababu ya kuwanyima umeme hawa watu wakati tumekwisha wafikishia pale. Nasisitiza hili kwa sababu hili ndiyo wanalodai wananchi wa hivi Vijiji nilivyovitaja, kwa hiyo, nafikiri ujumbe umefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 tulitunga Sheria hapa inaitwa Sheria ya Nishati Vijijini (*The Rural Energy Act* ya mwaka 2005). Sheria hii, pamoja na mambo mengine, iliunda vyombo, kwanza ikaunda Wakala wa Nishati Vijiji, pili ikaunda Mfuko wa Nishati Vijiji. Lengo la Wakala ilikuwa ni kufikisha umeme Vijijini, kule ambako Vijiji viko,

mbali sana ama viko ndani kabisa kwa makusudi kabisa kwamba Wakala alitakiwa apeleke huduma hiyo kwa Vijiji vya mbali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna mfuko ule ulikuwa ni kwa ajili ya kukusanya fedha na kutoa ruzuku kwa waendelezaji wa miradi ya miundombinu ya umeme Vijijini. Sasa yapata miaka minne katika Jimbo langu sioni Wakala inafanya nini, sioni mfuko huo unapeleka fedha wapi! Tegemeo letu kwa mfano mimi katika Jimbo langu nilikuwa nimesema kwamba Jimbo langu, nusu ya eneo linapitiwa na Gridi ya Taifa, lakini nusu iko mbali sana na Gridi ya Taifa, nilikuwa nategemea kwamba hawa Wakala ndiyo wataenda kwenye zile Tarafa zilizobaki za Kwamtoro na Farkwa kuangalia vyanzo vingine vya umeme. Nilikwishawaambia chanzo cha umeme, ni bwawa la Farkwa, kwa hiyo, nilikuwa nategemea REA watakwenda kwenye bwawa la Farkwa, wazalishe umeme na kupeleka umeme kwenye Vijiji hivyo vya Tarafa ya Farkwa na Kwamtoro, lakini mpaka leo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natoa wito, Wizara ya Maji na Umwagiliaji wameafiki kwamba sasa Bwawa la Farkwa litajengwa lakini wao wanataka kuchukua maji hayo kwa ajili ya umwagiliaji na pia kuleta maji katika Mji wa Dodoma lakini mradi huu ulivyoasisiwa ni kwamba pia kuna uzalishaji wa umeme. Naomba basi Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iweze kutumia *site* hiyo izalishe umeme kwa ajili ya maeneo haya ambayo nimeyataja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nilikuwa na haya machache ya kuchangia lakini kilio cha wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondo Kusini, wapatiwe umeme hasa vile Vijiji ambavyo nimevitaja, viko karibu na umeme na hawaoni sababu gani waendeleo kusubiri baada ya miaka kumi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Nishati na Madini.

Awali ya yote, napenda niungane na wananchi wa Kata ya Magu Mjini kwa kuondokewa na Mheshimiwa Diwani wao Lazaro Madata na kwamba kwa Chama cha Mapinduzi tumepata pigo kwa sababu alikuwa ni Diwani Mahiri na shujaa mkubwa sana kwa ajili ya kutekelekeza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kukilinda Chama cha Mapinduzi. Naomba familia, ndugu na jamaa tuweze kumwomba marehemu na Mwenyezi Mungu aweze kumlaza mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na wenzangu wote, kwanza kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri. Wizara hii ni Wizara ngumu sana na kihistoria imekuwa ni Wizara iliyojaa changamoto nyingi sana. Kwa sasa hivi ni Wizara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi. Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima, ni vijana ambao ni wachapakazi ambao kwa kweli wanastahili pongezi. Wengi walidhani kwamba Wizara hii labda angepelekwa mtu mwingine mkubwa mkubwa lakini ni vijana ambao wameonyesha kwamba wanaweza kuimudu Wizara hii. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuwapongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Kiti chako kimekuenea vizuri kwa leo, napenda nisema kwamba Wizara hii ina changamoto nyingi sana, hasa ukizingatia kwamba historia ya mfumo wa Wizara hii kidogo na wenyewe unaleta utata mkubwa sana. Ni Nishati na Madini, Nishati na Madini ni pana ndio maana unakuta kuna mambo mengi yanajitokeza.

Sasa hivi ukiangalia baadhi ya nchi ambazo wamekuwa na madini kwa mfano kama Ghana, Afrika Kusini na kwingineko kote kumetokea migogoro ya namna hii inayotokea hapa Tanzania. Migogoro iliyopo sasa hivi katika migodi karibu yote ni changamoto kwa nchi. Lakini kama Serikali lazima ichukue hatua mahususi za kuweza kuikabili migogoro hii. Matarajio ya Watanzania, ni kuona kwamba rasilimali hizi zinawanufaisha Watanzania lakini inapotokea kwamba rasilimali hizi hawanufaika nazo ndiyo chanzo cha migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na Tume mbalimbali na Tume ya mwisho ilikuwa ni Tume ya Jaji Bomani. Imetoka na mapendekezo mazuri sana, lakini mapendekezo mengi bado hatujaanza kuyatekeleza, ndiyo maana unakuta kwamba matatizo yanazidi kuibuka kila kukicha. Ninachoomba Waheshimiwa Mawaziri pamoja na wahusika, hebu jaribuni kuangalia ni kwa namna gani tuanze kukabiliana na changamoto hizi na hasa kutekeleza yale ambayo yameazimiwa katika utekelezaji wake kupitia Tume mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mtanzania wa leo hawezi kuelewa kwa nini Tanzania ni maskini yaani haingii akilini. Sasa hivi tuna migodi mitano mikubwa, tuna madini mbalimbali ambayo hayapatikani sehemu zingine kama Tanzanite lakini Tanzania ndiyo nchi ambayo wanasema ni tegemezi kwa zaidi ya asilimia 34 ya bajeti yake. Hivi ni lini hizi rasilimali zitachangia katika pato la Taifa? Ni lini umaskini wa Mtanzania utapungua? Ni lini Mtanzania atatembea kifua mbele akisema yeye sasa anatoka katika nchi ambayo ina uwezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni changamoto, nilikuwa najaribu kuiangalia na kuisoma hotuba ya Kambi ya Upinzani, kuna baadhi ya vitu ambavyo ni msingi sana. Tujiulize kwa nini wamehoji, kuna maswali ya msingi ya kujiuliza sasa tunaelekea wapi? Leo hii watu wa Tarime, North Mara wamefikia hatua ile, sasa wamekosa uvumilivu. Ukienda kule Buzwagi kuna matatizo, ukienda Bulyanghulu kuna matatizo, ukienda *Geita Gold Mine*, nashangaa, Waheshimiwa Wabunge wanaotokea kwenye Migodi hii nadhani wana matatizo makubwa zaidi. Mimi siamini kwamba sasa hivi Mbunge akiwa anatokea katika mgodi wowote wa dhahabu au mgodi wote, ana furahi hapa alipo, ni kero tupu kwa sababu gani, kwa sababu Serikali bado haijaona namna gani ya kuondokana na matatizo haya. Leo Halmashauri palipo mgodi wanapewa shilingi laki mbili kwa mwaka. Sasa shilingi laki mbili kwa mwaka hata haioani kwamba pale panapotoka dhahabu pafanane na dhahabu. Hivi kweli siku mashimo yakibaki halafu mkasema kwamba nyie watu wa Geita mlikuwa na mgodi wa dhahabu mkubwa sana na mmebaki kama mlivyo itakuwa haiwajasaidia Watanzania. Watu wa North Mara, watu wa Buzwagi, watu wa Kahama, kwa kweli naomba sana katika hili tuliangalie upya. Kama ni matatizo ya sheria zetu hebu tufikie mahali sasa tuachane nazo na tubadili. Kwa sababu inafika mahali rasilimali hizi zinakwisha na zinapokwisha Watanzania tutabaki kama tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha, najua hata Peramiho kuna machimbo madogo madogo, sijui ni kwa kiasi gani wananchi wa Peramiho wananufaika na machimbo hayo. Hili ni tatizo na bila kuwa na mambo ambayo sisi wenyewe tunadhamiria kuyafanya tatizo hili haliwezi kuisha. Tunabaki tunajisifu tuna migodi lakini haina manufaa kwa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nchi imepata mtikisiko wa kiuchumi wa kidunia, tunadhani kwamba kwa sababu bei kama dhahabu imezidi kupanda, ingeweza kusaidia sana kuwa-*stabilize* wakulima na wananchi ambao wameguswa kwa kiasi kikubwa sana na mtikisiko huu. Hizi ni changamoto ambazo kwa kweli Serikali lazima izifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na Nishati na Madini, unajua walipokuwa wameingia watu wa *Net Group Solution* pale *TANESCO*, niliamini kwamba Wazungu

watatusaidia. Lakini walivyoingia akiwa ni ovyo. Baadaye tukapata Watanzania wetu, tukasema *Alhamdulillah*, labda hawa sasa walau wana uchungu wa nchi hii watatusaidia lakini nadhani Shirika la Umeme Tanzania *TANESCO* bado linapitia msukosuko mkubwa sana wa kimfumo na hasa wa kiutendaji. Sina haja ya kuingia kwa ndani lakini napenda nisikitike kwa kusema kwamba hebu naomba Serikali mtusaidia kuitengeneza *TANESCO*. *TANESCO* sasa hivi kuna matatizo makubwa sana, wao wanasema hawana fedha na lazima wapewe fedha kutoka Serikalini, lakini hata fedha wanazopata bado kuna matatizo ya matumizi bora ya fedha hizi. Kwa hiyo, kuna changamoto ambayo kama Serikali naomba kupitia bajeti hii tuangalie namna gani *TANESCO* tunaibadilisha na inafanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nina barua karibu tano kutoka Serikalini, zikisema utekelezaji wa umeme katika Vijiji na baadhi ya miji na hasa katika Jimbo la Busega, tuna kiwanda cha kuchambua pamba pale Ngasamo kimefungwa sasa ni mwaka wa tano hakina umeme na imeshindikana kukiendesha, matokeo yake, wananchi wameshindwa kuongeza thamani na ku-*process* pamba yao. Hii ni tatizo la kiuchumi, kama Serikali tunakosa kuongeza uchumi kwa sababu *ginnery* ya Ngasamo haifanyikazi zaidi ya miaka mitano sasa na tatizo ni umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hospitali moja kubwa sana Mkula, iko chini ya Kanisa la *AIC*, haiwezi kufanya baadhi ya matibabu yake makuu na hasa upasuaji na kadhalika kwa sababu hakuna umeme. Tuna hoteli kama *SpeakBay* haina umeme na tunasema kwamba hebu tukuze uchumi wa nchi hii, tutakuzaji uchumi kwa stahili hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hapa, nampongeza Mheshimiwa Waziri ameanisha miradi yote ambayo itatekelezwa lakini swali langu ni kwamba, ni lini hii miradi itatekelezwa? Kwa sababu huu ni mwaka wa tano narudia kusema kitu cha namna hii, umeme kutoka Lamadi kuja Nyashimo mwaka wa tano wa kilomita 20, imeshindikana. Nimeahidiwa mara nyingi na *TANESCO* kwamba mwaka huu tumeshatenga fedha shilingi milioni 97, tutatekeleza mradi, mpaka leo hakuna kitu. Sasa najjuliza kwamba hii miradi itatekelezwa lini? Ndio swali na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake nipate majibu kwamba ni lini utekelezaji huu utafanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda hata kule Sengerema, kuna *ginnery* ya Buyagu, kuna *ginnery* ya Nyamililo hazina umeme. Kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa umeme, hakuna umeme, sasa hebu tujulize hivi kweli tunakuza uchumi kwa namna gani, hauwezi kujisemea, hebu nikusemee Mheshimiwa Waziri, najua wananchi wako, wa Jimbo la Sengerema wanakukamata wewe Waziri wa Nishati wa Madini, umeme hakuna unafanyakazi gani huko? Lakini si kwamba utajigawia umeme kama wanavyojigawia barabara, hapana! Kwa sababu hizi *ginnery* zipo muda mrefu, tunaziombea umeme kama ilivyo Ngasamo. Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja hizi, naomba aniambie, Nyamililo na Buyagu na Ngasamo, Mkula, tunapata umeme lini? Napenda mwaka ujao urudi humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *ginnery* ya *Alliance* ambayo wenyewe waliamua kujenga *line* baada ya kukubaliwa na *TANESCO* kwa fedha yao, wakakopa fedha benki wakajenga *line* ya umeme ili kuweza kuokoa zao la pamba na kumuokoa mkulima lakini leo wanadai fedha yao hawataki kurejeshewa na *TANESCO*. Jamani sasa haya mambo tutayafanyaje? Hivi mpaka tuseme hapa, tukasirike au tufanye nini jamani, au mnataka tufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, najua ni kazi ngumu lakini ninaomba suala hili utupe majibu hapa kwa sababu leo hii watu hawa wakisema sasa wana-*withdraw*, atakayeumia ni mkulima wa nchi hii. Watu wamekopa fedha, leo mabenki yanawadai, ninaomba Waziri atufahamishe juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tukija suala la *TPDC* Shirika la Mafuta Tanzania, ni shirika la Muungano kwa sababu suala la nishati limeleta utata lakini sote ni Watanzania. Rasilimali zote zilizopo hapa nchini, ni za Watanzania wote. Leo hii Zanzibar inapata shilingi bilioni 4.5 kila mwezi kutoka kwenye bajeti ya Serikali, ina maana madini yanachangia kwenye bajeti hiyo! Kwa hiyo, hata tunaposema kwamba *TPDC* iwe ni kwa ajili ya manufaa ya Watanzania basi iwe ni kwa manufaa ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni na hasa kwa kuwakumbuka pia wapiga kura wa Peramiho na wapiga kura wa Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara wa Nishati na Madini.

Kabla sijafanya hivyo, naomba kwa idhini yako, nitoe salama za rambirambi kwa ndugu, jamaa na marafiki wa wahanga wa ajali ya jana ya gari iliyotokea Korogwe iliyohusisha basi la Mohamed Transport lililotokea Mjini Arusha kwenda Dar es Salaam. Wengi wa wahanga hao waliofariki wanatoka Mkoa wa Arusha na siyo hivyo tu baadhi yao wametoka kwenye Jimbo langu la uchaguzi la Arumeru Magharibi. Naomba niungane na wananchi wangu wa Arumeru Magharibi, kuwaambia wahusika wavute subira katika wakati huu mgumu na Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za marehemu. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji, kwa kazi nzuri wanayofanya na hasa ya kuandaa hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kero za Jimbo langu la Uchaguzi. Katika Jimbo langu la Uchaguzi, Serikali iliahidi kupeleka umeme katika baadhi ya Vijiji vya Arumeru Magharibi hiyo ilikuwa mwaka 1996. Kwa miaka yote hii 14, nilijaribu sana kufuatilia ahadi hii ya Serikali ambayo ilitolewa kwa maandishi. Kila wakati, kila mwaka, kila Waziri aliyepitia Wizara ya Nishati, akiwepo Daniel Yona, akiwepo Msabaha na sasa Mheshimiwa Ngeleja, wote katika ziara zao kwa nyakati tofauti katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi, wametoa ahadi kwamba watatupa umeme. Ahadi ya mwisho ilitoka kwa Mheshimiwa Waziri William Ngeleja mwaka jana alipotembelea Jimbo langu la Uchaguzi na akakutana na Madiwani na wananchi kwenye Kata mbalimbali na akaahidi kwamba Vijiji vya Oldonyosambu, Mbuyuni, Mirongoine, Likamba na Sambashaelikinang'a, watapewa huduma hii ya umeme. Ninapenda leo Mheshimiwa Waziri, anapotoa majumuisho ya bajeti ya Wizara yake, anijibu kwamba hawa wananchi wa Arumeru ambao wamengoja kwa miaka hii 15 licha ya ahadi mbalimbali, licha ya maandishi kutoka kwa Naibu Waziri ambaye ndiyo Waziri mwenzake kwamba tutapata umeme, anieleze kwamba nitakwenda kuwaambia nini wananchi hawa kuhusu kero hii ya uhaba wa umeme.



Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo juu ya wachimbaji wadogo katika nchi yetu na hususan katika machimbo yetu ya Mererani ambayo yako katika Mkoa wa Manyara lakini watu wengi katika machimbo haya wanatoka katika Wilaya ya Arumeru, Monduli na Mkoa wa Arusha kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji hawa wadogo wadogo, wana hali ngumu sana. Kwa sasa hivi, wengi wao wanafanya kazi katika hali ngumu sana katika machimbo haya ya Mererani ambayo nina hakika nayo. Hawana zana za kisasa, hawana teknolojia ya kisasa ya kuchimba madini na zaidi ya kufanya kazi katika hali ngumu, miundombinu ya machimbo hayo ni duni sana kiasi ambacho inahatarisha maisha yao kila wakati majanga yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa kwamba Serikali kwa mara nyingi imeahidi kwamba utawaangalia hawa wachimbaji wadogo lakini sidhani Serikali imeshawahi kutazama suala hili kwa mapana yake. Hawa ndugu zetu wanachangia kwenye pato la Taifa, wanachangia kwenye maendeleo ya nchi yetu na kwa kweli wanastahili wawezeshwe, wawe na zana bora za kuchimba haya madini. Wawezeshwe wawe na teknolojia sahihi ya kutambua haya madini, wawezeshwe wapate soko na njia ya kupata soko lazima tuwe na kiwanda cha kuchoronga madini haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itamke leo kwamba inawasaidiaje hawa wachimbaji wadogo siyo Mererani tu bali katika nchi yetu ya Tanzania kwa sababu wanaonekana kwamba ni watu ambao wamenyanyasika sana. Naomba Serikali iwawezeshe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya gharama za juu za kuunganisha umeme Vijijini. Pamoja na jitihada za Serikali, pamoja na jitihada za shirika letu la umeme TANESCO kuongeza idadi ya wateja wanaotumia umeme, wameongezeka kutoka 30,000 mpaka 56,000 hii ni dalili nzuri. Lakini naomba niseme kwamba idadi hii ingeweza kuongezeka zaidi kama gharama ya uunganishaji wa umeme majumbani ingepunguzwa. Najua kabisa kwamba hali ya TANESCO siyo nzuri, najua kabisa kwamba labda ninachosema hakiwezekani kutekelezwa kwa sababu ya hali ya uchumi lakini ninachotaka kushauri hapa ni Serikali iangalie jinsi gani wanaweza kuruhusu gharama hizi za kuunganisha umeme zilipwe kwa mikupuo miwili au mitatu. Gharama hii ya kuunganisha umeme ifanywe kwa *phases*. Mteja aweze kupatiwa umeme akilipa *deposit* ya kiasi fulani na kiasi kile kingine kiende mbele na iwe inakuwa *recovered* kutoka kwenye matumizi yake ya *bill* za kila mwezi kulingana na matumizi. Nafikiri tukifanya hivyo, watu wengi Vijijini watapata umeme. TANESCO nayo itaweza kuwa na wadau wengi ama wateja wengi katika matumizi ya umeme. Vinginevyo tunaweza kufika mahali tukazalisha umeme nchini, umeme ukawa labda unatosha lakini wananchi wa Vijiji, wa hali ya chini, wakashindwa kutumia umeme huu kutokana na gharama za juu za kuunganisha umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya uzalishaji wa umeme nchini. Natambua kabisa jitihada za Serikali za kuzalisha umeme nchini. Naona kuna nyongeza ya uzalishaji wa umeme katika nchi yetu. Hilo napongeza Serikali. Lakini mimi nafikiri kwamba wakati umefika tusiogope gharama, twende kwenye miradi ile ya kuzalisha umeme ambayo ina *impact* kubwa katika Taifa letu bila kujali gharama. Mradi wa *Stigler's George* imeandikwa hapa, Waziri ametuambia kwamba hii ingekamilika, ingetumalizia shida zetu zote za umeme na tukawa na umeme wa ziada ambao tunaweza kuuza nchi za nje. Mimi nasema wakati umefika sasa Serikali iipe *Stigler's George* kipaumbele kinachostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wazo la kushirikisha sekta binafsi katika jambo hili, katika dhana nzima ya *Private Public Partnership*. Ninaomba Serikali ilichukulie jambo hili kwa uzito wake, kwa makini na kama itabidi tuhusishe sekta binafsi ili tusaidiane, tuondokane na shida hii ya umeme ya kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie kwa kifupi *capacity charge*, naipongeze Serikali kwa kuwa imetuambia hapa kwamba wamezungumza na wazalishaji wa umeme wa *Songas* na wamekubali kupunguza *capacity charge* ambayo inatuingizia dola milioni moja kwa mwezi. Hii ni dola milioni 12 kwa mwaka. Naomba niishauri Serikali iendele na jitihadi hizi kwa wale wazalishaji wengine wa umeme katika nchi yetu ili tuweze kuwa na kipato katika uzalishaji huu wa umeme ambao ulikuwa unaenda kama *capacity charge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizingumzie suala zima la msamaha wa kodi kwa wawekezaji wa sekta ya madini, inayotokana na matumizi ya mafuta mengi, litizamwe na Wizara hii; ushauri wa Tume ya Mheshimiwa Jaji Bomani uchukuliwe *seriously*. Kwenye taarifa ya Tume hiyo, ilisema tutizame kwa upya mikataba ya hawa wawekezaji, haikusema tutizame *future contract*, mikataba ambayo sasa hivi ipo *operational*, tuitizame na tuierekebishe kwa maslahi ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizingumzie juu ya usambazaji wa nishati Vijijini kwa kutumia ama kwa huduma za *REA*. Tumeanzisha *REA* na tumeanzisha mfuko ambao unaendana na *agency* hii, lakini, nashindwa kuelewa, Sheria ni nzuri lakini bado mimi nina utata kidogo maana nashindwa kuelewa, hawa ndugu zetu *REA* wana fedha kiasi gani? Wana uwezo gani kifedha wa kutimiza haya majukumu mazito ya umeme? Wasaidiwe ili waweze kutimiza jukumu hili la kusambaza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na bila kuchelewa naunga mkono hoja hii ambayo imewasilishwa vizuri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuzingatia sana Ilani ya CCM katika uwasilishaji wake. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kama walivyosema baadhi ya wenzangu walionitangulia, inaongozwa na Mawaziri vijana lakini wametuonesha kwamba wanaimudu kazi yao vizuri sana na nawapa hongera sana. Mimi kama miongoni mwa wazee katika Bunge hili, niliyezekea humu ndani tangu nina umri wa miaka 26 na leo nina miaka 66, nina kila sababu ya kujivunia vijana hawa hasa kwa vile Mheshimiwa Waziri ni mjukuu wangu, Mheshimiwa Naibu Waziri ni mjomba wangu, mtoto wa dada yangu, mjukuu wa Mhehe maarufu hayati Chelestino Mwafivao. Namwita Mhehe maarufu kwa sababu alikuwa mkulima hodari kule Isimani na akawa miongoni mwa Wahehe wa kwanza kununua pikipiki, kununua gari, akaona bado ana hela nyingi akaenda mpaka kwa Bwana DC kuulizia uwezekano wa kununua ndege. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo tuliopewa katika Bunge hili kwa hotuba ya Waziri, napenda nipongeze sana mkakati wa mchanganyiko wa vyanzo vya umeme, yaani *Multiple Sources of Energy* ambayo unajitokeza. Katika miaka mingi iliyopita, tulizingatia sana umeme wa nguvu ya maji na tulishauriwa na Benki ya Dunia kwamba umeme wa *Hydro* ndiyo rahisi, ndiyo unafaa kwa nchi kama zetu lakini tukaja kupata matatizo makubwa sana lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri imezingatia vyanzo tofauti sita, ukichukua maji

yaani kwa maana ya *hydro*, gesi asilia, upepo, mkaa wa mawe, mabaki ya mimea na jua vyanzo vyote sita vinajitokeza vizuri. Mimi napongeza kwamba huu ni mkakati sahihi, tusitegemee chanzo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze Serikali kwa kuanza kutekeleza miradi ya *Millennium Challenge Corporation* inayopeleka umeme Vijijini. Napongeza sana kwa sababu umeme Vijijini, ni sera muhimu ya Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, utekelezaji wa *MCC* ni jambo zuri na inaonesha kwamba baada ya kuingia Serikalini, Serikali ya CCM inaendelea kwa bidii sana kutekeleza kile ilichowaahidi wananchi wakati tulipoomba kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo tuliyopewa katika vikao, ndani ya Wilaya yangu ya Mufindi na Jimbo langu la Uchaguzi, kuna maeneo mawili ambayo yanajitokeza kwamba yatapata huduma hii ya umeme Vijijini. Katika eneo la kwanza katika Jimbo langu la Uchaguzi, vimo Vijiji vya Kinanyambo, Lungemba kuelekea kijiji cha Ulete hadi kuunganisha na Ifunda na kwa kufanya hivyo itakuwa moja kwa moja *substation* ya Mgololo imeunganika na *substation* ya pale Iringa na *stability* ya utoaji wa umeme itaimarika zaidi. Naomba katika kutekeleza katika eneo hili, isisahaulike kufikisha umeme katika Chuo cha Maendeleo ya Wanawake cha Lungemba pia sekondari ya Mnyigumba, pia kijiji cha Kitelewasi na shule zote za msingi zilizo katika Vijiji hivyo. Pia kuna wazalishaji muhimu ambao wanatoa huduma za kiuchumi, kwa mfano ile hoteli ya kitalii ya *Old Farm House* na kuna shamba kubwa linalozalisha sana ng'ombe bora pale na yule mwekezaji bwana *Tailor* aliyehamia kwetu kutoka Kenya amekuwa akiomba umeme kwa muda mrefu, naomba katika kusambaza umeme, eneo hili wasisahauliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni ule umeme unaochukuliwa kutoka Makambaku kuelekea Malangali ambao utafika pia katika shule ya sekondari Malangali, ni sekondari ya kwanza kujenga katika Nyanda za Juu, lakini miaka yote hii wamekuwa wakitegemea umeme wa *generator*. Kwa hiyo, napongeza sana kuona katika *MCC* imewekwa kupeleka umeme kutoka Makambaku kupitia Vijiji vya Mbalamaziwa. Nashauri Vijiji vyote vya njiani visirikwe, vione nyaya za umeme zinapita na pia izingatiwe asasi muhimu zilizo katika eneo hilo; kwa mfano sekondari ya Itandula, sekondari ya Mbalamaziwa, sekondari ya Nyanyembe, sekondari ya Itengule na kule Malangali kisisahaulike kituo cha afya na shule za msingi na pia Parokia za Itengule na Isimikinyi na Vijiji ambavyo asasi hizo zimo, kwa mfano kijiji cha pale Itengule mpaka kijiji cha Ihuwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ukifika katika shule za msingi, ni moja kwa moja utafika katika nyumba za Walimu na umeme katika nyumba za Walimu, ni faida ya kuimarisha elimu wanayopewa watoto wetu kwa sababu Walimu watajiandaa vizuri zaidi. Umeme ukifika katika zahanati na vituo vya afya, ni kuimarisha pia huduma ya tiba kwa jamii, kwa hiyo, nashauri sana kila umeme unapofika katika Vijiji, maeneo hayo yapewe uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Awamu ya Nne kwa ujumla, kwa kutoa msukumo mkubwa kwa miradi midogo ya umeme inayoendeshwa na sekta ya binafsi kwa mfano *mine-hydro* na hasa kwa kuchukua hatua ya kuwa na mkataba tayari. Huu utaratibu wa kuwa na *Standard Power Purchase Agreement*, ni jambo zuri sana, lakini ninapenda kutoa angalizo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba upo urasimu unaokwamisha juhudi hiyo na namwomba Mheshimiwa Waziri azingatie mambo matatu na asaidie kuyakwamua. (*Makofi*)

Kwanza, kuna ucheleweshaji wa kutoa barua za *TANESCO* yaani *Letter of Intent* ambayo barua hii ikitolewa na *TANESCO* ndiyo wawekezaji wananweza kwenda kukamilisha taratibu zao za kupata fedha.

Pili, bei, sasa hivi wawekezaji wanasema ile bei shilingi 100 iliyowekwa kwa mwaka wa kwanza haitoshi, wanasema inatakiwa iwe senti 10 za dola yaani kama shilingi, iwe kiasi cha kama shilingi 120 kuelekea kwenye shilingi 130. Tukibaki tumeng'ania katika shilingi 100 miradi inakwama kutekelezwa.

Tatu, kuna kukwama kutolewa idhini ya mazingira kutoka kwenye Baraza la Taifa la Mazingira. Naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, msaidie kukwamua vikwazo hivyo ambavyo vinatucheleweshwa katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ndani ya Wilaya yetu ya Mufindi, kuna miradi mitatu ambayo ninaiombea msaada wa Waziri ili iweze kusonga mbele kwa haraka. Mradi wa kwanza ni *Minihydro* wa Mto Mwenga ambao Waziri ameueleza, unaweza kuzalisha mpaka *megawatt* tatu, unaendeshwa na kampuni ya *Mufindi Tea Company (MTC)* ikishirikiana na *TRIT* na itafikisha pamoja na vile Vijiji 14 ambavyo vitafaidika na umeme huo, kwa hiyo, naomba sana, Mheshimiwa Waziri usaidie kukwamua mradi huo katika maeneo ambayo wanaonekana wamekwama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili, ni mradi wa umeme unaotokana na mabaki ya mbao ambao nao ameuelezea katika hotuba yake, ule wa *SAO HILL*, utakaoendeshwa na *SAO HILL Energy Limited* wa *megawatt* 15, hizi ni *megawatt* nyingi lakini umekwama kwa mambo mawili, barua hiyo ya *TANESCO* na suala hili la kuwa na bei sahihi inayokisiwa kuwa isiwe chini ya senti 10 ya dola ya Marekani. Mradi huu unasafisha mazingira, kwa hiyo, tunategemea Baraza la Taifa la Mazingira halitacheleweshwa kutoa kibali lakini mpaka sasa kibali chao kinasubiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa tatu, ni mradi wa *Mini-hydro* ya Igomaa ambapo ni wa *megawatt* 3 - 6; Igomaa au wengine wanaoita *Maluluma* ingawa neno *Maluluma* ni la Kihehe maana yake maporomoko sasa watu walipouliza wale wanaoandika wapi hapo, wakasema *Maluluma* wakaita mradi wa *Maluluma* lakini uko katika kijiji cha Igomaa unaendeshwa na kampuni ya *Fox Track Limited* wao wanasubiri *design* ya bwawa litakalojengwa katika mto Ndembela kule *up stream* ili waweze kurekebisha michoro yao na *size* ya *megawatt* hizo iwe tatu kuelekea sita maana bwawa *design* ikitoa maji mengi zaidi na wenyewe wataongeza *megawatt* zitakazozalishwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atusaidie miradi hii *i-take off* kwa sababu jumla yake ni zaidi ya *megawatt* 20 na sehemu kubwa za *megawatt* hizo pamoja na kutoa umeme katika Vijiji vyetu zitaingia katika *Gridi* ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchukua nafasi hii, kushauri *TANESCO* ianzishe utaratibu wa kusafirisha umeme wa wazalishaji hawa wengine kwa malipo nafuu badala ya kuuzia *TANESCO*, lakini utumike utaratibu wa *TANESCO* kulipwa *charge* ya kuusafirisha mwisho unapofika upande wa pili wauze wao wenyewe. Katika nchi nyingine, utaratibu wa namna hii unatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuhusu umeme kwa ajili ya kijiji cha Ifwagi, niliongozana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Mheshimiwa Diwani Naused Nyaganilwa, tukafika ofisini kwa Mheshimiwa

Waziri, nakushukuru sana ulitupokea vizuri na ukatuhidi kwamba utawaagiza *REA* watekeleze mradi huu wa umeme mwaka huu na kwa idhini yako uliyotupa tumeshawatangazia wananchi kule, wengine wamekwishafunga hata nyaya katika nyumba zao. Kwa hiyo, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu ahadi hiyo na napenda niseme ahsante, ulitupokea vizuri, tuna matumaini makubwa sana, *mwaweja*, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mungai ingawa lugha uliyotumia ya mwisho sio lugha ya Bunge lakini imeeleweka kwa wananchi na hasa Waziri mwenyewe.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utanisamehe naongelea chombo cha Mheshimiwa Mwambalaswa, cha kwangu nafikiri kimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja na Naibu wake, Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yao ambayo Mheshimiwa Waziri aliwasilisha juzi kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Kyela, naomba vile vile nipongeze uongozi wa Wizara kwa kuanza utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka umeme wa gridi kwenye fukwe za kitalii za Matema na vile vile hospitali ya Matema na hivyo kuchochea maendeleo kwenye Vijiji kadhaa ambamo umeme utapita, Vijiji vya Ngamanga, Bwato, Mpunguti, Mpegele, Kateela, Mababu na Kisiyosyo na vile vile kuzihudumia sekondari nyingi tulizojenga za Makwale, Matema *Beach Secondary School* pamoja na *Laeshore*, kwa hiyo naishukuru sana Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimeombwa na wafanyakazi wa *Kiwira Coal Mine*, kupitia kwako, nimweleze Mheshimiwa Waziri kwamba uamuzi wa Serikali wa kuurudisha mgodi wa *Kiwira Serikalini*, ni uamuzi muafaka. Wanasema wao walikuwa wamedai hivyo kwa muda mrefu lakini wanamkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba asisahau hawajalipwa mishahara kwa zaidi ya miezi kumi na mbili, jambo ambalo ni ukiukwaji wa haki za binadamu na unakiuka hata Katiba ya nchi ambayo inalinda haki ya kupata malipo au ujira stahili kwa kazi ambayo mtu anafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri imeongelea mambo mengi sana. Mimi naomba nigusie mambo manne tu kufuatana na muda tulionao. Kwanza, nianze na habari njema ambayo anaelezea ukurasa wa 48 wa hotuba yake kwamba tumegundua mashapo ya madini ya *uranium* na pengine Tanzania tutaanza kuzalisha *uranium* katika miaka miwili ijayo. Hizi ni habari njema sana na zinaleta matumaini kwa nchi yetu kufaidika kutokana na madini hayo. Lakini natoa angalizo, ikiwa sisi viongozi na watendaji hatutaweka maslahi ya Taifa mbele, tukiendekeza ubinafsi, tukiendekeza umimi, basi tutazalisha ma-Richmond, ma-EPA, ma-Radar mengine na kupoteza muda mwingi sana na fedha za umma tukisafishana kama tunavyofanya sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama uadilifu wetu sisi viongozi tuliopo sasa una mgogoro, heri tuyaache hayo madini chini ya ardhi watachimba kizazi kijacho. Mwalimu alifanya hivyo, aliacha madini yote hapa chini lakini leo inawafaidia zaidi wageni kuliko sisi Watanzania, bado sisi tuna viraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu Baba wa Taifa na Sheikh Karume, walikuwa hawataki hata kuchimba mafuta, wakasema tuchimbe sisi, ona leo kunatokea nini? Uroho umetutawala, tumeanza kutoana macho hata kabla ya utafiti kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye hotuba yake kuhusu maandalizi ya Sheria mpya itakayozingatia uchimbaji na usafirishaji wa madini ya mionzi. Hii ni hatua nzuri sana, nakupongeza Mheshimiwa Waziri lakini naomba nitoe angalizo pia. Sisi si nchi pekee iliyogundua *uranium* katika Afrika. Ukienda kwenye *internet*, unagundua kuwa nchi 18 za Afrika zina *uranium*. Kwa hiyo, tuna sehemu kubwa ya kujifunza kuhusu makosa yao ya uwekezaji, pale walipofanya vizuri, sisi tutaiga. Hata majirani zetu wengi wamepata *uranium*, Uganda, DRC Kongo, Malawi na Zambia, wana madini hayo, kwa hiyo, tutajifunza kutoka kwao. *In fact* Malawi wameshaanza mgodi wa *uranium* sehemu inayoitwa Kayelekela, iko Kaskazini, sehemu za Karonga, ni umbali kama kilomita 30 kutoka Kyela, wenzetu wameshaanza kuchimba *uranium*. Mkataba walioingia na kampuni ya Australia inayoitwa PALADIN, ni mkataba mzuri sana. Kwanza Serikali ya Malawi ina asilimia 15 ya hisa katika mgodi huo, mrabaha asilimia 25 na vile vile kwa sababu uchimbaji wa madini haya unaonekana unaweza kuhatarisha mazingira, wameingia mkataba maalum na hiyo kampuni. Kampuni hiyo lazima na imeshafungua sasa akaunti katika benki mojawapo Malawi na kwa kukubaliana na Serikali wawekeze fedha inayoweza kutosha kuhuisha mazingira. Sasa huko ndiyo ku-*negotiate* miKataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachosema tu, changamoto yetu kubwa ni kufikia viwango hivyo vya Malawi na hata kupita. Kwa upande wetu, hakuna sheria inayowabana wawekezaji kiasi hicho katika kuhuisha mazingira, hatuna na nikumbushe tu kwamba hilo tulilionna kwenye Kamati ya Rais ya Madini iliyoongozwa na Jaji Mark Bomani. Lakini mapendekezo ya Kamati hii kuhusu uhuishaji wa mazingira pamoja na mapendekezo mengine bado hayajatekelezwa. Huu ni ugonjwa wa kawaida Tanzania wa kutokutekeleza vitu haraka lakini hali tuliyonayo kuhusu uhuishaji mazingira, unatishia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja mdogo. Tumepata taarifa kupitia vyombo vya habari kwamba mgodi wa Barrick wa Tulawaka unafungwa. Waheshimiwa wameshakomba kila kitu pale, dhahabu yote imeshakwenda, kwa hiyo, wanafunga. Sasa mimi nataka kumuuliza Waziri, je, fedha ya kuhuisha mazingira ipo? Kama ipo, ipo iko wapi? Kama utatuambia iko wapi na ni kiasi gani, na nasema hayo na nahitaji majibu kwa sababu tumechoka Watanzania kuachiwa mashimo. Mheshimiwa Limbu amesema hapa leo, hatutaki kuachiwa mashimo ili tuzibe sisi wenyewe kwa pesa zetu sisi maskini na mashimo yaliyojaa sumu hii ya zibaki ya kuwaumiza watu wetu. Kwa hiyo, tunataka tupate uhakika huo kama wenzetu wa Malawi walivyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa za ndugu zetu kijiji cha Nyamongo, Wilayani Tarime za kuathirika sana na mifugo yao kuangamia kutokana na kemikali zinazotiririka kutoka mgodi wa Barrick wa North Mara. Taarifa hizi zinasikitisha. Pamoja na mapenzi makubwa tuliyonayo kwa wawekezaji, *this time* lazima tu-*act*, lazima tuchukue hatua dhidi ya mgodi wa North Mara. Naelewa kampuni ya Barrick ni kampuni kubwa ya dhahabu kupita zote duniani, ina nguvu kubwa, inaweza ikaamua kukutesa ukapata tabu lakini nchi hii ni yetu, tutaongea kwa ujasiri tu. Hii kampuni ina rekodi mbovu duniani kote kwa kuharibu mazingira, imefikia hatua Serikali ya Norway kuiondoa au kuizuia kampuni yake ya pensheni, sio kampuni ila taasisi ya pensheni ya Serikali, isiwekeze Barrick kwa ajili ya uchafuzi wa mazingira duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba na napendekeza tufunge mgodi wa North Mara mara moja. Tusisuesue mpaka watu wetu wafe kwa mamia. Kipindi tutakachofunga, wafanye mambo makubwa mawili, la kwanza warekebishe mfumo wao wa kuhudumia taka za sumu, huo mfumo wao una matatizo! Mara ooh, wananchi wanaiba *carpet*, wanaiba wao wenyewe wanakuwa wapi maana wamejaza Maaskari wengi pale! (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tuhakikishe tunatumia kipindi hiki, kuhakikisha kuwa tunaweka mipaka ya kutosha *bufferzone*, kati ya mgodi na makazi ya wananchi, suala hili lilishapendekezwa na Kamati ya Jaji Bomani lakini kama nilivyosema, tunarudi pale pale kwenye ugonjwa wetu wa utekelezaji wa maamuzi kwa kususua. Tena hayo maamuzi ya Kamati ya Jaji Bomani yalitiliwa mkazo na Azimio la Bunge hapa. Hatua hizo hizo napendekeza, zichukuliwe dhidi ya Geita *Gold Mine*, ambayo imekuwa ikitiririsha kemikali za sumu kwa wananchi kijiji cha Nyakabale, kwa muda mrefu. Kamati ya Bomani ilijionea yenyewe tatizo hilo. Wananchi wamedhoofika kiafya, mifugo yao inatisha. Marehemu Mheshimiwa Rwilomba, Mungu aweke roho yake pema peponi, amelalamika muda mrefu kweli kuhusu *GGM*, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Hata baada ya kuchukua hatua hizo, tusiishie hapo, Wabunge wanaohusika katika hayo maeneo, nawaomba wawahamasishe wananchi wao, Wanasheria na *Legal Aid*, pamoja na wanaharakati, wawasaidie wananchi wapeleke kesi Mahakamani kuishtaki Barrick kuweza kupata fidia, hakuna atakayewasaidia kwa kupigapiga kelele tu na kusimama kwenye majukwaa, waishtaki Barrick. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kitu kimoja tu maana muda ni mfupi. Tumeamua kufuta Tangazo la Serikali, Na. 99 la mwaka 2005 ili kuondoa msamaha wa ushuru wa mafuta ya petroli kwa kampuni za madini. Lakini msamaha huo si kwa kampuni zote za madini, ni kwa kampuni zile tu ambazo zitaingia mkataba na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2009 na Serikali imesema itajadiliana na kampuni ambazo zimesajiliwa siku za nyuma au zimeingia mkataba na Serikali siku za nyuma ili kipengele cha msamaha kwenye miKataba yao kiondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa uelewa wangu, msamaha huu wa kodi ya mafuta ya petroli hauko kwenye miKataba hiyo, ulikuwa kwenye hilo Tangazo la Serikali Na. 99 la mwaka 2005. Sasa kujadiliana na kampuni hizo kunatoka wapi? Mimi naomba Mheshimiwa Waziri, hakuna cha kujadiliana hapa, tunataka kusikia kauli ya Serikali kuwa msamaha huu umeondolewa kwa kampuni zote. Tena ninapenda kusikia kwa nini tunaingia miKataba hii wakati hatuifuati. Kila mkataba wa madini, unakifungu cha *force majeure* yaani nguvu kubwa kupindukia ambayo haikutarajiwa. Kipengele hiki kinatumika pale ambapo majanga yanatokea, mvua kubwa gharika, volcano, tetemeko, hata huo msukosuko wa uchumi wa duniani ni moja ya aina ya *force Majeure* na *parties* wale wenye mkataba wanaruhusiwa kutumia kifungu hicho ku-*suspend* au kutokutekeleza sehemu fulani fulani za miKataba. Nafikiri ndiyo muda wetu Watanzania kufanya hivyo sasa kuwaaambia wenzetu jamani eeh, tuliwapa nafuu wakati wa neema sasa maisha ni magumu tuna-*invoke force majeure*, hatuwapi msamaha wowote ule. Sasa kama hatutumii vifungu hivyo, tunaviweka vya nini kwenye miKataba? Kwa nini tunaogopa wawekezaji kama wakwe? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la uagizaji wa mafuta, kwa dakika chache zilizobaki, uagizaji wa pamoja yaani *bulk procurement*. Naungana na wasemaji waliotangulia, kumtia moyo Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, waendeleo kwa kasi moja na utekelezaji huo. Utekelezaji huu, una tija kwa Taifa. Leo hii mafuta ya *diesel* Kenya, ni bei

nafuu kushinda Tanzania! Kwa nini? Ni kwa ajili ya *bulk procurement* ununuzi wa mafuta au kuingiza kwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa Zambia mafuta yao yote yanapitia bandari ya Dar es Salaam na ni mafuta ghafi, yanaingizwa kwenye kwenye bomba la mafuta, linasukuma mafuta kwa gharama kubwa mpaka Ndola, yakifika Ndola, yanapelekwa kwenye kiwanda kusafisha yanauzwa. Bei ya mafuta Zambia na Tanzania haitofautiani sana, kwa nini tuna matatizo haya? Matatizo yetu ni kwamba tumeruhusu kila mtu kuagiza. Wenzetu bei zimeenda chini kwa ajili ya *bulk procurement*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni tatizo la uchanganyaji dizeli. Naona muda umeisha, nitagongewa sasa hivi, uchanganyaji na mafuta ya taa. Kwa hili nawalaumu sana *EWURA*, kila mtu anajua hata Viongozi na wafanyakazi wa *EWURA* wanaelewa kwamba wachanganyaji wakubwa wa mafuta wako kati ya Kibaha na Mdaula. Wanajua hata simu zao. Kinachowashinda kuwadhibiti hawa ni nini, kama mmeshindwa kazi kwa nini msiwapishe wengine? Tunahangaika hapa, tunatumia fedha za kigeni kuagiza magari, magari haya yana-*knock* kila siku kwa ajili ya uchanganyaji wa mafuta. Yote ni kwa sababu tumeshusha kodi ya mafuta ya taa kuwa shilingi 52 kwa lita na tulifanya hivyo kwa madhumuni ya kumsaidia Mtanzania wa kawaida, lakini hawa wenzetu, mafisadi kwenye hii sekta ya mafuta wanatumia mafuta ya taa kuchanganya na dizeli ili wa- *maximise profit*. *EWURA* tunawapa muda, nafikiri mimi nawapa miezi mitatu Mheshimiwa Mwenyekiti nitakuja mimi hapa na *motion* binafsi kuhusu *EWURA* kama hawawezi kazi, wakae pembeni. Hatuwezi kuwa tunapigapiga kelele huku mnajua kabisa fulani, fulani na fulani wanachanganya mafuta. Kama ni mshiko unawasumbua, sasa wafumbe macho wahakikishe kwamba hili tatizo halipo tena Tanzania. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiri kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Lakini sijui kama mkwe anaogopwa ama anaheshimiwa, sasa hapo ni shughuli kweli.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikia Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Felix Mrema na kama nilivyosema Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella atakuwa mchangiaji atakayefuata baada ya Mheshimiwa Felix Mrema.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwanza kwa kupeleka rambirambi zangu na pole zangu kwa familia ya wale abiria zaidi ya 35 waliopoteza maisha kule Korogwe. Wote hawa walianzia safari yao kutoka kwenye Jimbo langu la Arusha mpaka hapo walipopata ajali hiyo. Mimi binafsi na wananchi wa Jimbo langu la Arusha, tunapeleka rambirambi zetu na pole zetu kwa familia za hawa wote waliofiwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa Jumamosi. Nimtoe wasiwasi, naunga mkono hoja. Katika Wizara ambazo ni ngumu kuzisimamia na kuziendesha, ni hii ya Nishati na Madini. Hayo yanayoendelea ndani ya Wizara hii na Taasisi zake, yanahitaji uchambuzi wa kina na wepesi wa kuelewa mambo, michezo gani inayofanywa na namna gani ya kuthibiti hiyo michezo ambayo inaweza



kuendelea katika Wizara hii. Lakini kubwa zaidi inahitaji uongozi ndani ya Wizara na kwenye Taasisi wenye uzalendo usio na mashaka. Niseme sina wasiwasi na wewe Mheshimiwa Waziri, sina wasi wasi na Naibu wako, ninyi ni vijana, mmeonyesha umahiri wa hali ya juu wa kuchambua mambo na kuelewa mambo na katika kipindi hiki kifupi hata uzalendo wenu, mmezidi kudhihirisha kwamba hauna mashaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mnachohitaji, ni ushirikiano wetu sisi sote, ili muweze kufanya kazi yenu kwa uzuri zaidi. Sekta zote mbili, hii ya Nishati pamoja na Madini, zina mvuto mkubwa kabisa ya wawashiriki wa kimataifa na mitandao ya kimataifa. Hilo kila mmoja anaelewa na baadhi ya hawa wanaopenda kuja kushiriki katika sekta hii wana mtazamo wa kuja hapa kama wamekuja kwenye Shamba la Bibi na mnawaelewa wanaokwenda kwenye Shamba la Bibi, hawana uchungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto yetu kubwa ya Wizara hii na sisi sote ambao tunawatakieni nyinyi kazi nzuri, ni kutambua nani katika hawa wanaokuja, wamekuja kwa mtazamo huo wa kuja kwenye Shamba la Bibi na tumdhibiti kwa namna gani, sasa wenzangu wamekwishakueleza vizuri sana maeneo ambayo yanahitaji udhibiti wa hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niendeleo kusisitiza tu juu ya vito. Wabunge wenzangu wamesema tuchukue hatua za makusudi kabisa kuibakiza mikononi mwa Watanzania. *STAMICO* wapewe kazi ya kuisimamia kazi hiyo. Wachimbaji wadogo na mimi pale Arusha ni shahidi, kama tukifanya tathmini ya wale ambao wamewekeza kutokana na utajiri na uvunaji wao kwenye hayo machimbo chini ya ardhi yetu, kama tukifanya tathmini ya uwekezaji wao, tutaona kwamba hawa wachimbaji wadogo wamewekeza kiasi kikubwa zaidi katika maeneo yetu hasa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara kuliko huyo mmoja ambaye Serikali imechukua mrahaba na kodi kutoka kwake. Ukilinganisha hayo mawili ni vitu tofauti kabisa, tukifanya tathmini ya kina. Kwa hiyo, tunahitaji kwa makusudi kabisa, wachimbaji wadogo watambuliwe, wapewe nafasi yao ya kusaidiwa kitaifa. Nimefurahi kwamba Waziri ametangaza nia yake ya kuanzisha Mfuko wa kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo. Mfuko huo uanzishwe, ufanye kazi ya kuwasaidia mara moja na hasa katika kipindi hiki kigumu cha msukosuko huu wa ulimwenguni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana wa Apolo wakikosa kazi, sisi ndiyo tunaathirika kule Arusha na njia ya kuwazuia wasikose kazi ni ule Mfuko kama ungekuwa unafanya kazi ungewasaidia wale wachimbaji wadogo kuhimili kipindi hiki cha mpito cha wakati mgumu mpaka hapo mambo yatakapokuwa mazuri. Mheshimiwa Waziri umetuahidi, ifanyie kazi ili tuone inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Arusha tunayo *Arusha Gemstone Curving Centre*, umeahidi utatafuta mitambo mahususi kwa ajili ya *Centre* ile ifanye kazi yake ya usonara na usanifu wa vito, isiwe kama jengo tu la *museum*, tuone inafanya kazi yake ya kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwenye sekta ya madini, hitimisha Mheshimiwa Waziri utekelezaji wa mapendekezo ya kizalendo yanayotekelezeka ya Kamati ya Mark Bomani. Kila siku isiendeleo kuwa wimbo, kamilisheni utekelezaji wa yale ambayo yanatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye nishati. Nishati ina changamoto nyingi lakini kinachonisumbua mimi ni mchakato wa mpango wetu wa kutatua hizo changamoto

zilizopo kwenye sekta hii ya nishati. Ulitumbia au tulisikiliza semina ya *TANESCO* wiki iliyopita, wanatumbia mchakato wa mpango, ni kuangalia uwiano wa mahitaji na uzalishaji wa umeme. Nikaanza kujiuliza kwani ni tatizo uwiano au ni matatizo ya kwamba hatuzalishi umeme wa kutosheleza mahitaji yetu? Maana kama tatizo ni uzalishaji wa umeme kwamba hautoshelezi, mambo ya uwiano hayawezi yakaingia ndani huku, yatatupotezea mwelekeo tu, tusipoteze wakati kwa vitu ambavyo vinatupotezea mwelekeo na wanaendelea kusema eti tufanye hivyo *under investment*. Mimi nafikiri tatizo hapa toka wakati wa uhuru kwenye mambo ya uzalishaji lilikuwa ni la *under investment*. Sasa tunahitaji kuwekeza zaidi katika suala la uzalishaji kuliko kusema kwamba tu-avoid over and under investment. Tuwe na mwelekeo huo kwa sababu tunahitaji Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema kuunganisha wateja 100,000, kila mwaka lakini tulitegemea pia tuwaunganishe watu 100,000 kila mwaka ili itakapofika mwaka wa 2030, asilimia 75 ya wananchi wetu watakuwa wameunganishwa, nikiangalia mahesabu haya hatutaweza kufika huko hata kidogo. Kwa laki moja kila mwaka itatuchukua sisi miaka 10 kuwaunganisha wateja milioni moja na miaka 20 wateja milioni mbili. Sasa hiyo asilimia 75 ya wananchi, tutaifikia lini wakati sasa hivi ni asilimia 14 tu ambao tumeweza kuwafikia. Hapa ni kiini macho lakini hatujaelewa nini cha kufanya cha kuweza kutufikisha huko tunakotaka kufika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema nini kinachohitajika, *Stigler's George* wameeleza vizuri sana. Tuwe *serious* katika kuusimamia huu mradi wa *Stigler's George* lakini ukiangalia maneno yanayotoka *TANESCO* na yanayotoka Wizarani, una wasiwasi kama kweli hapa kuna *seriousness* ya kusimamia mradi huu vizuri ili kuhakikisha tunaufanikisha kwa muda ambao tunataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wote tuonyeshe *seriousness* katika mradi huu wa *Stigler's George* kama tungekuwa *serious* toka miaka ya 1970, mwaka huu tungekuwa sisi tunauza umeme Kenya na Uganda kutokana na mradi huu lakini kutokana na kuyumbayumba kwetu huko mpaka leo hatujaonekana kwamba tuko karibu kuanza. Halafu hata hilo lengo la miaka 2020 inaonekana ni mbali sana, hatutaweza kufikia kama hatuonyeshi *seriousness* kuanzia sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni tatizo la *IPTL* na *Songas*. Katika hotuba ya Waziri alisema na ninamsifu sana kwamba *capacity charge* ile imepungua kwa dola milioni moja kila mwezi. Mimi naamini kwamba inaweza kupungua zaidi, mkiangalia zaidi yale wanayoweka huku ndani ya hii *capacity charge*, kuna michezo mingi sana inayofanywa pale. Tazameni tu ya *IPTL* muone michezo ambayo ilikuwa inafanywa pale na *Songas* pia iko michezo mingi sana. Hawa watu wanapata *gas* kutoka kwetu, tumeigharamia sisi, tumechukua mikopo ya kujenga miundombinu ya kuleta *gas* kutoka huko ilipo mpaka hapa wanapoitumia lakini wanachovuna hakioani kabisa na uwekezaji wao. Iangalieni tena, mpunguze gharama za umeme katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonisumbua mimi zaidi ni lile la *IPTL*. Ukiangalia katika ukurasa wa 10 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kuchelewa kwa mpango wa kubadili mtambo wa *IPTL* kutoka kutumia dizeli na kutumia *gas* asili, ni kutokana na mgogoro wa kisheria ulioko Mahakamani. Sijui kama huo mgogoro ndiyo ambao unazua sisi kuabadili. Mimi napenda kuamini kwamba pamoja na huo mgogoro, kubadili mitambo hiyo itumie *gas* ni sehemu ya makubaliano yao kwa hiyo *issue* sasa ni utekelezaji wa hilo, siyo tena kukubaliana tuanze kufanya lini. Lakini kubwa zaidi linalonisumbua mimi ni kwamba hatua za awali za kurekebisha mitambo hiyo imekwishafanyika na nimekwishawambia watu wa Finland wamekwishakamilisha kazi za usanifu. Sasa napenda kujiuliza, hasa baada ya kumsikiliza Mwenyekiti wa *TANESCO*

kwenye semina ile ya juzi, Mtendaji Mkuu alipotuambia kwamba ubadilishaji wa IPTL kutumia gesi asilia umekwama kutokana na gesi ya Songosongo kutotosheleza mahitaji. Sasa nauliza TANESCO wanatuambia hili, Wizara inasema hivi, kweli hapa mnaelewana nini kinachotakiwa kufanywa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbaya zaidi mwaka jana, bajeti hii imeidhinisha shilingi bilioni 24 zitolewe kwa ajili ya kubadilisha huu mtambo wa IPTL kutoka mafuta kuja kwenye gesi. Sasa najiuliza tulipitisha kiasi hicho cha hela, je, kazi hiyo kwanza ilifanyika? Kama haikufanyika inakuwaje leo hii mnakuja mnatuambia eti imekwama, kwamba gesi eti haitoshelezi. Mlipokuwa mnakuja kuomba hizo shilingi bilioni 24 mwaka jana hamkuwa mnajua kwamba kuna tatizo la gesi kutosheleza? Mimi ninachoona kinachoendelea hapa ni ule usanii unaoendelea katika sekta hii, siyo kitu kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alivalie njuga suala hili, uangalie huu usani, kweli hatuna gesi ya kutosha? Wewe uliomba kwenda kufungua mtambo mpya kwa ajili ya kutumia gesi iende mpaka kwenye magari, juzi ulifungua nafikiri pamoja na Mheshimiwa Rais, wanapeleka gesi moja kwa moja kwenye viwanda, lakini hii ya kuweza kupata umeme wa kuingiza kwenye gridi tunaambiwa eti gesi haitoshelezi, aaa! Hainiingii kichwani, nafikiri hata Mheshimiwa Waziri hiyo haitakuingia kichwani. Naomba ulivalie njuga, kawaangalie watu wako hawa.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, namalizia tu kwa kusema na kule Peramiho pia wanahitaji umeme, wawafikirie ndugu zangu. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tu kuwapa taarifa kwamba shughuli ambazo zilimwondoa Mheshimiwa Spika kwenye Kiti ameweza kuzikamilisha na hivyo basi kwa heshima zote, ninaomba sasa niache Kiti ili nimruhusu Mheshimiwa Spika aweze kuendelea na atakapokuja Mheshimiwa Spika, basi msemaji atakayeendelea ni Mheshimiwa Balozi, Dr. Getrude Mongella.

*Hapa Spika (Mheshimiwa Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

Kwa hiyo, sasa ambaye anafuata kuchangia, ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella!

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii. Kwanza kabisa, kwa leo kuna mambo mawili mazuri. Moja ni hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri na pia Kauli iliyotolewa na Waziri anayeshughulikia na Mambo ya Maendeleo ya Akina Mama ambayo italeta mapinduzi na wakati tunapitisha suala la umeme, natumaini akina mama wengi watapata nafasi ya kujiimarisha kiuchumi, tuweze kulipa bili za umeme. Hapo hapo nataka kukumbuka kwamba wapo waliotangulia kuifanya hii kazi nao nataka niwapongeze, Mheshimiwa Sophia Simba na

Marehemu Mheshimiwa Salome Mbatia ambaye alichakarika kweli kweli katika suala hili na akina mama wote hapa Bungeni na wote ambao wameshiriki katika kukubali jambo hili, haya ni mapinduzi ya kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, ninaomba tu niseme kwamba nitaendelea kuishukuru na kuishukuru na kuishukuru na kuishukuru Serikali ya Tanzania na Viongozi wote ambao wameiwezesha Wilaya ya Ukerewe na Visiwa vyake visivyopungua 28 kuanza kuona umeme kwa mara ya kwanza. Naomba niwashukuru sana. Umeme Ukerewe umewaka kama vile Serikali ya Chama cha Mapinduzi inavyotaka watu wake wafaidi matunda ya uhuru. Sasa wenzenu na sisi tunauliza bia baridi au bia ya moto. Kwa hiyo, naomba niwaambie kwamba Wakerewe wamefurahi Sana. Maprofesa wetu, hakuna mahali ambapo kuna wasomi kama Ukerewe. Tumeshafikia zaidi ya Maprofesa 68 katika nchi hii, wameanza kukimbilia viwanda na sasa hivi ni harakati kweli kweli kupata hata robo eka katika Wilaya ya Ukerewe ni tabu kwa sababu ya umeme na mimi mwenyewe nimejenga kajumba kadogo lakini kazuri na kana umeme. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme haya yafuatayo:-

Kazi ya umeme iliyofanyika ni nzuri sana. Tuna DC anaitwa Kwini kwa Kikerewe mgole. Kwini Mlozi, kwa muda mfupi aliokuja amesimamia kulipa fidia na imeenda vizuri katika wiki moja tu aliifanya kazi hiyo na ikakamilika vizuri. Nataka na yeye nimpongeze pamoja na viongozi wa *TANESCO* lakini nataka niseme haya kwa Mawaziri, moja, lazima tunapopeleka miradi mikubwa kama hii, tutafute kitu kinachosema *value for money*, ukipeleka umeme ukapepeapepea, ukaacha maeneo muhimu unakuwa unapata pato dogo katika kazi kubwa uliyofanyika na hii imetokea katika Wilaya ya Ukerewe. Kuna sehemu za Taasisi ambazo ni za muhimu sana ambazo *added value* yake siyo tu kupata malipo ya umeme lakini pia kuimarisha na kuboresha Taasisi hizi zikiwemo za Serikali ambazo ni Shule, Zahanati na maeneo ambayo yataimarisha uvuvi katika eneo hili. Shule za Sekondari kama Lugongo, Buguza, Pius Msekwa, Nduruma, Mibungo, Busangu, Shule ya Msingi Getrude Mongella, Mugu, Muriki, Igala, Bukanda na Bukongo, ni kati ya Sekondari zote ambazo ziko katika eneo la umeme, lakini hazikupelekewa mchepuo wa umeme. Kwa hiyo, sina haja ya kusimama tena, usiponipa maelezo kamili, nitasimama kuuliza kwa nini shule hizi za Serikandari zisipate umeme na unatujua Wakerewe tunakula samaki, *brain* ipo, tupe umeme watu wasome tuweke makopyuta tuweze kufanya uvumbuzi unaohitajika katika nchi hii. (*Makofi*)

Pili, zahanati kama ile *Health Centre* ya Kaziramkanda ya miaka mingi na Buzegwe na Kaseni. Maeneo haya yote yameachwa tu, yaani *cut of point* ingeweza kuwa ni Kijiji cha Kaseni ambako ni mahali pa mazalia ya samaki na tunaweza tukafanya uvuvi ambao siyo haramu katika Kijiji hiki. Tafadhali sana Kaseni, Kazilamkanda, Buzegwe wapewe umeme. Chuo cha Murutunguru kilichojengwa miaka ya 1952, umeme umeingia katika Kijiji cha Murutunguru, wote tumebaki mdomo wazi, Chuo kile hakikupewa umeme. Hapo ndiyo kulikuwa Makao Makuu ya mradi huu. Nguzo zote zilizopelekwa katika Wilaya hii, ma-transfoma yote yalilindwa na Chuo cha Murutunguru katika eneo lao lakini wao ndiyo hawakupata umeme katika kijiji hiki, kulikoni?

Mheshimiwa Spika, pia *Rubya Forest* ni msitu wa zamani sana ambako kuna harakati za uzalishaji mali wa mbao katika eneo hili na tunauza mpaka katika Mkoa wa Mara na Mwanza. Kwa nini hawakuwekewa umeme, bado wanatumia majenereta na hiyo inaongeza gharama. Maeneo mengine muhimu ambayo ni lazima yakumbukwe ambayo yamekosa umeme ni eneo la Tarafa ya Mumulambo, Mumbuga, kutoka Lugezi mpaka Nansio hapa

ndipo walipovushia umeme ulipotoka majini ukitokea Bunda lakini umeachwa ni umeme wa moto mkali, haukupozwa. Kwa hiyo, Tarafa nzima ambayo ndiyo iliyopokea umeme, ikajitolea, hawakupata umeme na hiki ni kitendawili, naomba tukitegue na tutegue haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Kijiji cha Mkasika, ambacho ndiyo Kijiji bora katika kujenga nyumba bora za kisasa na kulinda mazingira, wanalima mananasi, wanapanda miti, wanafanya *intercropping*, haikupatiwa umeme na kiko karibu sana kama kilomita mbili tu kutoka *point* ambayo ina umeme.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia niseme, Vijiji hivi vinafanana majina. Kimoja ni Kaseni ambacho nimekitaja, hiki sasa ni Muruseni. Muruseni na Kitale ambao ndiyo wanazalisha matofali ya kuchoma kwa ajili ya ujenzi katika Wilaya hii. Haya yote nimeyasema kwa nia ya kusema kwamba Waziri, ni suala la kucheki tu, mimi ninaona kuna mpaka nguzo ambazo zimebaki, zitaenda wapi? Zipelekwe huko.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba kabisa uhakikishe na wewe hupati tabu, si umeoa huko? Wewe au Naibu wako Mheshimiwa Malima, mkija wewe na mtani wako tukapita *point* kwa *point* kucheki kama utekelezaji ni nzuri na tupate ripoti.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kunishangaza, nyie vijana mmesifiwa sana sana, mimi siwasifu. Naanzia na Mheshimiwa Malima. Mheshimiwa Malima kwa nini mradi ule wa Kiparang'anda, mimi ninapafahamu kote huko Uzaramoni, nimepita nikiwa nashughulika na kazi za UWT, Kiparang'anda, Mwarusembe, Mji wa Kimanzichana hata Kilimahewa pale Hospitali hamna kitu. Maeneo yote hayo hayana, kitu giza tupu. Unafikiria kuna mtu atasifu eti Naibu Waziri kwake giza basi ni Mtakatifu, haiwezekani! (*Makofi*)

Hivyo hivyo na Mheshimiwa Ngeleja, kule kwake Katoro, alikochukua mtoto wa Kikerewa, kucha zimekwisha kwenye miguu yake kwa sababu ya kujigonga kwenye mawe gizani, peleka umeme, binti yetu azidi kung'ara. (*Makofi*)

Mimi nawaombea kwa sababu hapa tuna tabia moja, mtu akijitengenezea kwake basi tunamlaumu, amtengenezee nani? Kwa hiyo, nyie vijana na sifa zote mlizopewa pelekeni umeme huko katika kijiji cha Kitoro, Kata ya Biagu, amfikishie umeme huyu binti aliyekaa mbele yake, nilikabidhiwa na watu wa Busani, mpelekee umeme Katoro ambako ndiyo soko kuu la dhahabu, shida iko wapi? Hakuna shida! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema jamani umeme ni mageuzi, ni mapinduzi makali. Mimi ninaonekana kijana kwa sababu ya umeme ulioingia pale. Hivi ndugu yangu hapa Blandes akipata mimi nina shida gani? Ndugu yangu Kijiko akipata umeme, mimi nina shida gani? Pia Mheshimiwa Kawawa mjukuu wangu, mtoto wa Kawawa akipata umeme, kuna shida gani? Wote mpaka huko Zanzibar, Pemba mpaka kule Kojani ambapo mimi ni mwanachama wa Kojani, wakipata umeme kuna shida gani? Kinachogombewa hapa ni ukosefu wa rasilimali ya kuendeleza umeme. Waziri aje na mkakati wa namna tutakavyotafuta uwezo wa kusambaza umeme kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, sisi kwa mfano Wilaya ya Ukerewe, viwanda vyote vya samaki viko Mwanza. Unapeleka samaki unafika katika soko la Mwanza samaki wameshachina, hiyo sio kisayansi. Inapaswa kutengenezewa pale pale na wana mazao ya kusindika. Katika Bunge hili, tunachogombea ni namna ya kupata pesa na hili tutakusumbua kila siku. Leta tuzungumze mkakati wa namna nchi hii tutakavyotafuta rasilimali, kama ni mfuko maalum

wa kusambaza umeme, tufanye hivyo. Wafanyakazi wa *TANESCO* acheni uzembe, *we are serious*. Watu tuko kazini, mnaweza kabisa kwa pesa kidogo zilizopo zikitumika vizuri zikasambaza umeme katika maeneo makubwa zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. (*Makofi*)

Nilipokuwa nawataja, nikamwalia Spika pale, watu ambao hawajipendi, sijui naye anajipenda, kule kwako kuna umeme Mheshimiwa Spika?

**SPIKA:** Nazungushwa tu. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Kwa hiyo, nataka kusema ndugu zangu tutakapokuwa tunahitimisha, tutasimama kwenye vifungu lakini nia ni kusema nchi hii lazima iwe *developed*, hatuwezi kuwa na Kilimo Kwanza, mazao hayasindikwi. Hatuwezi kuwa na Kilimo Kwanza eti mama mjamzito Ukerewe ukitaka *X-Ray* au *Ultra Sound* mpaka avushwe majini na wimbi lile kwenda kupimwa Mwanza, wanakufa njiani. Hatuwezi kuwa na maendeleo kama watoto wetu hawasomi kompyuta, kama sasa mimi nina kompyuta 20 nimefungia, utaziwekaje? Lakini sasa ninazifungua na wengine wote nawatakia mazuri hayo hayo. (*Makofi*)

Ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri, watu wamesema maneno mengi, watu wa busara, watu wenye hekima wamekuwa ni watu ambao wameaminiwa, muwasikilize. Hili la sumu, sumu, sumu ya madini kwa kweli ni jambo baya, baya. Mimi naogopa zaidi hasa sisi tunaotoka kwenye visiwa hivi vilivyo kwenye ziwa Victoria, madini yote haya yatatumaliza, tutakuwa na hadithi ile ambayo ni ya almasi za Sierra-Leone, ambazo wanaita *blood money*. Kama hatutachunga mambo ya sumu, *it's a blood money*. Watu watakuwa wamechukua pesa, wametuachia sio mashimo tu, lakini wameuwa na watu kizazi hata kizazi. Hizo zebaki zinabaki mwilini, tena zinapitia kwenye samaki na unaweza kuzimeza kupitia kwenye samaki. Ndugu zangu Mawaziri nyie vijana mmesifiwa mno, hakuna kungoja, hili la sumu *it's immediate*, mnafunga, tujue moja, maji yale yanatiririka kuingia Ziwa Viktoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja (*Makofi*)

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hoja hii muhimu sana.

Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa siha njema na fursa ya kuchangia katika hoja hii.

Vile vile, ninapenda kuwapongeza na kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Mkinga, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakinipa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Tunashukuru kwamba, kutokana na ushirikiano wao na ushirikiano wa Serikali, tumeweza kutekeleza takribani yale yote ambayo yameagizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Ni imani yangu kwamba hata Wizara hii nayo itatoa ushirikiano huo kwetu ili tuweze kuikamilisha kwa ukamilifu. Wananchi tumeshirikiana nao katika kujenga shule nyingi, madarasa mengi, zahanati, barabara, miradi ya maji, miradi ya kilimo, ambayo yote kwa kiasi kikubwa inategemea sana upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana au kuwapongeza sana hawa wajukuu zangu hawa, bahati nzuri hawa Mawaziri wawili, wote ni wajukuu zangu. Mmoja anatoka Usukumani, mwingine anatoka Uzaramoni, kwa kihistoria ni wajukuu zangu. Ninawapongeza sana kwa kazi yao nzuri ambayo wameifanya. Kwa kusema kweli, ni kazi nzuri ya kuongoza Wizara hii nzito yenye utata mkubwa sana, lakini wamejitahidi kwa kadri

walivyoweza. Pamoja na wao namshukuru sana, Katibu Mkuu, nawapongeza sana Wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zao kwa jinsi walivyoshirikiana kutekeleza vizuri Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kazi kubwa waliyofanya kuelezea maeneo ambayo yanahitaji kuendelezwa Kisera, kwa hiyo, mimi kawaida yangu, kusema kweli, ni kuzungumza mambo ya Kisera kwa ujumla. Lakini kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengine wameeleza vizuri sana, sidhani kama itakuwa ni vizuri kwenda kinyume cha Kanuni ya Bunge, kuyazungumzia hayo. Lakini ninawashukuru na ninawapongeza, kwa hiyo, nina amini kwamba Waheshimiwa Mawaziri na Wataalamu wao watayazingatia na kuyatekeleza ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga, tunashukuru tumefaidika na huduma za Wizara hii, lakini bado kunahitajika jitihada kubwa sana kuweza kufaidika zaidi. Wilaya ya Mkinga, karibu shughuli zote zinazoshughulikiwa na Wizara hii tunazo. Kwa upande wa madini, Wilaya yetu ya Mkinga ina madini ya aina mbalimbali sehemu mbalimbali, lakini kwa bahati mbaya bado hatujaweza kuyatumia vizuri sana. Ni maeneo mawili au manne ambayo madini haya yanachimbwa. Tuna Doda, ambapo wanachimba mawe ya aina fulani, mazuri sana ya ujenzi wa nyumba, ni mawe maalum, Doda na Mbuyuni pale wanafanya kazi hiyo lakini bado hawajafanya vizuri. Vile vile kuna madini ya aina nyingi ambayo yanachimbwa Kata ya Mwakijembe na Kata ya Daluni. Lakini kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge walionitangulia, bado madini haya hayajachimbwa kwa ufanisi unaostahili kwa sababu ya ukosefu wa teknolojia, ukosefu wa utaalumu na ukosefu wa mtaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, nami naona kuna haja kubwa sana ya kuchukua hatua thabiti za kuiimarisha *STAMICO*, ili iweze kuwa na ule mfuko wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo ili wachimbaji hao waweze kufaidika na huduma yao. Naamini wachimbaji wa Wilaya ya Mkinga, ambao tayari wanafanya kazi na wale ambao hawajaanza kazi, waweze kufaidika kutokana na utaalumu, mitaji na teknolojia ambapo *STAMICO* itaweza kusimamia na kuwaendeleza. Kwa hiyo, ninaamini hilo Wizara italishughulikia na kuliendeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili, tuna nishati ya mafuta. Mwambao wa Kaskazini wa Wilaya ya Mkinga, ni moja ya maeneo ambayo kwa muda mrefu sana, yalibainika kuwa na fununu ya kuwa na gesi na mafuta. Utafiti ulianza kwa muda mrefu kidogo au labda *TPDC* ilikuwa inatafuta wahisani au wawekezaji wa kuweza kufanya utafiti huo lakini hali hii imedumu kwa muda mrefu sana bila mafanikio yaliyotarajiwa kuweza kupatikana. Tunaamini kwamba ipo haja kubwa ya kuendeleza jitihada hizi, kwa sababu majirani zetu kule Visiwani Pemba na Zanzibar, suala hili wanalishabikia sana, basi inaelekea majirani zetu wanayo, bila ya shaka na sisi yale mafuta yapo, kwa hiyo, ninaomba jitihada hizi zifanyike ili na sisi tuweze kuchangia katika pato la Taifa, iwapo gesi na mafuta yatapatikana kule.

Mheshimiwa Spika, sasa nishati ya umeme ndio kero kubwa sana katika Wilaya yetu ya Mkinga. Tunashukuru Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake ameeleza kwamba Makao Makuu ya Kasesa yalikwishapata umeme na kusema kweli yalipata muda mrefu kidogo na tunashukuru kwa hilo lakini hata katika Makao Makuu yenyewe bado kuna sehemu nyingine umeme haujapelekwa, ninapenda kukumbusha kwamba baadhi ya fedha zilizotumika zilikuwa ni fedha maalum ambazo ziliombwa katika Wizara ya Miundombinu wakati walipoanza kujenga Makao Makuu, fedha zile zililetwa kutoka kule lakini bado ziko fedha *TANESCO*; *TANESCO* wameanza kazi katika Vijiji vilivyotajwa katika hotuba ya

Mheshimiwa Waziri, lakini bado Makao Makuu yenyewe haijakamilika, kwa hiyo, tunaomba shughuli hiyo ikamilishwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini kero kubwa hasa yenyewe, ni kwamba tumekuwa na maombi ya muda mrefu sana, maombi ambayo yalianza tokea wakati wa Awamu ya Kwanza, maombi ya kuweka umeme Vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale. Haya maombi yaliombwa Awamu ya Kwanza, yakaombwa Awamu ya Pili, yakaombwa Awamu ya Tatu na siku zote tunaambiwa wananchi wetu wanaombwa wavute subira mpaka ilipofika mwaka 2003, nikabahatika kuwa na aliyekuwa Naibu wa Wazara ya Nishati na Madini, nikaenda naye huko, bahati nzuri naye alikuwa ni mjukuu wangu, tulipokwenda naye huko, akaambiwa bwana tafadhali wewe bwana wa Kizaramo, usilete utani hapa bwana, sisi tunataka umeme sio masihara, akaahidi na kusema kweli tokea wakati huo jitihada zilianza. Jitihada zilikwenda vizuri, utafiti wa awali ukaanza kufanyika, lakini tokea wakati huo hapakuwa na maendeleo. Mpaka ilipofika mwaka 2007, nikaauliza swali mimi hapa Bungeni, nikaambiwa kwamba tayari Vijiji vitatu vimeshawekwa katika mpango vipa na vitatekelezwa chini ya MCC, nikaelezwa na fedha zake zimeshatengwa.

Mheshimiwa Spika, mara ya awali ilielezwa kwamba fedha hizo zilikuwa takribani shilingi 598,967,000,000/= lakini siku zikapita, nikaauliza maswali tena mwaka huu mwanzoni, Februari na bahati nzuri yote hayo yako katika *Hansard*. Majibu yaliyotolewa, yanagongana na majibu ya awali. Nikabishiwa hapa kwamba hapana, miradi hiyo haiko chini ya MCC na zile fedha ambazo zimetengwa katika bajeti sikuelezwa zimeyeyukia wapi? Zilitengwa tayari katika bajeti ya 2007/2008, nikaambiwa bwana hii sasa hivi iko tayari chini ya REA na tayari zimeshatengenezwa bajeti yake, REA inafanya kazi ya kutafuta fedha hizo. Sasa awali niliambiwa ni shilingi milioni zile 598 na kuendelea, safari hii nikaambiwa zimefika shilingi bilioni 3.6 na REA ilikuwa inafanya kazi ya kufuatilia masuala hayo, nivute subira. Suala hili nimekuwa nikilifuatilia Wizarani, Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Wataalamu, tumeandikiana barua, baadhi ya barua nimezikopi kwako Mheshimiwa Spika, juu ya suala hili, lakini mpaka leo nimeambiwa nivute subira. Subira, Awamu ya Kwanza imepita, subira, Awamu ya Pili, imepita, subira, Awamu ya Tatu imepita, subira, Awamu ya Nne imepita, pamoja na kuhakikishwa kwamba ipo, subira hii mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, sasa kusema kweli, hili ni jambo ambalo wananchi wetu wa Mkinga, linawasikitisha sana. Wamefanya jitihada kubwa sana kuitikia wito wa Ilani yetu ya Uchaguzi na jitihada zote za maendeleo wakiamini kwamba umeme una mchango mkubwa sana katika maendeleo lakini ndugu zetu hawa wanakatishwa tamaa, wanaona kwamba mimi nawaongopea, wanaona kwamba hawa Wazaramo na Wasukuma watani zetu, wanatutania. Sasa mimi ninaomba pamoja na utani jamani, tuwe *serious* juu ya masuala haya, kwa sababu haya ni mambo ya kufa na kupona, ni mambo ya katika Ilani. Mheshimiwa Rais, alipokuja alielezwa juu ya kilio hiki; Mheshimiwa Rais, akahakikisha kwamba mambo haya yatatekelezwa. Sasa jamani kutoyatekeleza ni kwenda kinyume cha Ilani, ni kutofuata maagizo au ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais na tunajua maana yake ni nini juu ya masuala haya. Mimi ninawasihi sana, jamani haya mambo muyafanye kwa bidii ili shughuli zetu nyingine zote za maendeleo ziweze kufanikiwa inavyotakiwa kutokana na kupatikana kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi, kilio changu kikubwa ni hicho. Kutokana na hilo, ninaona kwamba nikiunga mkono moja kwa moja, nitakuwa ninavunja Ilani, nitakuwa ninawavunja moyo wananchi wangu, kwa hiyo, ninaunga mkono shingo upande, nikiamini kwamba wataelewa suala hili na wanieleze humu ndani, katika maandishi yote nimetazama sijaona. Hii miradi ya Mkinga, mmesema tu miradi ya Mkinga, lakini Vijiji vile vilivyotajwa,



Kwale, Daluni, Gombero na katika maelezo ya badaye walisema hata kijiji cha Vuga na Vijiji vya Boma wanaweza kuviweka, naomba ithibitishwe hivyo, ikithibitishwa hivyo nitakwenda nao, bila hivyo ninaunga mkono shingo upande.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Nashukuru kwa Hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri ametupatia. Mimi huwa nina furaha sana na kazi ambazo zinafanywa na Serikali, lakini kwa siku ya leo, nina masikitiko makubwa sana juu ya suala zima la umeme katika Mkoa wa Ruvuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukizingatia wazungumzaji wengi sana hapa wamezungumzia suala la umeme katika Vijiji, katika Wilaya na kadhalika lakini mimi ninazungumzia suala la umeme katika Mkoa wa Ruvuma. Ukifika Makao Makuu ya Mkoa hivi leo, ni giza totoro, hakuna mawasiliano, tukipiga simu, simu hazina chaji, umeme haupo, hakuna viwanda, hakuna masuala yoyote yanayoendelea. Nina uchungu mkubwa sana na ninaungana na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, hususani Manispaa ya Songea, ni hatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umeme katika Mji Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, siku zote tumekuwa tukiletewa mitambo ambayo ni *used*. Tumeletewa mitambo *used* kutoka Kihansi, tumehangaika nayo, tumelalamika, Serikali ikasema mtulie tutawaletea mitambo mingine, wameleta tena *used* kutoka Mtwara. Hiyo ndio Manispaa ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma, ni matatizo makubwa. Wafanyabiashara wanahangaika, viwanda hakuna, shughuli za Ofisini ni matatizo makubwa. Hivi majuzi wanafunzi wa *Songea Boys* waliandamana maandamano makubwa kabisa, wakidai umeme. Hivi majuzi Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, alikuwa anasoma taarifa na hotuba zake kwa kutumia simu ya *Nokia*, Ofisini, inatia huruma katika Manispaa ya Songea. Watu wanajiuliza jamani, hivi kweli sisi tuna wawakilishi Bungeni? Mbona umeme Songea hakuna? Tatizo ni nini? Leo wananchi wetu wanasikiliza habari za umeme Vijijini, kijiji fulani, Kata fulani, Tarafa fulani, wakati sisi Manispaa hakuna umeme! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo ni nini? Kwa nini Mkoa wa Ruvuma, ile Manispaa isinunuliwe mitambo mipya? Tumepewa ahadi ya Gridi ya Taifa, Gridi ya Taifa hatuiKatai, lakini Mheshimiwa Waziri, ukurasa ule namba 70, anasema hiyo Gridi ya Taifa ni mpaka mwaka 2013, hivi watu wa Songea wataishije? Mpaka mwaka 2013! Leo hapa tumeambiwa Wilaya zote zina umeme, Wilaya ya Namtumbo, hakuna umeme. Hivi tatizo ni nini katika Mkoa huu wa Ruvuma? Jamani, ajenda ya umeme ni kubwa, Mheshimiwa Waziri anajua na anafahamu jinsi ambavyo tumesogea mwaka 2010, anatumia mema? Hatutakubaliana Mheshimiwa Waziri, tunaomba ujitahidi. Kwa kweli, tunaona ni tatizo kubwa sana, mimi ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kwa suala zima la umeme katika Mkoa wa Ruvuma, alichukulie jambo hili ni kama jambo la dharura, ili aweze kurekebisha hali hiyo iliyoko huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwezi wa tano katika matatizo haya, Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma, tulimwomba kwa dharura Mheshimiwa Waziri Mkuu, akatembelee mitambo hiyo. Tukaarifiwa pale mitambo hiyo itatengenezwa kwa haraka na kwa vile Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa amefika pale, basi tukapewa ahadi nzuri; mpaka sasa hivi hakuna kitu! Waziri mwenyewe akaahidi pale, sasa inakuwa ni mbaya, kwa sababu wananchi wakashapewa kauli ya Waziri Mkuu, halafu wanaona mambo hayaendi, ni mbaya jamani. Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Malima, kwa umri wenu, Watanzania tunategemea kwamba mtachakarika kupita kiasi na kwamba Ruvuma haitakuwa na matatizo ya umeme, tatizo ni nini? Hebu uchukulieni Mkoa wa Ruvuma, kwa suala la umeme kwamba ni la kidharura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie pia katika kuleta mtandao wa umeme katika Manispaa, ile Manispaa ule mtandao wake wa umeme ni huo huo miaka nenda rudi. Umeme hausogei Mletele, Subira, Mwengemshindo wala Matogoro kule Mahilo, uko palepale CBD tu. Hii ni hali gani jamani? Hivi Mheshimiwa Waziri, anajua kwamba mahali palipo na giza na maovu yanaongezeka? Sasa anataka pale kwenye Manispaa pawe na maovu? Tunaomba aendeleze mtandao wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kitu kimoja, katika Mikoa yote, *TANESCO* ina majengo mazuri na Ofisi nzuri, nimwombe Mheshimiwa Waziri atuambie, pale Songea Manispaa kuna gofu baya ambalo ndio jengo la *TANESCO*. Gofu hilo linasababisha matatizo mengi na hivi karibuni mpaka ajali, lori zima liliingia kwenye hilo gofu. Tatizo ni nini? Kwa nini *TANESCO* ya Songea haijengewi Ofisi kama ilivyo katika Mikoa mingine? Kwani huu Mkoa wa Ruvuma mnauonaje? Kuwepo kwetu Kusini, isiwe ni tatizo. Mimi nilifikiria kwamba Mikoa ya Kusini, itapewa kipaumbele kwa sababu kila mtu anajua kwamba ina matatizo mengi, lakini matokeo yake imekuwa ni tofauti kabisa. Mikoa ya Kusini ndio tatizo kwa kila kitu; tumechoka na tunaomba mwaka huu uwe wa mwisho, macho yenu Waheshimiwa Mawaziri, pelekeni Kusini, hususani Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la nishati na wanawake wa Tanzania. Wanawake wa Tanzania tuna balaa, suala la kupikia majiko ya gesi, majiko ya umeme ni hadithi, tangu enzi ya mawe mpaka sasa hivi tunapikia mafiga haya matatu, itakuwaje? Masuala ya nishati, wadau wakubwa ni wanawake. Tunapenda kupikia katika majiko ya gesi, majiko ya umeme, ili kuweka uwiano. Mwanaume yeyote ukimwambia nisaidie kupika, kama una jiko la mafiga, anaKataa lakini kukiwa na jiko la umeme, anakubali kwa sababu ni rahisi na ni zuri sana. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, tusaidie wanawake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaona ni ajabu sana, sielewi Mheshimiwa Waziri, atajibu nini mbele za Mungu, kwa sababu tumeambiwa kuna wanawake Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, wanauwawa kwa sababu ya macho mekundu, kutokana na kupikia kinyesi cha ng'ombe au kuni, sisi viongozi, kama hatujawawezesha wanawake wapike katika teknolojia nzuri, tutajibu nini jamani? Hebu tujitahidi jamani, tumepewa huo wajibu tuweze kuongeza changamoto za kuwawezesha wanawake wapike kwa raha mustarehe na chakula kiweze kuwa kitamu, hapa hakuna mtu asiyekula, lakini kila siku vyakula tunavyokula vinanuka moshi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala zima la nishati mbadala. Mimi ninapenda kuwapongeza sana, wameanza na Waheshimiwa Wabunge, mimi ninaomba tuwasaidie *REA* tunavyowapa nguvu ndio sawasawa, kwa sababu wamenza karibuni, waendeleo kuchakarika. Matatizo ya nchi hii ni umeme Vijijini, kwa hiyo, tukiwawezesha *REA*, watafanya kazi nzuri sana. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, angalie pia taasisi nyingine zinazofanya kazi nzuri kama vile, *TATEDO*, *TASEA*, *CARMATEC*, *PROBEC*, ili ashirikiane nao, umeme Vijijini uwe mwingi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninaomba mafunzo yafanyike hususan kwa wanawake katika nishati za kupikia, lakini vile vile shule zetu, sekondari zote zinapikia kuni, mazingira yanaharibika. Mazingira yanaharibika kwa sababu ni tani nyingi sana zinaenda katika kupikia kwenye shule, Magereza na kadhalika. Kwa hiyo, ninaomba Wizara ya Mazingira na Wizara ya Nishati zishirikiane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie wachimbaji wadogo wdogo. Pale Mkoani Ruvuma, ukifika Kata ya Mfaranyaki, kuna eneo linaitwa Mkomi, utawakuta wachimbaji wadogo wadogo wamejirundika pale, hawana ufadhili, hawana mafunzo, hawana teknolojia, wanahangaika. Naungana na Wabunge wenzangu kusema kwamba tuwawezeshe wachimbaji wadogo wadogo, jamani hakuna kitu kizuri kama kujithamini. Hebu tujithamini, kama kuna watu wameonesha kwamba wanaweza kuchimba, hata kama wanachimba kidogo, tuwathamini. Tuwape nyenzo, tuwape elimu, na wenyewe watakuja kukua. Hivi hakuna uwezekano wa *BARRICK Tanzania*? Tunataka hawa wachimbaji wadogo wadogo, tuwakuze waje kuwa kama ma-*BARRICK* hayo, kama sijui ma-*GEITA Mining*, lakini bila kuwakuza hawa, hatutakuwa hata na *BARRICK* ya kwetu, tutaendelea kuwa hivyo. Kwa nini tunapenda kuthamini vitu vya nje? Mimi ninatoa wito Mheshimiwa Naibu Waziri, atusaidie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, kwamba wananchi wa Kijiji cha Peramiho, wamejiandaa kula *Christmas* na umeme. Wanaamini kwamba wameona zile nguzo zilivyoenda, nyaya zilivyoenda na nini, kwa hiyo, *Christmas* mwaka huu wanakula kwenye mwanga mkubwa. Kwa kweli, ninaomba ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta nyingine uwe mkubwa, kwa sababu tumeona kwa Vijiji kama Wemba, wana umeme ambao ni wa *Missionary*, Mavanga wana umeme, kwa hiyo, tunaomba basi mjitahidi kufanya ushirikiano mkubwa na *Mission* hata ile ya Peramiho, ili tuweze kupata umeme. Pia kule Chipole, Mheshimiwa Mama Lucy Nkya alienda, akaambiwa Chuo kile cha Wananchi hakina umeme lakini Chipole, kama mita 200 tu pana umeme. Mheshimiwa Waziri Ngeleja, naomba fanya mazungumzo nao pale Chipole, ukifanya nao mazungumzo mazuri kama Waziri, mimi nina imani watakubali na tutapata umeme kwenye Vyuo vyetu vya Maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuungana na Wabunge wenzangu, suala la nishati ni suala muhimu na litaleta maendeleo makubwa sana katika nchi yetu. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Devota Likokola, kwa kutetea Mkoa wa Ruvuma, Serikali itakuwa imesikia.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kuendelea na michango. Nadhani kutakuwa na fursa fupi sana saa 11.00 jioni lakini nitatamka baadaye tutafanyaje.

Waheshimiwa Wabunge, jana wakati Mheshimiwa Mwenyekiti, Zubeir Ali Maulid, akiwe amekalia Kiti...

**WABUNGE FULANI:** Juzi!

**SPIKA:** Ni juzi kweli, jana ni Jumapili, kweli, samahani sana.

Juzi, alisimama Mheshimiwa Anna Abdallah, akadai chini ya Kanuni ya 68, kwamba Mheshimiwa Mwanawetu, hakusema kweli pale alipotamka kwamba Waheshimiwa Mrope na Mbilinyi, walijitoa kwenye Kamati ya kusukuma maendeleo, kwa sababu walikuwa wamepata nyadhifa kubwa.

Hii ndio *Hansard*, ninayo hapa, alichokisema Mheshimiwa Mwanawetu na ninaomba ninukuu alisema:-

*“Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba hawa, (akiwa na maana Waheshimiwa Mbilinyi na Mrope), waliukana Umoja huu baada ya kupata nafasi kubwa kama za Uwaziri. Wakati huo kabla hawajapata hizi nafasi walikuwa pamoja na wananchi wa Mikoa ya Kusini.”*

Sasa kwenye Kiswahili mtu akisema “kama,” maana yake amelinganisha, kwa hiyo, hakusema kwamba walipopata nyadhifa za Uwaziri, alisema nyadhifa nyeti kama za uwaziri. Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Mwanawetu, hawezi kusemekana kwamba alisema uwongo. Kwa hiyo, sihitaji kumtaka asahihishe usemi wake, kwa sababu ukisema nyadhifa kama, basi inaweza kuwa Ukatibu Mkuu wa Wizara, inaweza kuwa Mwenyekiti wa Bodi, inaweza kuwa nyadhifa kama hizo. Kwa hiyo, huo ndio uamuzi wangu kuhusu hilo.

Ninawaomba tu Waheshimiwa Wabunge, tuwe tunasikiliza vizuri hizi hoja, ili neno moja linaweza kuleta tofauti, neno “kama” tu, limemsaidia; asingesema hivyo, angesema nyadhifa za Uwaziri, haikuwa hivyo sasa, angekuwa tayari kasema uwongo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Injina Laus Mhina na atafuata Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kama atakuwepo, naona wengi wanatokatoka. Sina hakika kama tutaendelea zaidi kwa sababu, Kamati inaweza kuwa ni ndefu, kwa hiyo, labda niwaachie hawa wawili tu, halafu tusemba mambo yatakavyokuwa jioni.

Baada ya matangazo hayo, niseme tu kwa Wizara hii, bahati mbaya Mkurugenzi wa Utawala ama sijui nani katika Wizara, hakutupa fursa ya kuweza kuwatambua watendaji muhimu wa Wizara. Kwa sababu ninachosoma hapa ni kile ninachopewa, majina ya wageni ninapewa hapa, sasa hayakuja.

**MBUNGE FULANI:** Wameleta mara mbili.

**SPIKA:** Wameleta mara mbili? Sijui, sasa hii tujisahihishe na sisi Ofisi yetu, yakija majina, ninatumaini Sekretarieti, mtanipa fursa hiyo jioni kwa sababu ni haki yao na ni lazima nisome majina yao ili kuweza kuwatambua. Muangalie ili yasije yakawa yamepotea na sasa basi ni wajibu wenu kuweza kuyapata kutoka kwa Wizara, kama hivi sasa hamuyaoni, ili tuweze kuwatambulisha, ni heshima tu na pia ni vizuri tu kwa Waheshimiwa Wabunge, kuweza kuwatambua Watendaji Wakuu wa Wizara maana ndio wanaofanya kazi, pamoja na kuwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wako mstari wa mbele lakini bila lile Jeshi zima linalowapa taarifa mbalimbali, isingewezekana kuweza kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutamka kwamba ninasitisha shughuli za Bunge, hadi hapo saa 11:00 jioni.

*(Saa 06.59 mchana, Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa hapa siku ya leo na kujaribu kutoa mchango wangu. Vilevile napenda kukushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuweza kutoa mchango huo ambao unahusu Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Naibu wake pamoja na Wizara nzima kwa ujumla, ikiongozwa na Katibu Mkuu ambaye kwa ufanisi mkubwa imeonyesha wazi kwamba Wizara hii wameimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa mfupi tu na nimeupanga katika makundi mawili makuu. Kwanza, itakuwa sekta ya nishati ambayo itafuatiwa na sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na sekta ya nishati, upande wa umeme, sote tunafahamu ni jinsi gani umeme unamgusa kila mtu, zamani tuliambiwa suala la umeme ni la anasa lakini sidhani kama suala la umeme ni anasa tena katika dunia hii ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa umeme kila mtu anaufahamu, awe wa kijini au wa mjini, umeme anaohitaji. Umuhimu wa umeme unafahamika wazi kwamba ndiyo nyezo kubwa katika viwanda vyetu, ndiyo nyezo kubwa katika majengo yetu ya huduma za jamii mbalimbali kuanzia shule, hospitali, ofisi na ndiyo pia nyezo kubwa hata katika nyumba zetu tunazoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kidogo kwa masikitiko, tumekuwa na miradi kipindi hiki kinachopita cha mwaka 2008/2009 kwa maana ya miradi ya *REA* na *MCC*, bahati mbaya miradi hii haikuingia katika Wilaya yetu ya Korogwe, hususani nizungumze Jimbo la Korogwe Vijijini, inawezekana Korogwe mjini imegusa kidogo lakini Vijijini, miradi hii haikufika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme wazi, bahati nzuri Korogwe kwanza tunayo miundombinu mizuri tu ya umeme kwa sababu tuna mashamba mengi ya chai, tuna mashamba mengi ya mkonge, tuna minara chungu nzima sehemu zote hizi, bahati nzuri *line* za umeme zimefika. Sehemu zote hizi zilipopita *line* hizi kuna Vijiji chungu nzima, lakini kwa bahati mbaya Vijiji hivi havina umeme hadi leo japokuwa utakuta Vijiji vingi au nyumba nyingi zimekwishafanyiwa *wiring* lakini umeme ambao tumeahidiwa miaka mingi iliyopita hadi leo hii havina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalizungumza kwa masikitiko makubwa sana, kuna Vijiji kwa mfano, Kijango, umeme upo karibu kabisa Magoma pale, kuna kijiji kwa mfano Kichungu Moto, umeme upo unaokwenda kwenye minara ya simu lakini kijijini pale umeme hawakupatiwa. Ni jambo la kuweka *transformer* tu wananchi wale wapatiwe umeme lakini bahati mbaya haijafanyika hivyo mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Vijiji kwa mfano vya Mkwajuni, Kwamazandu, ambavyo viko katika Kata ya Magoma, Kata ya Magoma mjini umeme upo, Vijiji hivi ni kama ni vitongoji tu vya Magoma lakini umeme haujafika. Kuna Vijiji kwa mfano vya Lusanda, Kibaoni umeme umefika katika kijiji cha Makaburini katika Kata ya Kelenge, lakini Vijiji hivi havina umeme. Dindira umeme umekatiza kabisa katika kijiji cha Dindira kuelekea katika mashamba ya chai lakini bahati mbaya ni suala la kuweka *transformer* na kuteremsha umeme, nyumba zimekwishafanyiwa *wiring* takriban miaka kumi iliyopita lakini huduma hii hakuna, inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kituo kikubwa kabisa cha afya kilichojengwa na wenzetu Kanisa la Katoliki cha Rose Min, katika Kata ya Mkalama. Kituo hiki cha Afya kina kila aina ya mashine za kisasa lakini cha kusikitisha mashine zile hazifanyi kazi kwa sababu umeme hakuna. Maombi yao wameyaleta siku nyingi sana takriban miaka kumi iliyopita

lakini mpaka leo hii wanatumia jenereta kwa gharama kubwa ya mafuta na huduma ni sisi wananchi maeneo yale ambayo tunazihitaji, hili linasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunazungumzia sekondari, karibuni kila Kata ina sekondari, sekondari zile zinatakiwa tujenge mabweni na tumeshaanza kazi ya mabweni, sekondari zile inatakiwa tujenge maabara na tumeshakwishaanza kazi ya kujenga maabara lakini vyote hivyo kama itakuwa hatuna umeme, itakuwa ni kama kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme chonde chonde katika awamu hii ya 2009, hebu Wizara hii itufikirie Korogwe Vijijini tunahitaji umeme. Tumeshajiandaa, *wiring* tumekwishafanya, tunangoja ahadi ambazo mmetuwekea, tuwekeeni umeme jamani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeongelea kidogo kwa machungu kuhusiana na suala la umeme sasa niongelee kidogo kuhusu suala la madini. Korogwe Vijijini inafahamika sana kwa madini ya vito, karibuni milima yote iliyoizunguka Korogwe Vijiji, ni madini tupu mle kuna rubi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali, safari hii kwa kweli imemfikiria mchimbaji mdogo, nasema hiyo makusudi kwa sababu gani? Nalisema kwa sababu Serikali imekamilisha sera ambayo tulikuwa tunaisubiri, Sera ya Madini ya mwaka 2009 ambayo kati ya malengo yake makubwa ukiangalia yanamlinda mchimbaji mdogo. Malengo hayo ni kumboresha mchimbaji mdogo, kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji hawa wadogo na pia kujaribu kuwatafutia namna ya kupata mikopo ambayo ninaimani kabisa itakuwa ni mikopo ya riba nafuu ili nao waweze kujikimu, waweze kuziweza hizi kazi za uchimbaji, hili nataka niipongeze Wizara kwa kweli kwa kuchukua hatua hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niishukuru au niipongeze Wizara kwa kuweka kipaumbele cha elimu kwa wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo ni lazima tuwajali usalama wao wanapokuwa machimboni, kitu ambacho Wizara imekiangalia na cha kusifika zaidi ni kutoa kipaumbele kwenye suala la mazingira katika machimbo yetu. Hili kwa kweli halina budi kusifiwa na kupongezwa kwani sehemu yote yenye machimbo ya madini, shughuli za machimbo ya madini zinapokwisha, mara nyingi yanayobaki pale ni mahandaki na mashimo matupu, ina maana ni uchafuzi wa mazingira mtupu lakini nashukuru kwamba Wizara sasa hili imeliona, hongera sana Wizara kwa kuliona hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka niseme wazi kwamba tunazona juhudi zinazochukuliwa na Wizara jinsi gani ya kuimarisha maisha ya mchimbaji huyu mdogo ambapo kusema ukweli ndiyo wachimba wengi katika nchi yetu hii ya Tanzania. Nataka niongee machache kidogo kuhusu machimbo ya vito yaliyopo katika Jimbo langu, kwa maana ya Kalalani Kigwasi Kata ya Mashela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee mgogoro unaodindima kule Kigwasi kwa maana ya Kalalani, kuna mgogoro wa siku nyingi. Mgogoro ambao nina imani kabisa hata Wizara unafahamu mgogoro huo. Mgogoro uliopo kati ya wachimbaji wakubwa na wachimba wadogo na vilevile na jamii iliyozunguka eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika, mgogoro huu Wizara unafahamu japokuwa unajaribu kuufumbia macho. Juhudi zilifanyika za kujaribu kuupoza mgogoro huu ambazo kwa kweli zimezaa matunda kwa kiasi Fulani, tumshukuru Mheshimiwa Mkuu wa

Mkoa aliyeondoka, Mheshimiwa Abdulaziz, kwa jitihada zake, naweza nikasema huu mgogoro kwa sasa umepoa, sio kwamba umezimika kabisa kabisa bali umepoa kwa kiasi fulani lakini mgogoro upo mpaka sasa na hili sio la kufumbia macho kwa sababu hili ni sawasawa na bomu ambalo wakati wowote linaweza likalipuka kama tutakaa tunafumba macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu kule Kigwasi Kalalani leo hii wanaishi na risasi mwilini. Inasemekana waziwazi kuna wanawake kule wamewahi hata kubakwa, inasemekana wazi wazi kuna nyumba zimechomwa lakini niseme kwa uchungu kidogo kwamba Wizara inafahamu na Wizara imekuwa ya mbele kabisa inaposikia malalamiko kama haya, Mawaziri ni wa kwanza kabisa kwenda katika maeneo hayo lakini eneo la Kigwasi hadi leo hakuna Waziri ambaye amelitembelea kwenda kuangalia juu ya haya yote ambayo nimeyataja yaliyotokea. Hili kwa kweli ni la masikitiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme wazi, niliwahi kuongea hata na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Malima, ajaribu kulitembelea eneo hilo, simlaumu kwa kweli kazi alizonazo ni nyingi na ameniahidi kwamba atanitembelea na *inshallah* nasema atembelee ayaone mwenyewe asipende kusoma taarifa zilizo kwenye makaratasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa kumalizia mimi nataka wakati wa kumalizia hoja hii nielimishwe vizuri suala la mrahaba, wenzetu wa dhahabu, madini ambayo yanatoka chini wanapata mrahaba lakini sisi ambao tuna madini ya vito, vito ambavyo vinatoka ardhini pia, Halmashauri zetu hazipati chochote, hatuna kodi yoyote tunayopata! Sasa sijui kuna tofauti gani kwani madini yote haya yanatoka ardhini, lakini yametenganishwa. Halmashauri yetu na wananchi wa Korogwe hubakiwa na mashimo matupu, tusibakie na chochote, si afadhali watupe chochote hivi sasa japo tuweze kuendeleza shule zetu, tuendeleze barabara zetu, tuendeleze vituo vya afya kwa sababu kwa hali yoyote madini haya yatakwisha na yakiisha tutababakia na nini, tuje tuwaeleze watoto wetu kwamba tunawarithisha mashimo matupu haya. Naomba wenzetu wa Wizara wanielimishe na wawaelimishe pia wapiga kura wangu watafaidikaje na madini au wanafaidika na huko kuchomewa nyumba zao tu basi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mchango wangu utakuwa ni mfupi sana, nimeyazungumza kwa uchungu sana na kwa huzuni sana lakini kwa heshima niliyonayo kwa Mawaziri, naunga mkono hoja hii, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai siku ya leo. Lakini pia napenda kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mbinga Mashariki, kwa kazi nzuri wanazofanya kwa kujitolea katika kujenga sekondari na majengo ya zahanati na pia kuvuna kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri, ni nzuri na imewasilishwa kwa umakini mkubwa, ila ninayo mambo machache kwa ajili ya Jimbo la Mbinga Mashariki ambayo naomba Serikali kupitia Wizara hii, iyazingatie.

La kwanza, ni kuhusu *license*, *license* hizi zinatolewa Makao Makuu na wale watu wanakwenda moja kwa moja katika maeneo na wanapofanya kazi kule wakikutwa na majanga au wakipata shida wanakuja Wilayani kuomba msaada. Kikiingia kipindupindu, wakiingiliwa na wezi wanataka Polisi, wanataka madaktari lakini wanapokwenda kule,

Wilaya hiyo haina taarifa. Kwa hiyo, naomba Serikali ifikirie namna ya kuweza kuleta taarifa za namna hii katika Wilaya ili Wilaya ziwe na habari na ziweze kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naishukuru Serikali kwa kuleta umeme Mbinga, ni jambo ambalo nalishukuru kila siku na mara kwa mara. Lakini ninapenda Serikali iende zaidi ya hapo, wamefunga jenereta mbili kubwa uwezo wa *megawatt* 2.5 lakini wananchi wa Mbinga wanashindwa kutumia umeme ule kwa sababu *service line* hazijajengwa kwa kiwango kikubwa katika maeneo ya Mbambi, Matalawe, Lusonga, Kihaha, Tank la Maji. Sasa mtu akitaka lazima alipe shilingi milioni mbili, shilingi milioni tatu, uwezo huo tutakubaliana kwamba kwa Watanzania si mkubwa kiasi hicho. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara hii kupitia *TANESCO* waweze kujenga *service line* ili angalau zile laki nne, ambazo wananchi wa Mbinga wanazimudu waweze kuvuta umeme. Iko shule ya walemavu pale Huruma wameambiwa walipe shilingi milioni 21 hawa wanasaidia walemavu, mimi nafikiri Serikali ingeweza kuwasaidia kwa kuwapelekea umeme. Iko pia *High School* na Mbinga hakuna *High School* isipokuwa hii ya *private* Agustive, nayo pia wameambiwa sijui shilingi milioni 10, mimi nafikiri miradi kama hii ingeweza kupewa kipaumbele kwa wenzetu hawa ili kuweza kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ili watu wa Mbinga waweze kuutumia umeme huu vizuri *at full capacity*, naomba maeneo ya Maguu, Litembo, Matili, Mbangamao na Ruanda ambayo ni miji midogo na kuna shughuli nyingi sana za kiuchumi yapatiwe umeme. Sasa hivi tunazungumzia juu ya Kilimo Kwanza na maeneo haya niliyoyataja, ni maeneo ya wakulima wa kahawa. Kwa hiyo, wakipata umeme ile mitambo yao badala ya kutumia *diesel* wanaweza wakatamia umeme utakuwa umerahisisha na umefanya kazi kwa bei nafuu zaidi na hivyo kuinua kipato cha wale wakulima wa kule Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sasa kuzungumzia juu ya wachimbaji wadogo wadogo. Yako maeneo kule katika Jimbo langu eneo la Makolo, Masuguru, Ngembambili na Customs, ni maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo, walikuwepo wakubwa wawili, naona wameondoka lakini wametuachia mashimo. Sasa la kwanza, naomba Waziri ahakikishe kwamba wale jamaa wanakuja kufukia mashimo yale. Lakini la pili, yale maeneo yatangazwe kwamba ni maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo. Imefanywa hivyo katika Mkoa wa Tanga na sioni kwa nini isifanyike katika Wilaya ya Mbinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa hawa wachimbaji wadogo wadogo, bado wanahitaji kupata elimu kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesema vizuri sana. Sasa tulikuwa tunangoja utekelezaji na pia ningefurahi kama utekelezaji huu ungeweza kufika katika Jimbo la Mbinga katika maeneo ambayo tumeyataja. Hata kwa Mheshimiwa Capt. Komba, Jimbo la Mbinga Magharibi, yako maeneo ya uchimbaji dhahabu mengi sana ambao wanahitaji huduma kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu katika mchango wangu ni kuhusu mkaa wa mawe. Mwaka 2006, ule mkaa ulikuwa unaungua kwa miaka mitatu iliyopita na mimi nilifanya juhudi ya kupeleka Waandishi wa Habari yalipotoka kwenye TV, Serikali na yenyewe ndiyo ikaanza kuamka na kuweza kusaidia na wamekwenda pale wakachimba makaa ya mawe tani 400 ziko nje na tulikwenda pale na Katibu Mkuu wa Wizara hii na alihidi kwamba angeweza kupeleka wataalam kuwafundisha akinamama kutumia ule mkaa kama nishati, mpaka leo wale wataalam hawajapeleka toka mwaka 2006 mpaka leo ni miaka mitatu. Kwa hiyo, naomba hii ahadi iweze kutekelezwa kwa maana wale akinamama na vijana wanasubiri lakini pia pale kuna udongo mzuri sana wa kuweza kufanya kazi ya ufinyazi. Ninaomba sana



Wizara iweze kutusaidia. Jambo hili nimefuatilia kwa kweli kwa muda mrefu, sasa ninaomba litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo Mbuyula pia wakati ule ilionekana hakuna mwekezaji aliyejitokeza kwa hiyo wakati ule tulizungumza na Wizara tukaona afadhili tuhamasishe wananchi waunde kampuni. Wananchi wakaunda kampuni mpaka leo hakuna majibu, nimefuatilia mara nyingi mpaka *pair* moja ya kiatu imekwisha pale Wizarani, hatujapata jibu mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni ofisi ya Madini ya Wilaya, Wilaya ya Mbinga ni Wilaya ambayo imejaliwa sana kwa madini katika Mkoa wa Ruvuma, tunashukuru Serikali imeweka pale ofisi ya Mkoa. Tunduru kuna ofisi sasa kwa sababu shughuli nyingi sana ziko kule Mbinga, tunaomba watujengee ofisi ya Madini ya Wilaya. Tulipeleka maombi haya mwaka 2007 mpaka sasa hatujapata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, iko kampuni ya *TANCOAL*, hii ni kampuni ambayo asilimia 70 inamilikiwa na kampuni ya *PACIFIC* kutoka Australia na asilimia 30 inamilikiwa na *NDC* yaani Serikali. Hii kampuni imekwenda kufanya utafiti katika maeneo haya ya Ngaka na imeonekana kuna mkaa mzuri na mwingi na wana mpango kuanza wa kuchimba, lakini pia kujenga *power station* kwa ajili ya kuzalisha umeme wa *megawatt 400*. Itakapofika mwaka kesho Desemba, watakuwa na uwezo wa kuzalisha *megawatt 50* ambazo ni kwa ajili ya kazi zao, lakini hizi zinatoshwa kuweza kuhudumia Mkoa wa Ruvuma, Mtwara hata na Lindi. Pia wanataka kujenga chuo kwa ajili ya kufundisha hawa watu watakaokwenda kufanya kazi pale. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna mahala popote panapotajwa juu ya maendeleo haya. Mimi nafahamu mradi huu unafanyika moja kwa moja na *NDC* ambao wako chini ya Wizara ya Viwanda lakini kwa sababu ni nishati ya umeme, nilidhani angalau ingetajwa hapa. Iko miradi hapa ambayo haijatafutiwa fedha ndiyo iko tu katika mipango imetajwa lakini mradi mkubwa wa namna hii na ukombozi kwa nchi na ni wa aina yake kwa sababu kwa mara ya kwanza tunaweza tukapata aina nyingine ya kupata umeme kutokana na mkaa. Tunapata umeme kutoka kwenye maji na sasa yako mawazo ya kupata kwenye upepo, tunawapongeza hawa wenzetu kampuni moja inafanya kazi kule Singida lakini sasa tutapata kutokana na mkaa na ni *megawatt 400*.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kulikuwa na mjadala mkubwa sana juu ya kununua mitambo ya *DOWANS*, inunuliwe au isinunuliwe, tukapata pia matishio ya *TANESCO* kwamba isipofanyika umeme utazimwa nchi nzima. Lakini hapa kuna watu ambao wanafanya hii kazi usiku na mchana, wameshawekeza kiwango cha shilingi bilioni 1.4 kufanya utafiti na sasa wanaendelea, *there is no mention at all* hata ku-*appreciate* ile kazi ambayo imefanyika mpaka sasa. Hawa ni wawekezaji ambao wanashirikiana na shirika kubwa la Tanzania hapa nchini. Serikali inapofanya jambo la namna hii, kwanza inataka tujifunze nini? Kama haiwezi ku-*appreciate* kazi ambazo shirika la *NDC* pamoja na kwamba linapewa fedha kidogo limetafuta huyu mbia mwenzake, huyu mbia anazo fedha ameweka shilingi 1.4 bilioni hakuna *mention* kabisa! Mimi sielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza suala hili katika semina iliyofanywa na *TANESCO*, tuliambiwa hawa jamaa hawajaweza kuthibitisha kama pesa wanazo na uwezo wanao lakini wamekwisha-*invest* shilingi 1.4 bilioni, kwa nini tusi-*mention* hata hiyo?  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizi za Kusini mwa dunia, zinalalamika kwamba zile nchi za Kaskazini zilizoendelea zinazionea nchi za Kusini ambazo hazijaendelea. Lakini dhambi hiyo inafanyika hapa nchini, miradi inayofanyika katika Mikoa ya Kaskazini inapewa umuhimu mkubwa sana na miradi inayopelekwa Mikoa ya Kusini haiwi *mentioned* hata kidogo na unaweza kuona juhudi za hata za kuhujumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nitoe tahadhari kwamba kwa hili mimi sitanyamaza na nina hakika kuna wengine pia hawatanyamaza. Tunaomba Serikali ishirikiane na wawekezaji hawa kama wamewaambia na wanaona kwamba hawana takwimu za kutosha, Serikali ituambie Mheshimiwa Kayombo hii kampuni ya kitapeli tumeshaichunguza na tumeona hivi lakini bila hivyo kwa nini hawasemiwi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakushukuru na nawashukuru wapiga kura wa Mbinga, nadhani Serikali itaweza kufanya juhudi za makusudi za kuona kwamba hii kampuni ni kampuni yenye thamani na inafanya kazi za uhakika. Ninaomba Serikali ifanye utafiti huo mapema ili wananchi wajulishwe, wasiwe na matumaini ambayo hayapo kwa sababu Serikali yenyewe haionyeshi kwamba hii kampuni inafanya kazi za maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka wameanza sijaona Waziri yeyote ambaye ametembelea mradi ule na hawa jamaa wanaKata tamaa. Lakini wanapokuja wawekezaji wengine wanapokelewa na *red carpet* pale uwanja wa ndege, *VIP treatment*, wanasema tunarudi, hawarudi. Wako wawekezaji wengi wamekuja hapa wamepokelewa vizuri sana lakini hawajafanya chochote. Hawa wanapita kwenye maeneo ya kawaida pale *Airport* lakini wamewekeza kiasi hicho, kwa nini tusiwajali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, katika kuangalia orodha yangu toka asubuhi, nimeona kwamba upande wa pili hajaongea Mbunge yeyote. Kwa nafasi hiyo basi, mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo atakuwa Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nilikuwa nimekata tamaa kwamba sitapata nafasi, lakini nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, kabla hujaendelea, naomba nichukue fursa hii kumkaribisha Mheshimiwa Spika kwenye ulingo hapa.

*Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo, endelea tafadhali.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nataka kutumia nafasi hii, kwanza kabisa kuwatakia wapiga kura wangu, kila la heri kwa msimu huu wa neema ambapo kuna ruzuku nzuri ya pamba, kwa hiyo, waitumie vizuri.

Mheshimiwa Spika, nataka kujielekeza kwenye mahitaji ya umeme, mwaka 2006 Mheshimiwa Rais alikuja kwenye Kata yetu ya Nkoma, akafungua bwawa zuri sana ambalo

lilishajengwa na *World Vision* kwa takribani shilingi milioni 450. Aidha, pale pia kuna kituo cha afya ambapo zimetumika sasa karibu shilingi bilioni moja kukijenga, hatimaye yale maji leo ni mwaka wa nne tunayaangalia tu maana yake hayawezi kufika kwenye kituo cha afya, wale wananchi hawawezi wakayatumia kwa sababu hakuna *pump*.

Mheshimiwa Spika, Nkoma ni kilomita nane tu kutoka pale ambapo kuna umeme, Mwanapalala. Kwa hiyo, nafikiri kwa sababu mwaka kesho kuna uchaguzi na nafikiri Mheshimiwa Rais atahitaji kura nyingi sana kutoka kule ninakotoka, basi ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Waziri kwa kujipalilia labda na wewe mwaka kesho ukaendelea na kazi uliyonayo, ukahakikisha kwamba kuna umeme kwenye bwawa hili, *pump* ile ipatikane na umeme uweze kufika katika kituo cha afya na njiani Mwanumu, Mitobo na sehemu zote hizo ili wananchi na wenyewe waweze kufaidika na matunda mazuri ya Awamu hii ya Nne. Kwa hiyo, hilo ni ombi Mheshimiwa Waziri, naomba tafadhali sana nimeangalia katika kitabu chako, Bariadi hatuna miradi ya kutosha. Ni miradi michache tu ambayo imo kupitia huu utaratibu wa umeme Vijijini, kwa hiyo hilo la kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, unakumbuka kwamba mimi nilikuwa katika Kamati ya Mheshimiwa Jaji Bomani na tukaweka mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu na baadhi ya mapendekezo hayo, mengi yalikubaliwa na kuadhimiwa na Bunge kwamba Serikali iweze kuyatekeleza. Lakini kitu ambacho kinatusikitisha sisi wote ni kwamba kuna mambo mazuri ambayo tunayahitaji, mojawapo ni kuhakikisha kwamba madini yanatumika sio tu kujenga uchumi ambao ni *micro-economics*, lakini kuongeza mapato ya Serikali. Kwa sababu nchi kama yetu hii ambayo ina tani 40 za zahabu kila mwaka ambapo mwaka jana tu peke yake, tumeweza kupeleka nje zaidi ya dola bilioni moja na ushei. Nchi kama hiyo haiwezi kupata fedheha ya kuwa nchi tegemezi. Kwa hiyo, kwa hali hii, kwa nini Serikali inakuwa kama vile inasuasua kutafuta vyanzo ambavyo vingeweza vikatuondolea adha hii ya utegemezi?

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa kuona kwamba mpaka leo kwa mfano tulisema kuwa mrahaba ungeongezwa kutoka 3% mpaka 5% kama Mheshimiwa Waziri angekuwa ameleta Sheria ya kurekebisha jambo hilo, nina hakika badala ya kupata pesa kama shilingi bilioni 33 tu kutokana na mrahaba leo tungepata zaidi ya shilingi bilioni 65. Sasa haya ndiyo mapato tunayoyatafuta, kwa nini Serikali inapata kigugumizi kukokotoa fedha hizo ambazo zinaweza kutusaidia kuondokana na fedheha hii ya kuwa wategemezi mwaka hadi mwaka na Mwenyezi Mungu katujalia rasilimali nyingi kama vile dhahabu na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, aidha, ukizungumzia sehemu ya kodi ambayo ingeweza kwenda kwenye Serikali za Mitaa, kwenye Kamati tulisema kwamba badala ya kuwa na ukomo wa laki mbili tu sasa watumie Sheria ya Serikali za Mitaa ambapo Serikali za Mitaa haziwezi kukokotoa kama asilimia 0.3 ya mapato ya dhahabu. Kwa hali halisi iliyopo sasa hivi ambapo dhahabu ni karibu dola 1000 au 965 hizi ni fedha nyingi sana, mimi nina hakika hizo Halmashauri zingeweza zikapata zaidi ya shilingi bilioni nne kutokana tu na mapato ya madini lakini leo hakuna. Bado nauliza, ni kwa nini Serikali haiendi kwa kasi inayostahili na inatuweka katika hali hii ya utegemezi mwaka hadi mwaka?

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, katika mapendekezo pia tulisema kwamba mali yetu iliyopo hapa inauzwa kwa makampuni ya nje na mara nyingine ni kwa urahisi tu. Hivi sasa ndugu zangu ambao ni wa Mtwara naambiwa Artimus yenyewe sasa inauza gesi yetu kwa dola milioni 10.6, *which is over 12 billion*, watu wa Mtwara watapata kiasi gani katika uuzaji huu? Katika Kamati tulisema wale watu wanaouziana hisa zao na msingi wake ni mahali iliyo Tanzania basi sisi pia tuweze kupata kitu chochote. Sasa hapa itakuwa ni kama mahali pa kutafuta lakini ukishapata utajiri siyo Tanzania bali kule nje. Hili tumeleta

pendekezo la kugeuza Sheria za Kodi, ili tuweze kukokotoa pesa kwa mfano kama hiyo 10.6 *million dollars*, ni hela nyingi sana ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anahitaji ili kuweza kuweka katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeona nizungumzie hili ili kuonyesha masikitiko yetu pamoja na kuahidiwa kwamba Sheria itakuja mwishoni mwa mwaka huu, ni muda mrefu mno. Mambo haya ya mapato ni kupata hiyo fedha sasa kwa sababu hiyo fedha hatuhitaji mwaka kesho tunahitaji sasa hivi kwa sababu kuna mambo mengi ambayo tunapaswa kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, kwa muda wa miaka mingi tukiangalia vitabu vya Mwadui kila mwaka hakuna pesa, kampuni imefanya kazi kwa hasara. Tumeambiwa kwamba Mwadui sasa imeuzwa lakini sisi tunajuliza kwa nini Serikali haikuwekeza kwa kupitia *STAMICO* badala yake imeza kwa watu wa nje na nimeambiwa kwamba ile kampuni ambayo ilinunua kwa *quarter* ya kwanza tu kwa miezi minne, imetengeneza faida lukuki. Hivi kwa nini Serikali basi haiundi hata Tume kuchunguza kama wale waliokuwepo mwanzoni walikuwa wanatudanganya? Tumepoteza fedha kiasi gani na kwa nini hizo fedha tusizikokotoe ili tuzilete katika mapato ya Serikali na sisi tukaweza kufanya maendeleo kwa kutumia fedha ya kwetu?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri, aliambie Bunge hili hatma ya Mwadui iko wapi? Nani kanunua? Tumepata fedha kiasi gani? Kwa nini sisi hatukutumia *STAMICO* wakati katika ile miKataba tuliyoona, nafasi ya kwanza ilitolewa kwa Serikali kuweza kununua hizo hisa? Ni kwa nini basi Serikali haikuchangamkia hisa hizo na sisi sasa labda tungekuwa angalau nusu kwa nusu kwa madini yetu ya kule Mwadui?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, *TANSORT* iko London, sasa pamoja na utaratibu uliopo sasa ambapo tumepata mwekezaji mpya hatma ya *TANSORT* ni nini? Ninapenda kupata jibu kwa sababu pale kuna watu wanakula pesa ya Serikali na sisi tunataka kupunguza matumizi ili chochote kinachobaki tuweze tukakutumia kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninalotaka kuzungumzia, ni lile linalohusu mambo ya kuagiza *petrol* kutoka nje kwa wingi. Najua jambo hili limezungumzwa sana katika *corridors* au katika sehemu mbalimbali za Bunge na kuna watu wengi ambao wanatoa ushawishi mkubwa sana kwamba Serikali isielekee katika utaratibu huu. Mimi nafikiri kwa nishati muhimu kama *petrol* kuliacha mikononi mwa watu binafsi tu ili waweze kuleta *petrol* wanavyopenda, ni hatari sana kwa usalama wa Taifa letu. Mimi naona Serikali inapaswa kuwa na mkono wake kupitia Shirika lake la *TPDC* ili kuhakikisha kwamba tuna uhakika wa nishati hii muhimu ambayo tunahitaji kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hivyo tu, ukiangalia takwimu za haraka haraka kati ya ambazo zimetokea, inaonekana wazi kwanza kuna unafuu wa zaidi ya shilingi bilioni 78 kwa kuagiza kwa wingi na hizi ni fedha ambazo tunapeleka nje, sisi tunapaswa kupata fedha kutoka nje kwa kuuza pamba na mazao mbalimbali tunazichukua hizi shilingi bilioni 78 tunapeleka nje. Kama tunaweza tukapata unafuu wa namna hiyo, kwa nini utaratibu huu usifanyike?

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, aidha tunaambiwa katika sehemu mbalimbali ambazo watu wamefanya utafiti kwamba kodi ambayo inafichwa kwa watu mbalimbali wanaoagiza mafuta na kama utaratibu ungewekwa, mimi nina hakika tungeweza tukapata mapato ya ziada ya zaidi ya shilingi bilioni 266. Shilingi bilioni 266 tulizihitaji jana ili

tuweze kujenga madaraja, ili tupeleke fedha kwa watoto wa shule ambao hawana vitabu na ili tuweze kuwafadhili watoto wengi zaidi katika Vyuo Vikuu. Kama tunaweza tukapata unafuu huo, naishauri Serikali iachane na *lobbyists* hawa, iachane na watu ambao wanaweka ushawishi mbalimbali bali iendelee na utaratibu huo ili nchi hii iweze kupata mapato ambayo yanastahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa sababu nina dakika moja, nataka kuliambia Bunge hili, jana nilikuwa na mtihani mgumu sana kutetea Mfuko wa Jimbo. Nataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, hakuna mambo ya Bunge kama hili liambiwe na mtu yeyote wa nje au wa ndani asiyekuwa humu ndani kwamba Bunge hili litunge Sheria gani. Hii ni haki yetu ya Kikatiba, tuendelee kwa nguvu zote, wanaolia walie tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Umeme ni nishati muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Serikali inasema nini licha ya *Power Master Plan* kutoa kipaumbele na kuweka umuhimu wa pekee katika ujenzi wa Mradi wa *Stiegler's Gorge* na Umeme wa Upepo katika Vijiji vya Kititimo na Kisesida, Singida na Njombe ambayo yote kwa pamoja ikitekelezwa mapema, itaitoa nchi katika mgao wa mara kwa mara; na isitoshe miradi ya upepo haina *Capacity Charge* na *Low Maintenance Costs*. Ni kwa nini Serikali inasita kuwekeza katika miradi hii muhimu, hasa wakati huu inapofikiria ku-review *power master plan*?

Tangu tulipopitisha Mpango na Mfuko wa *Rural Electrification* ni zaidi ya miaka kadhaa sasa:-

- (i) Je, Serikali inaweza kueleza hadi sasa Mfuko huo una fedha kiasi gani?
- (ii) Kama Mfuko huo haujaanza ni kwa nini haujaanza?
- (iii) Kama Mfuko umeanza ni Wilaya zipi hadi sasa zimenufaika na Mfuko huo na Wilaya ya Karatu ambapo vijiji vingi kama vile Tarafa nzima ya Eyasi, Tarafa ya Mbulumbulu haina umeme kabisa; imepata au imetengewa kiasi gani?

Kwa nini TANESCO imeacha kutuma bill kwa wateja wake hadi wateja wazifuate, jambo ambalo ni usumbufu mkubwa kwa wateja. Je ni tatizo au sababu gani zinaifanya TANESCO kutotuma bills kama zamani na wakati huo huo ina utaratibu wa kukata umeme bila hata kutuma bills hizo kwa anuani zilizoko, jambo ambalo ni ukiukwaji wa mkataba kati ya mteja na TANESCO?

**COAL MINE:** Kwa kuwa Serikali imekiri kuwa, kampuni binafsi ya Anbem iliyokuwa inamilikiwa na Rais Mstaafu, ilijitoka au iliondolewa 10 Januari, 2005, siku 13 tangu kuanzishwa kwa *Tanpower Resources*:-

- (i) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hatua hiyo ya Rais Mstaafu na Waziri wake (*Sitting Minister*) kuwa na hisa katika kampuni ya umma, ambayo kwa mujibu wa maadili ya umma, walitakiwa kuilinda na kuisimamia na hasa kwa kuzingatia kauli ya Waziri

huyo ndani ya Bunge, kuhusu mchakato wa ubinafsishaji wa kampuni hiyo, jambo ambalo sasa ni dhahiri kabisa kuwa alilipotosha/kulidanganya Bunge?

(ii) Waziri anasema nini kuhusu \$7,000,000 zilizokopeshwa kwa Kampuni ya Kiwira kwa dhamana ya asilimia 100 na Serikali kutoka Mfuko wa NSSF ambazo muda wa kulipa umepita na riba inazidi kuongezeka?

Serikali itoe tamko rasmi wawekezaji wana hisa kiasi gani na Serikali yetu imewekeza kiasi gani kwenye Mradi wa SONGAS? *Capacity Charge* kwa Mradi huu ni kiasi gani na katika miaka 20 tutakuwa tumelipa kiasi gani kwa *capacity charge*?

Serikali ya Tanzania, imedhamini (*guarantee*) mikopo kiasi gani toka vyombo mbalimbali vya fedha vya ndani na nje vya fedha kwa SONGAS?

Serikali ina nafasi ipi katika Menejimenti ya SONGAS kwa sasa?

Je, Mkataba wa SONGAS unatazamwa upya?

Mheshimiwa Spika, wajibu wa Bunge ni kuisimamia Serikali kwa niaba ya Wananchi. Ni imani yangu kuwa, maswali haya yatajibiwa kikamilifu ili Watanzania wawe na uhakika na usalama wa rasilimali zao na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote, kwa kuandaa hotuba nzuri.

Napongeza Mpango wa kuendeleza umeme kama ulivyoainishwa wakati wa semina ya EWURA. Kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, Mpango huo siyo msahafu, unaweza kubadilishwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Naomba kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu, Wizara iangalie na itushauri *way forward* ili umeme utakaopatikana Mjini Kibondo, baada ya *generators* kuwasili, uvutwe hadi Mji Mdogo wa Kakonko (48km). Kwa hakika, Barabara ya Nyakanazi – Kigoma ikijengwa na umeme ukipatikana, maendeleo ya uchumi katika Jimbo la Buyungu yataongezeka kwa kasi kubwa.

Naomba ushauri katika jambo hili; je, kwa uhakika *generators* za Kibondo zitapatikana lini? Upatikanaji wa maji katika maeneo mengi yanayozunguka Maziwa kama Miji ya Kigoma na Mwanza, unategemea upatikanaji wa umeme. Kwa mfano, pamoja na miundombinu ya maji iliyopo Mjini Kigoma, upatikanaji wa umeme unaweza kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 38 hadi 75. Mchakato wa ununuzi wa *generators* za Kigoma na Kibondo, ingefaa upewe kipaumbele.

Kuna dalili kwamba, baadhi ya madini hasa dhahabu, yanapatikana katika Vijiji vya Nyakayenzi na Muhange katika Wilaya ya Kibondo. Kinachoonekana ni uchimbaji holela, usiotanguliwa na utafiti wa kijiolojia. Tupeni ushauri ili wachimbaji wadogo watumie maarifa.

Chokaa ina matumizi mengi yakiwemo ujenzi, kutengeneza mbolea, chaki, *Plustic of Paris – PoP*, kusafishia ngozi na kadhalika. Madini hayo yanapatikana kwa wingi katika Wilaya ya Kibondo. Uchimbaji wa chokaa na biashara yake, inaweza kuongeza ujasiriamali

kwa vijana wengi. Naomba Wizara itoe ushauri wa kitaalamu *on way forward*. Vile vile Sera ya Biofuel iharakishwe.

Naipongeza Wizara kwa hatua mahususi inazoendelea kuchukua katika mambo mengi yenye maslahi ya Kitaifa, hususan suala la Mgodhi wa Kiwira, uendelezaji wa Gesi ya Songosongo, Mikataba ya Umeme na mengine mengi. Mungu awatie nguvu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yake nzima ya Wataalamu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa bajeti nzuri iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, napenda kujua ni lini Wareta, Dirma na Simbay, watapatiwa umeme? Mheshimiwa Waziri atakumbuka kuwa, nilimwomba maeneo hayo yapate umeme kutokana na kuwa karibu na *line* ya umeme inakopita kuna Kituo cha Afya, Shule ya Sekondari, pamoja na taasisi nyingine muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kupatiwa umeme eno hilo, kutasukuma maendeleo ya kiuchumi ya uhakika wa upatikanaji wa huduma za kijamii.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Timu yao yote, kwa kazi nzuri na hotuba inayoleta matumaini makubwa kwa sekta mbalimbali. Kwanza, naomba ieleweke mimi ni mdau wa Sekta ya Mafuta, nina vituo vya mafuta Morogoro na Chalinze; hivyo Sekta hii ninaiielewa vyema.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mafuta ni nyeti sana katika nchi yoyote duniani; inabeba nguvu kubwa ya uchumi, pia inachangia Pato la Taifa; hivyo basi, eneo hili linahitaji kuwekewa uangalizi wa hali ya juu. Naomba kuwapongeza wote wanaofanya jitihada mbalimbali za kusimamia eneo hili, wakiwemo Wataalam wa Wizara, EWURA, TRA, Jeshi la Polisi na Taasisi nyingine, bado kazi iliyopo mbele yao ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa ni kushikamana kwa umoja na kuwa makini zaidi kwa eneo lote la Sekta ya Mafuta. Naomba kutamka kuwa, naipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla, kwa mpango wa kuamua kusimamia Sekta hii na kuleta mpango wa chombo kimoja kuleta mafuta (*Bulk*). Huo ni mpango mzuri sana, nina imani utasaidia kwa kiwango kikubwa, kudhibiti udanganyifu na utaokoa mapato mengi yanayopotea kutokana na wanaoleta mafuta kutoka nje ya nchi kutokuwa waaminifu. Udanganyifu mkubwa umetawala katika eneo hili, ushauri wangu usimamizi wa karibu unahitajika katika eneo hilo. Naunga mkono hilo.

Mheshimiwa Spika, bado eneo hili lina mianya mingi inayohitaji kuangaliwa na kusimamiwa hususan katika eneo la Bandari, Maghala (*Depots*), Usafirishaji, *Transist – Goods, Filing Stations* na *Local Transporter*, ambao wengi wao ni madereva wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, mapato mengi hupotea kila siku kutokana na uchanganyaji wa mafuta ya taa na *diesel*; eneo hili limetawaliwa na ujanja wa hali ya juu. Pamoja na kazi nzuri

ya EWURA na TRA, lakini bado ipo kazi ya ziada inahitajika kufanywa tena kwa misingi ya haki na uwazi.

Mheshimiwa Spika, suala la *Bulk*, nashauri lisiwe na mjadala, hili ni jambo la nchi na litaokoa mabilioni ya fedha. Naunga mkono, ushauri wangu ni utekelezaji wake usimamimiwe na Serikali kupitia vyombo vyake. Hofu yangu ni ujanja uliopo miongoni mwa makampuni yanayoagiza mafuta kuwa na watu wao katika vyombo vya usimamizi wa Sekta hii. Suala kubwa katika zoezi hili ni kuwa na akiba ya Taifa ya mafuta na *stock* kukaguliwa kila mara. Pia vyombo vyote vitakavyosimamia eneo hili, kupata uzoefu wa wenzetu katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, wananchi vijijini wamefarijika sana na suala la Miradi ya Umeme inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani, chini ya Mpango wa MCC, kuanza kutekelezwa kwa hatua za awali.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Mkoa wa Morogoro, hususan Wilaya ya Mvomero, Miradi yote ya MCC ianze kutekelezwa mapema, hasa kipindi hiki cha kiangazi katika maeneo ya vijijini ili kuepuka usumbufu wa barabara katika kipindi cha masika.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri na kazi nzuri anayofanya, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima na kwa ushirikiano mzuri mnaoupata kutoka kwa Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara ya Nishati na Madini, naomba Jimbo langu la Temeke, nyumba zote za Wananchi wa Temeke wafungiwe luku, kwa sababu imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wangu kuletewa bill kubwa na umeme wenyewe kupatikana kwa shida na sasa kuna Kampuni ya Yono inapita kuwatishia wananchi wangu kuuza nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili nilichangia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu na Waziri alinieleza nitapata majibu katika Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na upendo walionao kwako, Wananchi wangu wa Jimbo la Temeke, watafurahi wakisikia tamko lako wakati wa majumuisho ya bajeti yako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Naomba kuwasilisha.

**MHE. OMAR SHEHA MUSSA:** Namshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, kwa hotuba yake ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha 2009/2010. Ninaamini hotuba hiyo imetayarishwa kwa mashirikiano ya hali ya juu ya Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu utakuwa kwa maandishi, kwa sababu yale ninayotaka kuyazungumza ni nyeti sana ili kujaribu kuweka uhusiano mzuri baina ya Bunge na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwenye eneo la Utafiti na Uchimbaji wa Mafuta, ikiwa ni suala la Muungano kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotawala hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, nilisikia kwenye vyombo vya habari kuwa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imeamua suala la mafuta, utafiti na uchimbaji wake, kulitoa kwenye



orodha wa mambo ya Muungano na kwamba, mikataba yote iliyokwishatiwa sahihi katika Jamhuri ya Muungano ni batili na haitakubaliwa kule Zanzibar kwa mafuta au utafiti utakaofanyika huko (hasa Block 9 na 12), kama ilivyokwisha saina na *Tanzania Petroleum Development Company (TPDC)*, yaani *Production Sharing Agreements (PSAs)*, zilizosaina wa Tanzania Bara ni batili kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho cha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na kwamba, Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pekee, hamna mamlaka ya kufanya hivyo bila ya kuleta jambo hilo mbele ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwamba, kwa kufanya hivyo, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, akiwa na dhamana ya Muungano upande wa Zanzibar, anapaswa kujua hayo yaliyofanyika kuwa ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano juu ya suala la mafuta na gesi asilia. Tamko la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mbele ya Baraza la Wawakilishi kama lilivyotolewa na Waziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, anayehusika na Nishati na Madini; ni uvunjaji wa Katiba ya Jamhuri.

Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke tu kuwa, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba, kwa Mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri (Kifungu kinchaohusika), bado sula la mafuta ghafi na gesi asilia ni mambo ya Muungano; na kwamba, Tamko la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mbele ya Kikao cha Bajeti cha Baraza la Wawakilishi (2009/2010) ni makosa yasiyoweza kusamehewa, wala kuachiliwa hivi hivi tu. Wanaohusika wawajibishwe kwa Mujibu wa Sheria za Nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, akakumbuke uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, juu ya jambo hilo katika Serikali ya Awamu ya Tano, yeye akiwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi wakati huo, akishikilia wadhifa wa Uwaziri mnamo miaka ya (1990's – Mid). Wakati huo iliamuliwa kuwa ni vyema pande mbili za Muungano, zikae na kuelewana juu ya ugawaji wa mapato yatokanayo na rasilimali hiyo na siyo kulitoa jambo hilo kwenye Muungano.

Mheshimiwa Spika, sasa inakuwaje kuwe na wazo jipya na kuvuruga nchi ya Tanzania kipindi hiki, hasa kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu ujao mwaka ujao wa 2010. Je, Rais wa Zanzibar kama mbia wa Muungano aeleweke vipi; amechoka na Muungano au la; au anataka kufunga Mikataba ya Mafuta Zanzibar kabla hajamaliza muda wake ifikapo Oktoba, 2010; na kwa lengo gani? Afaidike yeye na wale walioko madarakani hivi sasa, ambapo wanatoa kauli zisizofaa dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Serikali ambayo inajali sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kuisaidia kila mwezi kuipatia gawio la asilimia nne na nusu la misaada na *Government Budget/Grants Support (GBS)*, fedha ambazo hazipungui Sh. 3.0 bilioni kila mwezi, tokea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Awamu ya Sita, iliyoko madarakani miaka tisa iliyopita. Je, kwa kupewa fedha hizo kila mwezi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaibiwa na Serikali ya Muungano Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikuwa na mawazo hayo, tokea awali walipoingia madarakani mwaka 2000, kwa nini wasikae na Serikali ya Muungano Tanzania (kwanza), wakaelewana awali, kuliko hivi sasa kuleta vurugu za kisiasa Visiwani Tanzania kwa jumla. Leo iweje Wawakilishi wa Chama Tawala na wale wa Chama cha Upinzani kule Zanzibar, wakubaliane juu ya jambo nyeti kama hilo, ambapo historia ya Zanzibar haioneshi hivyo? Kuna nini kilichopangwa na Watawala wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, namalizia hapo na naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nini hatima ya umeme Mwandoya (Kisesa), Line ya Nghoboko – Semu – Mbaragane – Lubiga Mwandoya – Igobe?

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mahitaji ya nishati ni muhimu sana, tatizo ni kipaumbele, lazima Serikali sasa itoe migao ya pesa kwa maendeleo kwa *priorities*. Wizara hii itengewe trilion mbili iweze kumaliza ruzuku 60% ya mahitaji yake. Wabunge waache ubinafsi wa kutaka maendeleo madogo madogo kwenye majimbo yao; tuwe na *national interest* kwanza. Tutumie *maximum resources* zetu, tuuze gas, tuwekeze kwa akiba zetu si kutegemea wahisani.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara hii na Taasisi zake, kwa Hotuba nzuri sana. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Lushoto hasa Tarafa ya Mlola – Kata za Ngwelo, Malibwi, Mlola na Makanya, napenda kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri William Ngeleja na Mheshimiwa Naibu Waziri Adam Malima, kwa kuelekeza mchakato wa kufikisha umeme katika maeneo hayo kwa kujenga njia ya KV 33 kutoka Nyasa (Lushoto – Mlalo Line) kupitia Hemtoye, Mshale Makole ambapo tawi moja litafika Ngwelo na Lingine Mlola.

Njia ya pili ya KV 11 itaanzia Kwemakame hadi Malibwi na Kwekanga. Nampongeza sana Meneja wa TANESCO Lushoto, Ndugu Saidi, kwa kukamilisha haraka *Preliminary Survey* ya Mradi huu na kuwasilisha Wizarani ndani ya wakati.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, awape kauli ya faraja wananchi wa maeneo hayo; ni lini Mradi huu utanza kutekelezwa. Gare Kizara kuna watu wengi sana wametandaza nyaya kwenye majumba yao. Umeme uko jirani Gare Mission na au minara ya simu Kwemashai, labda nguzo kumi hivi. Naomba sana wafikishiwe umeme hawa na wenzao wa Mshizii, Miego, Kireti, Ntambwe, Handei, Kwaboli, na Ubiri Mission.

Mheshimiwa Spika, Umeme wa *Minihydro* utakuwa mkombozi kwa vijiji vingi Lushoto, ambako *grid* itakuwa ghali na ngumu. Je, Serikali iko tayari kufanya *survey design* na kujenga mitambo hiyo ikianza Kijiji cha Mdando?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Jaji Mark Bomani na mapendekezo yake yamepuuzwa na Serikali.

Kufutwa kwa GN 99 inafuta misamaha; kwa nini makampuni bado yanaendelea na misamaha?

Utekelezaji wa maagizo ya Waziri Mkuu kuhusu eneo la Mgusu limetekelezwaje?

Nini hatima ya Wananchi wa Lusu kuhusu fidia yao ambayo haikupatikana tangu mwaka 1998? Serikali iunde Kamati Maalum kushughulikia suala hili.

Wizara imeomba shilingi bilioni 226.9 wakati Hazina imetenga shilingi bilioni 285.5; kwa nini?

PSMP kununua umeme kutoka Ethiopia; kwa nini tusitumie *uranium* kuzalisha umeme? PSMP ina upungufu mkubwa (umetajwa kwenye hotuba).

Shilingi 50,000,000 hupotea Kiwira. Shilingi bilioni 17 za Serikali zimetolewa, lakini mwenye hisa kubwa hajatoa. Mitambo inang'olewa na kuuzwa!

Serikali imewekeza SONGAS 85% ya hisa lakini siyo mmiliki na Wawekezaji 15%; kwa nini?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wa Wizara na Mashirika yaliyoko chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri mnayoifanya maeneo mengine. Bila kuwa mnafiki, nawalaumu sana kwa kusahau kwamba, mnatakiwa kutoa huduma ya umeme Iramba Mashariki kama mnavyotoa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na Mradi wa Umeme Mtinko, Nkangi, Iambi, Nduguti, ambao hata hivyo Wizara yako haikutekeleza kwa muda mrefu mpaka Rais Mkapa alipokuwa bado yuko madarakani, akalazimisha Mradi huo uanze kutekelezwa na kweli ukatekelezwa mpaka Nkangi. Hata hivyo, kwenye huo Mradi kulikuwa na *component* ya kuweka *Transformer* Kijiji cha Singa. Kwa masikitiko makubwa, pamoja na ahadi za Mheshimiwa Waziri, huu ni mwaka wa nne *transformer* haijawekwa Singa. Namshauri sasa atekeleze ahadi yake. Pia akumbuke ahadi ya kutoa umeme toka Nkungi kwenda Iambi hatimaye Nduguti, Makao Makuu ya Jimbo, kama Serikali ilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kupeleka umeme Shule ya Sekondari Iguguno, kilomita mbili toka *line* inayopita Shule ya Sekondari Tumuli, kilomita moja toka *line* inakopita. Chuo cha Maendeleo Msingi, kilomita nne toka *line* ya umeme inakopita, mpaka leo kazi hiyo bado haijafanyika. Pamoja na wewe na Naibu Waziri, kila mara kuniahidi, nawaamini sana na hamfanani na kusema uongo; hebu tekelezeni hizo ahadi.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwezi wa sita, nimekuwa nawaomba mnapatie utaratibu au *action plan* ya kupeleka umeme Iramba ya Mashariki, mpaka leo sijapata. Kwa mchango huu, naomba niwajulishe maeneo ambayo sisi wa Iramba Mashariki tungependa umeme usambazwe: (a) Kinyangiri, Iambi na Nduguti; (b) Iguguno na Kingangiri; (c) Nkungi, Nkalakala, Kinyambuli, Nkinto na Matongo; (d) Nkungi, Ntwanga na Kiderata; (e) Kinampanda na Msingi; (h) Kiomboi, Kidaru na Ibagu. Haya ndiyo yawe maeneo ya kuanzia.

Mheshimiwa Spika, pia tunakuomba sana, endapo kuna makampuni yanakuja kwako kwa lengo la kutaka maeneo ya kuzalisha umeme wa upepo. Nakuomba sana waelekeze yaje Iramba Mashariki, tunayo maeneo ya kutosha mazuri na yana upepo wa kutosha kama vile Kikhonda, Kata ya Kinyangiri; Senen na Lukomo, Kata ya Gumanga; Nkalakala na Kidarafu, Kata ya Mwanga; Mwangeza na Dominika, Kata ya Mwangeza; Mpambala na Ibagu Kata za Ibagana; Mpambala na Gumanya.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu ambao kwa bahati umeme ulishafika, bado wanalalamikia sana gharama za nguzo na gharama za kuvuta na kuingiza umeme kwenye nyumba zao. Wanaomba gharama hizo zipunguzwe ili wananchi wengi waweze kuvuta umeme.

Mheshimiwa Spika nimalizie kwa kuomba tena, *transformer* ya umeme ifungwe Nkungi, umeme uende Shule za Sekondari za Iguguno na Tumuli. Vile vile umeme uende Chuo cha Maendeleo Msingi na utoke Nkungi uende Iambi na Nduguti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa michango yangu, yenye kilio cha Wananchi wa Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera una rasilimali nyingi ikiwemo mito isiyokauka, yenye kuweza kutuzalishia umeme wa kutosha; ni lini tutaondokana na kutumia umeme wa nje wa Uganda?

Siku mashetani ya Waganda yakiamka; je, tutapata umeme? Je, Serikali huwa inashindwa nini kufanya utafiti au kutafuta wataalamu wa kuvuta umeme? Je, ni lini Wizara italetta punguzo kwa wananchi waweze kujikomboa na kufaidika?

Wizara hii ina mikakati gani kuhusu nguzo? Miti ya kutengeneza nguzo tulime wenyewe kuliko kutoa nje, hasa Kagera miti hiyo inakubali sana.

Mheshimiwa Spika, tuache mchezo wa kudanganya tutawaletea umeme hasa kwenye uchaguzi kutandaza miti au nguzo kwamba, mtapata umeme hivi karibuni, uchaguzi ukiisha ndio kwa heri.

Matatizo ya mita; kuna kero kubwa sana kwenye makato tunayokatwa kama inavyoitwa *service line*. Wanafanya mchezo mchafu, makato yao ni wizi mtupu. Je, mmeshafanya utafiti kuyabaini matatizo hayo?

Tutumie makaa ya mawe na chuma cha Liganga, tuweze kufaidika na madini. Tanzania tuna rasilimali za madini nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, hatuna ulinzi wala mipangilio, ndio maana wawekezaji wanaendelea kuchuma tu wakati sisi tunalia uchumi umeshuka. Kwa mfano, hawa tuliowaleta wanashindwa kutengeneza hata barabara na hospitali, kuwasaidia wananchi ambao wanayalinda madini hayo. Ukiangalia, ndio masikini wa mwisho, kazi ni kuwanyesha maji machafu, matokeo yake wananyonyoka nywele. Ninao mfano wa Geita (GGM). Nilitafakari mwenyewe na kuona hiyo ndio faida ya wawekezaji na kuwaramba risasi wananchi. Umeme umekuwa kero kwa wananchi, wanaona unapita karibu; uwezo wao ni mdogo na gharama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mali hiyo imelala, hatimaye kama kamati tulikwenda kuwaambia baada ya mwaka mmoja. Je, hatima yake ni lini? Wananchi walioko karibu na wanakochimba gesi ya Mnazi Bay, hawana umeme, tuliambiwa wanaletewa *wiring* ambazo zinahimili kwenye nyumba zao za udongo. Je, tayari wameshapelekewa na kufungiwa? Je, wamewapatia elimu?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri wananchi wazowee matumizi ya gesi ili waondokane na kukata miti ovyo. Mheshimiwa Rais, anaposafiri na Mawaziri kwenda kwenye ziara, kwa nini wasiwe na mikakati ya kuleta zana za wachimbaji kuwakopesha kuliko kuwapa pesa zaitwazo JK ambao zina migogoro?

Mheshimiwa Spika, mashine za kuchimbia ni muhimu kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, nawatakia bajeti njema, Mungu awatangulie maana Wizara ni nzito.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye taarifa muhimu za msingi kuhusu Sekta ya Nishati na Madini. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa jitihada zao za kuboresha huduma za Nishati na Madini nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kauli yake ya tarehe 23 Julai, 2009, kuhusu hali ya Mgodhi wa Makaa ya Mawe Kiwira. Kama nilivyoeleza katika mchango wangu wa maandishi kwa Wizara hii wakati wa Bajeti, mwaka jana, Wilaya ya Ileje ni mdau mkubwa wa mgodi huo. Kufungwa kwa Mgodhi huo, ilikuwa ni pigo kubwa sana kwa Wananchi wa Ileje na Wilaya ya Kyela na Rungwe. Kauli ya Serikali, inaleta matumaini mapya kwa wananchi na maeneo hayo. Pamoja na kupongeza hatua za Serikali kuuchukua Mgodhi huo na kushughulikia malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa Mgodhi huo, naomba Serikali izingatie na kushughulikia changamoto zifuatazo:-

(a) Mgodhi wa Kiwira uko Wilaya ya Ileje kwa sehemu kubwa. Kwa hiyo, Mgodhi huo unawajibika kutoa mchango kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kwa mujibu wa sheria. Hadi sasa, kuna limbikizo la deni la karibu shilingi milion kumi. Naomba Wizara izingatie deni hili na kulilipa maana ni la muda mrefu.

(b) Mimi nikiwa Mwenyekiti wa Bonde la Maji la Ziwa Nyasa, linaudai Mgodhi huo karibu shilingi milion kumi na mbili, kama malimbikizo ya ankara za matumizi ya maji katika Mgodhi huo. Kwa hiyo, naomba Wizara izingatie deni hili na kulilipa ili Bonde la Maji la Ziwa Nyasa lisije likalazimika kufuta kibali cha matumizi ya maji kwa Mgodhi huo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Wakala wa Nishati Vijijini, hazijaeleweka sawasawa. Ningependa kufahamishwa mipango na mkakati wa usambazaji umeme vijijini katika Wilaya ya Ileje, ikiwa ni pamoja na uainishaji wa vyanzo vya umeme ndani ya Wilaya (mfano maporomoko ya maji katika Kijiji cha Lusulala, Kata ya Sange, Ileje). Haja ipo kwa Wakala kujitangaza zaidi na kushirikiana na Viongozi katika ngazi ya Wilaya ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mdogo, naunga mkono hoja hii na nawatakia mafanikio mema.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nawapongeza sana Timu ya Mawaziri hawa Vijana, kwa kazi nzuri wanayoifanya na changamoto na matatizo makubwa wanayokabiliana nayo katika Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo, naomba nitoe maoni yangu kama ifuatavyo :-

Wilaya ya Tunduru iko Ukanda wa Kusini kijiografia, lakini kwa bahati mbaya, imewekwa Ukanda wa Kusini Magharibi kiutawala. Hali hizi mbili, Tunduru imewekwa katika mazingira ya kutonufaika na miradi inayoelekezwa Ukanda wa Kusini na ile ya Ukanda wa Kusini Magharibi.

Mradi wa umeme wa gesi ya Mnazi Bay umeelekezwa uhudumie Mikoa ya Kusini, yaani Lindi na Mtwara. Tunduru haipo kwa kuwa licha ya kuwa Kusini kijiografia, lakini iko Kusini Magharibi kiutawala (Ruvuma). Hata hivyo, Mradi wa Umeme wa Grid ya Taifa unaishia Namtumbo; Tunduru pia haikuhusishwa kwenye Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi, ilielezwa kuwa, umeme wa Mnazi Bay utaunganishwa kwenye Grid ya Taifa kupitia Namtumbo, lakini hivi karibuni tumejulishwa kuwa umeme huo utaunganishwa kwenye Grid ya Taifa kupitia Mkoa wa Pwani/Dar es Salaam. Kama wazo la mwisho ndilo litakalotekelezwa, Wilaya ya Tunduru itakuwa imetelekezwa kabisa na kasi ya maendeleo iliyopo sasa Wilayani hapo itafifia.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, itekeleze wazo la awali la kuiunganisha Grid ya Taifa umeme wa Mtwara huko Namtumbo, ukipitia Wilayani Tunduru. Tunduru ndiyo Wilaya iliyo katikati ya Mtwara Corridor, inapanuka kwa kasi kubwa sana na wawekezaji wanazidi kumiminika siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni lini Shirika la TANESCO litawalipa wananchi waliopitiwa na Mradi wa Umeme uendao Kigamboni. Uthamini wa mali za wananchi hawa, ulifanywa mwaka 2005, leo takriban zaidi ya miaka minne, bado hawajakamilishiwa malipo. Wanaishi katika mazingira magumu, tangu mwaka huo wameambiwa wasifanye marekebisho yoyote wala kuyaendeleza. Hawa ni wapiga kura, kutowalipa mapema kunaamanisha hasira zao ziangukie Chama Tawala. Hili haliwezi kukubalika hata kidogo; Waziri atueleze TANESCO watalipa lini?

Mheshimiwa Spika, takriban mara nne, nimekwenda TANESCO Makao Makuu ili kupeleka mrejesho kwa Director wa TANESCO, lakini mara zote hakuwa tayari kuonwa nami na kutoa maagizo niende nikamwone mtu wake wa chini. Hali hii haifurahishi, sisi Wabunge tunawawakilisha Wananchi na nyakati nyingine tunaweza kuwa na hoja mahususi, ambazo ni vyema azipokee yeye kwanza, ndiyo azielekeze kwa anayeona anafaa. Kwa kweli sikufurahishwa kabisa na hili.

**MHE. ZABEIN M. MHIJA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote, kwa kuandaa bajeti nzuri, yenye malengo yanayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Uk.103, katika orodha ya vijiji ambavyo vimo katika Miradi inayofadhiliwa na MCC, ambayo inatekelezwa na TANESCO, Kijiji cha Kingale – Gereza la King'ang'a hakikuorodheshwa. Tafadhali, naomba maelezo kwa niaba ya Wananchi wa Kijiji hicho kwa nini hakikuorodheshwa?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kheri katika upitishaji na utekelezaji mwema.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba hii

yenye kuonesha mwelekeo na kazi zitakazofanyika katika bajeti ya 2009 – 2010. Aidha, nawapongeza kwa jinsi wanavyosimamia utendaji wa kazi za Wizara na kazi zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Bahi kutoka Dodoma, umekwama na haujafika. Naomba Serikali itoe maelezo kwa nini umeme uliopangwa kufika katika Vijiji vya Wilaya ya Kondoa ikiwepo Pahi na vingine mpaka sasa haujapelekwa?

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini Dodoma ni cha muda mrefu mpaka kinasuasua, kwani kinachukua wanafunzi wachache wakati tuna tatizo la watumishi wa fani hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua ni lini Chuo hiki kitapanuliwa na kuweza kuchukua wanafunzi wengi?

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna kipindi fulani kulipatikana madini ya dhahabu Nzuguni na wananchi wakachimba kwa muda mfupi na baadaye kusimama. Wananchi wa Dodoma, wangependa kujua ni kwa nini machimbo haya yalisimama wakati hotuba imeonesha Wananchi wa Nzuguni watapewa mafunzo ya uchimbaji wa madini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa zaidi ya miaka mitatu sasa, nimekuwa nikifuatilia juu ya tatizo la wachimbaji wadogo wadogo Mpanda na hata kumwomba Mheshimiwa Waziri, atembelee na kuongea na wachimbaji hao na kulipatia ufumbuzi suala lao. Aidha, maeneo ambayo yana madini na hadi sasa hayajawavutia wawekezaji wapimiwe na kumilikishwa viwanja hivyo na kupewa msaada wa vifaa ili kuwasaidia wachimbaji hawa wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, TANESCO ni Shirika kubwa lenye mtandao nchi nzima, lisilokuwa na ufanisi wa kujivunia. Pamoja na matatizo mengi ya TANESCO, nilikuwa nashauri ingekuwa vyema wakatoa mamlaka kamili katika Kanda kuliko ilivyo sasa kila kitu Makao Makuu; mafuta, vipuri na hata maamuzi ni lazima yatoke Dar es Salaam. Ili kuweza kuboresha utendaji kazi wa Shirika hili, kila Kanda ingejitegemea kwa rasilimali watu na vifaa na kuwa na mamlaka ya matumizi na ununuzi wa vifaa na kuendesha kwa kadiri ya mipango ya maendeleo ya kanda hiyo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo malalamiko juu ya ankara (bill) za umeme, hivyo kuondoa kadhia hii ni kuhakikisha mita za luku (*Prepaid*) zinasambazwa kwa kasi nchi nzima.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kulipongeza Shirika la Madini (STAMICO), kwa kazi nzuri wanazofanya kulikomboa Shirika hili, lakini Serikali iwaongezee fedha zaidi. Ningependa kujua ni lini Serikali itarejesha majengo yote 18 ya STAMICO? Hii italiwezesha Shirika kufanya kazi vizuri na kuimarisha mizania yao.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili likipata fedha za kutosha, tunaweza kupunguza malalamiko mengi yanayotolewa ya kupoteza fedha nyingi, kwa sababu mchanga hupelekwa nje kuchekechwa na sisi kama Watanzania, hatufahamu mchanga ule nje ya nchi pengine kuna madini mengine.

Mheshimiwa Spika, STAMICO ikiwezesha na madini yote yanayosafirishwa nje yakichakachuliwa hapa, Taifa litapata pato zaidi na ajira zitapatikana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Shirika la TPDC limejitahidi katika utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Kwa kuwa wanaagiza mafuta (wafanyabishara wa petrol/diesel), huwa wanaagiza mafuta kutoka nje kwa mtu mmoja mmoja na hii inapelekea wafanyabiashara hawa kutuuzia mafuta kwa bei ya juu. Hata bei za mafuta duniani zikishuka, lakini hapa kwetu kila kukicha bei za mafuta zinapanda bei tu?

Mheshimiwa Spika, Shirika hili liwezeshe ili liagize mafuta *in bulk*, halafu wafanyabiashara wanunue mafuta kutoka TPDC. Hii itakuwa na faida sana kwa watumiaji, bei itakuwa tayari imekuwa *controlled* na TPDC, hayatachanganywa. Hata hivyo, EWURA wanajitahidi ku-*control*, kwa ushauri wangu kuna umuhimu wa TPDC kuagiza mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa TIPER imebinafsiswa; je, TPDC wakileta mafuta watahifadhi wapi? Wakikodi kutoka TIPER bei hazitakuwa ghali hivyo hivyo? Nashauri TIPER irudishwe TPDC ili iweze kuhifadhi mafuta.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha bei za kuunganishiwa umeme ni ghali sana na sababu kubwa ni bei ya nguzo kuwa kubwa. Kwa nini TANESCO inanunua nguzo kutoka South Africa wakati tunazo huko Mbeya? Siyo hilo tu, pia TANESCO Arusha wanazalisha na wanatengeneza transformer na vifaa vingine vya umeme, lakini TANESCO bado wanaagiza vifaa hivyo nje ya nchi!

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Tanzanite One imekuwa ikiwadhalilisha Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Mererani kwa kuwapitisha kwenye mionzi kwa kuwavua nguo ili kuchekiwa kama wanaiba madini. Hii ni hatari sana kwa Watanzania wetu; hivi hiyo mionzi haitawaathiri wachimbaji hawa wanapovuliwa nguo?

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali isitishie mara moja, utumiaji huo wa mionzi unaofanywa na Tanzanite One na mtu ambaye hana ujuzi. Je, Serikali imefikia wapi kutokana na mapendekezo ya Jenerali Mboma ya kumaliza mgogoro wa mpaka kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo kule Mererani?

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu Serikali italetwa kwa dharura Ripoti ya Sumu huko North Mara. La sivyo, baada ya miaka michache ijayo, hatujui ni madhara kiasi gani watakayoyapata wakazi wa eneo lile. Tusijali pesa sana, tujali utu wa Watanzania wenzetu.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, kwa kupata nafasi ya kuichangia hoja hii. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Adam K. Malim (Mb), Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kushiriki kuandaa hotuba nzuri na mpango uliomo katika bajeti ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maandalizi mazuri yaliyoonekana katika bajeti hii na kazi nzuri ya Wizara hii, nina hoja zifuatazo, ambazo Mheshimiwa Waziri, namhitaji afafanue kwa kutoa maelezo katika Bunge lako Tukufu:-

Kuna uhaba mkubwa wa nguzo za umeme kwa miradi yote iliyotengewa fedha ili kusambaza umeme iliyoidhinishwa katika Jimbo la Mikumi. Kulikoni wakati nguzo zinatengenezwa nchini? Miradi ya Vijiji katika Kata za Mabwerekwere, Kilangali, Masanze,



Mikumi, Kidodi na Ruhembe (Wilaya ya Kilosa), vilivyopangwa kusambaziwa umeme na kazi ambayo ilikuwa imeanza kwa baadhi ya vijiji, sasa yote imesimama kutokana na uhaba wa nguzo za umeme na nyaya.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, aeleze nini chanzo cha uhaba mkubwa wa nguzo na nyanya? Kuna fununu zilizoenea kwamba, nguzo nyingi zinazozalishwa nchini (Mufindi), zinanunuliwa na Wakenya huku Tanzania inalazimika kuagiza nguzo kutoka Afrika ya Kusini. Je, hii ni kweli?

Mheshimiwa Spika, *Economics* za utaratibu huu ni za faida au hasara kwa Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, napenda Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini aeleze ni kwa jinsi gani atalimaliza tatizo la uhaba wa nguzo hizi ili miradi niliyoitaja ikamilike katika muda mfupi ujao?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliahidi mwaka jana kuwa, Wizara inatarajia kukamilisha mchakato wa kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwenye nyumba za kuishi, pamoja na tatizo kwa matumizi ya umeme kwa mwezi. Napenda Mheshimiwa Waziri, alijulishe Bunge lako, mchakato huo umefikia wapi na matokeo ya punguzo yakoje hivi sasa ?

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwa sasa, Wizara iandae Muswada wa Sheria utakaoilazimu TANESCO kufidia wateja walioharibiwa vifaa vya umeme na TANESCO bila urasimu mkubwa, uliojaa ukandamizaji wa wateja kwa kutumia visingizio vya kiufundi kwa kuwanyima haki halali!

Mheshimiwa Spika, katika kesi nyingi za aina hii, kila mara dosari ya uharibifu wa vifaa vya wateja hubambikizwa ubovu au hitilafu katika vifaa vya wateja, badala ya hitilafu zinazotokana na umeme katika eneo linalohusu TANESCO.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la uharibifu wa vifaa, hutokea mara nyingi kutokana na kuzimika na kuwaka au kurudi ghafla kwa umeme uliokatika, kutokana na uharibifu wa mitambo ya TANESCO. Suala hili inabidi litazamwe kwa lengo la kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwekezaji M/S Kaston Mining Co. Ltd., anayetarajiwa kujenga kiwanda cha kuchimba na kutengeneza shaba katika Kata ya Uleling'ombe (Wilaya ya Kilosa), TANESCO ilikuwa na mpango chini ya MCC wa kupeleka umeme huko.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, alijulishe Bunge lako ni kwa nini Mradi huu umeachwa pasipo Mradi mbadala kuandaliwa?

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la uendelezaji wa kazi nzuri inayotekelezwa na Wizara hii, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuipongeza Wizara hii, kupitia Waziri wake na Naibu Waziri na Watendaji wote walio chini ya Wizara hii, mashirikiano yao yameifanya Wizara hii kutoa mchago mkubwa wa Pato la Taifa, pamoja na matatizo makubwa yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kwanza, ninawekeza katika kutoa kipaumbele kwa uhamasishaji wa umeme wa nguvu za upepo, kwani mpango huu pindi ukifanikiwa, basi tatizo la umeme nchini mwetu litakuwa la kihistoria. Pamoja na kuwepo kwa mpango wa kujenga kiwanda cha uchujaji wa mafuta na kuweka miundombinu ya kuweka bomba la kupeleka mafuta Dar es Salaam hadi Mwanza, mpango huu mzuri wa siku nyingi umalizwe kiutekelezaji haraka, kwani mpango kama huu wenzetu wa Kenya wameutekeleza mapema; baada ya kugundua faida yake, wameweza kuwekeza bomba hilo kwa kilomita 800 toka Mombasa Port hadi mipaka ya Ziwe; hivyo kimsingi soko la mafuta kuliwahi kama walivyopanga.

Mheshimiwa Spika, inasemekana mipango mizima ya masuala ya madini inataka maridhiano ya wadau husika. Hii itapelekea kuvuna, kunufaika na pato halisia, hivyo naomba Wizara ishirikishe katika namna zozote zile pale pote panapogunduliwa madini, kutoa mashirikiano ya kimazingira yashirikishe wadau; vinginevyo, madini hayatanufaisha pande zote, yaani Serikali na wadau badala yake kitakachodumu ni migogoro.

Mheshimiwa Spika, kimazingira, Chuo cha Madini ni muhimu sana ndani ya nchi yetu, hivyo naiomba Serikali itoe kipaumbele kwa kukipa uwezo unaokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuwa kikatiba suala la mafuta ni la Muungano, lakini linapaswa kuwa viongozi wetu wakuu wakae pamoja na kuliboresha kwa maongezi ya busara. Kihistoria, masuala ya mafuta katika nchi zilizotangulia kuchimba, wamekosana baada ya kupatikana kwake; hivyo hapa si kuangalia Katiba tu bali uzalendo, utu, makubaliano ya ana kwa ana na elimu yanahitajika.

Mheshimiwa Spika, Gas ni biashara nzuri sana hapa duniani, hivyo naishauri Wizara iandae mpango mahususi wa kuliboresha zao hili muhimu, ikiwezekana ichukuliwe taaluma ya Urusi katika biashara hii.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tuliletewa semina na Wizara hii kuhusu mpango wake wa muda mrefu katika usambazaji wa umeme. Naomba tathmini hii iangaliwe upya, pamoja na kwamba, imeshirikisha wataalam toka nje, lakini hapa pana maslahi ya kila namna katika dunia hii ya kisayansi na yenye kuona mbali. Ahsante.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye uzalishaji na usambazaji umeme.

(I) Wakati wa Semina ya Nishati na Madini, nilitoa mchango wangu juu ya kuendeleza Kihansi Project Phase II. Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. I. Rashid, alijibu kuwa maji hayatoshi kuendeleza Mradi huu, ambao una uwezo wa kuzalisha MW 120.

Mradi huu ulifanyiwa *Feasibility Study* na ulionekana kuwa *viable*. *Viability* ya mradi wa kufua umeme kwa maji ni upatikanaji wa maji ya uhakika. Chanzo cha maji ya mito mingi katika Wilaya ya Kilombero na Iringa katika Wilaya Mufindi na Kilolo. Mufindi haijawahi kukosa mvua na Hifadhi ya Milima ya Mdurungwa ambayo inatengeneza *Catchment*, ya *Rain Forest* ambayo inalisha chanzo hicho cha Kihansi. Mufindi *has never, been dry*.

Mheshimiwa Spika, katika Mradi huo kulikuwa na kujenga *Reservoir* nyingine ya DAM 2, ambayo ingehakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya ufuaji wa umeme wa Kihansi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara iwatume wataalam kwenda Kihansi na kuona jinsi Mradi huu wa Awamu ya Pili utakavyoendelezwa kwa sababu ulishaanza.

Umeme kwenda Malinyi (Ulanga) kutoka Kihansi, chini ya Mradi wa MCC ulipitishwa katika mwaka 2008/2009. Nashauri Mradi huu lazima uwaufuate watu na siyo kuwakimbia. Kama ulivyosikia ni kweli, sikubaliani na wazo la kupitisha njia za umeme porini, kwa lengo la kufanya *short cut*. Njia hii inapita katika maeneo yenye mito mikubwa mitatu na itakuwa vigumu kufanya *repairs*, pindi ikitokea hitilafu katika nguzo. Njia ambayo inafaa katika utekelezaji wa Mradi huu ni kupitia Vijiji vya Mpanga, Utengule, Ngalmila, Biro na Malinyi.

Tarafa ya Mngeta na Mlimba ziko pua na mdomo kutoka *Kihansi Hydro Electric Power Plant*. Inasikitisha kuona Wizara haitaki kuwapatia Wananchi wa Tarafa hizi umeme, licha ya kazi kubwa wanayofanya ya kulinda *pylons* zinazopeleka umeme katika Grid ya Taifa.

Vijiji katika Tarafa hizi vina uzalishaji mkubwa wa chakula kama mpunga, mahindi na shughuli nyingine za biashara. Ningetegemea Wizara ingevipatia vijiji hivi umeme angalau kwa awamu. Kwa mfano, kutoka Kihansi Tarafa ya Mngeta, Vijiji vifuatavyo vingefikiriwa: Kihansi – Chita – Ikule – Mkangawalo – Mchombe – Njage (Awamu ya Kwanza); na Mbingu, Kisege, Namwawala, Mofu, Idete, Ihanga, Michenga (Awamu ya Pili).

Kutoka Kihansi Tarafa ya Mlimba, Vijiji vifuatavyo vingefikiriwa: Matema, Msolwa, Ngwasi, Kalengakero (Awamu ya Kwanza); na Mponga, Utengule, Ngalmira chini ya mpango wa MCC.

Nashukuru kuona Mji wa Ifakara umepangwa kwenye jedwali ili upatiwe fursa za kusambaziwa umeme. Tayari katika mji huo, kuna watu wameshajiorodhesha kupatiwa umeme. Katika Mtaa wa Mlabani, kwa mfano, watu 70 wameshapeleka maombi TANESCO Ifakara. Aidha, Mtaa wa Michenga na Kilosa Road, kuna watu ambao wako tayari kupatiwa umeme.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Naibu Waziri wa Wizara, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Kelele za Waheshimiwa Wabunge, hazina maana ya kuwa hamfanyi kazi nzuri, bali ni kielelezo cha umuhimu wa Wizara hii kwa maisha ya Mtanzania na ufinyu wa bajeti katika kutekeleza yale mnayokusudia.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha nchi yetu inanufaika na mapato ya madini yetu, pamoja na rasilimali nyingine, upo umuhimu mkubwa wa kuanzisha *an economic intelligence unit* hapa nchini. Tumeshinikizwa na Wamarekani tuanzishe *a financial intelligence unit* ili kuzuia *money laundering*. Jambo hili ni la faida ndogo kwa nchi yetu kuliko EIU, huku likiwanufaisha zaidi rafiki zetu hawa.

Mheshimiwa Spika, shinikizo la kuanzisha EIU linapaswa kutoka katika Wizara na Taasisi zinazosimamia rasilimali za nchi, hususan Wizara za Viwanda, Biashara na Masoko,

Fedha na Uchumi; Madini na Nishati; Maliasili na Utalii; Mifugo na Uvuvi na kadhalika. Naomba Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, walitafakari hili kwa pamoja na kuona namna ya kumshauri Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara iwashirikishe wenye migodi na watakaouza nishati ili uundwe Mfuko wa kuwasomesha Wataalam wa Madini wa Kitanzania. Tuisubiri vijana waamue wenyewe kusomea fani hizi; tuweke *incentive* ya wazi kabisa ili vijana hawa tuwapeleke katika nchi zinazoongoza kwa utoaji wa taaluma hizi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Ngeleja, kwa kuagiza matatizo ya umeme Jimboni Moshi Vijijini yatatuliwe haraka. Aidha, natanguliza shukrani kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa vile naamini ataukubali mwaliko wangu na Mheshimiwa Waziri atamruhusu kuja kuitembelea Miradi ya Nishati Moshi Vijijini, mwezi August 2009. Barua ya mwaliko imeshawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri; naunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa huduma ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo na uchumi wa nchi; na kwa kuwa Mji wa Mpwapwa una huduma ya Umeme wa Gridi ya Taifa; na kwa kuwa nguzo nyingi zinazopeleka umeme Miji ya Kongwa, Gairo, Mpwapwa na Kibakwe zimechakaa na kusababisha nguzo hizo kuanguka na kusababisha umeme kukatika mara kwa mara na wananchi kukosa huduma ya umeme; je, Serikali ina mpango gani wa kuweka nguzo mpya na fedha kiasi gani zitatumika katika shughuli hiyo?

Kwa kuwa kuna mpango wa kupeleka umeme Vijiji vya Nghambi, Chunya, Msagali, Kisokwe, Idilo na Lupeta Wilayani Mpwapwa, kwa ufadhili wa fedha za *Mellinium Challenge Corpration (MCC)*; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme Vijiji vya Mzase, Berege, Chitemo, Igoji Kusini, Inondo, Makutupa, Bumila, Mbori, Tambi, Mlambula, Mugoma/Mzogole, Kisisi, Godegode, Kimagai, Inzomvu, Mkanana na kadhalika? Huduma ya umeme katika vijiji hivyo itachochea maendeleo na uchumi wa vijiji hivyo.

Kwa kuwa bei ya mafuta ya petroli na dizeli inapanda mara kwa mara na kusababisha gharama za maisha kupanda hasa nauli; je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ya mafuta na kudhibiti mwenendo mzima wa bei za mafuta ya petrol?

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, narudia tena kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Najua mnafanya kazi katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti, unaowafanya mtekeleze majukumu yenu katika mazingira magumu sana.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa hatua za kuukwamua Mradi wa Kiwira.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara, fedha zilizoikopesha Kampuni ya ARTUMAS zitumike kwa kununua hisa. Hizo hisa wanaweza kusimamia watu wa TPDC.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Malima, wamefanya kazi nzuri. Hali mliyoikuta ilikuwa mbaya. *I am sure that you can now begin to see the light at the end of the tunnel!*”

Mheshimiwa Spika, aidha, naipongeza timu nzima ya Wizara kwa ripoti/bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu kuhusu maombi ya PMLs kama 95 hivi ya Nseronero Mining Co-operative ya Mkoa wa Mara, ambayo yanapuuzwa kwa manufaa ya watu binafsi. Taarifa za maombi haya, zilipelekwa Wizarani takriban miaka miwili hivi iliyopita, lakini hakuna ufumbuzi uliopatikana pamoja na kwamba, Co-operative hii ina kila haki ya kupewa hizo PMLs.

Mheshimiwa Spika, nakiri kuwa na *interest*, Mwenyekti wa Ushirika huu (Dkt. Chogo) ni *family friend*.

**MHE. ARTCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote, kwa kutuletea hotuba hii pamoja na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukumbushia umuhimu wa kusambaza umeme katika maeneo mengi zaidi, pale ambapo umeme umeshafika/umeshapita au upo umbali mdogo, kwani ndiyo njia mojawapo ya kuongeza mapato kwa TANESCO na hivyo kuwa na uwezo zaidi wa kutoa huduma. Mfano ni kule Wilayani Hai, ambako usambazaji unaongezeka mfano Vijiji vya Mungushi, Mijengweni, Masama Magharibi na kwingineko, TANESCO wangepata mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nipatiwe majibu ni nini kinachoendelea katika Kituo cha Kikuletwa cha kuzalisha umeme?

Mheshimiwa Spika, ninashauri tuwe waangalifu tunapogusa Uranium, kwani madhara yake ni makubwa lakini pia angalizo kubwa ni katika mapato yake, ikiwa msisitizo katika mikataba. Ninaomba tuyaangalie madini ya vito, kwani tulishasema na kupitisha sheria kuwa, haya madini yachimbwe na Watanzania tu pasipo kuingiliwa na Wageni.

Mheshimiwa Spika, kuna unyanyasaji mkubwa sana katika Kampuni ya Tanzanite One kuhusu mionzi ya kuwamulika wafanyakazi ambayo inawaathiri sana.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kuratibu zoezi la ugawaji wa viwanja kule Kibakwe, kwani kuna malalamiko kuwa watu wadogo wamenyang’anywa au watanyang’anywa *plots* zao za uchimbaji ruby.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza kulikumbuka Shirika letu la STAMICO, lakini tunahitaji kuliongezea uwezo zaidi, kwa kutambua umuhimu wake kwa Taita letu.

Mheshimiwa Spika, ninashauri TPDC iwezeshe zaidi na hata ile *retention* yake wapewe mapema ili waweze kukidhi mahitaji yake na kuiwezesha kushiriki vizuri kwa niaba ya Taifa katika biashara ya gesi na mafuta, hapa kikubwa kinachohitajika ni uzalendo.

Mheshimiwa Spika, ninashauri huu mchakato wa *bulk procurement* ufanyike haraka na kwa uangalifu mkubwa sana ili kuliokoa Taifa letu na hasara kubwa tunayoipata hivi sasa,

kutokana na baadhi ya wafanyabiashara ya mafuta kutokuwa waaminifu na hivyo kusababisha hasara na matatizo kwa wananchi na ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, ninashauri biashara ya usambazaji wa gesi majumbani, vituo vya kujazia magari viwe vya Shirika la TPDC, kwani watu/makampuni binafsi wao watataka kurudisha gharama mapema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kazi kubwa na muhimu ya maendeleo ya Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, umeme Jimbo la Shinyanga Mjini Nhalangani (Mashariki) – Kizumbi: Napenda kurudia ombi langu la umeme upande wa Nhalegani Mashariki ; narudia kwa mara ya nne! Upande huu ndiko anakoishi hata Mbunge wa sasa, ambaye alikwishaomba umeme muda mrefu. Nafahamu azma nzuri ya Serikali kupitia TANESCO. Hata hivyo, azma hiyo imebaki kuwa tumaini lisilo na muda bayana kuwa itatatimizwa lini.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze lini umeme utawafikia Wananchi wa Nhalegani Mashariki akiwemo Mbunge ?

Mheshimiwa Spika, kuna Wananchi wa Bugayambelele – Kizumbi wanaoomba umeme muda mrefu lakini hawajapata. Hata hivyo, eneo hili linapitiwa na nyaya za umeme kuelekea maeneo jirani na kuwafanya wananchi washangae kwa nini nao wasipatiwe huduma ya umeme! Kijiji cha Bugayambelele kimezungukwa na Chuo cha VETA na Shule ya Sekondari Buhangiya, vyote vikiwa na huduma ya umeme, Bugayambelele nao wapatiwe umeme kutoka mojawapo ya majirani hawa.

Chamagulu kuna wananchi wengi wanahitaji huduma ya umeme katika Kata ya Chamaguka. Naomba TANESCO iwafikie wananchi hao.

Pamoja na maombi hayo hapo juu, naipongeza TANESCO Mkoa wa Shinyanga, hususan katika Jimbo langu la Mjini, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusambaza huduma ya umeme. Kazi yao naiona na kuithamini. Hivyo, maombi yangu hapo juu yanazingatia kazi nzuri ya Shirika ndani ya mahitaji makubwa ya huduma ; ndiyo maana nimevumilia kukosa umeme kule Nhelegani hadi leo, uvumilivu ambao sasa nami nieleweke na kupelekewa huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu Sheria mpya ya Madini itaambatana na mabadiliko stahili kwa baadhi ya sheria kama vile ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kuwa, Sheria mpya ya Madini itazingatia kuwa, Watanzania wanastahili ya ardhi na vitu vilivyoko chini ya ardhi. Hivyo, sheria iwatambue pale wanapokuwa na hati miliki ya ardhi. Hii itaondoa tatizo la wananchi kusukumwa nje ya maeneo ya migodi bila kufaidika na mapato ya madini katika uhai wa mgodi wowote mkubwa. Kwa nini Mtanzania afe maskini wakati anaishi na kumiliki mali chini ya ardhi yake?

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la heri na naunga mkono hoja.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kututengea fedha mwaka huu. Kwa kuwa Mradi wa Umeme Mchinga I & II unaotarajiwa kukamilika ndani ya miezi minne na utahusisha pia kuunganisha wateja, tunaweza sasa kuwahamasisha wananchi waanze kufanya *wiring*?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utengenezaji wa chumvi ni moja ya njia ya kujijiri, lakini Serikali bado haijaweka mkazo mkubwa katika eneo hili; na kwa kuwa Ofisi za Madini Kanda zinajishughulisha zaidi na leseni na utawala kuliko elimu; Wizara sasa haioni umuhimu wa kututembelea wazalishaji wa chumvi ili kwa pamoja tupate *the way forward*?

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa TPDC ina shughuli nyingi sana ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Hali hii inasababisha TPDC ihitaji mtaji mkubwa zaidi na wataalamu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza kuruhusu ajira za ndani ya TPDC, pamoja na kuruhusu *retention scheme*. Nashauri Serikali iidhamini TPDC ili iweze kukopesheka katika mablenki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uwezo kwa kuishika kalamu, nami nikaweza kutoa maoni yangu katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini imani ya Waziri kwetu, Naibu Waziri, pamoja na Wenyeviti wako wote kwetu, natoa shukrani na kumwomba Mola akujaliene kheri.

Mheshimiwa Spika, nianze kusema hongerni Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Malima na timu nzima iliyoandaa bajeti hii, ambayo imejengeka na kuwa na sura ya kuinua uchumi wa nchi yetu na kufanya apate maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, nianze kule kunakoitwa North Mara. Eneo hili tumebahatika kuwa na mgodi. Kwa hali ambayo inahatarisha maisha ya watu; ni hivi karibuni tu ambapo *chemicals* zilizotoka ndani ya machimbo, zimeingia katika mito ambayo inatumiwa na watu na kupelekea kuathiri maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali itueleze ni kwa jinsi gani itaweza kuwaondolea kadhia hiyo? Mara nyingi, maeneo ya migodi hutokezea matatizo ya kivita kati ya mwekezaji na wananchi, kwa kukosa haki zao za msingi. Yanapotokea haya ili Jeshi la Polisi kutuliza hali ili ipatikane amani, wao hutumia nguvu, jambo ambalo wananchi wasio na makosa huadhibiwa bila ya sababu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, kwa kuzingatia uzindukaji kwa Watanzania juu ya mahitaji ya umeme ni mkubwa; Watanzania wengi wamehamasika na kuwa tayari kutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme ni njia mojawapo ya kuikomboa nchi yetu katika dimbwi la umaskini. Tatizo ambalo ni kubwa katika Sekta hii ni ughali wa mambo yake. Huduma ya umeme imekuwa ni biashara badala ya matumizi yake. Mtu anayeishi katika nyumba ya nyasi na akiuhitaji umeme ni lazima awe na malaki ili afanikishe matakwa yake. Kwa nini Wizara isisambaze umeme kwa bei nafuu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta, kwa kuzingatia kauli za pande mbili za Serikali zetu, yaani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano, kuhusu uchimbaji wa mafuta Zanzibar; ni kitu gani kinachopigwa danadana katika Serikali zetu hizi? Muungano hapana mafuta, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tutachimba mafuta kwani si Muungano! Kwa kuzingatia gas ambayo ni wazi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina haki, lakini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haijapewa chochote.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limetoa sura mbaya na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kulazimika kutafuta njia ya uchumi, kwani uchumi wa Zanzibar ni mdogo sana. Ukweli ukidhihiri uongo hujitenga; kuna kosa gani la uchimbaji wa mafuta huko Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, kuna utofauti kwa wafanyabiashara wa mafuta katika baadhi ya maeneo katika nchi moja, ambayo ina chombo mahususi cha kusimamia bei ya biashara hiyo. Chombo hiki ni EWURA. Je, ni kitu gani kinachopelekea udhaifu huo?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi kubwa ya wananchi wamejiari binafsi; eneo la ajira ya watu wengi ni la wachimbaji madini katika nchi yetu. Tuna wachimbaji wadogo wadogo wengi, ambao hawana maeneo yao juu ya kazi yao ambayo ndio ajira. Ni vizuri Wizara hii inayoongozwa na vijana wenye maumivu na vijana wenziwao, wawapatie maeneo ili waweze kujijiri na kufanikiwa na mlo wao. Pia Wizara iweze kuwapatia mikopo ili wapige hatua katika kuzalisha. Baada ya maelezo yangu hayo, nachukua fursa hii kuwapongeza wafuatao; Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Adam Malima.

Mheshimiwa Spika, Mungu awape uwezo. Ahsante.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote, kwa kazi nzuri mnayofanya katika mazingira magumu ya upungufu/ukosefu wa bajeti. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kumpelekea malalamiko yangu Mheshimiwa Waziri, muda mrefu sana, kutokana na TANESCO kuweka nguzo ndani ya Kiwanja changu kule Gongo la Mboti Dar es Salaam. Nguzo hii ni kubwa na imekula sehemu kubwa sana ya kiwanja changu. Nina hakika, alitoa maelekezo kwa viongozi wenzake wa chini. Kama ni hivyo, kwa nini hadi leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa? Iwapo maelekezo yake hayatekelezwi, niende kwa nani atakayenisikiliza ili kilio changu hiki kiweze kusikilizwa? Ninaomba suala hili lipatiwe ufumbuzi. Nachelea sana, kupiga makelele hadi watu wote wajue kuwa sisikilizwi/sisaidiwi na Mheshimiwa Waziri, ambaye ni mdogo wangu. Nisingependa kulipeleka suala hili Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naomba Kijiji cha Ihayabuyaga, Kata ya Kisesa, Jimbo la Magu, nacho kipatiwe umeme. Ni kijiji kikubwa, kina wafanyabiashara, Shule za Sekondari, Makanisa na Makazi mengi ya kudumu. Naomba kijiji hiki nacho kifungiwe transform.

Mheshimiwa Spika, Umeme Tarafa ya Ndagalu, Jimbo la Magu yenye Kata Nne; Sukuma, Ng'haya, Nkungulu na Shishani, yote haina hata tone moja la umeme. Tarafa inazalisha mazao yote kwa wingi, inachangia kwa kiasi kikubwa sana kwenye pato la mkoa na pia kwenye mapato ya Serikali. Kuna viwanda vya kusindika mazao mbalimbali, vimeshindwa kufungwa kwenye Tarafa hii kwa sababu ya ukosefu wa umeme. Tarafa hii ina sekondari nne, ina kituo cha afya kimoja na zahanati kumi. Jamani, Tarafa hii imekosa nini



kwa Mungu? Niliwahi kuomba umeme utoke Mjini Magu kwenda Mahala kupitia Lumeji, Ngihaya na Kabila, lakini nikajibiwa gharama ni kubwa sana (3.7 billion). Tukaomba walau sasa umeme utoke Shule ya Sekondari Talo katika Jimbo la Sumve upitie Kadashi, Maligisu na hatimaye uende Kabila. Hii ni njia fupi zaidi na gharama zake ni ndogo zaidi kuliko kupeleka umeme Kabila kutoka Magu. Naomba Waziri aniambie mpango huu utatekelezwa mwaka huu fedha? Kama gharama ni kubwa vile vile, kwa nini Serikali/Wizara isiangelie uwezekano wa kupeleka umeme Ndagalulu kutokea Ginnery ya Kasoli?

Mheshimiwa Spika, *Alliance Ginnery* (Kasoli), walitumia fedha zao kupeleka umeme kwenye *Ginnery* yao iliyoko Kasoli Wilayani Bariadi, kwa makubaliano kwamba, wangerudishiwa fedha zao. Kwa kuwa TANESCO hawakuwa na fedha na kuchambua pamba kutumia Diesel ni gharama kubwa sana ukilinganisha na umeme, kwa nini sasa kuna kigugumizi kikubwa kisichoeleweka kwa TANESCO kuwarejeshea fedha walizotumia? Nafurahi sana umeme ukifika Kasoli unaingia Tarafa ya Ndagalulu, nikiamini kuwa vijiji vilivyokuwa karibu na Kasoli kama vile Kijiji cha Salama, Bugatu, Ng'haya, Chandulu, Nkuughulu na Kabila, vinakuwa na matumaini makubwa ya kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, TANESCO wana mpango gani kabambe wa kumaliza/kuwalipa *Alliance* fedha walizotumia ambazo nazo walikopa benki? Binafsi, sioni kwa nini bado kuna kigugumizi kwa sababu suala hili liko wazi kabisa mpaka watu tulete hoja binafsi ndiyo litekelezwe?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini tutakutana kwenye kamati.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Viongozi wa Wizara, wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wote, kwa hotuba na kazi nzuri wanayofanya katika kukabiliana na matatizo yanayoikabili Wizara hii. Pamoja na hayo, yapo matatizo ambayo yanahitaji kurekebisha.

Leseni zote hutolewa kutoka Makao Makuu ya Wizara. Matokeo ya utaratibu huu umesababisha matatizo yafuatayo:-

(a) Maeneo ya uchimbaji huhodhiwa kwa miaka mingi kinyume na sheria ya maeneo hayo kurejeshwa kwa Kamishna wa Madini.

(b) Wamiliki wanaohodhi maeneo ya uchimbaji madini Wilayani Chunya, wengi wao wanaishi Mjini hasa Dar es Salaam na hawajawahi kuyaona kwa macho maeneo wanayomiliki, bali mipango yote hufanyiwa na Wataalam wa Makao Makuu Dar es Salaam.

(c) Kutokana na utaratibu huo mbaya wa utoaji wa leseni, baadhi ya maeneo ambayo hutolewa kwa wawekezaji, maeneo hayo mengine huchukuliwa kwenye vijiji vinavyokaliwa na wananchi. Mfano, maeneo kwenye Kijiji cha Saza, yamegawiwa kwa watafutaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya kuna *deposit* kubwa ya makaa ya mawe kama kule Magamba na Chalangwa. Kazi ya uchimbaji imekwishaanza sehemu za Magamba. Makaa hayo huchimbwa na kusafirishwa kupelekwa Malawi na Zambia.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ukoloni, makaa ya mawe baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mbeya, yalikuwa yanatumika kwa matumizi ya ndani (*domestic use*). Hali hiyo ilisaidia

sana kuhifadhi mazingira na misitu. Kwa nini makaa ya mawe yasianze kutumika kwa matumizi ya ndani?

Mheshimiwa Spika, Wilayani Chunya kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira. Wachimbaji wa aina zote, watafutaji wadogo wadogo, kazi yao kubwa ni kutafuta dhahabu kwa kuchimba; wakishachimba huondoka na kuyaacha mashimo kadhaa kwenye maeneo. Pia ukataji miti hufanyika ovyo ovyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri sheria imtake mchimbaji, kufukia maeneo ambayo yanachimbwa na kuachwa wazi.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuwatengea maeneo ya uchimbaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Mbona Wilayani Chunya kazi hiyo haijaanza kutekelezwa?

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliahidi miaka mitatu iliyopita kusambaza umeme kutoka Makao Makuu ya Jimbo la Songwe, Kijiji cha Mkwajuni, kupelekwa Galula umbali wa kilomita 29. Kwenye maeneo hayo, wananchi tayari walikwishaambia nguzo wanasubiri kutandika nyaya.

Mheshimiwa Spika, ni lini umeme utasambazwa kwenye Vijiji vya Kaloleni, Iseche, Mbala, Kanga hadi Galula?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ahadi ya kupeleka umeme kutoka Itigi kwenda Mgandu bado mbichi.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa toka ahadi hiyo itolewe na wananchi wana hamu kubwa ya kuona mradi huo unatekelezwa ili nishati hii muhimu iwafikie Mgandu, ambako kuna uzalishaji mkubwa wa mazao ya biashara na chakula, pamoja na asali na nta. Kuna Vijiji vya Mlonghoji, Itagata, Lulanga, Kayui/Ukimbu, Makale/Mtakuja, Mtundu, Kalangali, Kijumbe, Kivumbi, Mwamagembe, Kimtanula na Rungwa, vyote vimejipanga Barabara Kuu ya Itigi – Rungwa – Chunya, tayari kwa usambazaji wa umeme. Vina shule za msingi, kijiji, zahanati na kuna Shule za Sekondari za Mgandu, Mitundu, Kalekwa na Rungwa na Hospitali kubwa ya Misheni ya St. Vincent ya Mitundu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhakikishiwa kama awamu ya kwanza ya kusambaza umeme itaanza mwaka huu wa 2009 kama ilivyopangwa? Napongeza hatua zinazochuliwa.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara kadhaa wa vituo vya kuuza mafuta hapa Mjini, wanalalamika kuwa EWURA inawaonea; mfano ni Kituo cha GAPCO cha African Motors, njia panda ya kwenda Area D, ambacho kimefungiwa kwa muda wa zaidi ya wiki mbili sasa, kwa kudaiwa kuuza mafuta yasiyo na kiwango (machafu). Mmiliki wa kituo hicho, anadai kuwa mafuta anayopata hayana dosari na ni hayo hayo yanayosambazwa kwenye vituo vingine vya GAPCO. Anadai mwaka jana alipigwa faini ya Sh. 3m/=. Sakata la sasa ni kwamba, hata sampuli ya mafuta hayo ilipopelekwa TBS, bado hayakupimwa na kituo bado kimefungwa. Mmiliki ni mwanamke na hivi sasa anasumbuliwa na Ugonjwa wa Shinikizo la

Damu. Anadai anaandamwa sana na mtu mmoja wa EWURA bila sababu na ni kinyume na maadili ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, naomba hili lichunguzwe na kurekebishwa ili apate haki yake ya kufanya biashara zake kwa uhuru na amani.

Mheshimiwa Spika, kazi mojawapo ya Mbunge ni kutetea mwananchi pale anapoonewa.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hii muhimu sana ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianzie Jimboni kwangu. Sina nia ya kupunguza mshahara wa Waziri, lakini nina nia ya kuuchukua wote. Jimboni kwangu, kuna viporo vingi sana vya nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo kubwa na Wananchi wangu wa Vijiji vya Kizerui, Kadando, Mtui, Kizangaze na Mroyo. Hivi ni viporo vya muda mrefu, njia kubwa sehemu nyingine ziko tayari, sehemu nyingine ni nguzo tu. Naomba Mheshimiwa Waziri, anihakikishie kumalizia viporo hivi ili nisimpokonye mshahara.

Mheshimiwa Spika, kuna Kata za Milimani ambazo Hazina umeme kabisa na sioni dalili ya Kata hizi kupata umeme; Kata ya Vunta na Kata ya Kirangare. Kata hizi ni za milimani, wananchi wanaishi gizani, usalama wao ni mdogo mno.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Maumba – Mvuta, njia kubwa nakiri imekamilika, lakini kusambaza umeme kwa makazi ya watu bado kabisa wananchi wamefanya *wiring* majumbani, kazi iliyobaki ni Serikali. Naomba Serikali ilisimamie hili kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanaoishi milimani bila ya umeme, wana maisha magumu mno.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nyingi na nzuri wazifanyazo kwa wananchi wa nchi yetu. Changamoto ni nyingi sana, lakini wasife moyo. Kila hatua ya maendeleo huja na changamoto zake. Hivyo, huwa hakuna kupumzika kila kukicha na changamoto zake, ninawatakia kheri kwa yote.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wote waliohirikiana naye katika kuiandaa na hatimaye kuiwasilisha Hotuba ya bajeti ya Wizara Hii. Hotuba ni nzuri na inawatia moyo wengi, kulingana na hali halisi ya uwezo wa nchi yetu na Shirika letu la TANESCO.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, napenda nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1995, nilipoanza kuliwakilisha Jimbo la Kwimba humu Bungeni, nilianza kuomba umeme kwa ajili ya jineri mbili za pamba; Mwalujo na Sangi. Nilifahamu kuzifikishia jineri hizo umeme, zingepolekeka Miji Midogo ya Hungumalwa, Mwamashimba, Kikubiji na Shilima, ingenufaika. Aidha, Kituo cha Afya cha Mwamashimba na Shule za Sekondari za Mwamashimba vingenufaika. Leo yapata miaka kumi na nne, hata nguzo moja tu haijatereshwa, achilia mbali Generator. Hata ukiuliza majibu ni laini na mepesi, yanayopambwa kwa maelezo marefu na matamu, kiasi cha awaye yeyote anaweza kuamini kiasi cha ukweli uliomo. Leo ni vyema niseme, wanachohitaji wakazi wa maeneo hayo pamoja na wenye jineri hizo nilizozitaja, hawahitaji sana utamu wa maelezo, wanahitaji mambo mawili tu ya uhakika; Kupata umeme au maelezo ya dhati na kweli kama watapatiwa umeme au la; na kama watapatiwa ni lini na maelezo yakitolewa yawe kweli. Ni vyema kila tutakapo kutoa maelekezo kwa watu, tamwogope Mungu. Tujizuie kusema uongo, tusije kulaumiwa nao. Ni vyema mtu akuchukie kwa kumweleza ukweli, kuliko kumfurahisha kwa maneno mengi ya uwongo, ambayo yatadumu kwa muda mfupi, kwani usemi kwamba njia ya mwongo ni fupi una uwongo?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Vijiji vya Jimboni mwangu vya Ilula, Hungumalwa, Buyogo, Mwalujo, Kanekamo, Mwamashimba, Sangu, Kikubiji na Shilima, vingalipatiwa umeme katika bajeti ya mwaka uliopita. Mwaka umepita hata dalili tu bado hazijaonekana. Baada ya mwaka kwisha, niliuliza Bungeni katika Mkutano huu wa Kumi na Sita, lilikuwa swali Na. 56. Jibu lililotolewa ni refu, maneno matamu yasiyotaja hata muda (*time frame*). Jibu hilo ukaja na msamiati wa *Electricity V*, usiokuwa na ufafanuzi wowote!

Mheshimiwa Spika, faraja pekee iliyokuja na jibu hilo ni kuwa hatimaye TANESCO wenyewe wameamua kutenga kiasi cha shilingi bilioni tatu kwa ajili Kituo cha ya kupozea umeme Mabuki. Kutenga ni jambo moja, upatikanaji ni jambo lingine! Hata hivyo, kwa dhati kabisa, naipongeza TANESCO kwa ujasiri huo, ninawashukuru sana wote walioshiriki katika kuifikisha TANESCO ifikie uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, kujenga Kituo hicho cha Mabuki si suluhisho la moja kwa moja kwa wananchi katika Vijiji nilivyovitaja kufikiwa na umeme. Bado kipo kitendawili kine, hata baada ya kituo hicho kujengwa, nacho ni Mradi wa kuusambaza umeme huo kufikia vijiji hivyo ni mradi unaofadhiliwa na AfDB. Kituo cha Mabuki kikijengwa na TANESCO, bado itahitajika fedha kutoka ADF kutekeleza Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho hakijajulikana na kama tayari AfDB imekwisha kutenga fedha hiyo. Hivyo, itakuwa vyema kwanza tujiridhishe kama fedha ya kusambaza umeme huo itapatikana mapema ili kuzipa thamani shilingi bilioni tatu zitakazotolewa na TANESCO kujenga Kituo cha Mabuki.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa kuhitimisha ajibu yafuatayo:-

(i) Je, ni kiasi gani cha fedha kitakachohitajika kutoa umeme Mabuki hadi Vijiji nilivyovitaja hapo juu (Ilula, Hungumalwa na Shilima)?

(ii) Je, kuna uhakika upi kuwa AfDB itatoa fedha hiyo?

(iii) Mradi wa Mabuki peke yake utachukua muda usiopungua miezi 16 tangu mkandarasi kupatikana. Je, Mradi wa kusambaza umeme kutoka Mabuki hadi Shilima na Vijiji vingine vilivyotajwa hapo juu?

Mheshimiwa Spika, kuna wakati najiuliza kama Wizara na TANESCO wako *serious* kusaidia wananchi na wenye jineri mbili katika Vijiji vya Mwalujo na Sangu na watumiaji wa Kituo cha Afya cha Mwamashimba na Shule za Sekondari takriban nne kuwapatia umeme. Kinachonitia mashaka ni taarifa zitolewazo na Wizara. Inavyoelekea katika uandikaji wa hotuba, maandalizi ya maeno hayapitiwi kuyahuisha upya. Kama zoezi hilo lingalikuwa linafanywa, kungalikuwa na mabadiliko ya uwasilishaji kuhusu maeneo husika. Mwaka jana, kwa mfano, vijiji vilivyoorodheshwa kupatiwa umeme katika Jimbo la Kwimba, viliorodheshwa katika Jedwali Na.12, Uk. 81 wa Kitabu cha Bajeti 2008/09. Kulikuwa na masahihisho niliyoyafanya, kwa mfano, katika vijiji vilivyomo Jimboni kwangu, hakuna Kijiji cha Mwambashimba (tuna Mwamashimba), Kijiji cha Mwabakagola hakipo cha Mwabagole na Kijiji cha Nyamilala hakipo (kipo kijiji cha Nyamilama). Makosa haya yalitokea mwaka jana, nikasahihisha makosa hayo yamejirudia tena mwaka huu (angalia Kitabu cha Bajeti 2009/2010, Jedwali No. 4 Uk. 99). Hii ni ishara wazi kuwa, hata ushauri na maombi yangu na hata hoja zangu hazikusikilizwa, hazikuzingatiwa na yaelekea wazi kuwa hazikuheshimiwa, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, leo ninaomba kupewa jibu la dhati na ukweli na kwa kumwogopa Mungu, nijulishwe na wananchi wa maeneo ambayo tangu mwaka 1996 nimekuwa nikiyaombea umeme wasikie kama umeme katika maeneo hayo, kweli utapatikana na ndani ya miaka michache ijayo. Maelezo hayo, yaambatane na uhakikisho wa upatikanaji wa fedha kutoka AfDB na kiasi gani kitatolewa na benki hiyo, kwa ajili ya usambazaji wa umeme kutoka Mabuki na *Electricity V* ina nini?

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe mchango wangu huu kwa ombi kuwa, umeme utakapopelekwa kwenye vijiji ninavyoviombea, uje na utaratibu wa luku.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumiea fursa hii kwa dhati, kumshukuru Mkurugenzi wa Nishati Mbadala katika Wizara ya Nishati na Madini, kwa kuniunganisha kwa Mradi wa Solar chini ya UNDP, ambao hadi sasa tumefanikiwa kuunganisha vituo vitano kwa solar katika Jimbo langu na vitatu zaidi viko mbioni. Nawashukuru sana Maafisa husika wa Mradi huo walioko Mwanza, kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa wanaonipa mimi na Wananchi wa Jimbo la Kwimba. Wasituchoke bado tunawahitaji sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya, kufuatana na Wizara hii kuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Mfanyakazi wa Serikali huko Ruvuma, tafadhali namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, auangalie na kuuonea huruma Mkoa wa Ruvuma hasa kwa upande wa umeme.

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri anatambua tatizo la umeme lililopo Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea. Waziri amefika pale TANESCO, lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kuwa, Songea kuanzia Manispaa mpaka Songea Halmashauri, hali ni mbaya sana. Siyo mchana wala usiku, umeme ni wa tabu.

Mheshimiwa Spika, hata kazi maofisini tatizo sana, kwani umeme tabu. Sehemu kubwa walishasahau kama umeme upo. Wafanyabiashara wanaotegemea umeme, kwa kweli

wanapata matatizo, hawana pato tena hasa kwa matumizi ya *fridge* kutokuwepo kwa sababu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, mashuleni hasa wakati wa usiku, hawawezi kujisomea kwa sababu hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme tabu Songea na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla (Songea, Namtumbo na Tunduru). Shukrani kwa Wilaya ya Mbinga, kwani *generators* zote mbili zilizopo Mbinga ni mpya na zinafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, tutaendeshaje viwanda bila umeme? Naishukuru sana Serikali kwa kujitahidi kuleta *generator* kutoka Mtwara, kuongezea nguvu *generators* zilizokuwepo Mjini Songea, lakini nimekwenda mwenyewe (TANESCO), nimeeleza na Wafanyakazi wa TANESCO *generators* ni mbovu. *Generators* hizo bado zinatengenezwa kila siku, lakini umeme wa uhakika hakuna; hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Songea waonewe huruma, angalau kwa kuanzia wanunuliwe *generator* mpya kati ya hizo zitakazonunuliwa au zisimamiwe vizuri *generators* zilizopo zitengenezwe ili tupate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa kurudisha umeme katika Shule ya Songea Boys, uliokuwa umekatwa kwa muda mrefu. Pia naomba kumweleza Waziri kuwa, katika Mkoa wa Morogoro na Ruvuma hata Pwani, kuna madini mengi lakini uchimbaji bado ni wa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, naomba uangalie.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hoja muhimu ya Wizara ya Nishati na Madini. Ningependa kuchukua fursa hi, kumpongeza Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima (Mb), Katibu Mkuu, Bwana Arthur Mwakapugi na Watendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake, kwa hotuba nzuri na jitihada nzuri ya kuiendeleza Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Mkinga, kutoa shukrani zetu za dhati kwa Wizara, kwa kuunganisha umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijiji vya jirani vya Mkinga Leo, Mwakiponda, Menjemenye na Karoyo. Hata hivyo, uwekaji umeme wa Makao Makuu – Kasera, bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo ya kuwekewa umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijiji vya jirani, kero ya umeme Wilaya ya Mkinga bado ni kubwa, hasa kutokana na mahitaji makubwa na maombi ya siku nyingi sana ya kuwekewa umeme Vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale. Maombi ya Vijiji hivi na vinginevyo kupatiwa umeme, yalianza tokea wakati wa Awamu ya Kwanza. Maombi yalipata msukumo mpya katika Awamu ya Pili, ambapo aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, pia alikuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, naye akawahakikishia wananchi kwamba, umeme ungewekwa katika Jimbo la Mkinga bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, nilipochaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mkinga mwaka 2000, nilifuatilia maombi haya ya umeme ambayo yalianzishwa na Mbunge wa zamani. Mwaka

2003, niliongozana na aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini katika ziara Wilayani Mkinga. Yeye aliwaahidi Wananchi wa Vijiji vya Daluni, Gombero, Kwale na Mkinga kwamba, Serikali ingetekeleza ombi lao la kuwekewa umeme bila kuchelewa. Tokea wakati huo, hatua mbalimbali zilianza lakini zikawa zinaendelea kwa kasi ya konokono. Kwa bahati nzuri, Kijiji cha Mkinga tayari kimekwishapatiwa.

Mheshimiwa Spika, ninasikitika kwamba, pamoja na jitihada zangu za kufuatilia kwa bidii mara zote Wizarani na Bungeni, kupitia maswali ya Bunge na mawasiliano ya ana kwa ana na maandishi na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wasaidizi wao, jitihada zangu hizo hazijazaa matunda. Nimekuwa nikipewa ahadi hewa na kila mara kuambiwa nivute subira.

Mheshimiwa Spika, jambo linaloudhi ni jinsi Wizara inavyobadili kauli zake na kubabaisha. Awali, Wizara iliahidi Mradi wa Umeme wa Daluni, Gombero na Kwale, ungefadhiliwa chini ya Miradi ya MCC. Hata katika bajeti ya mwaka 2007/2008, fedha zilitengwa kwa utekelezaji wa Mradi huu. Mradi huu haukutekelezwa na nilipouliza kupitia swali la Bunge, nilijibiwa kwamba, Mradi huu ungetekelezwa chini ya Mfuko wa Umeme Vijijini (REF). Niliombwa nivute subira. Subira hii ina gharama kubwa, kwani mpaka sasa hakuna dalili ya Mradi huu kutekelezwa; pamoja na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kuwaahidi wananchi na Mradi huu kuwemo katika Plan, Mipango na Bajeti. Linaloudhi zaidi ni hatua za Wizara kubabaisha kiasi kwamba, Mradi huu umo hatarini kuuawa. Hauonekani popote kwenye mipango wala bajeti.

Mheshimiwa Spika, ubabaishaji wa Wizara na jitihada zake kufunika Mradi huu, zinabainishwa kwa Wizara kusema kwa nguvu sana kwamba, Mradi wa kupeleka umeme Makao Makuu, upotoshaji huu haikubaliki. Napenda nikumbushe kwamba, zipo kumbukumbu za Hansard na nyingine ambazo zinaonesha ukweli wa mambo.

Mheshimiwa Spika, ubabaishaji huu sio tu unainyima Wilaya ya Mkinga fursa ya maendeleo, bali pia kudhalilisha na kuwakatisha tama, Wananchi wa Wilaya ya Mkinga. Hali hii pia inaitia dosari kubwa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kumdhalilisha Mheshimiwa Rais na kupunguza heshima na imani kwa CCM. Kwa hali hii, nitaunga mkono hoja hii kwa shingo upande, nikiamini kwamba, Wizara hii itaachana na ubabaishaji wake na kuchukua hatua thabiti za kuutekeleza Mradi huu. Aidha, haya yasipotekelwa, natarajia kuandaa hoja binafsi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini vile vile ni mdau mkubwa wa Wilaya ya Mkinga, kwa maeneo mengine ya madini na nishati ya petroli.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga imebahatika kuwa na madini mbalimbali katika sehemu nyingi. Hadi sasa shughuli za uchimbaji rasmi wa madini, zinafanyika katika Kata za Mwakijembe na Daluni. Hali kadhalika, mawe ya ujenzi ya urembo yanachimbwa katika Vijiji vya Doda na Nkagaoni. Maeneo mengi yanayosadikika kuwa na madini mbalimbali, bado hayajaendelezwa. Pia kwa hayo maeneo ambayo madini yameanza kuvunwa, uchimbaji haufanyiki kwa ufanisi na tija stahili, kutokana na teknolojia hafifu, ujuzi mdogo na upungufu wa mtaji. Nadhani ni wakati sasa wa kuzindua Mfuko wa Maendeleo wa Wachimbaji Wadogo chini ya STAMICO, kwa madhumuni ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo kiteknolojia na kimtaji.

Mheshimiwa Spika, Mwambao wa Kaskazini wa Wilaya ya Mkinga ni moja ya maeneo yaliyoonesha dalili za kuwa na gesi asilia na pengine petroli. Ni jambo la kushangaza

kwamba, hatua za utafiti na maendeleo zimekuwa zikisuasua kwa muda mrefu. Naomba Wizara ilifahamisha Bunge lako Tukufu, hatua iliyofikiwa katika utafiti na maendeleo kwa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Wilaya ya Mkinga, wanasikitika sana kuona mdau wao, Wizara ya Nishati na Madini, amewanyima fursa za maendeleo na maisha bora kwa kila Mtanzania. Naamini Wizara itajikosoa na kuchukua hatua chanya za kuziendeleza fursa za Nishati na Madini, zilizopo Wilaya ya Mkinga. Kuhusu umeme kwa Vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale, Wananchi wa Wilaya ya Mkinga wamechoka kupuuzwa na kudanganywa. Naomba tafadhali Wizara hii iachane na ubabaishaji na itekeleze wajibu wake kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa shingo upande, nikiwa na imani kwamba, Wizara itakuwa sikivu, kufafanua masuala yote na kuchukua hatua zipasazo.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote Wizarani na katika Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, kwa mtazamo wa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kubwa sana na ina majukumu makubwa ya madini na umeme. Nianze na madini. Katika Jimbo langu ni wawekezaji walioweka mitambo ya kupasua mawe (wazawa).

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hawa wanazalisha kokoto, lakini tatizo ni soko, pia ni misamaha gani wanayoipata kuhusu kodi. Cha kushangaza, ipo Kampuni ya NOREMCO, wanapewa misamaha ya kodi, kwa maana wazalisha kokoto na wazifanyie kazi za ujenzi hapa nchini, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, lakini wanazalisha kokoto na wanauza nje ya nchi na bado wana misamaha ya kodi eti wanafanyia kazi nchini. Nataka ufafanuzi kwa nini NOREMCO wanafanya hivyo? Pia nataka ufafanuzi ni muda gani sasa tangu walipomaliza kujenga barabara lakini hadi leo bado wanapata misamaha wakati ni kosa na wizi?

Mheshimiwa Spika, ili nisizuie mshahara wa Waziri, nipeni ufafanuzi. Wachimbaji kokoto wazawa wanapata PMC, kwa nini wao wasipate misamaha?

Mheshimiwa Spika, niliahidiwa kupitia Mradi wa Umeme Vijijini, kupata Miradi minne ya Umeme tangu 2006: Chalinze – Magindu; Makole – Mbwewe; Msota – Kiwangwa; na Msoganje – Msoga Ndadni.

Nataka ufafanuzi; TANESCO wamewadanganya wananchi. Meneja wa TANESCO Kibaha nilimfuata na kumuuliza amenijibu vifaa vipo, pesa zipo ila Makao Makuu hawataki! Sasa je; ni nani hataki huko Makao Makuu? Naomba jina lake.

Mheshimiwa Spika, TANESCO imeweza kupeleka umeme Mjoga, kwenye Makazi ya Mheshimiwa Rais peke yake. Vile vijiji vingine mmewadanganya, lakini pia mmewagombanisha Wananchi na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanasema mmepeleka Mjoga kwa kuwa ni kwa Rais. Je, mnapoacha kupeleka umeme vijiji vingine mnamjengea jina gani Mheshimiwa Rais



mkizingatia akimaliza muda wake anarudi Kijijini Msoga ? Je, mnataka asipokelewe na wananchi wa vijiji ambavyo mmewaahidi lakini hamtaki? Huku ni kumdhalilisha Mheshimiwa Rais. Naomba majibu mazuri, pamoja na kupata jina la Mkuu wa Makao Makuu anayekwamisha miradi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia 40.

**MHE. FELIX KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, kama alivyoisoma kwa umahiri wa hali ya juu. Pongezi za dhati kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mwenyekiti wa Bodi, pamoja na Wataalam wote. Kwa mantiki hii, naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kutoa ushauri kwa Wizara hiyo kufanya yafuatayo katika Wilaya ya Kibondo, mahali ambapo katika Hotuba ya Waziri amewahakikishia Wananchi wake kuhusu kuwanunulia *Generator* ya kuwapatia huduma Wananchi wa Kibondo Mjini.

Mheshimiwa Spika, wakati Wizara inaandaa utaribu wa kununua *generator*, ninaishauri Wizara ianze kazi ya kusambaza miundombinu ili ikifika umeme uwashwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri wakati akihitimisha, atoe maelezo ya kueleweka kwa Wananchi wa Kibondo Vijijini kuhusu lini *generators* zinaagizwa ? Lini kazi ya kusambaza miundombinu itanza katika Mji wa Kibondo kwa kuwa fedha zipo ?

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara, kwa hotuba nzuri na utendaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi kama ifuatavyo:-

(i) Dosari moja kubwa ni kutokamilika kwa mabadiliko ya Sheria ya Madini kufuatia Tume ya Jaji Mark Bomani hasa kuhusu utaratibu wa wazi utakaowezesha wachimbaji wadogo wadogo kupewa maeneo yao wenyewe kama Tume hiyo ilivyobaini.

(ii) Mapema mwezi huu nilimwandikia Waziri/Naibu Waziri, juu ya mambo matatu ambayo nilitumaini yangekuwa na majibu kabla ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara. Mambo hayo ni:-

(a) Nilishauri Kituo cha Zamani cha Umeme cha TANESCO kifufuliwe kwani hivi sasa kiko *dormant* baada ya *National Grid* kufika.

(b) Nimeona katika kifungu cha 121 cha Hotuba kuwa, Tosamaganga imetajwa. Nisingetegemea maelezo marefu katika Hotuba. Kwa hiyo, naomba kujua kwa uwazi mipango gani imeandaliwa kuhusu kituo hiki ?

(c) Mwaka uliopita ilipangwa kupeleka umeme Pawaga, Jimbo la Ismani. Umeme huo ungepitia Kata ya Kiwere katika Jimbo la Kalenga. Nimefahamishwa kwamba, Mradi huo umeahirishwa. Nashauri angalau kwa mwaka huu, Mradi huo ufufuliwe chini ya REA hata kama ni kwa awamu, toka Iringa hadi Kiwere kama awamu ya mwanzo.

(d) Kifungu 22 cha Hotuba kinazungumzia umeme wa Kilolo unaoendelea. Kabla ya kufika mpakani, *line* inapitia Vijiji vya Nyabula, Igula, Kilambo, Ndiwili na pembeni kuna

Vijiji vya Negabihi na Mlanda. Swali langu ni je, isingewezekana kuingiza vijiji hivyo katika ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa sababu Waziri na Naibu Waziri, wanajitahidi sana katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa maoni yafuatayo:-

(1) Suala la ujenzi holela wa vituo vya mafuta. Kuna ujenzi wa vituo vya mafuta karibu na makazi ya watu, karibu na nyumba za kulala wageni na karibu na sokoni. Kamati ya Nishati na Madini, ililijadili suala hili na kuudhibiti ujenzi holela. EWURA izipelekee Halmashuri kanuni au mwongozo ili wanaojenga vituo vya mafuta, waweze kuzitumia kuepusha madhara ya kiafya na mazingira

(2) Katika maeneo mengi hapa nchini, bado yapo malalamiko ya wananchi kutolipwa fidia kwa maeneo yao waliyoyaacha walipopisha migodi. Wakati tunasubiri sheria mpya, Serikali itafute mkakati mwingine ili kuhakikisha kero hii inaisha katika maeneo yanayolalamikiwa, ambayo ni chanzo cha uhasama kati ya wawekezaji na wananchi.

(3) Mwaka 2007, Rais Kikwete alizindua Mradi wa MCDP, uliokuwa umelenga kuanzisha miradi mbalimbali ili Vijiji vya Ng'wigimbi, Idukilo, Nyene, Buchambi, Masagara, Bulima na Utemini, viweze kupata umeme zikiwemo Shule za Sekondari za Kata kwenye Vijiji hivyo. Naiomba Serikali itoe msukumo katika utekelezaji wa Mradi huu wa MCDP.

(4) Serikali ishaahidi umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu kupitia Mpango wa Umeme Vijijini (REA), gharama ni ndogo, naomba Serikali ieleze itatekeleza lini ahadi hii.

(5) Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka umeme kwenye Mji wa Ndoleleji, ambao una fursa za kukua kiuchumi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Umeme Wilayani Mbozi, ambayo ilianza mwaka 2001/2002, haijatekelezwa hadi leo (zaidi ya miaka saba sasa); inashangaza na kusikitisha sana. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo: Ruanda – Iyula – Idiwili (km 26); Mahenje – Igunda (km 5); na Vwawa – Hasamba (km 13).

Mheshimiwa Spika, Miradi yote mitatu ilishaanza kujengwa kwa kuchimbia nguzo na kuweka vikombe. Baadhi ya nguzo zimeanza kuoza na nyingine zimeungua moto, kwa kuwa zimekaa chini (ardhini) muda mrefu bila uangalizi wowote.

Mheshimiwa Spika, nimelipigia kelele sana suala hili, lakini bila mafanikio yoyote. Aidha, ikumbukwe kwamba, zaidi ya Sh. 200 milioni zilishatumika kwa kazi ambayo haijakamilika. Naiomba Serikali ikamilishe Miradi hiyo mapema inavyowezekana; na katika hili nataka Serikali itoe tamko, vinginevyo sitaunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Novemba, 2008, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya ziara Mkoani Mbeya na Wilayani Mbozi. Akiwa Wilayani Mbozi, Mheshimiwa Rais alifanya ziara Kata ya Itaka, ambapo alifungua Kituo cha Afya na kuhutubia mkutano mkubwa wa hadhara. Moja ya ombi ambalo wananchi walimwomba Mheshimiwa Rais ni kupatiwa umeme. Katika majibu yake, Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi kwamba, ombi lao limepokelewa na kwamba, Waziri mwenye dhamana ya umeme ataagizwa alifanyie kazi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumfikishia rasmi Mheshimiwa Waziri, ahadi hiyo ya Rais kwa Wananchi wa Kata hiyo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aliweke jambo hili kwenye program ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba, Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbozi imeunganishwa kwenye Grid ya Taifa, lakini umeme ambao umekuwa ukitumika ni ule wa kutoka Zambia. Hata hivyo, umeme wa kutoka Zambia hukatika ovyo ovyo na mara kadhaa umewasababishia hasara kubwa sana, baadhi ya wateja kwa kuharibu vyombo vyao.

Mheshimiwa Spika, ombi la Wananchi wa Mbozi ni kuunganishwa kwenye Grid ya Taifa ili kuwaondolea usumbufu mkubwa wa kukatika katika kwa umeme ovyo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, itachukua muda mrefu sana kuwafikishia Watanzania wengi umeme kupitia Grid ya Taifa. Hivyo, umeme wa jua (*Solar Power*), ndiyo ungekuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wengi. Hata hivyo, umeme huo nao siyo rahisi kiasi cha wananchi wengi kumudu gharama zake. Kwa kawaida, gharama za kununua vifaa na kufunga umeme wa jua si chini ya shilingi milioni moja. Sasa hapa unajiuliza ; ni Watanzania wangapi watamudu bei hiyo ? Dhahiri ni wachache sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali izungumze na wafanyabiashara wa vifaa vya *solar power* ili waone namna ya kupunguza bei ya vifaa hivyo. Aidha, wafanyabiashara hao waombwe watoe vifaa hivyo kwa mkopo. Mimi naamini wananchi wana uwezo mdogo kiuchumi na njia pekee ya kuwafaa watumie umeme huo ni kwa njia ya mkopo tu.

Mheshimiwa Spika, vituo vingi vya mafuta hasa vya Mikoa ya Morogoro na Pwani, hujihusisha na uchakachaji wa mafuta. Jambo hili ni baya sana, kwani magari yote yatakayotumia mafuta hayo *pump* zake hufa.

Nashauri pamoja na adhabu zinazochukuliwa na kutolewa kwa wahasika na kwa kuzingatia kwamba, kwa sasa kuna vituo vingi sana vya mafuta nchini, vituo vyote vya mafuta vitakavyojihusisha na biashara hiyo chafu sana, wafungiwe kabisa kufanya biashara ya mafuta. Aidha, EWURA pamoja na kazi nzuri wanayofanya, sasa wazidishe jitihada kuwasaka wafanyabiashara wote wanaojihusisha na uchakachaji mafuta.

Mheshimiwa Spika, yamegunduliwa makaa ya mawe kwenye mipaka ya Wilaya za Mbozi na Chunya. Kwa upande wa Mbozi, makaa hayo yapo katika Kijiji cha Magamba. Hata hivyo, kuna mvutano wa chini chini kati ya Halmashauri hizo mbili, kuhusu hasa yalipo makaa hayo ya mawe. Naiomba Wizara itoe mwongozo, najua kinachogombewa ni mapato, hili lisuluhishwe mapema inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ninalotaka kujua hapa ni je, Wizara inajua kwamba magari kubwa sana (*Trucks*) yamekuwa yanabeba tani nyingi sana za makaa hayo kwa

kisingizio kwamba yanapelekwa nje ya nchi kuya-test kama yanafaa au la? Hivi kupima ubora wa makaa hayo kunahitajika tani gapi ?

Mheshimiwa Spika, mafuta ni suala la Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, hivi karibuni Waziri mwenye dhamana ya mafuta kwa Zanzibar, alikaririwa akisema kupitia Baraza la Wawakilishi na Baraza hilo kuunga mkono kwamba, Zanzibar inatoa mafuta kwenye orodha ya Mambo ya Muungano. Hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini Viongozi wanavunja Katiba waliyoapa kuilinda? Nashauri Serikali ya Muungano, ishughulikie jambo hili, likiachwa hivyo lilivyojitokeza, linaleta ufa mkubwa sana kwenye Muungano wetu. Ahsante sana.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vilivyomo vyote, kwa kunijalia uzima wa afya na kuniwezesha kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa uwasilishaji mzuri wa Hotuba yake. Pia kwa kazi ngumu aliyokuwa nayo na jinsi anavyokabiliana nayo, pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Watendaji wote, kwa namna wanavyoshirikiana na Waziri katika kutekeleza majukumu waliyopewa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu aliweka ahadi ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya wakati wa kampeni na wakati wa ziara mbalimbali. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali mara tu baada ya kupitisha bajeti hii, itimize ahadi ya Rais wetu, tukizingatia bado mwaka mmoja tu tunaingia kwenye Uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, itakuwa aibu na fedheha kama ahadi hizo hazikutekelezwa, pia tutamuweka pahala pagumu Rais, pamoja na Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Mungu katujalia katupa asilimia nyingi sana za kuipatia nchi yetu mapato ikiwemo wanyama, madini, Ziwa Victoria, Mlima Kilimanjaro, pamoja na watu wazuri wa makabila mbalimbali kwa kutumia rasilimali hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni Siku ya Nishati na Madini, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wataalamu wake, waangalie upya mikataba iliyopo katika madini, kwa sababu ni ya zamani na mapato makubwa zaidi yanakwenda kwa wawekezaji na Taifa linakula hasara kubwa. Hii ni kinyume na matakwa ya Mwenyezi Mungu, aliyetuletea neema hii ambayo aliileta kwa Watanzania na si kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakigugumizi gani kuifanyia marekebisho mikataba hii? Madini ni yetu tunashindwa nini hadi leo? Hata mirabaha hailipwi vizuri, Watanzania wanalalamika; tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, Rais aliunda Tume kuchunguza mikataba lakini hadi leo hakuna kinachoeleweka. Ninamwomba Waziri atuambie kuna nini baada ya kuundwa Tume hiyo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Hotuba ya Waziri. Hata hivyo, nina hoja ya dharura juu ya umeme katika Manispaa ya Songea:-

Manispaa ipo gizani, mitambo kila siku inashindwa kufanya kazi, mji wote ni giza tu. Hivi kwa nini mitambo inayoletwa Songea ni *used* tu? Mara itoke Kihansi mara Mtwara yote ni *used*.

Umeme wa Grid tumeambiwa hadi 2013, lakini wakati huu wananchi wamechanganyikiwa, wafanyabiasha wanaona bora wahame Mji wa Songea.

Mkoa wa Ruvuma ndio wazalishaji, lakini viwanda hakuna kwa sababu ya umeme.

Wanafunzi mpaka wanaandamana hali ni mbaya. TANESCO Songea hata ofisi hawana, wanapanga tu. Jengo la TANESCO katika Manispaa ya Songea ni gofu, baya, linaharibu sura ya Manispaa, lakini pia hadi ajali zinatokea hapo.

Mheshimiwa Spika, je, mbona mikoa yote ina majengo mazuri tu ya TANESCO; kwa nini Ruvuma hali ipo hivyo?

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania tangu enzi ya mawe hadi sasa wanapikia mafiga matatu tu. Wazee wa Shinyanga, Mwanza, wanauawa kwa sababu ya Wizara hii, nishati ya kupikia hakuna. Mashule, Magereza hali ya mazingira ni mbaya na majiko sanifu ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, REA wameanza vizuri, wapewe uwezo zaidi. Wazalishaji na wadau wa nishati kama TASEA, TATEDO, CARMATEC, Probec na nishati mbadala, wasaidiwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kutuletea hotuba inayowatia moyo wananchi hasa sisi wa Rufiji.

Mheshimiwa Spika, hoja zangu:-

1. Serikali iharakishe mpango wa kufua umeme wa *Stiegler's Gorge Hydropower*. Mradi huu peke yake ni ukombozi wa Taifa. Mradi utatoa umeme kwa matumizi ya ndani na ziada ya kuuza nchi za nje. Soko lipo tayari. Aidha, programu za umwagiliaji zingalikalisha mazao ya nafaka na mazao ya biashara kwa wingi. Hii ingaliinua uchumi wetu na kupunguza umaskini.

2. Tunashukuru umeme wa Songosongo utapitia na kutumika katika Vijiji vya Somanga, Muhoro, Nyamwage, Kindwitwi mpaka Utete (Makao Makuu ya Wilaya). Aidha, kwa umeme huo kufika Ikwiriri, Kibiti, Mchukuzi Mission na Nungu ni jambo la kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya, vijiji vifuatavyo vya Kiwanga, Chumbi na Utunge (kati ya Nyamwage na Kindwitwi), naomba navyo vipate umeme huu wa Songosongo katika Mradi huu.

3. Serikali itoe ruzuku kwa wajasiriamali wa *solar equipment* ili bei ya vifaa hivyo iwawezeshe watu wengi kuvinunua na kuongeza matumizi ya *solar power* katika nchi yetu (*Rural Electrification*).

4. Somangafungu, Kilwa na Utete, ziko upande mmoja wa Mto Rufiji. Kwa hiyo, wakati tunasubiri utaratibu wa kupitisha nyaya za umeme kuvuka Daraja la Mkapa, sisi wa ng'ambo ya Utete, Nyamwage, Muhoro, Somanga na Kilwa, ambao hatuna haja ya kusubiri Daraja la Mkapa, tuanze kupata umeme wakati Serikali inasubiri kupitisha umeme huo katika Daraja la Mkapa.

5. Pindi umeme wa Songosongo ukifika Ikwiriri, basi tunaomba *generator* moja toka Ikwiriri ipelekwe katika Kijiji cha Biashara ya Ufaki cha Mloka. Kijiji hiki kina kambi za utalii zaidi ya 20 na wanaweza kulipia gharama za umeme huo. Tafadhali sana, tunaomba *generator* hilo moja lipelekwe Mloka. Pale Ikwiriri pana majenereta mawili (*used, under capacity*).

*Generator* hilo litaongeza chachu katika biashara ya utalii kwenye Kijiji cha Mloka katika Hifadhi ya *Selous Game Reserve*.

Mwisho, Mheshimiwa Waziri tusaidie sisi Warufiji hususan Mji wa Utete (Makao Mkuu ya Wilaya ya Rufiji) tutoke Kizani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri majenereta ambayo yamepangwa kuagizwa 2009/2010, tunashauri *strongly* kuanza kujenga miundombinu ya majengo, uzio na hata sehemu ya kuweka mashine zitakapofika katika Wilaya ya Kasulu na Kibondo.

Mheshimiwa Spika, shilingi 1.5 bilioni zilizotengwa tangu mwaka jana, zianze kutumika sasa. Ningependa kufahamu kazi hii itaanza lini?

Mheshimiwa Spika, chini ya Programu ya *Tanzania Energy Development and Access Expansion Program (TEDAP)*, sasa ni zamu ya Kigoma na hasa Kasulu. Tafadhali, Programu hii ianze mara moja kwenye Shule za Sekondari za Kata za Kasulu na Vituo vya Afya. (Barua yangu kwa *Director General* wa REA yahusika). Nitashukuru sana, iwapo mpango huu utaanza sasa kabla ya October, 2009.

Mheshimiwa Spika, *Malagalasi MCC Project (from Uvinza to Kasulu)*, utekelezaji wake tunaubiri sana. Ninashauri *line* ya kupeleka umeme Wilaya ya Kasulu uongeze sura ya pili kama ifuatavyo:-

1. Mpango ulioko Uk.102 wa Kitabu cha Hotuba, ninauunga mkono sana.

2. Eplion II iwe Uvinza – Basanza – Rungwe mpya – Ahsante Nyerere na Sogeeni; eneo hili ni *potential* sana kwa kilimo na kuna sehemu mbili za umwagiliaji Basanza na Rungwe mpya. Ninaomba sana njia hii ya pili iongezwe katika usanifu wa kina kwa Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Wamissionari wa Kabanga wanaendesha Mradi wa *Mini-Hydro* na kuzalisha umeme katika Kituo cha Kabanga Mission, Kabanga Hospital na Kabanga TTC. Ninaomba na kushauri REA waone uwezekano wa kufanya *Joint Effort* kati ya Mission, REA na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ili kusambaza umeme huo katika Vijiji vya Kabanga na Msambara.

Mheshimiwa Spika, nashukuru REA wamechukua hatua za awali za kufikia azma hii. Ninaomba REA wasaidiane na Halmashauri ya Wilaya ili kuupanua Mradi huu uwe na manufaa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba REA ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ili kuona uwezekano wa kuzalisha umeme wa *Mini-Hydro* katika Mto Ruchugi. Niombe REA ipeleke Wahandisi Washauri katika Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu mbalimbali katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za EWURA wanazozifanya katika udhibiti wa bei, bado kuna upungufu katika uchakachaji wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua EWURA wamekwishawachukulia hatua gani wafanyabiashara wa mafuta waliogundulika wamechanganya mafuta?

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali za kupeleka mashine za kufua umeme Kigoma, ningeomba ifanye haraka kwa sababu wananchi wanaendelea kupata matatizo makubwa sana. Wanawake na watoto wanapata shida sana, hata wengine kupoteza maisha kutokana na ukosefu wa umeme katika hospitali zetu zilizopo Mkoani Kigoma, wanakosa huduma ya vipimo mbalimbali kutokana na ukosefu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, wanawake na vijana wanashindwa kuzalisha kutokana na ukosefu wa umeme; mashine hazisagi, uzalishaji wa mafuta yanayotokana na mawese haupo kwa sababu ya kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, kodi ya mafuta ya taa iende sambamba na petroli na dizeli ili kukomesha uchakachaji wa mafuta. Bila kuongeza kodi kwenye mafuta ya taa, tatizo hili haliwezi kwisha.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma una madini mengi, nilikuwa naomba Wizara ilete watafiti ili waweze kusaidia kutafiti madini yaliyopo, kusudi wananchi waweze kupata fursa ya kujipatia kipato na kukuza uchumi kutokana na madini yaliyopo Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri, ambayo ni ngumu kuliko Wizara zote. Wizara hii ina changamoto nyingi za Nishati na Madini, ambayo yote ni muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia utafiti wa madini katika maeneo yote kwenye nchi yetu. Sehemu kubwa ya wilaya yetu ina madini, lakini hakuna utafiti unaoeleweka kujua aina ya madini na yako maeneo gani, jambo hilo ni muhimu sana kujulikana kwa ajili ya kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika miaka minne iliyopita, sikuunga mkono Wizara hii, kutokana na ahadi ya kila mara bila kupelekewa umeme. Kwa mara ya kwanza umeme umewaka toka Kenya. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na Wataalam wako. Nilitamka kwamba, kama umeme hautapatikana Jimboni Longido, sitagombea Ubunge kwenye Jimbo langu. Napenda kushukuru kwa umeme kufika Namanga. Naomba Serikali waharakishe umeme kufika Makao Makuu Longido. Kazi hii imeanza kwa nguvu, lakini kasi imepungua kwa ajili ya kutokuwa na nguzo. Cha kushangaza, nguzo zinapita kwenda Kenya toka kwetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Longido ni miongoni mwa Wilaya zenye eneo kubwa. Ni vigumu sana kutoa umeme Longido kwenda maeneo mengine ya Kamwanga au Tingatinga, ambazo zinapakana na Wilaya za Rombo na Siha.

Mheshimiwa Spika, nategemea Mheshimiwa Waziri atakumbuka barua yangu niliyomwandikia, kuhusu umeme toka Rombo kufika Kamwanga ni kilometa kumi tu na umeme kutoka Sanya Juu kupita Ngarenairobi kufika Kata ya Tingatinga, Jimbo la Longido. Napenda kukumbushia kwamba, Mradi wa Umeme Vijijini unaweza kuvuta umeme huo kufika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya zote tunazopakana nazo zina umeme kwa muda mrefu. Hii imeleta Wananchi wa Longido kujiuliza kuna nini mbona Serikali inabagua wananchi wake kwani wenzetu wana barabara za lami, wana umeme lakini Longido hawana chochote? Naomba Waziri akumbuke barua yangu ya umeme kufika maeneo hayo, ambapo umeme toka Longido hauwezi kufika kutokana na umbali.

Mheshimiwa Spika, endapo Kiwanda cha Lake Natron kitafunguliwa na kuanzishwa, umeme wa Longido unaweza kupelekwa huko na hapo itakuwa rahisi umeme huo kufika Vijiji vya Ngorongoro na kuelekea Makao Makuu ya Ngorongoro/Loliondo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa nguvu zote. Hii ni mara yangu ya kwanza, kuunga mkono hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Wizara kuwa, migogoro kati ya wananchi na wawekezaji wa madini itapungua ama kwisha kabisa, endapo Serikali itakuwa na sera ya kuwa watakaofaidi kwanza na uwekezaji huo ni wananchi wa maeneo hayo. Wananchi waliopo maeneo yanayozalisha dhahabu ni lazima wafanane na dhahabu, vinginevyo matatizo hayawezi kwisha kati ya wananchi na wawekezaji wa migodi ya madini.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, ningependa kuishauri Serikali kuhusu uendelezaji wa Kituo cha *Southern and Eastern Africa Mineral Centre (SEAMIC)*, kilichoko Kunduchi Dar es Salaam. Kituo hiki kilianzishwa mwaka 1977, kwa nia nzuri sana ya



kuunganisha nguvu ya nchi husika za Kusini na Afrika Mashariki za kuendeleza na kulinda soko la madini kwa faida ya wananchi na mataifa yao.

Mheshimiwa Spika, kituo hiki kina vifaa vyote muhimu vya kupima viwango vya madini, ikiwa ni pamoja na tathmini ya miamba. Hivi sasa Tanzania ni Mwenyekiti wa Nchi Wanachama, lakini malengo yaliyokuwepo ya kituo hiki yametekelezwa. Malengo hayo ni pamoja na: Kuratibu utafutaji wa rasilimali za madini na huduma husika; kuendeleza wachimbaji wenyeji wa madini; kujenga uelewa wa *potential* ya madini; kuwezesha na kusimamia *responsible investment and free flow of capital and labour* kwa nchi husika; na kuwezesha ukuzaji wa rasilimali ya madini (*promotion of mining prospects and social impact*).

Mheshimiwa Spika, Je, nini hatima ya Kituo hiki kilichoanzishwa na Baba wa Taifa ambaye alikuwa anaona miaka 50 mbele?

Mheshimiwa Spika, Sera ya Madini inasema uchimbaji wa vito ni kwa wazawa tu; vipi Tanzanite One walipata leseni wageni?

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Waziri anieleze *copy right* ya jina la Tanzanite ni ya nani? Kama Tanzania haina *copy right*; maana ya hati miliki ya jina hilo itafanyika lini?

Mheshimiwa Spika, Starbucks Coffee ya Marekani, kwa muda mrefu walikuwa wanatumia Ethiopian Coffee kama yao. Ethiopia walipostuka walikataa, lakini baada ya malumbano mahakamani, Copy Right International waliwapa haki Ethiopia kwa kuwa ndio wazalishaji wa kahawa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nani ana Copy Right ya jina la Tanzanite?

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba nzuri. Pia nimpongeze Naibu Waziri na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kweli nimepokea ushirikiano mkubwa sana, pale ninapofuatilia kero za wachimbaji wadogo na suala zima la umeme katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri na utekelezaji wa Miradi ya MCC katika Vijiji vya Katoro, Lwamgasa, Nyangusu na Bukoli, iliyoelezwa katika Jedwali Na.4 (d), Ukurasa 102 na utekelezaji wake kukamilika mwaka 2012. Ningependa kujua ni lini hasa Mradi huu unaanza rasmi utekelezaji wake katika vijiji hivi?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwenye mchango wangu huu, wakati wa ziara mbalimbali za Viongozi Waandamizi wa Wizara hii, Waziri na Naibu Waziri, kwa nyakati mbalimbali wamefika Jimboni kwangu na wamekutana na Viongozi na wametoa ahadi kwenye mikutano ya hadhara Bukoli, Nyamgusu, Lwamgasa na Katoro.

Mheshimiwa Spika, naomba nitambue na kwa maana hiyo niishukuru Serikali, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu, kwa Miradi hii ya MCC. Hata hivyo, kwa kuwa tarehe za utekelezaji zinakuwa zinatamkwa, lakini wananchi hawaoni utakelezaji wa moja kwa moja unaanza, naomba Mheshimiwa Waziri, atoe kauli itakayowafikia Wananchi wa Jimbo langu na Wilaya ya Geita, ambayo wataridhika nayo kuhusu ratiba ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hii itanisaidia kujua na kuwasiliana na Wananchi wa Jimbo la Busanda kwa uhakika zaidi. Kumbuka tatizo la umeme ni kubwa na kulingana na ahadi kwa wananchi zilizotolewa na Waziri wa Nishati na Madini wakati wa kampeni za Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Busanda ni kwamba, umeme utawaka Katoro, Bukoli, Nyangasa na Lwamgasa kufikia mwisho wa mwaka 2009. Hivyo, ninaiomba Serikali inisaidie kutatua tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili ni suala la wachimbaji wadogo, hawana maeneo kwa ajili ya uchimbaji. Ninaiomba Serikali iwaongeze maeneo wachimbaji wadogo katika maeneo ya Nyarugusu, Nyajagwe, Lwamgasa na Kaseme, maana maeneo waliyopewa hayatoshi kabisa. Hii itaongeza na kuinua uchumi wa wananchi hawa ambao tegemeo lao ni uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, ombi la pili kwa Serikali ni mikopo kwa wachimbaji wadogo wadogo, maana hawana vifaa vya uchimbaji. Hata hivyo, wako katika mazingira magumu. Hii itawapa moyo wachimbaji hawa na watainua hali za maisha yao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ili nisiwe mchache wa fadhila, nichukue nafasi hii, kuishukuru Serikali kwa kuwa imewajali wachimbaji wadogo, kwa kuwatengea kiasi cha shilingi bilion moja katika Mfuko wa kuwakopesha wachimbaji. Ingawa kiasi hiki cha pesa ni kidogo sana, ukilinganisha na idadi ya wachimbaji wadogo waliopo nchini.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ninaiomba Serikali iangalie namna ya kuongeza Mfuko huu. Jimboni kwangu tayari wananchi hawa, yaani wachimbaji wadogo, wamejiunga kwenye vikundi vya maendeleo na wanasubiri tu ukopeshwaji kama Ilani ya Uchaguzi inavyosema. Hivyo, ninaomba utekelezaji uanze mara moja.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa msisitizo mkubwa kwamba, Serikali kupitia Wizara hii, itimize ahadi hizi kama ilivyoahidi suala zima la umeme, kuongeza maeneo kwa wachimbaji wadogo na mikopo kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa, kabla mwekezaji hajakabidhiwa eneo kwa shughuli zake, Serikali ihakikishe inawalipa wananchi na kuwatafutia maeneo ya kuishi ili kuhakikisha kuwa, hakuna uhasama kati yao. Hata kama wawekezaji wanatoa fedha, Serikali isimamie ulipaji.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii, kwa kazi nzuri ya kusimamia maendeleo ya Sekta za Nishati na Madini hapa nchini. Baada ya pongezi hizi, naomba kuwasilisha maombi ya Wananchi wa Manyoni kama ifuatavyo:-

(a) Tunashukuru sana Mradi wa Umeme Manyoni – Kilimatinde – Kintinku (Manyoni), kuingizwa katika Progamu ya REA. Ombi ni kuharakisha utekelezaji, kwani bado haujaanza na matazamio ya wananchi wa maeneo hayo ni makubwa sana.

(b) Ombi la Mradi mpya kutoka Tarafa ya Nkonko (Manyoni) ni kwamba, Wananchi wa Tarafa ya Nkonko hasa maeneo ya Chikola – Iteka – Nkonko hadi Sanza nao waingizwe katika Mpango wa REA. Tarafa hii imo pembezoni mwa Mhuasi Game Reserve na Kizigo Game Reserve, kuna shughuli za uwindaji wa kitalii, kilimo, ufugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kilio cha Wananchi wa Tarafa hii (Nkonko), kifikishwe REA na kifanyiwe kazi.

Wizara hii ilifanya jambo jema kuwatambua Wachimbaji Wadogo wa Londoni na kuanza kuwapa leseni 2003/2004. Utoaji leseni huo unafanyika pole pole mno. Yapo maombi mengi Wizarani, ambayo bado hayajafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ombi la wachimbaji hao ni kwamba, wapewe leseni zao kama walivyoomba ili kuhalalisha kisheria umiliki wa maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maombi haya ya wananchi, sasa natamka rasmi kwamba, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Wataalamu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kutuletea hotuba yenye dira, mipango mikakati ya kuibua uchumi, kupiga vita umaskini na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Timu yake, wameonesha njia ya kuthubutu na kuchukua hatua. Leo hii tunaweza kuzungumzia uchimbaji wa *uranium*, Tanzania. Naomba waendeleo na moyo huu wa kizalendo na uchungu walionao kuhusu umaskini uliokithiri ndani ya utajiri tuliopewa na Mungu.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja hii ya kishistoria, kwa kutoa ushauri/maombi kwa lengo la kuiboresha na kusisitiza mambo machache katika hotuba hii kama yafuatayo:-

Ibara ya 141 Uk. 78, Sheria ya Madini ya Mwaka 1998. Nashauri marekebisho ya Sheria yazingatie mpango wa kuainisha maeneo nchini, ambayo yamefanyiwa utafiti kuhusu upatikanaji wa madini, vito na gesi. Ramani inayoonesha maeneo hayo, ipatikane wakati wowote Mbunge anapohitaji.

Ibara ya 144 Uk. 80, STAMICO imefanya kazi nzuri kuratibu na kusimamia shughuli za madini na gesi nchini. Ipewe fungu la kutosha la fedha katika bajeti ili iweze kusimamia shughuli ya kuhudumia wachimbaji wadogo wadogo.

Mafunzo yatolewayo na STAMICO yapanuliwe katika maeneo yote nchini, hususan maeneo ambayo hakuna rigid, lakini madini yamegunduliwa na wachimbaji wadogo wadogo wameanza kuchimba hususan Wilaya ya Rorya. Naomba wataalamu kutoka STAMICO, watembelee maeneo ya Rorya ili kuonana na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu sasa, naomba Viongozi wa Wizara watoe tamko kuhusu gesi ya Hiliium, ambayo inapatikana Wilaya ya Rorya. Naomba Mheshimiwa Waziri na Wataalam kutoka STAMICO, waje Rorya kukagua gesi ya Hiliium katika Kijiji cha Nyamusi Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri atoe tamko hapa Bungeni kuhusu gesi ya Hillium, iliyogunduliwa miaka kumi iliyopita na hadi leo hakuna dalili yoyote ya kuendelezwa. Wananchi wanauliza kulikoni?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba baada ya kulizungumzia hilo, nipate majibu yenye matumaini.

**MHE. DKT. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba angalau na mimi nijiunge na Wabunge wenzangu katika kuchangia hoja hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujikita katika uchangiaji huo, ningependa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, ambao ni vijana wachapa kazi usiku na mchana bila kuchoka; na laiti kama Watendaji chini ya Katibu Mkuu wakiiga mfano huo, basi matatizo ya Watanzania yatapungua kama sio kuisha kabisa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijikite kwenye uchangiaji. Mkoa wa Morogoro ndiko unakozalishwa umeme wa maji (*Hydro power*) kwa wingi zaidi, lakini cha kusikitisha, vijiji vingi inakopita Gridi ya Taifa hawapati umeme. Hii siyo sahihi hata kidogo, kwani Waswahili husema kwamba safari huanzia nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kuwapa/kuwapatia umeme watu hawa, hakuhitaji gharama kubwa kwa vile gridi imepita katika maeneo yao; hivyo basi, kilichobaki ni kuwafungia transform ya kupozea umeme ili nao wafaidi matunda ya umeme katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandaji kiholela wa bili ya umeme, hii ni kuwaumiza wananchi watumia huduma. Naomba hili lifanyiwe utafiti, TANESCO wakusanye fedha bila kuwaumiza watumia huduma. Hapa nina maana kubaini, ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukubwa wa nchi yetu, si rahisi wananchi wote wa Tanzania kufikiwa na umeme wa TANESCO; hivyo basi Serikali ijitahidi kuwatafuta wawekezaji wengine ili wajenge vituo vidogo vidogo vya kuzalisha umeme ili waiuzie Serikali kupitia Shirika la TANESCO ili wananchi walio wengi waweze kutumia umeme kuharakisha maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza na suala la bei ya mafuta aina ya petrol. Bei ya mafuta ni biashara huria, kutokana na uhuria huo kila mfanyabiashara anapanga bei kulingana na alivyonunua. Hapa naishukuru Serikali kupitia EWURA kuwa, bei ya mafuta isipande zaidi ya Sh.1,400, lakini cha kushangaza ni kwamba, EWURA hiyo hiyo inahimiza wale wote wanaouza chini ya bei hiyo, EWURA inawachukulia hatua, yaani na wao wapandishe kufikia Sh.1,400 eti kwa kigezo kwamba, wanashusha bei wanachanganya mafuta. Je, EWURA hiyo kwa nini isitumie vyombo vyo kugundua kama kuna uchanganyaji wa mafuta badala ya kutumia kigezo cha bei? Hii siyo haki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uchanganyaji mafuta, dalili za hujuma zinaonekana; mfano katika Barabara ya Chalinze - Dar es Salaam, hasa katika eneo la kuanzia Mlandizi hadi Kibaha, kuna vituo utitili na vilivyojengewa ukuta mrefu sana nyuma ya vituo hivyo. Tujiulize; hivi kweli katika maeneo hayo kuna wateja wengi zaidi kuliko maeneo mengine ya Tanzania? Cha kushangaza, ukipita barabarani vituo vingine viko kimya kabisa, hakuna hata mteja mmoja; sasa najiuliza hawa wanapataje faida? Hii maana yake, wanapata faida ya kuchanganya mafuta (chakachuwa).

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali haiwezi kuweka sheria ya kutoruhusu ukuta mrefu kwenye vituo hivyo? Wabunge na wananchi wengi wamekuwa wakilalamikia maeneo hayo,

sasa kuna kigugumizi gani kuchukua hatua mara moja au kuna mkono wa mtu? Hii inalitia Taifa aibu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zao zote, kwa kazi nzuri na kuwezesha kuwa na mpango elekezi wa umeme wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kupewa maelezo na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Dhamira ya Serikali ya kuanzisha Mpango wa Ununuzi wa Mafuta ya petroli kwa shehena kubwa (Bulk Purchasing); ulilenga katika kupunguza gharama katika mfumo wa bei, gharama za usafirishaji na kupunguza msongamano wa meli za mafuta ya petrol bandarini. Inaelekea mpango huu kukwama. Kwa nini Taifa likubali kupoteza unafuu huo muhimu kwa faida ya Wananchi na Taifa kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maandalizi ya utekelezaji wa mpango huo, yanahitaji kujenga uwezo wa kupokea meli kubwa za uwezo wa shehena kubwa. Kwa nini maandalizi hayo hayaanzi kwa kuijenga upya UBM iweze kupokea meli kubwa?

Mheshimiwa Spika, kwa nini maandalizi ya hifadhi ya mafuta yasifanyike wakati Serikali ina hisa katika kampuni inayomiliki hifadhi kubwa za matenki yaliyokuwa kampuni ya kusafisha mafuta TIPER?

Ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Mafuta ghafi na bomba la mafuta – Dar es Salaam – Mwanza. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha kuwepo kwa Mpango huo chini ya Kampuni ya *Noor Oil Industrial Technology (NOIT)*. Je, dhamira hiyo inaashiria nini?

(i) Kuanza upya usafishaji wa mafuta kwa kuagiza mafuta ghafi kutoka nje.

(ii) Au tayari au zipo dalili za uhakika za kupata mafuta ghafi hapa nchini ili yasafishwe katika kiwanda hicho kipya?

(iii) Je, sasa Kampuni iliyonunua Kiwanda cha TIPER haikusudii tena kutumia eneo hilo kama kiwanda na hifadhi kubwa ya mafuta ya petrol?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kupata maelezo ya mwongozo kwa jambo hilo.

Ujenzi wa Bomba la Kusafirishia Mafuta – Dar es Salaam – Mwanza ulikwama kwa muda mrefu na pia ulikuwa na mgogoro dhidi ya kampuni ya kizalendo. Je, mgogoro huo sasa umefikia wapi? Hivi kweli dhamira hiyo ipo baada ya Kenya kukamilisha usafirishaji wa mafuta kwa bomba kutoka Mombasa hadi Kisumu na Uganda?

Kutotekelezwa kwa Ahadi za Wizara ya Nishati na Madini kuweka Transforma Kijiji cha Songa. Songa ni kijiji karibu na Hale na kinaitikia TANESCO Korogwe:-

- Tarehe 14 Novemba, 2006, Mheshimiwa Naibu Waziri (wakati huo Mheshimiwa Bernard Membe), aliahidi kupeleka transformu Songa.

- Tarehe 4 Aprili, 2007 nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kumkumbushia ahadi hiyo. Barua Kumbukumbu Na. NJM/224/02.

- Tarehe 2 Julai, 2008 nilimkumbusha tena Mheshimiwa Waziri barua Kumb. Na. MB/JMZ/WNM/224.

- Niliuliza pia swali Na.78 Mwaka 2008.

- Tarehe 14 Januari, 2009 nilionana na aliyekuwa Kaimu Meneja TANESCO Korogwe, Bwana Julius Mbuya (Meneja Bwana Hussein Mwamkuja alikuwa safarini). Nilimpa Barua Kumb. Na. MB.JMZ/TNS/KOR/601/14/1 na nilikwenda nae maeneo ya Songa, Mandela, Makole na Kwafungo. Pamoja na yote hayo, transformi moja tu ya ahadi haijafungwa. Pamoja na kwamba, Songa ingekuwepo katika Mpango wa MCC, utekelezaji bado unakwama.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ione umuhimu wa kutekeleza ahadi za namna hiyo kwa wananchi.

Umekuwepo ucheleweshaji wa uanzishwaji wa Mfuko wa Mradi wa Umeme Vijijini licha ya kwamba sasa watendaji wamekwishateuliwa. Kutokuwepo kwa fedha, kunachangia kukwama kwa ahadi kadhaa, pamoja na zilizotolewa, kuweka umeme wa jua katika Zahanati za Kambai, Mashewa, Kisiwani, Kwatango, Zirai, Kiwanda na Kumburu katika Wilaya ya Muheza. Ni lini fedha zitatolewa na ahadi hizo kutekelezwa?

Mpango wa awali wa MCC Mkoa wa Tanga 2007/08, ulikuwa na vijiji 19, Wilaya ya Muheza vikiwemo Ngomeni/Bagamoyo. Ninayo nakala ya Miradi hiyo kutoka TANESCO Mkoa na Wilaya Muheza. Tarehe 03 Julai, 2006 nilimwandikia Meneja wa TANESCO Muheza, Kumb. Na. MB/JMZ/TSC/112/6/9 kuhusu dharura ya kupeleka umeme Ngomeni. Mradi wa Maji Pongwe Mlingano unatekelezwa kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais na kuwa tenki linakamilishwa kujengwa hapo Ngomeni na kwamba, umeme utahitajika hapo kukwamua Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, badala yake tarehe 4 Julai, 2009, uliitishwa mkutano wa wadau uliofanyika Mkongwe Hotel, lakini Mbunge hakualikwa na hapo ikatolewa taarifa mpya ya Miradi ya MCC! Mkoa wa Tanga uliandaliwa na Eng. Yusuph A. Mkindi na kuhudhuriwa na TANESCO Mkoa na Wilaya na Vijiji vya Ngomeni/Bagamoyo vikaondolewa; na Muheza kubaki na vijiji 9 badala ya 17. Kibaya zaidi, vimeondolewa vijiji vilivyolenga kutelekeza Mradi wa Maji – Pongwe – Mlingano; ahadi ya Rais!

Mheshimiwa Spika, nashauri Vijiji hivyo virejeshwe, licha ya kuunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, gesi asilia ni suala la Muungano la muda mrefu, imegundulika hapa nchini. Kwa kuwa nchi hii inakubali kuwepo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; ni kwa kiasi gani Serikali hiyo imefaidika na gesi asilia?

Mheshimiwa Spika, umeanzishwa Mradi wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga. Je, Mradi huo utakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, ukiangali Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 48, kifungu cha 80 na 81, umezungumzia juu ya utafutaji wa *uranium* hapa nchini. Utafiti huo acha uendelee, lakini

nitoe tahadhali, baada ya kukamilika utafiti huo na kuanza kuchimbwa *uranium* hiyo, faida itakuwa ndogo kama ilivyo kwenye migodi ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 53, kifungu cha 83, kinazungumzia juu ya Mgodini wa North Mara na mgogoro uliotokea baina ya mgodi na wananchi. Licha ya tatizo la fidia kwa wananchi wa eneo, pia inawezekana wananchi wa eneo hilo kiasia wameathirika na mazingira ya mgodi. Je, watalipwa fidia?

Mheshimiwa Spika, Mgodini wa North Mara uko karibu sana na Vijiji na matokeo yake, wananchi wameathirika kwa vumbi na miripuko. Je, Serikali inaweza kuwaondoa wananchi hao vijiji ambayo viko karibu sana na mgodi?

Mheshimiwa Spika, nia ya Wizara ni kuliboresha Shirika la TANESCO ili liweze kujitegemea na kusambaza umeme nchini. Shirika hilo lina wateja ambao ni watu binafsi, pamoja na Taasisi za Serikali. Watu binafsi wamebanwa walipe ankara zao za umeme au kwa kutumia Luku; vinginevyo umeme unakatwa. Je, hawa wateja wa Ofisi za Serikali na Nyumba za Serikali wanalipa ankara zao za umeme? Je, Kambi za Jeshi na Vituo vya Polisi zinalipa umeme au zinatumia umeme bure?

Mheshimiwa Spika, kama Serikali hailipi umeme kwa matumizi ya taasisi zake, hilo ni tatizo na TANESCO itaendelea kuwa tegemezi, badala ya kutoa mapato yao kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ya kupunguza adha kubwa ya ukosefu wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Musoma, tunazo sekondari kumi na sita zilizo kando kando ya Manispaa ya Musoma, pamoja na Kata za pembezoni na zote hazina umeme na mahitaji makubwa ya umeme kwa matumizi ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua lini Mheshimiwa Waziri atakuja Musoma na atembelee maeneo hasa ya sekondari zetu ili wanafunzi waweze kusoma na kujifunza kwa kutumia mtandao?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri akumbuke gharama za mtu kuweka umeme nyumbani nazo ziko juu. Napenda kujua mpango wa Wizara kuwapa unafuu hata kwa kulipa kwa *installment*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini. Pili, namshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya Tanzania. Nchi yetu ina neema kubwa kwa kuwa na madini mengi ya aina mbalimbali kama dhahabu, almasi na tanzanite. Pamoja na madini mengi, bado nchi yetu ni maskini, baada ya kuingia kwa mikataba ambayo haina manufaa kwa wananchi. Kazi ambayo imebaki kwa Watanzania ni kuomba omba kwa nchi ambazo zinachuma dhahabu kutoka hapa nchini. Je, nchi yetu itaendelea kuomba misaada hadi lini?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuingia ubia na makampuni ambayo yanachimba madini hapa nchini, kuwa na hisa kwa makampuni yote ili nchi iweze kunufaika na migodi ya madini tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kwenye Sekta hii ya Madini. Nimeshaongea maneno mengi hasa kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu na Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia mazingira, lakini kwa leo naomba kutoa ushauri ufuatao:-

- (a) Serikali kuwa na hisa na makampuni yote ya migodi hapa nchini.
- (b) Wachimbaji wadogo wadogo wapewe maeneo ya kuchimba, pamoja na kupewa mkopo hasa Wananchi wa Nyamongo, ambao ni Kata za Kemambo na Matongo.
- (c) Wananchi wa Nyamongo walipwe fidia na mwekezaji ili Wananchi hao wasipate madhara ambayo yanatokana na uchafuzi wa mazingira.
- (d) Kampuni ya North Mara itoe ajira kwa wananchi wanaoishi jirani na mgodi hasa Wananchi wa Kata za Kemambo, Matongo, Nyamwaga, Nyarokoba na Kibasuku ili kuleta mahusiano mazuri.
- (e) Kampuni ya Barrick ifanye biashara na wananchi kama kuleta stationary, chakula na mahitaji mengine.
- (f) Kampuni ya North Mara (Barrick), itoe huduma za muhimu kwa jamii kama vile barabara, zahanati, umeme, michezo, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchafuzi wa mazingira ambao umeathiri sana Wananchi wa Kata za Kemambo, Matongo, Kibasuku, Nyamwaga na Nyarokoba hasa uchafuzi wa Mto Tigite, ambao unapata kemikali kutoka mgodini; ni kweli uchafuzi mkubwa umefanyika kwenye Mto Tigite, ambao umesababisha madhara makubwa kama vile wananchi kufa na mifugo mingi imekufa. Serikali ichukue hatua za haraka, kuwachimbia visima kwa matumizi ya nyumbani. Matongo:-

- Kampuni ifanye juhudi za haraka kuzuia kemikali zisingie Mto Tigite mara moja.
- Wananchi walipwe fidia yao mara moja ili wahame wasiendeleo kupata madhara makubwa.
- Waliopata madhara, wahusika kama Serikali au mwekezaji wawajibike kulipa fidia kwa wale waliopoteza maisha na waharamikie matibabu ya wagonjwa wote na wafikishwe mahakamani.
- Wantanzania wanahitaji Taarifa ya Kamati ya Bunge iliyokwenda North Mara itolewe Bungeni. Wananchi wa Tarime na Watanzania, wanataka kufahamu ni lini Taarifa hiyo itatolewa rasmi Bungeni?



Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limekuwa na tabia ya kuua wananchi mara kwa mara. Mauaji hayo hupelekea mahusiano mabaya kati ya Wananchi na Jeshi la Polisi na wananchi na mgodi (mwekezaji). Wananchi wengi wameuliwa na polisi nao ni Marwa Nyansinge, Mohono Marwa Gibare, Hezroni Mangwena, Clever Jackson na Christopher.

Vilevile hivi karibuni wameuliwa wananchi wawili pale Nyamongo: Chacha Nyamakomo, aliyekuwa Darasa la saba ; na Mwitwa Chacha Matiko. Wengine wamepata majeraha makubwa ya risasi, nao ni Amina Mussa, aliyekuwa mjamzito lakini Mungu alimuepusha; na kijana wa Darara la Tano, alipata majeraha makubwa ya risasi. Naitaka Serikali iwachukulie hatua za kisheria wale waliohusika.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kuwa, kwenye bajeti ya mwaka 2009/2010, tumepangiwa kupata umeme kutoka Tarime – Itingo. Umeme huo utasaidia Wananchi wa Vijiji vya Nyamwigura, Rosana, Nyarero, Kemakorere, Nyamwaga, Keisangora, Masiba, Koberi, Bungurere, Itingo, Kangandui, Kegonga na Masanga, kunufaika sana na umeme. Wananchi wa maeneo hayo watapata maendeleo makubwa. Naitaka Serikali ianze haraka, kutekeleza mradi huo mara moja kwa pesa za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nampongeze Wazira, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa taarifa nzuri walivyotoa hapa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia umeme. Umeme ni kitu muhimu katika suala zima la maendeleo. Sijaona mkakati wa ujenzi wa Kituo cha Kupozea Umeme eneo la Mabuki; nitapenda kuona mkakati ukoje.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa MCC kuonesha nia za kuwapa umeme Wananchi wa Vijiji vya Buhingo – Seeke – Nyamayinza.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa maeneo hayo, wanasubiri kwa hamu kubwa umeme huo. Ombi ni kwa Vijiji vya Nyang’homango, Isesa, Mbalama na Mbarika kupitia Igenge. Nashauri TAENESCO watumie umeme uliopo Ihele ni karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Kanyerere, Kolomije na Bugomba vimepitiwa na nguzo za umeme uliokwenda Sumve. Cha ajabu hakuna kinachoendelea mbali na ahadi za Wilaya, naomba kufahamu nipate majibu ya kupewa umeme Vijiji vya Kolomije, Kanyerere na Bugomba.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wananyanyaswa sana na makampuni makubwa, tunaomba safari hii eneo la Bulunda litolewe kwa wachimbaji wadogo. Kampuni ya IAM Gold Tanzania zamani East Africa Mine Ltd., ambayo utafiti umeanza 1992. Tunaomba sana eneo hilo liwe la wachimbaji wadogo wadogo; wapo na wamekwishaunda ushirika wao na wengine wana vikundi vyao.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na matumaini makubwa sana kwamba, REA ipo Vijiji vya Nduha, Kasololo, Matate, Sumbugu, Bugisha hadi Mbarika, eneo hili linahitaji huduma ya umeme awamu ijayo, naomba sana. Vikumbukwe pia Vijiji vya Isakamawe, Kijima na Mwamaguhwa. Visiachwe lakini ikumbukwe umeme wa MCC unatokea Inonelwa Buhingo –

Seeke – Nyamanyinza, sehemu ya Kabale - Busongo – Mwagiligili hadi Mwawile hawakuguswa na Mradi huo. Kama Mradi utakuwa endelevu, basi vijiji hivyo vipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza umekuwa ni historia tu; hivi utekelezaji wake hasa utanza lini? Ikumbukwe kuwa Mradi huu utatia changamoto ya uchelewaji wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini ya almasi Kijiji cha Mabuki, Wilayani Misungwi ni sehemu ambayo wachimbaji wadogo wanahitaji msaada wa vifaa na pia masoko. Wizara ilifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwatakie kazi njema na utekelezaji mwema bila kusahau Vijiji vyangu vya Kolomije na Kanyerere katika bajeti hii. Ahsante.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara ya 2008/09, Ludewa ilipangiwa kujengewa Ofisi ya Madini. Ofisi haikujengwa. Katika bajeti hii, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Afisa Madini Ludewa, haujatajwa tena. Je, fedha za 2008/09 zilikwenda wapi na kwa nini sasa Mradi huo hauko kwenye Bajeti ya 2009/2010?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua na kushukuru ujio wa umeme Ludewa Mjini, lakini umeme huo umebaki kwenye eneo dogo la katikati ya Mji na kuitia hasara TANESCO, kwa vile watumiaji umeme ni wachache. TANESCO wavute umeme na kuusogeza kwenye maeneo mengi ya Mji wa Ludewa.

Mheshimiwa Spika, inaelekea mchakato kuelekea uchimbaji wa madini ya *uranium* umeanza kushika kasi. Kwa nini suala hili linafanywa kwa siri hadi inafikia kampuni kama ya Mantir Tanzania Ltd. kutaka kuanza uchimbaji 2012? Kuna haja ya *debate* ya wananchi (wadau) kuhusu hatima ya madini haya. Kuna haja ya kufanya *Strategic Environmental Assessment* ili kutuongoza katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, nimewasilisha kwa Waziri, barua ya malalamiko ya wanaushirika wa Tumaini Mining Coop. Society Ltd. (Ludewa), kuhusu kupuuzwa kwa maaagizo ya Waziri kupitia barua ya tarehe 08 Desemba, 2008 kuhusu mgawanyo wa machimbo ya Nyamigwina – Ibumi (Ludewa), ambapo hadi leo wanaushirika wale hawajapata leseni yao. Badala yake, kuna dana dana nyingi na ufiada unaofanywa na Maafisa wa Kanda ya Mbeya hususan Bwana Mtui. Naomba maelezo kuhusu uzembe huu, danadana hizi na ufiada huu na nijulishwe ni lini leseni itatolewa kwa wapiga kura wangu?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18 (sehemu ya 29), inaonesha kuna Mradi wa Makambako – Songea KV 132 *Transmission Line*, unafadhiliwa na Serikali ya Uswisi; wakati mwaka jana (2008/2009), tulielezwa kuwa Mradi huo unafadhiliwa na SIDA (Swedeni) na kwamba, tayari fedha ilikuwa imetolewa. Vipi kumekuwa na mabadiliko ya ufadhili?

Mheshimiwa Spika, kazi saba zitakazofanywa mwaka 2009/2010, zimeorodheshwa Uk.69 (sehemu ya 123), lakini Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2013. Tuambiwe kwa uwazi ni kazi zipi kati ya hizo saba zitakamilika 2009/2010 kwa fedha iliyooombwa kwenye bajeti?

Mheshimiwa Spika, UNDP wametoa Sh.59.0 milioni kwa ajili ya kugharimia hatua za awali za Mradi wa Maporomoko ya Maji (*Mini-Hydro*), Kata za Mlangali/Lupanga Wilayani Ludewa, kwa makubaliano ya maandishi ya REA kwamba, REA wataendeleza Mradi huo. REA walitembelea Mradi huo, lakini katika ukurasa wa 64 REA wanawadanganya wapiga kura wangu?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini, kwa ujasiri, umahiri na kazi nzuri. Hongera kwa hotuba nzuri ya bajeti. Nampongeza kwa dhiti, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima (Mb), Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa kazi nzuri. Aidha, nampongeza rafiki yangu, Arthur Mwakapugi, Katibu Mkuu, Kamishna wa Nishati, Bashiri Mrindoko na Kamishna wa Madini, Peter Kafumu, kwa kutayarisha mpango mzuri. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Viongozi na Watendaji wa Wizara, kwa mpango wa kupeleka umeme katika Vijiji vya Ngulu, Kwakoa, Toloha na Kigonigoni. Mradi ulio chini ya REA, bado haujaanza kutekelezwa japo ulikuwa kwenye mpango wa mwaka 2008/2009. Naomba Mradi huu utekelezwe mapema, *Quarter* ya kwanza ya mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, naomba pia TANESCO iharakishe utekelezaji wa miradi midogo ya umeme katika Wilaya ya Mwanga. , Vijiji hivyo ni Handeni, Kiverenge, Kiwanja, Kuchama Ndambwe, Kisangiro na Lambo eneo la Kiverenge.

Mheshimiwa Spika, nawatakia heri katika bajeti hii nzuri sana.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 96 wa Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, unaonesha Miradi inayosimamiwa na Wakala wa Umeme Vijijini, yaani REA. Hivi kwa nini Wilaya ya Makete haijapewa Mradi hata mmoja wa REA wakati Wilaya nyingine zinaonekana kwenye ukurasa huo zina miradi hata zaidi ya miwili? Wilaya ya Makete, imeathirika sana na janga la UKIMWI kutokana na umaskini na hivyo inahitaji sana kipaumbele katika mikakati ya maendeleo. Kwa nini REA haikuona umuhimu wa kuweka kipaumbele cha kupeleka umeme katika vijiji vya Makete?

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Umeme Vijijini iwekewe mkakati wa wazi. Napenda kuipongeza Wizara kwa kukamilisha Mpango wa Taifa (mkakati wa uzalishaji umeme), yaani Power System Master Plan (PSMP), PSMP unaonesha mipango ya muda mfupi, ya kati na ya muda mrefu ya uzalishaji umeme. Mpango huu utapunguza malalamiko, kwani kutakuwa na utaratibu wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Umeme katika Vijiji vya Mfumbi, Matamba, Ujuni na Mpangala – Makete, TANESCO waliahidi katika mwaka huu wa 2009 watasambaza umeme kwenye vijiji vilivyotajwa hapo juu. Fedha tayari zimetengwa, lakini hadi leo ni robo ya pili ya mwaka imepita hakuna kilichofanyika. Naomba maelezo utekelezaji wake utakuwa lini? Wananchi walikwishaambiwa kuhusu kuanza kwa miradi hii, hivi sasa tutawaambia nini?

Mheshimiwa Spika, Miradi ya MCC, inaonekana kusuasua sana. Tupewe maelezo kwa nini Miradi hii inachelewa? Tupewe ratiba ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, bei ya nguzo za umeme iko juu sana. Miti ya nguzo za umeme inastawi sana Mufindi, lakini cha ajabu ni kwamba, nguzo zinazotoka Afrika Kusini, bei iko juu; kwa nini nguzo hizi za Mufindi zinazauza ghali sana?

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kushusha bei ya nguzo ili wananchi wengi wapate fursa ya kuunganishwa kwenye mtandao wa umeme.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, suala la mahitaji ya umeme ni la watu wote. Umeme unatumika katika nyanja zote za maisha kuanzia kuendesha viwanda, kutumia majumbani, mashuleni, kuendeshea treni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hii ni moja na mpango wowote wa usambazaji umeme, usipokuwa unajali kugawa sawa sawa, basi kwa vyovyote vile maeneo ya jamii yatatofautiana sana. Sehemu ambazo zitakuwa zimepitiwa na mgao wa umeme, maendeleo yao ni mazuri na makubwa na ya kisasa sana. Ni dhahiri kuwa, wale ambao hawana hata tone la umeme, watoto wao wanakuwa nyuma wakati wote. Pale wenzao wanapozungumzia kompyuta, internet, televisheni na kadhalika. Wale ambao hawajafikiwa na umeme wao, lugha hii ni miujiza na kwao huona giza tupu badala ya kuwa mwanga.

Mheshimiwa Spika, wakati TANESCO inashughulikia umeme wa mijini, najua REA inashughulikia umeme wa vijijini. Hapa lazima niseme kweli kwamba, kama REA haitakuwa na Master Plan ya jitihada zao za kueneza umeme katika nchi hii, ingekuwa vizuri sana wakiweka wazi mikakati yao ya utendaji mwaka hadi mwaka. Hii itawezesha sehemu zile ambazo hazina umeme kule vijijini, wataweza kuishi kwa matumaini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Morogoro Vijijini, haina umeme kabisa. Hivyo, lugha ya kudai umeme ufike kwenye vijiji ni sawa na msemu wa Marehemu Indira Gandhi, aliposema wakati wewe unalia na kudai huna viatu, mwenzi analia hana mguu wa kuvalia viatu. Hali hii ndiyo iliyoko katika Wilaya ya Morogoro Vijijini.

Kwa uwezo na baraka zake Mungu, Wilaya hii kubwa ya Morogoro Vijijini, kwa mara ya kwanza tangu dunia imeumbwa, Serikali kwa kupitia Mradi wa MCC, sasa itapata umeme toka Morogoro Mjini hadi Matombo.

Mheshimiwa Spika, Matombo ni Kata ya kwanza ya Jimbo la Morogoro kusini. Wakati umeme unategemewa kufikishwa Matombo, Halmashauri ya Morogoro Vijijini imeamua kwamba, Makao Makuu ya Halmashauri yake ihamie kwenye Kijiji cha Mvuha.

Kutoka Matombo hadi Mvuha ni kilometa 16 tu. Mvuha patakuwa na Hospitali ya Wilaya, Ofisi ya Polisi Wilaya, Ofisi ya Wilaya ya CCM na vyombo vingine ambavyo vinastahili kuwepo Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ombi rasmi kwa REA kupeleka umeme Mvuha.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Morogoro Kusini, lina vyanzo vya umeme sehemu mbalimbali za maporomoko ya maji katika mito midogo midogo.

Mheshimiwa Spika, naomba niendeleo kuiomba TANESCO, iende Kisaki Station na kuona lile jenereta kubwa la TAZARA Station Kisaki, kama linaweza kugawa umeme Kijiji cha Kisaki Station.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. EMMANUEL J. NCHIMBI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri William Ngeleja, Naibu Waziri Adam Malima, Katibu Mkuu Arthur Mwakapugi na Watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wa Songea Mjini, kuishukuru sana Serikali kwa kufanikisha upatikanaji wa Dola za Marekani milioni 70.4 kutoka Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la DIDA ili kufanikisha mradi wa laini ya umeme ya KV 132 kutoka Makambako mpaka Songea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri, kwa ahadi ya Wizara yake mwaka 2007 kuwa, wakati Wananchi wa Songea Mjini wanasubiri kukamilika kwa Mradi wa Gridi ya Taifa 2013, Serikali itanunua mashine mpya za kusaidia kupunguza makali ya mgao wa umeme, ambao sasa imefikia saa 18 mpaka siku 3.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Songea Mjini, wana imani kubwa na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Dkt. Idrisa Rashidi; hivyo wana imani kuwa ahadi zote zitatekelezwa. Kwa niaba yao, natanguliza shukrani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa hotuba iliyosomwa na Waziri wa Nishati na Madini, yenye kuonesha wizara ilikotoka, ilipo na mwelekeo wa utekelezaji ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji katika eneo la Mgusu, wamenyanyasika sana. Kwa kuwa tatizo hili liko mikononi mwa Serikali, naomba lishughulikiwe na kupata majibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono uchimbaji wa wachimbaji wadogo wadogo ila tatizo kubwa ni uangalifu wa sumu za madini, mfano, mercury; madini yanayotumika kuchambua dhahabu. Madini haya kama hautatolewa utaratibu mzuri za kutoathiri wananchi, iko siku kutajitokeza madhara makubwa ndani ya jamii. Hivyo, nitoe ushauri kwa Wataalam wa Wizara hii, kuelekeza nguvu machimboni, kutoa elimu ya jinsi gani wananchi wasidhurike na madini hayo pindi wanapochimba.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu mashimo ya Machimbo ya Buhemba yametelekezwa, baada ya wachimbaji kusimama. Tatizo ni mashimo yaliyoachwa. Serikali inasema nini juu ya mashimo hayo? Naiomba Serikali itembelee eneo hilo na kutoa majibu, kama uchimbaji umekwisha basi mashimo yafukiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma, tuliingia gizani mwaka 2007 mwezi Oktoba; na kwa kuwa Wizara ya Nishati na Madini ilijua hilo; na kwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini alipotembelea Kigoma na kuahidi kuwa yatatengenezwa majenereta ambayo yataweza kukidhi Mji wa Kigoma (Manispaa); na majenereta hayo Mheshimiwa Waziri aliahidi kuwa yatatengenezwa kwa muda wa miezi 18; na kwa kuwa katika Bunge hili hili aliahidi kuwa yako tayari, na kama yako tayari ni lini sasa yataletwa katika Mji huo? Leo tuambiwe muda husika ni mwezi wa ngapi?

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Nishati na Madini, kwa kuleta Hotuba ya Bajeti, ambayo inatekelezeka. Nawapongeza pia Viongozi hawa kwa kuhimili mikiki mikiki ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika suala la umeme wa Kusini, yaani gesi ya Mnazi Bay inayotengeneza umeme. Tunashukuru kuwa, Mradi wa Mtwara Energy Project karibu utakamilika na kuleta umeme wa uhakika katika Wilaya ya Masasi, Nachingwea, Ruangwa, Newala, Tandahimba na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ihakikishe kukamilika kwa Mradi wa Umeme wa Mtwara ili Wilaya za Kusini, ziweze kuwa na umeme wa uhakika na wa kudumu. Hili linawezekana, endapo Wizara itasimamia utekelezaji wa Mradi huu. Hivi sasa ARTUMAS wanaunganisha Nyangao – Ndanda ili hatimaye Miji ya Masasi, Nachingwea, Ruangwa, Newala na Tandahimba, waweze kupata umeme wa kutosha. Waziri atuthibitishie kuwa hakutakuwa na mabadiliko yoyote yale.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kampuni mpya kununua hisa 51% za ARTUMAS, sasa tuna uhakika zaidi wa kutekeleza Miradi mikubwa kwa mfano ya kuzalisha MW 300 ili kuunganisha na Gridi ya Taifa. Hivyo hivyo, Miradi mikubwa ya viwanda vya sementi, mbolea na chuma chakavu ili kuzalisha chuma na kadhalika. Miradi hii itatoa ajira kubwa kwa Wananchi wa Mikoa ya Kusini na nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke umuhimu kwa miradi mikubwa, umeme wa vijijini peke yake hautoshi, miradi niliyoitaja sasa ishughulikiwe.

Nakubaliana sana na maudhui ya hotuba yao, inafurahisha kwa kweli nami naunga mkono hoja.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Katibu Mkuu, Author Mwakapugi na Makamishna wote na Watendaji wao. Nawapongeza katika uandaaji wa bajeti yao, iliyowasilishwa vizuri na Waziri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nianze na miradi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya na Umeme Vijijini. Waziri alisema namnukuu, aya ya 111, ukurasa wa 64: “Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini na TANESCO, itaendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya zilizobaki, ukiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 43 (b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, kuhakikisha kuwa Makao Makuu ya Wilaya zote zisizo na umeme yanapatiwa umeme.”

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Namtumbo haina umeme kabisa na nimekuwa naahidiwa toka mwaka 2006. Serikali inataja na kupanga Miradi kupitia Wakala wa Nishati Vijijini na TANESCO, bila hata kuiona Namtumbo kama haina umeme. Namtumbo hakuna umeme Jamani!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wanaweza kuja kunieleza kuwa Namtumbo ipo katika Mradi wa kuunganishwa katika Gridi ya Taifa wa Makambako – Songea wa KV 132/33. Sisi Namtumbo hatuna umeme kabisa, lakini wilaya nyingine zitakazofikiwa na Mradi huu, ndio zina umeme; hivyo Mradi huu ambao unategemewa 2013 utakuja kuziunganisha tu katika Gridi. Naomba tuwekeni katika Mradi wa (REA) kama Wilaya nyingine ili tuanze kuwa na umeme hasa katika vijiji ambavyo havitafikiwa na umeme huu wa Gridi. Kuna tarafa ziko kilomita zaidi ya 220 karibu na Msumbiji, ambazo hazitafikiwa na Mradi huu mkubwa, lakini pia kuna mambo yanaweza kutazamwa kama *potential* kwa Miradi ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini? Naomba tuanze ili kuvutia wawekezaji.

Naomba pia nipate ufafanuzi wa Miradi iliyotajwa katika Hotuba ya Waziri, aya ya 113, itakayofanyiwa upembuzi yakinifu kwa kugharimiwa na Serikali ya Norway, kwa Ruvuma umeandikwa KWITANDA badala ya jina tunalolifahamu la KITANDA. Naomba ufafanuzi kama kulikuwa na *typing error* urekebishwe.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama nchi nyingine duniani, tunategemea uchumi wake kukuza kwa mapato yatokanayo na maliasili tulizonazo hasa kama tutazisimamia vizuri, tutahamasisha uwekezaji katika utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani katika maliasili zetu hususan madini.

Ninachotaka kushauri, simamieni vizuri utajiri wa madini tulionayo kwa kufanya utafiti na kuangalia kitaalam mapato yatakayotokana na miradi husika. Hivyo, tusimamie hatua zote tusiache kama tulivyo achia katika migodi ya dhahabu na matokeo yake ikatugharimu kupeleka timu ya wataalam kuanza kuchunguza toka walipoanza. Naamini kuna mali nyingine imetoka wakati ule bila kodi yetu kupatikana ilivyopasa.

Naomba sasa iimarishwe STAMICO, iweze kufanya *prospecting* yenyewe kwa hatua zote za Drilling na kutambua kiasi gani cha mashapu tulionayo katika maeneo watakayofanya hivyo na thamani yake na kuyatangaza katika *stock exchange* za Toronto, Australia, UK na America, kwa ajili ya kupata wawekezaji ambao tuta-*negotiate* nao katika *shares*, kulingana na *Deposit* tuliyonayo katika ardhi yetu kama ndio mtaji wa mradi husika.

Mwisho, nawashauri Waziri na Naibu Waziri kwamba, wao ni *combination* nzuri sana hapo Wizarani. Waziri ni Mwanasheria mzuri. Naibu Waziri ni Mchumi mzuri.

Tuitumie taaluma yenu kuinua Sekta hii. Naamini hatutarudi katika mikataba isiyo *favourable* kwa nchi yetu. Naunga mkono hoja

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizarani hii, kwa kazi nzito wanayoifanya katika kuhakikisha wanatekeleza yale yote yanayotakiwa kutekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi la kwangu ni swali tu; ni lini mashine zote zilizokuwa Njombe zitaletwa Mafia kama Serikali ilivyoahidi? Pili, ni lini mitambo ya umeme

inayotumia upepo itaanza kuwekwa katika Wilaya ya Mafia hasa katika Tarafa ya Kaskazini katika Vijiji vya Bweni, Kanga, Jimbo, Benja, Jojo, Kirongwe, Baleni, Chunguruma na Ndagoni na katika maeneo yote ya upande wa Tarafa hiyo ya Kaskazini?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nawatakia maisha bora na hekima, Viongozi wetu wote wa Wizara hiyo na Mola awalinde na Mahasidi wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa ujumla.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kutembelea Miradi ya Umeme Vijiji vya Msindo, Kizungu, Ijinyu, Bangalala, Mhezi, Kijomu na kadhalika?

Je, maandalizi ya Miradi hiyo yamefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, kwa kupata fursa ya kuchangia. Nampongeza Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima (Mb), Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Naomba Waziri atimize ahadi ya kupeleka umeme eneo la Kijiji cha Mgongo kilichopo umbali wa kilomita tano toka eneo la Shelui, ahadi aliyoitia mwaka wa fedha wa 2008/09.

Miradi ya Umeme Vijiji vya Maluga, Kutusha, Zinziligi, Mkulu, Simbalungwala na Kibigiri, naomba ikamilishwe kama ambavyo TANESCO Mkoa, ilishakubali kuitekeleza. Waziri atoe msukumo kwa TANESCO Mkoa.

Wachimbaji wadogo wadogo wa Madini eneo la Maluga, wanaomba kugawiwa eneo la uchimbaji. Naomba Wizara kupitia Kamishna wa Madini, kuliondoa tatizo hilo kwani sasa ni muda mrefu, maombi ya Wananchi wa Kijiji hiki hayashughulikiwi; pamoja na juhudi za mara kwa mara kupitia kwangu (Mbunge wao) na hata kumwona Waziri na kadhalika.

Utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Upepo uendao kasi wa Kijiji cha Kisasida utaanza lini ili uzalishaji wake usaidie matumizi kwa Wananchi wa Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam, kwa kuandaa Hotuba nzuri ya Bajeti.

Nishati ni Sekta kubwa na yenye matatizo mengi na changamoto zake ni nyingi sana. Madini ni hivyo hivyo. Wizara iandae pendekezo na hoja za kuzigawa sekta hizi ili kuwepo na Wizara kwa kila sekta.



Leseni za uchimbaji madini bado zinatolewa bila ridhaa ya wenyeji wa vijiji husika. Aidha, leseni hizi zimekuwa zikitolewa na kuchukua sehemu kubwa mno ya ardhi ya vijiji na kusababisha migogoro mikubwa. Wizara izuie tabia hii na kufuata taratibu za sheria zilizopo.

Usambazaji wa umeme vijijini, ufuate ratiba zinazopendekezwa na kupitishwa Bungeni.

Usimamizi wa umeme uzingatiwe na Wizara iibane TANESCO, ipunguze uzembe unaosababisha ajali nyingi za nyumba kuungua kwa sababu ya shoti ya umeme.

Ratiba ya umeme wa Kiperesa, Matu, Engusero hadi Dosidosi, izingatiwe ili mradi ukamilike kwa wakati.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati na Madini. Ninaanza kwa kuunga mkono hoja hii.

Nilipokuwa nachangia kwa maandishi hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, niliomba kukipatia umeme wa uhakika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rengemba, kilichoko Wilayani Mufindi. Chuo hiki kipo karibu na Barabara Kuu iendayo Mbeya na nguzo za umeme zipo. Chuo hiki kina historia kubwa, kwani kilikabidhiwa kwa Serikali kwa lengo la kuwaendeleza wanawake. Chuo kimekuwa hakina umeme wa uhakika. Naomba nipate majibu lini watapatiwa umeme?

Umeme ni muhimu sana katika maendeleo ya Elimu. Kwa vile Serikali kwa kushirikiana na Wananchi, imefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba, kila Kata inakuwa na shule, mpango ambao umewezesha watoto wengi vijijini kupata elimu, watoto hawa watapata elimu bora zaidi kama shule zitawezeshwa kuwa na umeme. Hivyo, Serikali ihakikishe shule hizi zinapata umeme wa jua, ikiwa ni pamoja na mabweni/hosteli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Nawasilisha.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu uko katika matumizi ya Nishati ya Umeme. Naunga mkono uanzishaji wa umeme mbadala wa kutumia madini ya uranium. Umeme wa kutumia uranium ni mzuri sana na bei yake ni ndogo sana. Hivyo, vituo vya nyuklia vikifunguliwa hata viwili hivi kwa ajili ya matumizi ya umeme kuendesha mitambo mbalimbali. Mimi nilikwenda Korea Kusini, wamekubali kuwekeza kwenye umeme huo na kuweza kununua uranium, kwani hadi sasa Korea Kusini kuna tatizo la uranium, wanaagiza toka nje ya nchi yao. Nami niko tayari kushirikiana na Wizara kuleta teknolojia hiyo mpya. Nimeshapeleka *documents* zote za uwekezaji nchini Korea Kusini na wao wamekubali kuleta teknolojia hiyo mpya. Nimekaa kule kwa muda wa siku tano. *Documents* hizo nimepata kwa Director General TIC, Mr. Ole Naiko.

Mwisho, nakushukuru sana kwa kunisaidia Jimbo langu kupata umeme hata kama bado kuwashwa katika Vijiji vya Igima, Mdandu na Mhadi katika Wilaya Njombe.

Hata hivyo, naomba umeme katika Shule ya Sekondari Ilembula – Njombe, kwani umeme upo Ilembula, kinachotakiwa ni kupeleka nguzo na transform.

Pia ninaomba umeme Shule ya Sekondari Wanike, Kata ya Mdandu – Njombe. Umeme wa Vijijini upelekwe Chuo cha Maendeleo – Ilembula – Njombe, Kata ya Igosi na Tarafa ya Imalinyi.

Mheshimiwa Spika, sina zaidi, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nawashukuru Wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe, kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni. Nami niko pamoja nao.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niipongeze Hotuba safi sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wananchi wengi sana wanaotumia umeme, wanasikitika na kulalamika kuwa, wanabambikiziwa madeni makubwa sana wakati wakipelekewa bili za umeme, jambo ambalo ni sugu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, ili TANESCO waepukane na malalamiko hayo, basi huduma ya umeme ya kutumia LUKU izidi kuboreshwa kwa watumiaji wote wa umeme hapa nchini, hasa Miji mikubwa kama Dar es Salaam na kadhalika. Matumizi ya Luku yatakuwa ndio suluhisho hasa la kuondoa malalamiko ya kubambikiziwa deni la umeme kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar wananunua umeme kutoka Tanzania Bara. Basi naiomba Wizara ya Nishati na Madini Tanzania, iishauri Wizara ya Nishati na Madini Zanzibar, nako wateja wawezeshwe kutumia LUKU.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mwananchi wa kawaida, ambaye anatumia umeme, wakati mwingine hupelekwa bili ambayo ina deni la Sh. 60,000. Fedha hizo kwa wananchi wa kawaida ni nyingi. Mwananchi huyo huyo anasubiriwa na kodi ya nyumba, kusomesha watoto na huduma za lazima za kila siku. Je, deni hili kweli atalikabili ghafla? Ndio maana Wananchi wengi sana huwa wanakatiwa umeme kwenye nyumba zao na kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme hivi sasa ni neno au jambo la starehe. Umeme ni jambo la lazima kwa kila mwananchi kupata huduma. Kwa hiyo, nashauri kuwa Wizara iwe na mkakati wa kutoa huduma ya umeme kwa kila mtu na kuondoa malalamiko kwa wateja. Kwa hiyo ni vyema hivi sasa Shirika liwape wateja fursa kubwa ya kutumia LUKU, kwa sababu mteja atakuwa mwangalifu sana kwa matumizi ya umeme. Pia atakuwa na bajeti yake ya matumizi, pale Luku ikimalizika, anakwenda kununua umeme papo hapo. Hapo patakuwa hakuna malalamiko ya kubambikiziwa madeni.

Mheshimiwa Spika, kama LUKU zinapatikana bei ghali, basi shirika lipunguze ughali huo ili wananchi wote wamudu kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kusiwe na urasimu wa kuzipata LUKU hizo kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake yenye kuelezea kwa kina, masuala mbalimbali kuhusu Nishati na Madini nchini. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hiyo, bila kuwasahau Wafanyakazi wote wa Wizara hiyo na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, naunga miono hoja ya Waziri, pamoja na juhudi zote anazofanya kuhakikisha masuala muhimu ya Wizara yake, yakiwemo matatizo, yanafanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Nishati ya Umeme ni kati ya nguzo kuu katika kuleta mapinduzi ya maendeleo yetu na kuhakikisha hifadhi ya mazingira kama chanzo cha nishati ya viwanda na majumbani. Naipongeza Wizara ya Nishati na Madini, kupitia Shirika la TANESCO, kwa kuweka bayana mpango wa kuendeleza Sekta ya Umeme 2000 – 2033. Katika mpango huu, yameelezwa mambo mbalimbali ya msingi, ikiwemo ya kupanua Gridi ya Taifa hadi kufikia mikoa yote nchini ifikapo 2020 na kuunganisha wateja wapya ili kuweza kufikia 75% ya wananchi wanaopata umeme ifikapo mwaka 2033.

Mpango huu ni wa kupongezwa, kwani unaweka wazi namna sehemu mbalimbali zitakavyofikiwa. Pamoja na kuwepo mpango huu, kuna haja ya kutazama upya hususan ratiba ya uzalishaji umeme. Stiegler’s Gorge kwenye Mto Rufiji, ilikwishafanyiwa utafiti na kubainika kuwa, ndiyo chanzo kikubwa kinachoweza kuzaliwa umeme wa nguvu ya maji. Kama nguvu zote zingewekwa kwenye chanzo hicho, kama Msumbiji walivyoweza kufanya katika kupata umeme kutoka Bwawa la Cabora Bassa kwenye Mito ya Zambezi, badala ya kuhangaika na vyanzo vidogo na kuweka uzalishaji wa umeme. Stiegler’s Gorge katika awamu tatu kuanzia mwaka 2020 hadi 2026, tungeweza kupata umeme huo kabla ya mwaka 2015. Hii ingeweza kuleta matumaini kwa maeneo mengi nchini, kupata matumaini ya kufikiwa na umeme katika kipindi kisichozidi miaka 15 kijacho. Naamini kama mpango huu ungepewa kipaumbele, hata Vijiji vya Makao Makuu ya Kata za Jimbo la Mbozi Magharibi, ambavyo kwa utaratibu huu wa sasa havitapata umeme kwa miaka 100 ijayo, vingeweza kufikiwa na umeme huo ndani ya miaka 20 ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika swali langu la msingi na la nyongeza hapo tarehe 21 Julai, 2009, nilitaka Serikali ifanye utafiti wa uwezekano wa kupata nishati ya umeme kutokana na vyanzo vya jua, upepo na ardhi joto, sehemu ya Bonde la Ufa la Jimbo la Mbozi Magharibi, lakini jibu lililotolewa halikuwa la kuridhisha kwani lilikuwa la kijumla mno. Ieleweke kuwa, Jiografia ya Mkoa wa Mbeya, inatofautiana kiasi kikubwa mno na si sahihi kufikiria kwamba, umeme joto ardhi kutoka Songwe au umeme wa makaa ya mawe kutoka Galula, unaweza kwa namna yoyote ile kufikishwa Kamsamba, Ivuna, Mkulwe, Chilulumo, Chitete, Nkangamo, Myumge, Kapele na Msangano Jimboni Mbozi Magharibi; na si sahihi kabisa kuanza na fikira za kuwa upepo uliopo kule Mavuma bila mpangilio, kabla ya kufanya utafiti na ikiwa itachukuliwa hivyo, hata jua lililopo kule litachukuliwa kuwa linawaka bila adabu na hivyo haliwezi kukidhi uzalishaji wa umeme. Nataka kuwahakikishia kuwa wananchi wachache, akiwemo Mbunge, wanaweka *panel* za solar na umeme wa uhakika kuzalishwa.

Mheshimiwa Spika, ni muda muafaka wa Serikali kufikiria yale maeneo ya pembezoni kuwa ni sehemu ya nchi hii na kwamba, wananchi wake wanahitaji huduma za umeme kama sehemu nyingine nchini. Maeneo hayo yanahitaji huduma ya umeme kwa ajili ya mchakato wa uzalishaji, usindikaji, huduma za jamii kwa mfano, afya na elimu. Hivi sasa tunaingia katika enzi ya kufundisha kwa njia ya TEKNOHAMA, ikimaanisha mafunzo ya masafa ya mbali (*E-learning*). Pia tunaondokana na taaluma ya analojia na kuingia kwenye taaluma ya

digital, mambo ambayo yanahitaji umeme kama nilivyoeleza. Jimbo la Mbozi lenye vijiji 75, lina umeme kwenye vijiji viwili tu.

Jimbo hili lina Shule za Msingi zaidi ya 80 na za Sekondari 15, zikiwa kwenye vijiji vilivyo kwenye giza totoro na haviko kwenye taratibu yoyote ya kupatiwa umeme. Hii ikiwa na maana, nadharia ya TEKNOHAMA kwao itabaki hadithi ya kufikirika tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maombi ya mara kwa mara kwa Serikali, hakuna lolote linalofanywa kuonesha kuwa Serikali ina mpango wa kufikisha umeme kwa njia yoyote katika Jimbo la Mbozi Magharibi. Nilitegemea labda hata kijiji kimoja mwaka huu kingetajwa katika orodha ya Vijiji vya Mkoa wa Mbeya, kinachofikiriwa kupatiwa umeme, lakini hilo halikuwa; inavunja moyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na miundombinu mibaya ya mawasiliano ya barabara iliyopo Jimboni Mbozi Magharibi, maeneo mengi yenye madini, wakazi wake wameyaelewa vizuri. Bwa bahati mbaya, kutokana na ukosefu wa mitaji ya kuanza kuchimba, kuna wizi unaoendelea kufanywa na wageni kutoka nje, wanaojifanya wanafanya utafiti. Kila wakichukua sampuli za madini na vito hivyo hawarudi tena. Hivyo, natoa wito kwa Serikali, kuchukua hatua za kuhakikisha rasilimali hii inatunzwa. Kwa uchache tu, vito vya thamani vilivyopo Jimboni ni Amethyst, Aquamarina, Carbonates, Red-Garnet na copper, sodalite, na chumvi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wa Wizara, kwa kuwasilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wanaochakachua mafuta, wapewe adhabu kali, ikiwa ni pamoja na kuzuiliwa leseni za biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, upandaji bei za mafuta usiofuata utaratibu, unapaswa kuangaliwa vyema, kwani mafuta yakipanda na bidhaa nyingine muhimu au mahitaji mbalimbali ya wananchi nayo hupanda na hivyo kuyafanya maisha ya wananchi yazidi kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, umeme ni chanzo muhimu sana katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa wananchi, lakini umeme bado ni tatizo kubwa katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini. Ni lini umeme wa uhakika utapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini?

Mheshimiwa Spika, mikataba tunayoingia katika Sekta ya Nishati na Madini ni lazima Serikali iwe makini sana, vinginevyo rasilimali hizi zitakuwa zinawanufaisha wageni zaidi na kuwaacha wazalendo katika umaskini usiokwisha.

Mheshimiwa Spika, madini ya vito yanaweza kuchimbwa na wachimbaji wadogo wadogo wa hapa nchini, wala hayahitaji wachimbaji wakubwa, kwani madini haya yapo juu juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa umeme haupatikani katika maeneo mengi, lakini hata zile sehemu ambazo umeme umefika, wananchi walio wengi, wameshindwa kuutumia katika majumba yao kutokana na gharama kubwa. Ni vyema gharama za umeme zikapunguzwa ili wananchi wengi waweze kumudu kutumia umeme.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza sana Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri, ninaomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika nchi hii kumekuwepo na uvamizi mkubwa wa misitu na kuvuna miti kwa wingi kwa matumizi ya kuni, mkaa, kwa matumizi ya Taasisi na Makazi ya Watu; Serikali ifanye jitihada kubwa kuharakisha Muswada wa Sheria ya Gesi Asilia hapa nchini. Nchi nyingine duniani, wako katika matumizi makubwa ya gesi asilia majumbani kwa shughuli mbalimbali na hata kwa uendeshaji wa vyombo vya usafiri na mashine za aina mbalimbali. Tutahifadhi mazingira ambayo hivi sasa yanaangamizwa kwa ukataji ovyo wa miti, ambayo hutumiwa kama chanzo cha nishati.

Iwapo ni kweli mwongozo wa uendelezaji Bio-Fuel hapa nchini umekwishatolewa, basi usambazwe haraka kwa wadau wote ili utekelezaji wa miradi uanze haraka. Kuna wawekezaji wengi ambao wangependa kuwekeza hapa nchini, ingawa naomba kutoa tahadhali wakati wa utekelezaji.

Ni muhimu kuwa makini ili maeneo yanayozalisha chakula, yasitumike kabisa kwa kuzalisha mimea ya kutengeneza Bio-Fuel. Maeneo makame ni mengi hapa nchini, hivyo hayo yatumike kwa miradi hiyo.

Wachimbaji wadogo wadogo wa madini ndio wachangiaji wakubwa wa uchumi wa kaya na kuondokana na umaskini hapa nchini. Hivyo, ni muhimu Serikali iwaunge mkono kwa hali na mali.

Kuna malalamiko makubwa ya wachimbaji wadogo hasa kutoka Wilaya za Chunya, Mbeya na Mbarali kwamba, kila wanapobahatika kupata maeneo ya uchimbaji yenye dalili za kupatikana kwa madini, mara maeneo hayo huporwa na wachimbaji wakubwa, ambao hudaiwa maeneo yao na hatimaye hufukuzwa. Hivyo, kusababisha kutangatanga. Tatizo ni hawa wachimbaji wakubwa kuwa na leseni za utafutaji wa madini za muda wa miaka saba, bila kuyafanyia kazi. Sheria Mpya ya Madini iletwe Bungeni haraka ili tufanye marekebisho ya maeneo yanayokwamisha maendeleo ya wachimbaji wadogo.

Nashauri pia Serikali iendeele kuhamasisha wachimbaji hawa kujiunga katika vikundi vya ushirika ili waweze kukopeshwa vifaa vya kisasa vya uchimbaji madini, kwani mazingira ya uchimbaji yaliyopo hivi sasa ni magumu sana na hayamsaidii kabisa kujiondoa katika umaskini.

Imekuwa ni tabia ya wachimbaji, kutotekeleza Sheria ya Mazingira ya kutofukia mashimo yanayotokana na machimbo ya madini sehemu zote hapa nchini. Masharti ya leseni za uchimbaji, lazima ziambatane na ulazima wa kutekeleza Sheria za Hifadhi ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nipongeze kwa kazi nzuri sana ya Wizara. Naomba kujua maendeleo ya Mradi wa Liganga na Mchuchuma.

1. Hakuna wawekezaji wadogo wala wakubwa ambao wameanza na Mradi huu, tangu uhuru upo katika Ilani ya Uchaguzi.
2. Hakuna ramani ya kuelekeza wapi kutawekwa viwanda (Linganga/Mchuchuma).
3. Hakuna bajeti na kazi ya bajeti inayoeleweka.
4. Hakuna fidia kwa waliohamishwa (Linganga/Mchuchuma).
5. Hakuna Elimu inayotolewa kwa wananchi juu ya uwekezaji na namna ya kujiandaa kupokea wawekezaji.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuifanya Nishati na Madini ya nchini hii, yatumike kwa manufaa ya nchi hii na watu wake.

Umeme Vijijini bado ni tatizo kubwa nchini. Umeme ni ufunguo wa maendeleo. Huwezi kuzungumzia maendeleo vijijini bila vijiji kuwa na umeme. Ni vizuri kujenga viwanda vinavyotumia mali ghafi ya kilimo (*Agro-industries*) katika maeneo ya vijijini. Itawezekanaje kufanya hivyo ikiwa hatuna umeme? Mamlaka ya Umeme Vijijini (REA) inafanya juhudi gani kupeleka umeme vijijini? Kazi hii haiwezi kufanywa na wawekezaji wa mjini.

Bei ya umeme bado ni kubwa sana na Watanzania walio wengi, hawawezi kuingiza umeme majumbani kwao. Napendekeza mpango ufanywe ili kampeni iwaruhusu wateja kulipa kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kamati nyingi zinazoundwa kuyafanya madini yamsaidie Mtanzania, bado juhudi hizo hazijazaa matunda. Hata hivyo, yako mambo ambayo tunaweza kuyasifia kama lile la kufuta Mkataba wa Umeme wa Dowans, ambao ni ndugu wa Richmond.

Tatizo la msingi ni manufaa duni yanayopatikana kutoka Sekta hii ya Madini, kutokana na mikataba mibovu kati ya wawekezaji wa Serikali, kiasi kwamba wawekezaji ndio wanaofaidi zaidi madini yetu. Jambo hili linaikosha Serikali mapato. Tatizo lingine ni uchimbaji wa madini ya vito unaofanywa na wageni. Jambo hili linahuzunisha sana, kwani uchimbaji wa madini ya vito hufanywa na wenyeji na siyo wageni. Serikali lazima irekebishe jambo hili ili wananchi wafaidike na rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, madini yetu yanatakiwa yaongezewe thamani ili kwayo Watanzania wafaidike. Chuo cha Mafunzo ya Kuongeza Thamani tunacho, lakini hatujakitumia ipasavyo.

Mwisho, nawatakia utekelezaji mwema wa bajeti ya mwaka wa 2009/2010.

**MHE. MAULIDAH A. KOMU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, nawatakia kheri na kuwaombea busara, hekima na mioyo ya kujaa utajiri; Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii nzito.

Mheshimiwa Spika, madini ni utajiri mkubwa. Nchi yoyote iliyojaa utajiri huu huwa wanajua jinsi ya kutumia utajiri wa madini kwa manufaa ya wananchi wao. Tanzania ni nchi mojawapo iliyojaaliwa kuwa na madini ya kila namna, vito vya thamani, chuma na hata tukichunguza zaidi, shaba pia tunayo, lakini Tanzania kuna maskini wanakosa hata mlo mmoja kwa siku. Maeneo ambayo yana madini ndio yangeongoza kwa kuwa na maendeleo, lakini ndio wao wanaongoza kwa kukosa miundombinu ya barabara na kukosa hata maji ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, kuliundwa Tume ya kupita kuangalia matatizo ya Machimbo yote na waishauri Serikali nini kifanyike ili madini yawe miongoni mwa maeneo yanayotoa mchango mkubwa kwa kipato cha Serikali, lakini tangu Tume hiyo itoe taarifa yake, mpaka leo hakuna kinachotekelezwa kwenye mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Tume hiyo husika ilitumia fedha kwa ajili ya kazi hiyo, basi matunda ya fedha hiyo wananchi wanasubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kushauri bila ya kuchoka, kwa sababu utajiri huu tuliojaaliwa la Mwenyezi Mungu, tuone ukifaidisha wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nashauri yale yote yaliyopendekezwa na Tume yatekelezwe ili tuone kazi hiyo nzuri inasaidiaje Watanzania. Wahusika waende kwa wenzetu waliosajiliwa Madini kama sisi, wakaone na wasome jinsi wanavyofanya na kufaidika.

Machimbo yetu wakabidhiwe Watanzania, wao ndio wahusike kusimamia uchimbaji, kwani hata wakiiba kitabaki hapa hapa.

Mikataba ya uchimbaji au kuwapa wageni kuchimba ipitiwe upya na tuache miaka mitano ya kusamehe kodi.

Tujitahidi kuangalia sana yale ambayo tunaweza kuyafanya sisi wenyewe tufanye, yale machache tunayoshindwa tukiwapa wageni basi na sisi tuwe nao pamoja, siyo kuwaachia wao tu eti tunaita wawekezaji, lakini hawaweki hapa huwa wanapeleka kuweka makwao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naendelea kuwaombea Watendaji wote kila la kheri.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuunga mkono hoja hii, napenda kwa dhati nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu sana waliyoyakuta. Pia nampongeze Katibu Mkuu na Wasaidizi wake, kwa kila msaada wanaoutoa kwa kumpatia Waziri hali halisi ya matatizo ya Wizara hii. Naunga mkono hoja hii ya Waziri na nitapenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 62 na 63, zinazoelezea Sera na Sheria za Madini, ninaona maelezo yake ni hafifu, kwa sababu Sera ndiyo msingi wa mazungumzo mengi na maukimo ya Waheshimiwa Wabunge. Nashauri wakati wa *winding up* ya hoja, Mheshimiwa Waziri atumie nafasi hii kuelezea jitihada za kuboresha Sera ya 1998, ambayo ndani yake imejibu mengi yahasuyo nafasi ya wachimbaji wadogo katika uchimbaji wa madini na maeneo ambayo wadau wamependekeza yafanyiwe marekebicho. Hii itawapa afueni Wabunge kwa kuona jitihada zilizofanywa hadi sasa kuja na Sera hii mpya tutakayoipitisha mwezi Novemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kujua ni suala zima la hatima ya IPTL kwamba, Mheshimiwa Rais alivyokuwa amependekeza kuona uwezekano wa kununua mitambo hiyo ili kuepukana na tatizo la *capacity charges* zao kubwa. Pia je, kesi yao imefikia wapi kwa sasa ili kujua maandalizi ya kutumia mitambo hiyo?

Mheshimiwa Spika, ibara ya 31 na ile ya 127, hazikufafanua kwa undani kuhusu uhakika na usalama wa kutegemea umeme toka nchi jirani. Suala hili ni budi likatumika mahali ambapo tunasubiri kupata Grid yetu wenyewe, badala ya kufanya suala hili la kutegemewa sana. Sisi tuishio mpakani, tumeona adha inayotupata kwa kutegemea umeme toka nchi jirani, pamoja na kuwa na ujirani mwema na wa amani. Mheshimiwa Waziri, aoneshe pia kuwa mpango wa *Western Corridor* kutokea Mbeya, Tunduma, Sumbawanga hadi Kigoma na kuungana hadi Bukoba (Kagera) unaendelea vipi?

Mheshimiwa Spika, uchimbaji ambao unatarajiwa wa uranium utahitaji ufafanuzi wa jinsi gani tumejiandaa kudhibiti athari zake kitaifa na kwa mashauri na mataifa makubwa duniani. Pia ni budi Mheshimiwa Waziri, athibitisha kuwa wachimbaji watatumia uranium kwa ajili ya ustawi wa binadamu na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, hivi tatizo la kuwapa kibali TPDC peke yao kuagiza mafuta ya Petroli ni nini? Ingawa wengi wanapinga, lakini naelewa tatizo la wafanyabiashara ni kuficha madhambi yao katika biashara hii. Ni vizuri Waziri akakaa na wadau aelezee uzuri wake.

Mheshimiwa Spika, bado namwomba Mheshimiwa Waziri, afike Rukwa akutane na wachimbaji wadogo wa Emerald na Burma Ruby ili atoe ushauri na kuwasaidia kupunguza kiu yao ya kukutana naye na kusikia kilio chao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilipouliza swali langu lihusulo Namwele Coal Mine (Sumbawanga Urban Area), nilitaka Mheshimiwa Waziri au Naibu na Katibu Mkuu au Kamishna wa Madini, wafike huko wajionee jitihada za mwekezaji binafsi na mkazi wa hapo hapo Sumbawanga, anavyohangaika kupata wawekezaji. Ni vizuri nikampa kila aina ya msaada kwa azma yake hii ya kuleta ufumbuzi wa nishati kwa Mkoa na Rukwa.

Naunga mkono hoja na kuwataki kheri na baraka katika kazi hii ngumu ya kulitumikia Taifa na watu wake. *It will be done, play your part.*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, baba yangu Mheshimiwa Adam Malima, kwa kazi yao nzuri wanayoifanya, pamoja na kuwa na kasoro za hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri, awe macho sana, Wizara hii ni kubwa na ina mambo mengi, kwani hawa wawekezaji wengi wao si wakweli. Wachimba madini wakubwa huwanyanyasa sana wafanyakazi wao, kwani ukaguzi wao baada ya kazi, haufai na hauna tija kwa afya ya binadamu. Ukaguzi wa kupitishwa kwenye mionzi kila siku baada ya kazi sio mzuri kabisa, kwani huku ni kumtia ubovu Mtanzania ambaye ni maskini. Hili ni jambo la hatari sana, hasa kwa watu maskini, kwani uwezo wao wa kupata maziwa na matunda kila siku ni mdogo sana na mionzi ina madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kusema kwamba, naomba Wizara iwaangalie sana wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapatia maeneo na kuwapatia vifaa vya uchimbaji,



kwani hawa nao wana familia ambazo zinahitaji matunzo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, awatupie macho wachimbaji wadogo wa pale Nyarugusu, kuangalia kazi ngumu wanayoifanya bila vitendea kazi hata vya usalama, hawana umeme, hata wa dawa, utu wa mtu ni vitendo na siyo maneno. Naomba muwaangalie kwa vitendo na sio kwa maneno.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa, umeme ni jambo muhimu kuleta maendeleo kwa wananchi, lakini hivi sasa inaonekana kama ni jambo la anasa, kwani gharama ya kuweka umeme kwa mwananchi wa kawaida ni jambo la ndoto. Gharama ya kuingiza umeme ni shilingi zisizopungua laki nne na kuendelea hadi laki sita na kidogo. Hapo kama nguzo ipo karibu na kama nguzo haipo karibu, utakoma mwenyewe. Kwanza, kupata nguzo ni kazi; pili, gharama ni kiboko; hivyo tunaomba Wizara itambue kama Tanzania ni nchi maskini na wananchi wanaoishi humo pia ni maskini. Tunaomba punguzo la kuingiza umeme majumbani.

Pia kama Mji wa Mwanza ni Jiji basi tunaomba iwe Jiji na siyo Kijiji. Tunaomba umeme wa kwenda Kata ya Sangabuye na Bugongwa sasa ushughulikiwe, kwani huko kuna uvuvi na ni eneo la Halmashauri ya Jiji. Bora wapate umeme kama walivyoahidi muda mrefu uliopita. Naiomba Wizara itembelee kwenye maeneo na ahadi mbalimbali. Kila Mtanzania ana haki ya kufanya kazi na kazi nyingine zinahitaji umeme wa uhakika.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya bajeti hii ya 2009/10.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mafanikio ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Ludewa, Mbinga, Simanjiro, Mkinga Musoma, Mto wa Mbu na Longido/Namanga, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa majenereta matano kwa ajili ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Aidha, naipongeza Serikali kwa kukamilika kwa mkataba wa kupunguza *capacity charge* ya Songas, kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni moja kwa mwezi. Hii ni Dola za Marekani milioni 12 kwa mwaka. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kumalizika kwa asilimia 90 ya ujenzi wa Mtambo wa Serikali wa kuzalisha umeme wenye uwezo wa MW 45, unaotumia gesi asilia katika eneo la Tegeta, pamoja na kuongezeka kwa uwezo wa kusafisha gesi asilia kutoka futi za ujazo wa milioni 70 hadi 90 kwa siku; ni mafanikio makubwa sana na itatuongezea uwezo wa utumiaji wa gesi asilia badala ya petrol kwa magari hapa nchini. Hatua hii ni ukombozi mkubwa sana katika kupunguza gharama za mafuta ya petroli hapa nchini na hatimaye kupunguza kiasi cha mafuta yanayoagizwa nje kwa fedha nyingi za kigeni. Napongeza hatua hii na tuzidi kuchukua hatua kama hii kwa wale wengine wanaofanana na Songas.

Mheshimiwa Spika, napongeza hatua ya Serikali, kufikiria suala la mgawanyo wa gharama na mapato ya mafuta katika pande mbili za Muungano. Muafaka huu ukifikwiwa, utajenga imani na hatimaye kudumisha Muungano wetu, kwa vile hivi sasa kero kubwa ya Muungano ni hii. Hatua ichukuliwe ili kufanikisha azma hii kwa nia ya kudumisha Muungano wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri, ibara ile ya 112, Mheshimiwa Waziri amesema, TANESCO itaendelea kukamilisha miradi mingine ya umeme vijijini, iliyofadhiliwa na Serikali na kwa kupitia Mfuko wa Umeme Vijijini (REA).

Mheshimiwa Spika, Serikali imeahidi kupeleka umeme kule Arumeru Vijijini tangu mwaka 1996, miaka kumi na nne sasa. Mawaziri wote walioingia katika Wizara hii tangu wakati huo, wamefika Arumeru Magharibi na kuahidi wananchi kupatiwa umeme. Mheshimiwa Waziri Ngeleja alifika Arumeru Magharibi na kuahidi umeme mwaka huu wa 2009/10, kwa Vijiji vya Oldonyosambu, Oljoro, Mbuyuni, Mirongoine na Sambasha/Ikidinga na Likamba/Olevols.

Mheshimiwa Spika, naomba katika bajeti hii, nimweleze Waziri atimize ahadi yake aliyotoa Arumeru Magharibi, alipokuja kwenye ziara yake na majibu ya swali hili aliyoyotoa Bungeni mara mbili tangu awe Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Uyui haina umeme; na kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi inasema itahakikisha unapatikana umeme kila wilaya; je ni lini sasa umeme utapatikana katika Wilaya hiyo ili Makao Makuu ya Wilaya yaweze kuanza kutumika kwani katika wilaya hiyo kuna maeneo mengi ambayo yamekwama kupata maendeleo ingawa kuna nyumba za kisasa? Hivyo basi, ningeshauri katika maeneo mengine, wangepatiwa umeme wa jua, kwa mfano, Kigwa, Igalula, Isikizya, Goweko na kadhalika

Mheshimiwa Spika, ningeshauri Serikali ipunguze gharama ya uingizaji wa umeme majumbani, kwani gharama ya Sh. 1,870,000 kwa Mtanzania wa kawaida, hawezi kuimudu. Hivyo, kwa kuanzia nguzo ambazo huagizwa toka nje ni vyema zikasimamishwa (sitishwa) ili kuleta unafuu wa bei.

Mheshimiwa Spika, Wizara ihakikishe kwamba, hivi sasa kila mteja mpya na wa zamani ameweka Luku ili kusiweko na upotevu wa umeme kwa watumishi ambao sio waaminifu (vishoka) na wapewe muda wa kukamilisha zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, maombi ya wateja ambao wanahitaji umeme yawe kwa wakati, kwani wateja wengi wanalalamikia huduma hiyo kususua.

Mheshimiwa Spika, itolewe elimu kwa wananchi, juu ya madhara ya kuunganishwa kinyemela kwa umeme, kwani wengi hawajui elimu ya matumizi ya Sera ya Luku; kutoa elimu ya matumizi ya umeme wa jua (solar) ili watu wa vijijini waweze kutumia, hasa kwenye Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne, ikiongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kusema na kutenda. Zamani watu walizowea siasa ni maneno tu; lakini si sasa, Serikali ya Awamu ya Nne, inasema au inaahidi na inatenda, yaani inatekeleza. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Mawaziri na kwa Wizara hii.

Wizara hii ni ngumu, tete, lakini Waziri na Naibu Waziri wanajitahidi kupunguza kero kidogo kidogo. Waingereza husema *slow but surely*. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye hoja yenyewe na hasa nitajikita kwenye Jimbo langu la Bukene.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kukumbushia kwamba, umeme kwenda Bukene ni:-

1. Ahadi ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.
2. Ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuwa anaomba kura, alisema anachukua kijiti, yaani amerithi ahadi hiyo na pili, alipokuja kushukuru na kuangalia shuguli za ushirika wa Igembe Nsabo, aliahidi na fedha zilikuwepo.
3. Matokeo ya ziara yake tumewekewa nguzo Ijanija kuonesha kwamba, sasa umeme unakwenda Bukene, yaani kuna kazi imeanza kufanyika.
4. Wabunge wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, walipotembelea Sao Hill Iringa, walikuta nguzo za umeme zipo na zimelipiwa. Nguzo hizo zinakwenda Bukene kwa umeme wa Bukene.
5. Kwa kukumbushana tu, Bukene ni Makao Makuu ya Jimbo, ndio maana hapo awali enzi za Dkt. Msabaha (Mb), Waziri Mstaafu wa Nishati; mimi na Mheshimiwa Jenista Mhagama, tulikabidhwa kwa Viongozi wa TANESCO ili umeme uletwe kenye Majimbo yetu. Mwendangu alishapata, mimi ilikuwa *priority* ya kwanza Bukene kabla ya Ndala, kwa sababu Bukene ni Makao ya Jimbo, ndio maana utaona umeme wote hata wa Ndala, ulikuwa umeandikwa umeme wa Bukene.

Sasa inashangaza; mimi sijapata umeme hadi leo na kuna mgao, Bukene na Ndala tunakuwa sawa.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri, umeme wa Bukene haujaoneshwa. Nimemuuliza Mheshimiwa Waziri kanithibitishia kwamba, umeme kwenda Bukene upo. Pia kwenye Randama za Makadirio ya Wizara, nimeona umeme wa kwenda Bukene.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kutoka Nzega kwenda Bukene ni karibu sana kuliko Nzega kwenda Puge; na kwa kuwa Bukene ni Makao Makuu ya Jimbo; na kwa kuwa tuna ushirika wa Igembe Nsabo ambao wananunua sana mpunga kutoka kwa walimaji; na kwa kuwa hatuna umeme Igembe Nsabo wanakwenda kukobolea mpunga na kufunga mchele Ziba na hivyo kuwanyima vijana na akina mama lishe biashara hivyo kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo, naomba Wizara iwe na busara tu, kuhitimisha umeme Makao Makuu ya Jimbo mapema iwezekanavyo ili kumaliza tatizo hili na hivyo kufunga kalomo (kufunga mdomo), hasa kwa Wapinzani wetu ambao wameanza kutubeza kwa kuona zile nguzo zimerudishwa pale Ijanija kwa muda sasa.

Mheshimiwa Spika, nalazimika kutumia methali ya Kinyamwezi inayosema “Kuzunya kwa Ng’ a Toma, mpaka kwiboneleja” maana yake kukubali kwa Thomas (hii inatoka kwenye mitume wa Yesu wale 12) mpaka kuona au kujionea. Hii ilikuwa Mtume Thomasi, alipoambiwa Yesu kafufuka hakuamini, mpaka Yesu alipowatokea tena, akamwambia weka

vidole vyako kwenye ubavu wangu na viganja vyangu, alipoona yale matundu aliyotobolewa, aliamini. Basi na ndugu zangu Wana-Bukene, wakiona zile nguzo zimesimama na kama alivyoahidi Meneja wa TANESCO, atakuwa anasimamisha nguzo na kuwasha kidogo kidogo kadiri pesa zinavyopatikana. Naamini wale ndugu zangu walionipa sauti hii, wataamini na watafurahi kweli kweli. Naomba basi na najua ni watendaji, mtanijibu wakati wa kuhitimisha ili ndugu zangu wasikie.

Naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mwanangu Mpendwa Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye mwelekeo wa kuboresha Wizara hii, pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kutamka rasmi kuwa, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia, nikitegemea kuwa hoja zangu zitapata majibu kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wakati wakijibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Umeme wa REA Vijiji vya Singida, naomba niendeleo kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuwapa wananchi huduma ya umeme hadi vijijini kupitia Mradi wa REA. Kama sijakosea, bajeti hii ni ya tatu tangu Serikali imeanza kutoa ahadi zake kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Muhalala, Sorya, Kilimatinde, Chibumaga, Chikuyu, Maweni na Kintiku, Jimbo la Manyoni Mashariki. Vile vile ahadi za kupeleka umeme Vijiji vya Sepuka, Ihanja, Jimbo la Singida Kusini na Vijiji vya Mgongo na Kibigiri kwa Jimbo la Iramba Magharibi, Vijiji vya Nkungi, Ilunda, Nduguti na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninatambua ahadi hizi za Serikali ni kweli zitatekelezwa, bali kinachosikitisha utekelezaji wake ni wa pole pole sana, kiasi kwamba unaathiri kura za Chama cha Mapinduzi. Nitashukuru Serikali ikitoa muda wa Mradi kuanza na kumalizika kwa Mradi kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa upepo, naipongeza Serikali kwa kugundua umeme huo kwenye maeneo mbalimbali, pamoja na maeneo ya Vijiji vya Manispaa ya Singida na Singida Vijijini, ambayo ni Kijiji cha Kisasida, Kata ya Unyambwa, Kijiji cha Ughanga, Kata ya Unamikumbi na Kijiji cha Unyakhanya, Kata ya Sinyu Singida Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, naipongeza Serikali kwa kuamua kutekeleza Mradi huu wa Umeme wa Upepo, kwa kuwa maeneo haya yameingiliwa na Wapinzani. Ninaiomba Serikali kuwa makini katika kuwafidia wakazi wa maeneo haya, kwa wale ambao nyumba zimeingia kwenye eneo la umeme wa upepo, mali na mashamba na kadhalika, kwa gharama zinazofanana na hali halisi ili kura zetu zisipungue tena, Waziri atoe kauli jinsi Serikali itakavyoshiriki katika kuona haki inatendeka.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa madini ni urithi wetu na mali ya nchi yetu. Vile vile walioshika maeneo hayo toka mwanzo ni wazawa. Hivyo, ninaiomba Serikali kutoa kipaumbele kwa wazawa kumiliki maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya wazawa kumiliki machimbo hayo, mfano, Mkoani Singida; Vijiji vya Sambaru, Londoni, Mpambala, Misigiri, Mgongo na kadhalika.

Ninaiomba Serikali kuwapa mikopo wawekezaji hawa wadogo wadogo ili wapate fedha za kununulia miundombinu za kuwasaidia katika kazi ya kuchimba madini kwa njia rahisi na salama. Nasubiri majibu ya Waziri, awakumbuke wananchi niliowapeleka ofisini kwake kutafuta msaada wa kukopeshwa fedha.

Mheshimiwa Spika, ni kweli usiofichika kuwa, maendeleo ni pamoja na miundombinu ya umeme. Tatizo ni gharama ya kupeleka umeme kwenye makazi ni kubwa sana, kwani imetoka kwenye shilingi laki tano hadi milioni moja na zaidi. Ninaiomba Serikali itumie utaratibu kama inavyofanya kwenye mazao ya pamba na kadhalika, ibebe mzungu kwa kiasi fulani cha fedha ili kuwapunguzia wananchi gharama hizi kubwa. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la mita zilizofunguwa miaka mingi iliyopita kufa na kutokusoma tena, hii inasababisha mgogoro wa wateja na TANESCO. Ninaishauri Serikali kubadili hizo mita haraka kwa gharama ya Serikali, kwani itasababisha gharama kujilimbikiza na baadaye wateja kushindwa kuzimudu. Ninasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuieleza Serikali kuwa, kuna tatizo la LUKU kufa mara kwa mara, hasa katika miji mikubwa mfano, Dar es Salaam na kadhalika, kisa Serikali hucholewa kutatua tatizo. Ninaomba kujua tatizo kuwa kwa nini Serikali hurudisha umeme kwa kuchelewa jambo ambalo linafanya majambazi kutumia mwanya huo?

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna tatizo la taa za barabarani kwenye miji yetu mingi. Kwa kuwa taa ni njia mojawapo ya kusaidia ulinzi, hivyo ni vyema miji yetu kuwekewa taa na kuzitengeneza mara kwa mara pale zinapokufa ili ulinzi uwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini, Mheshimiwa Mohammed Gulam Dewji, kwa juhudi zake kubwa, kuwawekea wapiga kura wake taa za barabarani katika Mji wa Singida, kwa niaba ya Serikali. Ninaiomba Serikali isaidie sasa kuweka taa maeneo mengine mfano, Mitunduruni, Unyankingi, Mandewa, pamoja na mitaa mingine. Ninategemea Waziri atamtambua pia Mheshimiwa Dewji.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali iwatambue wanawake wanaotengeneza chumvi huko Nkonkilangi Shelui, kwa mazingira magumu wakiwa na nia ya kutupatia chumvi kwa matumizi ya nyumbani na pia kujipatia vipato vyao kwa nia ya kuondokana na umaskini.

Ninaomba Serikali iwawezeshe wanawake hawa kifedha ili waweze kununua vifaa vya kisasa vya kurahisisha shughuli zao za kutengeneza chumvi.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la wachimbaji wadogo wadogo kuingiliwa na wawekezaji wakubwa na kutaka kuwaporu maeneo yao. Naomba Serikali kupitia sheria ya kuwalinda wachimbaji wadogo wadogo, sasa itumike ilivyo kwani bado kuna dhuluma kutoka kwa wachimbaji wakubwa, kwani hata wanawake wako mstari wa mbele kuchimba wathaminiwe sasa.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Pia natumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Nawatakia afya njema ili waendeleo kuwatumikia Watanzania wenzao. Nina imani sana na Uongozi wa Mawaziri hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Jimbo la Mbeya Mjini lilipata bahati ya Miradi mitatu ya MCC: umeme – Tsyesyey; umeme – Bible School – Itende; na umeme – Iyela I.

Juhudi imekuwa kubwa kupeleka umeme Isyesyey, lakini mpaka sasa maeneo mawili ya Iyela – I na Bible School Itende, sijaona/au sijajua shughuli za kupeleka umeme maeneo hayo. Naomba kujua ni lini maeneo haya yatafikiwa?

Lipo tatizo la gharama kubwa za kuingizia umeme kwa wananchi wenye nafasi ndogo kimapato na jambo moja linalosababisha hali hii ni gharama za nguzo, kwa nini nguzo ziagizwe toka Afrika Kusini wakati tunazo nguzo za kutosha hapa nchini? Changamoto iwe ni kupunguza gharama za kuingiza umeme ndani ya nyumba. Umeme si anasa, bali ni huduma muhimu ya kupunguza umaskini wa Tanzania.

Pamoja na kuwepo kwa msongo wa Taifa, ni vyema Wizara ikaacha kutegemea Msongo wa Taifa tu. Mathalani, Kiwira *potential* yake iwe kwa kuhudumia, Mbeya, Rukwa Ruvuma na Iringa, ziada ya umeme iingizwe kwenye Gridi ya Taifa. Hale, Pangani na Nyumba ya Mungu, ihudumie Taifa. Kilimanjaro na Arusha, ziada iingizwe kwenye Gridi ya Taifa. Mtwara, Lindi, umeme wa gesi; Mtera/Kihansi iwe Dar es Salaam, Dodoma na Mikoa ya Kati na Ziwa na pia Stiegler's itafutiwe utaratibu wa kuanza.

Vyanzo chini ya Ardhi (*Geo-Thermal Power*), ipo *potential* kuwa maeneo ya Songwe – Mbeya, nguvu ya umeme toka ardhini. Naomba utafiti uanze ili tutumie vyanzo vyetu kwa umeme. Nawasilisha.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, tunaomba umeme, Wilaya ya Mpanda bado ina matatizo makubwa hivi sasa, hakuna umeme sasa kwa siku sita; kwani kuna matatizo gani?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi mpaka sasa haina umeme kabisa; kuna mikakati gani ya Serikali?

Wilaya ya Mpanda ina wachimbaji wadogo wadogo wengi, hawana mafunzo wala vifaa, tunaomba msaada kwa ajili ya Vijana wa Mpanda.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

1. Mradi wa SMMRP ni wachimbaji wadogo wangapi waliofaidika kwa kupatiwa vifaa na kuongeza kipato?

2. Idadi ya wachimbaji wadogo wadogo ni wangapi nchini na ni katika madini gani ndio ina idadi kubwa?

3. Fedha zilizokuweco TANSOLT tokea 2004; je, zimerudishwa kwani TANSOLT haijarudi Tanzania na kuweka BOT Twintower kufanya uchambuzi wa mradi?

4. Mirabaha kwa copper, silver na vito ni kiasi gani?

5. Miradi mikubwa ya uchimbaji wa dhahabu ambayo inalalamikiwa sana katika kukosesha mapato Serikali. Je, majadiliano na makampuni haya yanafikiwa wapi? Serikali imeanza kupata mapato ya kiasi gani kila mwaka?

6. Almasi zinazozalishwa hivi sasa zinazuzwa na kukaguliwa na nani?

7. Umeme wa makaa ya mawe ambao ungekuwa umefanyiwa kazi hasa Kiwira, Mchuchuma na Ngaka, hali ingekuwa bora zaidi; Waziri aeleze upungufu wa umeme wa mara kwa mara unakabiliwa vipi?

8. Mmboreshaje utoaji wa leseni mbona bado kuna urasimu na kadhalika?

9. Je, gesi ni ghali sana melini?

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwanza, ninawapongeza kwa hatua ya kuweka fedha kwa ajili ya Mradi wa Umeme wa Puge Ndala. Ninachoomba ni utekelezaji wa haraka uanze ili pesa zilizotengwa 2008/09 zianze kutumika.

Nawapongeza zaidi kwa kuanzisha REA na kwa kuweka pesa za ndani katika kutekeleza miradi hiyo. Nashauri vyanzo viongezwe ili kuupa pesa za kutosha Mfuko huu ili miradi mingi itekelezwe.

Kwa kuwa kumejitokeza baadhi wa wafanyabiashara kujihusisha na kuchanganya mafuta; na kwa kuwa udhibiti wa bei ni mgumu na usiotabirika; nashauri mtindo wa kununua mafuta uwe wa Jumla (*bulk*) ili kuondoa namna yoyote ya wauzaji mafuta wasichanganye na bei itapungua. Vyema tukajifunze kwa wenzetu wa Kenya na Msumbiji, ambako mtindo huu unafanywa.

Wizara haijaweka mipango madhubuti ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo, kuwaendeleza na kuwapa zana na fedha ili kuwezesha wao pia waje kuwa wachimbaji wakubwa.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuwasilisha vizuri Bajeti ya Wizara yake. Pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na kazi nzuri wanazozifanya kila siku, ikiwa ni pamoja na kutujibu maswali vizuri Bungeni, kutuletea semina ya *Power System Master Plan* na kufanya maandalizi ya Sheria mpya ya Madini. Kwa namna ya pekee kabisa, naipongeza Serikali kwa kuiwezesha ARTUMAS kifedha na kwa kusaini mikataba husika ili kuhakikisha kuwa, Mikoa ya Kusini inapata umeme wa uhakika ifikapo 2010. Vile vile mkataba baina ya Serikali na ARTUMAS umekuwa ndio mkataba wa mfano kwa ubora. Kwa hiyo, Serikali iboreshe zaidi mikataba itakayofuata siku zijazo.

Ningependa kutoa ushauri wangu katika mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu *Power System Master Plan* inavyoonesha kuwa itachukua muda mrefu sana kuwafikia wananchi walio wengi. Kwa maneno mengine, hata zile shule za vijijini hazitapata umeme mapema. Napenda kuishauri Serikali, ifanye zoezi la kuwafikishia wanafunzi umeme wa jua (shule za Vijijini) ili nao waweze kujifunza na kutumia computer.

Jambo la Pili ni kuhusu bei za umeme za TANESCO zisizoeleweka, pia ubovu wa mita. Inashangaza kuona kuwa, mtu hatozwi bili kwa muda wa miaka sita kutokana na kwamba, nyumba yake ina *tubelight* mbili tu na baada ya kipindi chote hicho ghafla anatozwa shilingi laki mbili na nusu. Tena suala hili anakuwa akiwauliza wahusika wa TANESCO wanapokuja kusoma Units za mita ya mashine ya kusaga kwamba, kila mwezi huwa analipa bili ya umeme na mashine je, kulikoni kuhusu umeme wa nyumba? Huwa wanamjibu kwamba, hadaiwi. Kwa upande mwingine, utakuta mtu mwenye *tubelight* tatu tu na pasi, hana feni, TV, jiko wala jokofu, lakini bili anadaiwa kuanzia shilingi elfu hamsini kwa mwezi. Ninachotaka kusema ni kwamba, mita ziangaliwe vizuri na vile vile LUKU zisambazwe haraka nchi nzima, maana hizi zitamwezesha mteja kununua umeme kwa kadiri ya uwezo wake na vile vile kuondoa bugudha ya kukatiwa katiwa umeme bila mpango.

La tatu ni kuhusu utafiti wa mafuta, ambao mara kadhaa ndugu mmoja aitwaye Mkinga amekuwa akitoa taarifa kwenye vyombo vya habari kwamba, wale wanaofanya utafiti wa mafuta nchini, wamesaini mkataba kwamba mafuta yakipatikana, wao watapata *shares* asilimia 90 na Serikali asilimia 10. Je, hili jambo ni la kweli? Tafadhali Mheshimiwa Waziri, alifafanue vizuri suala hili kwa wananchi na kama si kweli basi ni vyema Serikali ikanushe.

Mwisho naiomba Serikali ipunguze gharama za kuvuta umeme, kwani ni kubwa mno kwa wananchi wa kawaida. Ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimeshauriwa kuwa kero zote zinazungumzika, basi naunga mkono hoja. Hata hivyo, yafuatayo naomba yazingatiwe:-

Kwa kuwa gesi iliyoko Songosongo na Kituo kilichopo Somanga Fungu na Bomba kuelekea Dar es Salaam wananchi wanasononeka sana hasa Jimbo langu la Kilwa Kaskazini kwamba, hawafaidiki na chochote kutokana na Mradi huo; napendekeza kungefanyika mkutano wa hadhara kuhusiana na Mradi huo ili wananchi wangu waelewe faida ya Mradi huo kwao.

Kwa kuwa Kituo cha Somanga Fungu kipo kwenye Jimbo la Kilwa Kaskazini, Kijiji cha Somanga, Kata ya Kinjumbi; je, Mheshimiwa Waziri huoni busara kuwapatia nishati ya umeme kwa bei nafuu angalau katika Makao Makuu ya Tarafa na vijiji lipitapo bomba?

Kulikoni mrabaha kwenye Halmashauri yetu hawapati wakati sisi ndiyo walenzi wakuu wa Songosongo Project? Napendekeza angalau kila Makao Makuu ya Tarafa (Kilwa Kaskazini), wangepelekewa umeme kwa bei nafuu. Mradi wa Umeme Vijijini kwetu sisi ni kama hadithi ya kusadikika; inauma sana.

Kwa kuwa utafiti mwingi katika miaka ya hivi karibuni wa kutafuta mafuta unafanyika katika Jimbo la Kilwa Kaskazini lakini nakueleza kuwa, wananchi wangu hawapati wakati miundombinu yetu inaharibiwa sana na mitambo mikubwa ipitayo ya kufanyia tafiti, lakini ukiwaambia ukarabati inakuwa hadithi tu. Hata Mbunge wao hataarifiwa chochote kabla ya utekelezaji wa utafiti huo.

Kwa kuwa mwanzoni wa Mradi huo tulielezwa kuwa, kungeweka T – Joint pale Somanga Fungu, lakini hadi sasa hatujui kama T – Joint imewekwa ili vijiji vilivyopo kusini ya Somanga Fungu viweze kuwa na matumaini ya kupata umeme. Je, Mheshimiwa Waziri unalielezaje hili? Kilwa Kaskazini ipo gizani. Shule zetu za Sekondari za Kata zipatazo 14



na Zahanati sawia, kuna mpango gani wa kupatiwa panels za nishati ya umeme wa jua kama walivyo wenzetu wa Bangladesh?

Mapango ya Nang'oma, Namaingo na kadhalika, wangewekewa angalu umeme wa jua ili kuongeza kivutio.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote, kwa kutuletea hotuba nzuri, yenye kuleta matumaini kwa Watanzania kama itatekelezwa na kukiwa na ufuatiliaji wa karibu. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wenye kipato cha chini kutokana na TANESCO kutoza gharama kubwa kwa ajili ya uingizaji wa umeme majumbani, ambayo ni kati ya Sh. 500,000 hadi milioni moja. Wananchi wengi wanaohitaji kuingiza umeme kwenye nyumba zao wanashindwa. Ni vigezo gani vinatumika kufikia gharama hizo?

Aidha, upandaji wa gharama za umeme wa mara kwa mara, umekuwa kero kubwa kwa watumiaji. Hata pale mwenye nyumba anaposafiri bila kuutumia umeme, bill inaletwa kubwa vile vile.

Nawasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa ushauri wangu ni kuwa Wataalam wa TANESCO wajitahidi kuzama kwenye mkakati wa *predictability* na *reliability* katika upatikanaji wa umeme. Vile vile Wizara ifuatilie kwa karibu suala zima la ukarabati wa nyenzo na mitambo, pamoja na *quality za spares* zinazotumika. Haiyumkini *stock ya spares* wilayani na mikoani inayokuwa huko iwe ya kutosha. Yakifuatiliwa haya, *we can generate* ziada ya MW 600 za sasa.

Mwisho, niliomba kwa kipindi cha miaka saba sasa kukamilisha mradi wa kuunganisha umeme tokea vibaoni Charuka Handeni hadi Turiani Kwachanga kupitia Magamba. Wananchi wa Handeni, tunaendelea kuomba Wizara itusaidie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa juhudi kubwa wanayofanya katika kutoa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Wizara hii ni kubwa sana, inahitaji bajeti kubwa zaidi. Hata hivyo, kama Nishati ya nchi hii itaendelea kutegemea maji, kazi ya utoaji umeme itaendelea kuwa ngumu. Vyanzo vingine vya umeme lazima vitafutwe.

Mheshimiwa Spika, licha ya Wizara/Serikali kuahidi majenereta manne kwa Sumbawanga, hali ya umeme Mkoani Rukwa bado ni mbaya sana.

Nashauri Serikali ifute kabisa wazo la kutoa umeme Zambia. Adha iliyokwishaipata Rukwa kutokana na umeme wa kutoka Zambia imekwishatosha. Naomba Serikali iharakishe kuleta jenereta kama ilivyoadhidi kwa manufaa ya Sumbawanga hata Rukwa nzima,

ninaomba umeme wa Grid. Tunavyo viwanda na tunapenda kuongeza vingine, kikwazo ni umeme.

Mheshimiwa Spika, Mpanda imepata adha kubwa ya kukatika kwa umeme mara kwa mara. Hatua za kuondoa hali hii haijachukuliwa. Hivi karibuni Mpanda ilikosa umeme kwa wiki moja; jana ndiyo umeme uliwashwa; kulikoni? Watu wanakosa maji na chakula, kwani vinu vya kusaga unga na mashine za kusukuma maji, zinategemea umeme. Mbaya zaidi, yalipelekwa matanki mawili ya mafuta machafu badala ya mafuta safi, kwa matumizi ya mashine za umeme. Wana-Mpanda walipomuuliza Meneja wa TANESCO, aliwajibu kuwa muhusika ni Afisa Uhusiano wa Wizara kule Dar es Salaam. Eti yeye anakaimu Sumbawanga; ya Mpanda hana habari! Hata kama kosa lipo Wizara/Serikali ijaribu kutoa majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kufika hapa leo na kuweza kuchangia Wizara hii. Pia nakushukuru na wewe kwa kuweza kuliongoza Bunge hili Tukufu, kwa makini na uangalifu ulio juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizi, ningependa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Watendaji wake wote, kwa kuweza kutekeleza yale yote yaliyomo ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu, ningependa kumpongeza tena Waziri kwa kuweza kutekeleza baadhi ya Sekta ya Nishati na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo bado yanahitaji nishati ya umeme, pamoja na maeneo ya vijijini, bado kuna kero kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Wizara hii, ilifanyie haraka sana suala hili hususan sehemu za vijijini, ambazo bado hazijapata au kufikiwa na nishati ya kutosha, zipatiwe nishati hiyo ili ziondokane na usumbufu uliopo katika maeneo pamoja na vijijini.

Mheshimiwa Spika, sina budi kuipongeza tena Wizara hii pamoja na Serikali, kwa kuboresha miundombinu ya usambazaji umeme Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki kilikuwa ni kilio kikubwa cha wananchi na malalamiko ya muda mrefu sana kuhusu kuboresha miundombinu ya umeme katika maeneo ya Mikocheni na Oysterbay, lakini Serikali pamoja na Wizara, iliweza kukisikia kilio na mamalamiko ya wananchi na kuweza kuchukua hatua ya kuanzisha Mradi wa Umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii kuwa na huo mradi ambao haujakamilika hadi ifikapo mwaka 2010, basi ukamilishwe haraka ili wananchi waweze kuendelea mahitaji yao ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuendelea tena na Waziri wa Wizara hii, kwa kuweza kurekebisha baadhi ya matatizo yaliyomo katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, matatizo mengine yaliyomo ndani ya Sekta ya Madini ni kama ujenzi wa Ofisi za Madini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Madini ni muhimu sana kwa wananchi. Watu wamefanya kazi za kuchimba madini, lakini utakuta baadhi ya maeneo ofisi ni chache sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Serikali kupitia Wizara hii, iweze kukamilisha Ofisi hizi za Madini kwa maeneo ambayo ni machache kama maeneo ya Mbeya, Mwanza na Singida.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuelezwa kuwa, Mradi wa Umeme Vijijini utakuwepo kama Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilivyoeleza. Je, Mheshimiwa Waziri anakumbuka katika swali langu nililouliza mwezi Juni 2009 kuhusu kuanza kuweka miundombinu ya kuwezesha umeme kupatikana katika vijiji kadhaa ndani ya Jimbo langu? Katika jibu lake alieleza kuwa, kuna maandalizi ya kufikisha umeme katika Kijiji cha Inalo kilichopo Manispaa, Kigwo, Igalula na Goweko, viko kwenye Jimbo langu. Je, maandalizi hayo yanaanza lini ili wananchi wangu katika maeneo hayo waweze kujaandaa kwa kuupokea Mradi huo? Ili kuingiza umeme ndani ya jengo, inatakiwa nyumba iliyojengwa vizuri, basi kusitokee athari yoyote kwa wakazi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, watafiti wa Madini katika Jimbo langu kwenye Kijiji cha Loya, Tura, walichimba mchanga mwingi tu tangu mwaka 2004 – 2005 hadi 2006 na kudai kuwa, kuna dalili ya madini kama vile dhahabu na mengine. Je, utafiti huo umefikia wapi? Wananchi wanasubiri matokeo ya utafiti ili wafurahie upatikanaji wa madini hayo ili wajipange kutafuta riziki. La sivyo, hamna madini, basi wafukie mashimo na mahandaki yaliyobaki baada ya uchambaji huo ili wakarabati ardhi hiyo kwa matumizi mengine, badala ya kukaa na mashine bila kujua hatima yake.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha kusubiri ufafanuzi.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, kimsingi, ninaunga mkono hoja. Hata hivyo, ninapenda kupata ufafanuzi kwa masuala yafuatayo:-

Katika Hotuba ya Waziri, uk. 57, kipengele cha 97, Waziri ameeleza kwamba, fidia katika Mgodi wa Buzwagi zimefanyika kwa awamu tatu. Ninaamini, awamu ya tatu ni ile inayotokana na ziara ya Naibu Waziri (kwa maagizo ya Waziri Mkuu – Aprili 2008). Ninapenda kujua malipo hayo ya Sh. 285,782,511.99 yalifanyika lini na wananchi 45 waliolipwa ni akina nani? Ningependa kujua/kupata majina yao ili kupata usahihi kama waliolipwa ni miongoni mwa waliokuwa wanalalamika?

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupata majibu haya kwa vile tangu mwanzo zoezi hili limefanyika kwa mizengwe kama vile watu waliohusika kulipwa fidia, fidia kulipwa pungufu au baadhi ya wananchi kulipwa tofauti na thamani iliyoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja (*Bulk procurement of petroleum product*), una tija nyingi ukilinganisha na upungufu wake. Je, ni kwa nini utaratibu huu haujaanza kutumika kama sheria inavyoagiza?

Mheshimiwa Spika, kitendo cha baadhi ya wafanyabiashara kuagiza mafuta, wanapinga mfumo huo. Kwa sababu gani Serikali inakumbatia hoja za watu hawa ambazo hazina tija na zinalenga kuwakandamiza watumiaji ambao ni wananchi maskini wa nchi hii?

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, waliohusika kuandaa bajeti hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa bajeti hii iliyowasilishwa leo, inatia moyo sana na kama itatekelezwa, basi tunatarajia kupata mabadiliko makubwa mno.

Mheshimiwa Spika, Waziri katika bajeti yake amesema kuwa, Soko la Madini limepanda na kama limepanda wananchi waishio karibu na madini hayo wamefaidika vipi na soko la madini kupanda?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kahama ina wawekezaji wengi, lakini ukiangalia barabara za Kahama ni mbaya sana. Je, Serikali haioni iko haja sasa kuongea na wawekezaji hawa ili nao wachangie utengenezaji wa barabara hizi; na hasa ukizingatia kuwa magari yao makubwa yamechangia kuharibu barabara?

Mheshimiwa Spika, ningependa nichangie kuhusu gharama za uvutaji wa umeme majumbani, iliyopo sasa ni kubwa mno, mwananchi wa kawaida hawezi kumudu gharama hizi. Serikali iangalie kwa upya gharama hizi ili angalau uweze kupatikana kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, wananchi waishio Ndembezi Mkoa wa Shinyanga, ambayo ni Shinyanga Mjini, wamekuwa wakisubiri umeme katika maeneo yao kwa muda wa miaka mingi sasa. Ndembezi iko mjini kabisa na wananchi wamefanya utaratibu wote unaohusiana na uvutaji wa umeme, sasa nini kinasababisha umeme usifike Ndembezi? Naomba wananchi hawa wapewe majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, bill za umeme zimekuwa zikipanda ovyo bila mpangilio, sijajua tatizo ni nini? Iko haja ya kuangalia vizuri mita, inawezekana nyingine zimeshakuwa mbovu, malalamiko kwa wananchi ni makubwa mno.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwenye Wizara hii. Hongera sana.

Kwanza kabisa, ningependa kutoa maoni machache kwenye Wizara hii kwa kuwa kuna Wilaya kadhaa hazijakamilishiwa miradi ya upelekaji umeme, kulingana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na pia kuna baadhi ya miradi ambayo haijakamilishwa.

Hongera kwa Serikali kwa kuiondoa STAMICO kutoka kwenye orodha ya Mashirika ya Umma ya kubinafishwa ili itumike kuwekeza katika Sekta ya Madini, kwa niaba ya Taifa na katika kuwasaidia wachimbaji wadogo.

Pili, naipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), kwa kudhibiti suala la upandaji holela wa bei za mafuta na kupanga bei elekezi kwa wauzaji wa mafuta nchini. Hongera sana. Pia waendeleo kudhibiti biashara haramu ya uchakachaji wa mafuta. Kero kubwa kwa wananchi, imeharibu magari na mitambo.

Tatu, nimewahi kuongea na Naibu Waziri kuhusu mauaji ya Albino yanayotokea mara kwa mara, yakishirikishwa na upatikanaji wa Madini. Naibu Waziri aliniahidi kuwa, ana

mpango akishirikiana na Waziri, kuongea na wenye kumiliki migodi kuona nini kifanyike ili kupiga vita hali hii inayozidi kuendelea. Naomba kwa pamoja tushirikiane, tuone nini kifanyike ili tukomeshe hali hii tukishirikiana na Jeshi la Polisi.

Mwisho, nazidi kuwapongezeni kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARGRETH AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara kuanzia na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote, kwa kuandaa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini. Cha msingi ni kujitahidi kutekeleza yote tuliyoenezwa. Uk. 49 wa hotuba imefafanua mchakato wa kuandaa kanuni za kusimamia kazi ya utafutaji na uchimbaji wa uranium. Kwa upande wangu, naona kanuni hizi zimechelewa kuandaliwa na hotuba imeeleza kuwa Makampuni kadhaa tayari yanatafuta uranium nchini. Sasa utafutaji huu unaelekezwa na kanuni hizo?

Mheshimiwa Spika, si vyema kuruhusu shughuli muhimu kama hizo kuanza bila miongozo yoyote ili kuepusha madhara kutokea. Daima ukweli ni kwamba, bora kinga kuliko kuugua.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwawezesha wachimbaji wadogo kupimiwa maeneo kamili, limeshauriwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa muda mrefu. Kinachosikitisha, utekelezaji hufanyika kwa dharura mara janga linapotokea. Tatizo la utekelezaji wa kusuasua ni nini hasa? Hatujachoshwa na migogoro ya mara kwa mara kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo?

Sambamba na hili ni muhimu kuongeza thamani ya vito vinavyochimbwa hapa hapa nchini. Kinachosikitisha ni kwamba; si wachimbaji wadogo wala Serikali, wanaopata faida ya kutosha kwa sababu wachimbaji hasa wadogo wanalanguliwa na wanunuzi kwa bei ndogo sana. Yafaa tuwaokoe wachimbaji wetu hao sasa toka kwenye unyonyaji huo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya usambazaji umeme, lakini Serikali iwe makini kutopandisha bei za huduma ya umeme kwa wananchi ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaojitokeza kwa matumizi ya kuni na mkaa. Hata hivyo, nashauri sambamba na nia nzuri ya kusambaa umeme TANESCO ihakikishe kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo ambayo tayari upo.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu ni kwa nini TANESCO hawajafikisha umeme kwenye shule hata zile za watoto/wanafunzi wenye ulemavu badala yake kuendelea kuzidai Taasisi/Serikali kulipa madeni hayo kwa wakati badala ya kuwaongezea adha ya kuishi shule/vyuoni na giza kwa watoto na wanachuo wenye ulemavu kama ilivyotokea huko Mkoa wa Ruvuma kwenye Shule ya Msingi ya Wasioona ya Luhira?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono umuhimu wa Serikali kushughulikia suala la udhalilishaji wa wachimbaji unaofanywa na wawekezaji huko Mererani na Kampuni ya Tanzanite One. Ni vyema Serikali ikachukua hatua za haraka kwa vile vilio na malalamiko yamekuwa mengi.

Baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo ya nini kinachoendelea juu ya ugawaji wa viwanja vya

uchimbaji madini vya Winza, Kibakwe Mpwapwa, maana Kamati ya Ugawaji ya Wilaya ilimaliza kazi yake lakini hadi sasa ni leseni 100 tu zilizokamilika?

Maombi yalikuwa mengi na hivyo kutoa leseni hizo chache ni kuchochea vurugu tu. Naomba ufafanuzi utakaosaidia kupunguza vurugu zinazofanywa na baadhi ya wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake, kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Maamuzi ya Serikali ya kurejesha Kiwira (madini ya makaa ya mawe Kiwira), mikononi mwa TANESCO na STAMICO wakati mgodi umechoka, umefilisiwa na makampuni yaliyoingia ubia wa kuendesha mgodi huu, tunaomba Serikali itueleze yafuatayo:-

Mgodi ulikuwa unafanya kazi na kuzalisha wawekezaji ikiwepo Kampuni ya ANBEN waliufikisha hapa ulipo, vipuri viling'olewa na kuuzwa, wafanyakazi wametumikishwa bila kulipwa mishahara na mapato mengine mengi. Je, nani atakayegharimia na kurejesha hali nzuri ya mgodi huu? Fedha za wananchi maskini zitatumika kulipa madeni ya watu wakati wawekezaji wamejichotea chao na kuondoka; mzigo huo anawishwa nani?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kukumbatia Makampuni ya Madini hapa nchini. Kwanza, Serikali imeingia kwenye uwekezaji wa Madini bila maandalizi yoyote. Matokeo yake taifa hatufaidiki vilivyo na rasilimali hiyo. Hatuna wataalam walioboea kwenye madini na ndiyo maana mali zetu zinavunwa kama vile hatupo au tumelala usingizi wa pono. Hatujui thamani halisi ya madini yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa rasilimali tuliyonayo Tanzania, hatustahili kuwa maskini. Kuendelea kwa umaskini ni sisi wenyewe tunasababisa kwa kushindwa kusimamia rasilimali zetu vizuri.

Tunauza madini ambayo hayajasafishwa, wawekezaji wanabeba hadi udongo wanapeleka kwao wananufaika, sisi huku tunapiga miayo na kulia njaa na kuomba msaada kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kukubali madini haya ambayo ni *non-renewable resources* yaondoke tu bila kujua thamani yake huku tukiambulia mrabaha na kuwaachia wananchi mashimo; ni fedheha kwa taifa hili. Ni lini sasa Watanzania watanufaika na rasilimali hii muhimu?

Mheshimiwa Spika, mataifa ya nje yanatushangaa kwa jinsi tunavyopanda ndege kwenda kuomba tusaidiwe, huku tukiwaachia wajanja wananufaika na rasilimali hii. Hivi kweli tunakuwa na viongozi waliokosa uzalendo kiasi hiki; tutafika wapi? Watu wanaangalia maslahi yao tu na siyo maslahi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Madini wa North Mara, umeendelea kuumiza wananchi wanaoishi jirani na eneo hilo huku Serikali ikiangalia tu. Kitendo cha kiwanda hiki kumwaga maji machafu na *chemicals* kutoka kiwandani kwenye maji yanayotumiwa na binadamu ni kitendo cha mauaji ya kukusudia. Vifo vilivyotokea kwa Wananchi wa Nyamongo vilikusudiwa, hivyo wawekezaji wa mgodi huo wanastahili kufunguliwa mashtaka ya mauaji. Tunashangaa mpaka sasa wanatamba mitaani huku kiwanda kikiendelea kufanya

kazi. Wananchi wameathirika vibaya, watoto wamebabuka huku Serikali inamkumbatia mwekezaji huyu bila aibu; hivi kweli Serikali inajali wananchi wake?

Mheshimiwa Spika, mojawapo kati ya haya mawili yanatakiwa kufanyika kwa haraka sana:-

1. Serikali iufunge mgodi huu kwanza, uchunguzi ufanyike kujua athari ambazo wananchi wameendelea kuteseka. Kitendo cha wamiliki wa mgodi huu kumficha hata Waziri wa Usalama wa Raia, eneo halisi ambapo uchafu unatoka ni udhalilishaji wa taifa letu au kuna 10% zinatolewa kwa viongozi wa juu?

2. Wananchi hawa wahamishwe haraka, watafutiwe eneo lingine la kuishi na kupewa stahili zao zote na kupatiwa miundombinu yote kwenye eneo hilo ili kupisha mgodi huu uendelee baada ya kufanyiwa marekebisha.

Mheshimiwa Spika, wapo Wananchi wa Kata ya Vumilia na Ushokola Wilaya ya Urambo, walivunjiwa nyumba zao kupisha nguzo za umeme tangu 2006 hadi leo hawajalipwa chochote. Waziri atueleze lini watalipwa stahili zao?

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii, wakishirikiana na Watendaji wote, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumejitokeza kwamba wafanyakazi (wachimbaji) wa Tanzanite One wanapata matatizo mbalimbali yatokanayo na waajiri wao hasa tatizo la kupigwa mionzi (X-ray) kila siku na kwamba, wengi wao wana wasiwasi kuwa miozi hiyo imewaathiri sana katika miili yao, basi nashauri Serikali ifuatilie kwa karibu sana ili kuweza kubaini ukweli na kuchukua hatua husika ili kuwaondoshea wasiwasi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo katika eneo la Mererani wanakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi, hasa wa eneo la kazi, elimu ya kazi yao, mazingira duni na kukosa mambo muhimu ya kuendesha biashara zao kama kukosa mikopo na misaada mbalimbali ambayo wao ni wachimbaji wadogo wazalendo; kwa hiyo kuwakosha kipato kizuri. Nashauri Serikali iwasaidie wachimbaji hao ili wajihisi kama ni Watanzania na na Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wafanyakazi wa Kiwira Coal Mine wanakabiliwa na matatizo mengi sana, yakiwemo ya kutokulipwa mishahara yao kwa kipindi cha mwaka sasa, posho na huduma muhimu mbalimbali, jambo ambalo linawadhalilisha sana Wafanyakazi hao hasa wanawake. Napenda kuishauri Serikali ifanye bidii mahususi, iweze kuwalipa kwa haraka Wafanyakazi hao na kuweza kuwaondolea matatizo wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi ambazo zimefanyika katika kipindi hiki, japo si za kuridhisha sana, hasa kutokana na kuchelewa kwa bajeti (yaani pesa zilizotengwa) katika kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Naipongeza Wizara kwa kuufanyia kazi ushauri wa Bunge, hususan Kamati ya Nishati na Madini ili kuwa na *Power Master Plan* ambayo sasa imekamilika na hivyo kutoa dira. Bado nipo katika suala la umuhimu wa Serikali kutoa pesa zilizotengwa mapema ili kuwezesha Wizara hiyo kutekeleza kazi zake kwa wakati. Mfano, mwaka jana, pesa za maendeleo zilizotengwa zilitolewa asilimia tano tu; hilo ni tatizo.

Shughuli za kazi za umeme zinahitaji kupitia taratibu mbalimbai za manunuzi ya vifaa na matayarisho mengine kama kuandaa washauri na makandarasi. Hivyo ni vyema wapewe pesa hizo mapema.

Uwezekano wa nchi kupata umeme kwa wakati upo, lakini tatizo ni utekelezaji unaochelewa.

Ripoti ya Richmond iliyowasilishwa ni vyema ipewe muda wa kujadiliwa ili tujiridhishe zaidi.

Sheria ya Gesi inaletwa lini? Suala la usambazaji wa gesi mjini mbona mkakati umekuwa hasa ukilenga viwanda tu? Je, hawa wananchi wengine watanufaika vipi?

TPDC ambayo ndiyo mlengwa wa kufanya kazi hizo amewezeshwa vipi? Ni vyema sasa Serikali itueleze kama kweli ina dhamira ya kuliwezesha shirika hilo?

Napongeza maamuzi ya Serikali ya kuuchukua Mgodini wa Kiwira, lakini pia nawapongeza wawekezaji hao kwa kuurejesha Mgodini huo Serikalini. Nadhani kama kungekuwa na tabia ya watu kufanya tathmini na kuridhia kukubali upungufu na kurekebisha, hata haya malumbano yasingekuwepo. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa na Serikali isichelewe kuhakikisha kuwa, inamaliza mara moja tatizo la Wafanyakazi wa Kiwira ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Mwisho, natoa masikitiko yangu kwa Wizara hii kwa kutojibu maswali yangu kwa wakati. Huku ni kuni-*frustrate* na pengine mimi naelewa vibaya, kwani sioni sababu inayofanya maswali yangu yasijibiwe kama nilivyoahidiwa. Hata hivyo, nitafuatilia katika Ofisi za Bunge kujua sababu zilizopo.

Umeme Songea bado ni tatizo, tunahitaji kufahamu kazi hiyo ya umeme wa gridi 132 KW, kama ambavyo niliuliza kwenye swali langu ni lini itaanza? Ukiacha pesa zimetolewa na SIDA, jibu hilo linatolewa kila bajeti toka naanza kuwa Mbunge. Naomba majibu ya kina.

Naupongeza Mradi wa Umeme Ngake, 400mw 400 KV ni dhahiri kuwa Mradi huu ukitekelezeka, utaokoa taifa.

Nazidi kushukuru kwa umeme wa Mbinga, ila tunaomba *more distribution lines extention*. *Big up*, naunga mkono hoja.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa bajeti yao ambayo ni nzuri na yenye kutia matumaini kwa Watanzania ambao wengi wao hasa wa vijijini, wanakabiliwa na tatizo la umeme, lakini pia ni bajeti ambayo kwa kiasi kikubwa inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.



Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuendelea kutafuta mafuta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kumejitokeza matatizo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi na kuamua kuyatoa mafuta katika mambo ya Muungano. Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusiana na tatizo hilo ambalo linatishia kuchafuka kwa Muungano?

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuendelea kushirikiana na Marekani, kwa kufadhili Miradi yote ya MCC nchini kote, kwa kuimarisha, kupanua, mifumo ya kusafirisha na kusambaza umeme katika mikoa mbalimbali nchini. Napenda kutoa wito kwa Serikali, kuhakikisha wale wote watakaathirika na zoezi hili, wafidiwe kabla miradi hiyo haijaanza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza wote kwa ushirikiano wa kuendesha nchi yetu kupitia Nishati na Madini. Najua ni kazi ngumu sana, lakini nendeni mbele kwani iko siku tutafika. Msingi, tumieni maarifa na akili mlizopewa na Mungu, kusaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana kwa umeme wa Peramiho. Ninashukuru sasa *installation* inakaribia nusu ya safari, Kijiji cha Likuyufusi. Ahadi ya Serikali ilikuwa mwaka huu wa 2009 umeme unawashwa Peramiho, ninaomba kuthibitishiwa hilo. Ninaomba TANESCO waongeze bidii mradi huu ukamilike. Naomba kufahamu na kupata majibu katika hili.

Nawapongeza Wakala wa Umeme Vijijini. Ushirikiano tulioupata kwao kushughulikia umeme katika maporomoko ya Kijiji cha Mahanje yametutia moyo sana, tunaomba mashirikiano hayo yazae matunda. Umeme ule utaongeza nguvu sana katika mkondo wa taifa, ambao utapita Mdaba na Mahanje, njia kuu kuelekea Ludewa. Hata hivyo, tunayo maporomoko mengine makubwa sana Kijiji cha Magagura tunawaalika mje kuyaona.

Ningependa yafanyike mapitio maalum na ya kutosha ya kuona ni kiasi gani madini yanaweza kutusaidia kuondoa utegemezi wa nchi yetu katika kujiendesha. Bado ni wategemezi, tunategemea fedha za nje katika kuendesha shughuli za kiutendaji za nchi yetu. Tujaribu sasa kuona ni kiasi gani tunaweza kutumia madini kama uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa letu. Jitahidini jamani, hali ya nchi ni mbaya, uwezo wa ndani unazidi kupungua lisaidieni taifa.

Suala la hifadhi ya mafuta na ununuzi wa pamoja lipewe msukumo.

Naunga mkono hoja na nawatakia kazi njema.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, kwa kunijaalia kuwa mzima na mimi kuweza kutoa maoni yangu kuhusu Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu wake, pamoja na Watendaji wake wote, kwa jinsi walivyoandaa bajeti hii; hofu yangu ni utekelezaji tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa, napenda kukupongeza wewe, Naibu na Wenyeviti wako wote.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kuhusu umeme. Hakuna asiyejua umuhimu wa umeme, kwani ndio maendeleo ya nchi, kwa sababu mambo mengi sana yanahitaji umeme. Cha kusikitisha zaidi ni namna ya Shirika la TANESCO kuunga umeme kwa gharama kubwa sana, kiasi wananchi wengi wanakosa umeme hata katika miji au mitaa yao. Umeme upo lakini wanakwazwa na bei, ambayo bado haijawalenga wananchi ambao wengi ni maskini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iliangalie jambo hili kwani hii siyo *luxury*, bali ni muhimu sana kwa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naamini Serikali ni moja na Wizara zake zinajua mambo wanayoyafanya. Katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Chuo chake cha DIT ambacho wanafunzi walifanya utafiti na kugundua chombo ambacho ukiunganisha umeme gharama zake ni ndogo na kinafaa hasa kwa vijijini kwani inaonesha *connecting* yake ni ndogo sana, unaweza kutumia taa za ndani na radio tu. Namwomba Waziri au Naibu waende Chuo cha DIT, wakaangalie chombo hicho na waweze kukitumia na kupunguza gharama, wananchi waweze kupata umeme kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la TANESCO, wanapenda kuagizia taa za barabarani Afrika ya Kusini wakati bado hicho hicho Chuo cha DIT kimefanya utafiti na kuweza kutengeneza taa nzuri. Vile vile naiomba Serikali ihakikishe inatumia taa hizo badala ya kutumia fedha nyingi kuagizia nje.

Mheshimiwa Spika, bado niko hapo hapo Chuoni, naiomba Wizara hii wawe karibu na Chuo hicho, kwani mambo mengi mazuri yanayohusu umeme nadhani kitawasaidia sana Wizara hii kuepukana na gharama zisizo za lazima na kuwasaidia wananchi kupata unafuu wa umeme.

Mheshimiwa Spika, nadhani wananchi wengi wanashindwa kuweka umeme kutokana na umeme usio wa uhakika. Naomba Serikali ipange mikakati mahususi ili umeme uwe wa uhakika ili nchi yetu ipate maendeleo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wawekezaji wa Madini, kwa maoni yangu naona Serikali inawapa kipaumbele wawekezaji kuliko wananchi wake, kwani malalamiko kila pahala unayasikia kuhusu wawekezaji hawa. Wananchi wa Tanzania tunaonekana watu wa ajabu sana, kwa kupenda kulalamika lakini mtu mzima na akili yake na vile vile aone jambo ambalo linamletea maslahi kweli awe analalamika ovyo; hasa ukizingatie Watanzania ni watu wa amani na upendo mkubwa hasa kwa wageni?

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali isikilize kilio cha wananchi wake, mateso mengi wanayopata wananchi wetu tunayasikia na Serikali inadharau au mpaka muone watu wanajichukulia sheria mikononi mwao ndio Serikali itajua kama wananchi wanapata tabu? Kwa mfano, North Mara, Mererani, Geita na kadhalika, kote huko kuna madhara makubwa ambayo tunayashuhudia, yakiwakumba wananchi wa migodi hiyo na Serikali inachelewa kuchukua hatua mpaka jambo liwe limeathiri sana ndio itume kamati. Je, Utamaduni kama huu utakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Hapo awali, nilileta mchango wa maandishi kuhusu umeme katika maeneo ya Waretu, Dirma, Simbay na Gisambolong, ambapo kuna huduma nyingi za jamii kama Vituo vya Afya na Zahanati, Shule za Sekondari na shughuli za kiuchumi. Hii ni ahadi ya Waziri na Naibu Waziri. Vile vile umeme wa Wilaya ya Hanang kuunganishwa na Gridi kupitia Mkoa wa Manyara, badala ya Wilaya kuhudumiwa na Mkoa mwingine wa Singida kwani Wilaya haipewi kipaumbele. Je, utekelezaji umeanza kama bado lini utanza kwani ni mpango wa muda mrefu? Niliona jitihada alipokuwepo Meneja wa Wilaya aliyehamishwa, lakini sasa hivi naona shughuli haziendelei.

Kuna mtu aliyeathirika kwa kuungua na nyaa za umeme zilizoanguka wakati wa mvua na upepo, lakini ilichukua muda kuinua nguzo na bila TANESCO kutoa tahadhari kwa wananchi wa maeneo hayo. Mtoto yule bado anateseka hospitali, miguu na mikono yake imelemaa. TANESCO wamemtelekeza mtoto huyo bila ya msaada wa matibabu ya kutosha. Pale awali walionesha nia nzuri, lakini hawajafanya jitihada za kumnusuru mtoto huyu ambaye wazazi wake ni fukara. Mheshimiwa Waziri, tafadhali aingilie kati ili mtoto huyu maskini wa Jimboni kwangu asaidiwe na TANESCO.

**MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara, kwa kuwasilisha hotuba nzuri. Aidha, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa jinsi wanavyoshirikiana vizuri katika kuiongoza Wizara waliyokabidhiwa. Wamekuwa mfano mzuri wa kuigwa.

Ningependa kuchangia mambo machache yanayohusu maendeleo na uwezeshaji wa wananchi hasa wachimbaji wadogo wa madini. Sera yetu na Ilani yetu, inatutaka kusaidia wachimbaji wadogo wa dhahabu na madini ya vito ikiwemo Tanzanite. Wakati wa Awamu ya Tatu, niliandaa Muswada Binafsi kuhusu uchimbaji, ukataji na uuzaji wa Tanzanite. Serikali kupitia Kikao cha Uongozi cha Bunge, waliupokea Muswada huo, walikubali msada huo na kuniomba niachie Serikali ilete Muswada wa Sheria Bungeni, jambo ambalo halikufanyika wakati ule. Serikali ilitaka kutoa Waraka wa kuzuia kuuza Tanzanite ambayo haijakatwa, lakini hali imebakia vile vile kuuza Tanzanite isiyokatwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alikwenda kusaidia Kampeni ya Ubunge kule Busanda, malalamiko makubwa yalihusu wachimbaji wadogo wadogo kutosaidiwa kupewa viwanja na zana za kazi.

Jambo lingine linahusu shida kubwa ya umeme Sumbawanga Mjini. Umeme huu unatoka Zambia, siyo wa kuaminika. Kutokuwa na umeme wa uhakika, kunaathiri maendeleo ya ujenzi wa viwanda na uendelezaji wa viwanda vichache vilivyopo.

Tunaomba Serikali ituwekee mitambo ya umeme, ambayo itasaidia Mji wa Sumbawanga kuwa na umeme wa uhakika.

Baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii kwa kuzingatia majukumu yake kwa nchi ni muhimu sana na ndio maana napenda kuwapongeza

Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa jitihada wanazozifanya. Hata hivyo, zipo changamoto nyingi ambazo zinapaswa kuwekewa mkakati kuzitekeleza. Mchango wa jumla ni katika yafuatayo:-

Mradi wa Kusambaza Gesi ni muhimu na tumechelewa sana. TPDC wanao utaalim wa kufanya kazi hii, wanahitaji fedha, lakini inaonekana Pan African ndio wanaofanya kazi kwa kuanza na sehemu za hoteli na Mikocheni. Wataalam wanasema Mradi huu ungefanywa kwa pamoja kwa kupeleka majumbani, Jiji la Dar es Salaam bei zingekuwa chini kuliko utaratibu wa sasa. Ukiondoa hao walaji wakubwa, unaweza kuweka bei ya kufaa kwa maeneo mengine.

Pili, nilifikiri sehemu za kuanzia ingekuwa Wilaya ya Temeke na baadhi ya sehemu zenye makazi mengi na matumizi yao makubwa ya nishati ni kuni na mkaa.

Jambo la pili ni utoaji wa leseni; wanaopewa leseni ni Wizara au Mkoa, huenda moja kwa moja kwenye maeneo. Wilaya hazina taarifa, yatokeapo maafa au shida mbalimbali, wilaya inatakiwa kuwahudumia. Tutafute mfumo wa kutoa taarifa kwa wilaya.

Jimbo la Mbinga Mashariki, tunaishukuru Serikali kwa kununua majenereta mawili yenye uwezo wa MW 2.5 kwa pamoja. Umeme unaotumika sasa hivi ni mdogo, kwa sababu *service line* hazijajengwa kwenye maeneo mengi. Watu wanashindwa kulipia nguzo shilingi milioni mbili na kuendelea. Naomba ujenzi wa *service line* ufanyike.

Ombi langu maalum ni kwamba, shule inayohudumia walemavu wapelekewe umeme. Kwa nini TANESCO inataka walipe shilingi milioni 20? Njia yote ina watu watakaofaidika na umeme huu.

Miji Midogo inaweza kabisa kutumia nishati hii. Magu, Litembo (pana hospitali kubwa sana); Matiri, Ruanda na Mbangamao. Mbinga haina hata Kijiji kimoja chenye umeme.

Niliandika barua mwaka 2007, kuomba Wizara ijenge Ofisi ya Madini Mbinga, ambako kuna shughuli nyingi za madini; naomba utekelezaji. Tunduru ipo; je Mbinga?

Eneo la Makaa ya Mawe Mbuyule lilikuwa linaungua na bado linaungua. Nilifanya kazi kubwa ya kufuatilia jambo hili 2006. Mkaa wa tani 400 upo nje. Katibu Mkuu, alifika katika eneo na aliahidi kuleta wataalam kuwafundisha wananchi namna ya kutumia mkaa huo na namna ya kutumia udongo mzuri uliopo. Napenda kufahamu maendeleo yake na wananchi wanasubiri.

NDC na Panfic Corporation kupitia Kampuni ya Tan Coal, wamekwishawekeza zaidi ya shilingi bilioni 1.6 katika utafiti. Mkaa ni mwingi na mzuri. Mpango wa sasa ni kufanya EIA ili kuanza uchimbaji na baadaye kujenga Power Station.

Mpango ni kuzalisha umeme wa MW 50 ifikapo Desemba 2010. Umeme huu unatosha kwa shughuli zao, lakini pia kulisha Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma, lakini ifikapo 2014 watakuwa wanazalisha 400 MW. Kampuni hii inaonesha inao uwezo mkubwa wa utaalim na fedha. Ajabu ni kwamba, habari hii haitambuliwi na Wizara, kwa maana Mradi huu haujatajwa mahali popote! Baada ya kuonesha bidii kubwa hiyo, Serikali hata kuwapongeza tu imeshindwa. Ipo Miradi imetajwa ndani ya Hotuba ya Wizara, haijaanza na wala haina fedha. Kwa nini Serikali inaona aibu juu ya Mradi huu?

Mchimbaji mkubwa aliyekuwa anachimba pale Misungwi, amesitisha kazi na kuacha mashimo. Naomba afuatiliwe ili aje kuyafukia.

Wizara itangaze eneo hili kuwa la uchimbaji mdogo mdogo. Wachimbaji wadogo hawa wapewe elimu na baadaye uwezo kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 inavyotaka.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumejitokeza kauli zinazoelekea kutikisa uimara wa Muungano wetu. Suala la mafuta, ambalo Baraza la Wawakilishi limeazimia kuliondoa kutoka orodha ya mambo ya Muungano. Ningeomba, Wizara yako na Wizara ya Maji na Nishati za Zanzibar, mkae pamoja na kujadiliana namna bora ya kushughulikia tatizo hili. Mafuta yakipatikana ni jambo la neema kwa nchi yetu. Si vyema neema hiyo ikawa chanzo cha kuvunja Muungano wetu. Kauli zinazoendelea hivi sasa, zinaashiria kutaka kuyumbisha malumbano na udugu wetu.

Naomba nitoe pongezi zangu nyingi kwa EWURA, kwa kazi yao nzuri. Kwa mara ya kwanza, tumeshuhudia bei ya mafuta ikipungua baada ya kazi nzuri ya udhibiti uliyofanywa na EWURA.

Mfumo wa Bulk Procurement utasaidia sana katika kudhibiti ukwepaji kodi. Kwa kuwa Wizara tumeshapata mtaalam mshauri anayesaida kupanga namna bora ya kutekeleza mpango huu, ushauri wangu hi kwamba, Wizara ifuatilie kwa ukaribu ili kazi hiyo ikamilike mapema na utaratibu huu uanze mara moja.

Bado Mpango wa Mradi wa Umeme wa Stieglers' Gorge, haujapewa umuhimu unaostahili. Huu ni Mradi ambao utazalisha MW 2100; hiki ni kiasi kikubwa cha umeme ambacho kinaweza kumaliza tatizo la umeme ndani ya nchi yetu.

Napenda nilipongeze Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), ambalo linafanya kazi nzuri katika mazingira magumu. Inawezekana upo upungufu katika baadhi ya maeneo, lakini ni vyema tukawa na utamaduni wa kupongeza pale kazi nzuri inapofanyika, kwani hali kama hiyo inawaongezea ari watendaji wa mashirika yetu.

Mwisho, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji na Makamishna wote. Wizara hii ni uti wa mgongo wa uchumi; inategemewa na wengi, lawama hazikosekani, songeni mbele chapeni kazi na Mungu atawajaalia.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mungu, kwa neema yake hata kuniwezesha kuwepo hapa nami niweze kutoa mchango wangu.

Nichukue nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote, kwa hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha hapa Bungeni leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu na suala la migogoro kati ya wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wadogo, kuhusu mipaka ya juu na chini katika uchimbaji wa madini ya vito; Tanzanite Merarani.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, ilitoa agizo kuwa madini haya yachimbwe wima wakati madini yote ya vito yanapatikana katika mwamba kwa kuambaaambaa. Unachimba wima mpaka mita 100 hadi 200, ndipo unaambaambaa kwa kufuata mwamba unakokuelekeza kwenye uzalishaji. Hivyo, unaambaambaa siyo uchimbaji wa kuchimba kama choo.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kwa nini Serikali imetoa Agizo hilo kwa wachimbaji wadogo wadogo tu? Ina maana kwamba, wachimbaji wakubwa kama Tanzanite One wanachimba wima? Ikiwa wanachimba wima mitobozano inatoka wapi kutobozana na wachimbaji wadogo wadogo? Je, Serikali ilipotoa eneo hilo haikujua kuwa madini hayo hayachimbi wima? Kwa nini Serikali ilitoa maeneo makubwa sana kwa wawekezaji hawa wa Tanzanite One na kuwapatia wachimbaji wazalendo kieneo kidogo cha mita 50 x 50 kwa kiwanja kimoja?

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wa Tanzanite One wanapigwa X-ray kila siku na Serikali inakubali wananchi wake kuathirika na mionzi hii. Hivi ni Serikali gani inatoa rasilimali yake kwa wawekezaji pamoja na maisha ya wananchi? Je, Serikali haielewi kwamba baada ya miaka kadhaa hao watu watapoteza maisha? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifikie mahali iseme kuwa, sasa inatoshia; tumeporwa uchumi wetu rasilimali zetu na wawekezaji huku tunalia Tanzania ni nchi maskini. Hivi kweli viongozi wetu wamefunga macho na kuziba masikio kwamba hawaoni wala hawasikii kilio cha wananchi wao? Hivi kweli wananchi ndio wanaona uchumi wao ukiporwa lakini viongozi hawaoni?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kwa nini Serikali ilikiuka Sheria ya Madini ya Mwaka 1998? Sheria ya Madini ya 1998 inasema kwamba, madini ya vito yatachimbwa na wazalendo tu. Ilikuwa je Serikali itoe maeneo haya kwa wawekezaji ambao ni wachimbaji wakubwa? Waziri anaweza kulielezea Bunge hili kwamba, kuna nchi nyingine Afrika ambayo imeachia rasilimali zake kama madini ya vito kuchimbwa na wawekezaji? Je, Serikali haikuona juhudi kubwa zilizofanywa na wachimbaji wadogo wadogo katika kuleta maendeleo makubwa?

Mheshimiwa Spika, majengo yote mazuri yaliyoko Mjini Arusha ni ya wachimbaji wadogo wadogo. Naomba sasa Serikali irejee Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 ili madini hayo yaweze kuchimbwa na wachimbaji wazalendo.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa uamuzi wake mzuri wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya Export Processing Zone (EPZ), likiwepo eneo la Mji Mdogo wa Mererani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umaskini mkubwa uliokuwa umelikumba eneo la machimbo ya Tanzanite Mererani, sasa ukombozi umepatikana; Wananchi watapata ajira, tena itakuwa faida na maendeleo kwa Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Tunataka madini yote yakatwe, tayari kwa ajili ya Export na Serikali ikusanye mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Madini na Wizara ya Miundombinu, wakae pamoja waone uwezekanao wa kuweka lami barabara inayotoka KIA kwenda Mererani ili kuweza kuwavutia wawekezaji ambao sasa watakuja kwa wingi kuanzisha viwanda.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kuwakaribisha wawekezaji kwa ajili ya kujenga viwanda. Tumetenga maeneo ya kutosha kabisa. Tunaiomba Serikali kupitia Shirika la NSSF, waje Mererani kuwekeza wajenge viwanda na makazi ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwaonee huruma wachimbaji wadogo wadogo, iwaondolee ushuru kwenye zana za milipuko. Imekuwa vigumu sana kwa wachimbaji wadogo wadogo, kumudu kununua zana za kulipua miamba.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwafananisha wachimbaji wadogo na wakubwa. Huo ni uonevu na uonevu huo umewapelekea wachimbaji wengi kushindwa kuendelea na uchimbaji wamefunga migodi yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina huruma na wananchi hawa? Je, inawatakia mema au ni kwamba Serikali inatafuta namna ya kuwafanya washindwe wenyewe waondoke ili kuwaachia wachimbaji wakubwa waendeleo na uchimbaji huo?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi, Serikali ina mpango gani wa kuondoa ushuru na kupunguza bei ya zana za uchimbaji wa wachimbaji wadogo wadogo?

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2005 wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapatia Elimu na maarifa mapya katika fani ya uchimbaji wa madini. Pia Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia katika kukuza shughuli, itanza utekelezaji wa mradi endelevu, utakaotekelezwa kwa miaka mitano katika kuongezwa thamani ya madini, pamoja na kujitangaza kwa kutumia takwimu mpya za kijiolojia. Mashine mahususi zitanunuliwa na kufungwa kwa shughuli za usanifu wa vito na usonara (*Lapidary and jewellery*). Haya ni maendeleo makubwa sana. Je, mashine hizo zimekwishaagizwa au bado kama bado zitaletwa lini?

Naomba kuunga mkono hoja, lakini nipate ufafanuzi wa masuala yote niliyouliza.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Mheshimiwa Dkt. Idrisa Rashid, CEO wa TANESCO na Watendaji wote.

Kwa muda mrefu nimekuwa nikieleza tatizo la siku nyingi la kutopatikana kwa umeme kwa Mji Mdogo wa Ihanja, ambako kuna *Technical Secondary School* na Sekondari nyingine, Kituo cha Afya, Msikiti na Makanisa, mashine za kusaga na kadhalika. Aidha, nimekuwa nikieleza tatizo la kutopatikana umeme Mji Mdogo wa Sepuka, ambako nako taasisi nilizozitaja hapo juu zipo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimeonana na Mheshimiwa Waziri kuhusu tatizo hili na amekuwa akiniahidi kuwa Miji Midogo hiyo itapata umeme. Aidha, Mheshimiwa Waziri ameniandikia barua ya kututhibitishia mwaka 2008 kuwa, Miji Midogo hiyo itapata umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo lililonisikitisha zaidi ni kuwa, katika Kitabu cha Hotuba ya Waziri, hakuna popote maeneo hayo yametajwa; si upande wa TANESCO wala upande wa REA. Sasa nauliza ahadi za Mheshimiwa Waziri kwangu kuwa umeme katika maeneo hayo utapatikana itatekelezwa vipi wakati bajeti haioneshi lolote?

Mheshimiwa Spika, ninamheshimu na ninamwamini Mheshimiwa Waziri, lakini safari hii sitakubali na hivyo sitaunga mkono hoja yake. Ninapenda kupata maelezo ya kuridhisha. Mradi wa Ihanja ni kiporo kwa miaka 10.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme majumbani ni kubwa mno na zinawakatisha tamaa wananchi kuweka umeme. Tatizo kubwa ni kwa wananchi wa vijijini; watakata wapi shilingi milioni moja na zaidi kuunganisha umeme? Naomba Serikali itafute njia ya kusaidia suala hilo. Narudia siungi mkono hoja hii mpaka kieleweke.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote Wizarani, pamoja na Mashirika (Taasisi), yaliyo chini ya Wizara, kwa matayarisho mazuri ya Hotuba hii ya Bajeti.

Shughuli zilizo chini ya Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu. Kutokana na umuhimu wa shughuli hizi (Nishati na Madini), napendekeza ziundwe Wizara mbili tofauti ili kila moja; Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini, ziweze kutumia muda wa kutosha kukabiliana kikamilifu na changamoto mbalimbali katika maeneo haya mawili, yaani Nishati na Madini kipekee.

Pamoja na ongezeko la mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini yetu \$ 1,075,943,000, nchi yetu haijafaidika ipasavyo kutokana na pato hili. Tatizo ni mikataba iliyopo chini ya Sheria yetu ya Madini. Changamoto hii itapata ufumbuzi kwa kubadilisha Sheria yetu ya Madini, pamoja na kurekebisha mikataba iliyopo kwa manufaa ya Taifa letu. Ushauri wa Kamisheni ya Jaji Bomani unatosha uzingatiwe.

Ianzishwe Benki ya Rasilimali kwa njia ya Sekta ya Madini. Aidha, Serikali inaweza kutumia Benki ya TIB kwa kuiongezea mtaji ili iweze kuwahudumia wachimbaji wa madini, pamoja kutoa mikopo kwenye sekta nyingine.

Wanahisa katika Kampuni ya Williamson Diamonds Ltd., wakubaliane kuhusu hoja ya kuiongezea mtaji Kampuni hii haraka iwezekanavyo ili iweze kuongeza kiwango cha uzalishaji wa almasi.

Mradi wa Bomba la Mafuta toka Dar es Salaam – Mwanza ni wa siku nyingi na utekelezaji wake umechelewa sana. Hivi sasa bomba la mafuta la Mombasa – Eldoret limekwishafika Kisumu na Uganda, mipango iko mbioni kulifikisha bomba hili Ruanda, Burundi na hatimaye DRC. Kwa hiyo, kuchelewa kutekelezwa kwa ujenzi wa bomba letu la mafuta Dar es Salaam – Mwanza/Kigoma, kutaufanya Mradi huu usiwe na faida za kiuchumi zilizotarajiwa. Nashauri Serikali isimamie kwa karibu sana utekelezaji wa Mradi huu ili uweze kukamilika haraka iwezekanavyo, kwa manufaa ya uchumi wetu.

Naipongeza Wizara kwa kuhakikisha kwamba, matumizi ya gesi asilia yanaendelea kuongezeka. Pamoja na matumizi viwandani, kuna mpango wa kuanza kuitumia gesi asilia katika Taasisi mbalimbali, kuendeshea magari na hatimaye majumbani.

Changamoto iliyopo ni kasi ndogo ya utekelezaji wa Mradi huu. Naishauri Serikali iongoze kasi ya utekelezaji wa Mradi huu kwa manufaa ya uchumi wetu. Kwa mfano, kwa nini tunaanza na magari 200 tu?

Nakipongeza sana Kitengo cha Ukaguzi (Gold Audit Program – GAP), kwa kazi nzuri kinayofanya. Nashangaa kwa nini Makapuni ya Madini inaelekea yanachelewa kulipa pengo



la mrabaha wanaodaiwa (page 45 ya hotuba aya ya 74)! Nashauri Serikali ihakikishe pengo linalojitokeza linalipwa mara moja na siyo kidogo kidogo.

IPTL ni tatizo la muda mrefu. Kila mwaka tunaambiwa kuwa, mazungumzo ya kumaliza tatizo yanaendelea. Je, yatakwishia lini mazungumzo au majadiliano baina ya TANESCO na wawekezaji ndani ya IPTL?

Serikali inaharakisha mchakato utakoiwezesha TPDC kuwa na uwezo wa kifedha wa kuagiza mafuta kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa.

Aidha, itakuwa vizuri zaidi kama kiwango kitakachoagizwa na TPDC kitakuwa kikubwa zaidi ya Hifadhi ya Taifa ili kitumike pia ku-*moderate* bei za mafuta katika soko la Tanzania.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kushauri yafuatayo:-

Suala la kupeleka umeme vijijini siyo *luxury* ni hatua mojawapo ya ku-*balance* hali za maisha kati ya vijiji na miji. Sababu zipi zimefanya Kata ya Kagoma isipate umeme chini ya REA au wafadhili wowote wanaowasiliana na Serikali?

Nimeomba umeme huu tangu 2001, hivi ni kweli hadi leo imekuwa vigumu kuipa umeme Kagoma?

Kagoma ina wahitaji kwa sasa zaidi ya 100, ikiwemo Sekondari Kagoma, Misikiti miwili, Kanisa moja, eneo lenye *view* nzuri ya uwekezaji inayotazamiwa na Ziwa Victoria na Visiwa vya Bumbire, pazuri mno.

Kagoma imezunguka kibiashara kwa sababu ya kukosa umeme. Kagoma ilikuwa na vituo viwili vya kuuza mafuta, sasa vimekufa. Ilikuwa na mashine za kusagisha na kukoboa nafaka, miradi hiyo sasa imekufa. Kagoma ina *lake shore* nzuri ya Pwani, lakini uendelezaji wake sasa unasuasua!

Naomba Wizara iiangalie Kagoma, itafutieni umeme kutokana na vyanzo vyovyote ili umeme uwake pale.

Nashauri Serikali itume wataalam wake waone uwezekano wa kuharakisha umeme Kagoma.

Mwenendo wa bei za mafuta ya petroli: Nawapongeza Serikali na Wakala wake EWURA, lakini hali hii itaendelea hadi lini? Kila wiki mbili tunapata bei mpya, japokuwa ni bei halali kwa sababu halali, naishauri Serikali ione uwezekano wa kufidia bei hizi zinazopanda mara kwa mara. Nashawishika kwamba, watu binafsi hata Serikali yenyewe, sasa inakuwa vigumu kupanga matumizi ya mafuta ya petroli maana hutajua bei ya wiki mbili zijazo ni kiasi gani?

Gesi asili itumike kuboresha maisha ya Watanzania mmoja mmoja na kwa pamoja. Haitoshi kusema kwamba, katika kipindi cha 2004 – 2009, matumizi ya gesi asilia ya Songo Songo na Mnazi Bay yameiwezesha Serikali kuokoa zaidi ya Dola za Marekani 1.38 bilioni na milioni 8.07 kwa ajili ya umeme na mitambo ya viwandani.

Gesi hii itumike kuboresha mazingira ya nchi yetu, yawekwe mabomba ya kusambaza gesi hii toka vijijini hadi mijini. Itumike viwandani na majumbani. Itaoko miti mingi, kazi kubwa ya kupika kwa kuni na mkaa itakwisha, vifo vya wazee wanawake wenye macho mekundu vitadhibitiwa na kadhalika. Wananchi mmoja mmoja tufaidike na gesi yetu asilia.

Naishauri Serikali ihakikishe tumefaidika na madini hayo. Pale unapopatikana mgodi, wananchi jirani wafaidike, ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mazingira na kuboreshewa huduma za elimu, afya na barabara kutoka kwa wawekezaji.

Naishauri Serikali isiwanyang'anye wananchi wetu ambao ni wawekezaji/wachimbaji, wadogo maeneo yao, kwa kisingizio cha wawekezaji wakubwa. Hawa wadogo ni wetu, wakipata faida wanachangia uchumi wetu moja kwa moja, wanasomesha watoto, wanajenga nyumba nzuri, wanakuwa na uwezo wa kumudu maisha yao.

Nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa jitihada zao katika kuboresha Wizara yao, wasonge mbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri na kwa kumudu vizuri katika kujibu maswali Bungeni. Aidha, ninawapongeza kwa hotuba nzuri, ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Nachukua fursa hii, kuwapongeza Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO na Wataalam wote, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuelezea matatizo ya umeme katika Wilaya ya Liwale. Umeme wa Liwale unatokana na Generator aina ya Rolls-Royce. Mashine hizi zimetumika zaidi ya miaka saba sasa, hivyo zinahitaji matengenezo ya mara kwa mara. Ingawa tuna wataalam wazuri wa TANESCO Liwale, tatizo kubwa ni kutopatikana kwa vipuri vya mashine hizo na hivyo kusababisha kupatikana kwa umeme usio na uhakika. Majenereta mawili hivi sasa hayafanyi kazi, yanasubiri vipuri kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Ahadi nyingi zimetolewa, lakini hadi sasa vipuri hivyo havijapelekwa Liwale. Naishauri Serikali iharakishe upatikanaji wa vipuri hivyo, vinginevyo Liwale itagubikwa na giza kubwa hivi karibuni. Je, ikitokea hivyo ni kwa manufaa au maslahi ya nani?

Mheshimiwa Spika, Liwale ni Wilaya mojawapo katika Mkoa wa Lindi, wakati Songosongo Gas imeanza kutumika, kama Mbunge niliambiwa Mnazi Bay ndio umeme wa uhakika utakaofikishwa Liwale chini ya ARTUMUS. Kilichojitokeza ni kwamba, hata Mnazi Bay umeme huo ni kitendawili kwa Liwale. Majibu ya maswali yangu juu ya Mnazi Bay, yalitoa ahadi mbalimbali kwamba, umeme huo utafika. Nilipouliza mbona nguzo za umeme hazijasimamishwa kati ya Nachingwea na Liwale (kilomita 136), nilijibiwa hiyo ni kazi ndogo na kwamba, kwa utalaam wa kisasa, kusimamishwa nguzo ni kazi ndogo.

Cha kushangaza, kwa swali aina hiyo hiyo lihusulo umeme wa Mnazi Bay kutumika Liwale, wakati wa Bunge lililopita, nikapewa gharama za kupeleka umeme Liwale ni 6.5 bilioni na kwamba, Serikali haijapata fedha. Je ni jukumu la nani kutafuta fedha hizo kama sio Serikali? Je, Serikali inajua kwamba Liwale iko Mkoa wa Lindi? Je, inafahamu kwamba umeme wa Mnazi Bay na Songosongo utawezesha kupatikana kwa umeme Wilaya zote za Mikoa ya Mtwara na Lindi isipokuwa ya Liwale? Hivi Liwale imekosa nini hata tukose umeme wa uhakika wa Gas ya Mnazi Bay au Songosongo?

Mheshimiwa Spika, inashangaza Liwale ina rasilimali nyingi ikiwemo wanyamapori ambao wanawindwa kitalii, misitu na madini. Je, umuhimu gani unaohitajika ili kupeleka umeme Liwale? Je, kama suala ni gharama kubwa wapi utapatikana umeme wa bure au usiokuwa na gharama nchini au hapa duniani? Hivi ni kweli kwamba, kutoa umeme Mnazi Bay, Mtwara kwenda Liwale, kilomita 250 au kutoa umeme Songosongo kwenda Liwale kilomita 231 ni mbali zaidi kuliko kutoa umeme Mnazi Bay kwenda Dar es Salaam zaidi ya kilomita 500 au kutoa umeme Songosongo hadi Dar es Salaam kilomita zaidi ya 300. Naiomba Serikali na ninaamini awamu hii ya nne, itafanya kila njia bila kujali gharama bali kwa kujali wananchi wake wa Liwale itapeleka umeme. Aidha, kutoka Mnazi Bay au Songosongo.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe majibu kwa yote niliyoyaeleza kuhusu umeme wa Liwale, kuanzia vipuri vya majenereta na umeme wa uhakika wa Mnazi Bay au Songosongo.

Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya yangu, Jimbo la Uchaguzi Siha, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba nzuri, yenye uchambuzi wa kina, iliyotolewa Bungeni wiki iliyopita, siku ya Jumamosi, 25 Julai, 2009. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa ushirikiano wa hali ya juu, anaoutoa kwa Waziri na hivyo kuleta ufanisi wa hali ya juu katika Wizara. Uchambuzi uliofanywa katika Hotuba ya Waziri ni wa hali ya juu na ninaunga mkono hoja hii.

Nakumbushia Miradi ya Umeme Wilayani Siha, Kilimanjaro.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, vijiji hivyo viwili; Mninga na Kihenga, viko pamoja na vina idadi kubwa ya watu na pia kule Kihenga kuna kiwanda cha kuzalisha nguzo kinachoitwa Mufindi Timber Polls Factory; mwenye kiwanda hiki amevuta umeme wa Grid ya Taifa kilaini, Kijiji cha Kihenge hakina umeme.

Mheshimiwa Spika, pia katika Hotuba Kijiji cha Mninga, umeme umepita pale takriban mita 15. Wananchi waliharibiwa mazao yao, lakini hawajateremshiwa umeme huo muda wote huu.

Ikizingatiwa kuwa, miaka miwili iliyopita TANESCO walifanya makisio ya vifaa kama transfoma, nyaya na nguzo. Gharama yake ilikuwa haifiki shilingi milioni 150.

Mheshimiwa Spika, jambo hili nimelihangaikia miaka mingi sana. Nimeahidiwa na viongozi wengi sana, akianza Mheshimiwa Dkt. Kigoda, Mheshimiwa Msabaha na sasa Mheshimiwa Ngeleja, lakini wote hawa ni ahadi zisizotekelezeka. Pia Viongozi wa TANESCO nao wamekuwa na ahadi kama wanasiasa, kwa kuwa asubuhi ya leo nimeongea na Mkurugenzi mmoja na ameniahidi kushughulikia jambo hili, sioni sababu ya kumtaja. Hivyo basi, nitaunga mkono hoja hii pale tu nitakapoelezwa kuwa umeme huu utateremshwa katika vijiji viwili.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza yeye Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wasaidizi wake wote, ndani ya Wizara na Mashirika yanayotoa huduma chini ya Wizara, kwa huduma nzuri. Mnafanya kazi nzuri na

nawapongeza sana. Nawapongeza pia kwa hotuba nzuri, yenye mwelekeo na inayozingatia Sera za CCM, zikiwemo Ilani ya uchaguzi, MKUKUTA, pia Malengo ya Milenia na kadhalika

Katika mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2008/09, baadhi ya mliyoyapitia ni kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini. Nawapongeza kwa kulitambua hili. Bali bado kuna matatizo ya migongano baina ya wachimbaji wadogo na Makampuni makubwa na pia baadhi ya wachimbaji wadogo kuvamia maeneo nje ya utaratibu. Naishauri Wizara, siku zijazo isimamie vizuri migogoro hii ili Sekta ya Madini ilete mafanikio tunayotarajia.

Katika bajeti iliyopita, Wizara ilitupa matumaini ya umeme vijijini, lakini utekelezaji umeishia matumizi pungufu ya asilimia 43.85. Matokeo yake, baadhi ya maeneo yalikosa utekelezaji. Kwa mfano, kule Kisarawe, ule mradi wa shilingi milioni 2,000, ambao ulipangiwa shilingi milioni 500 wala haukuanza.

Mheshimiwa Spika, wakati unajibu naomba niambiwe kwa Mradi huu nini kilifanywa mwaka 2008/09 na nini kimepangwa katika bajeti hii ambacho mimi nimeshindwa kukiona?

Kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi jirani katika kutaka kukidhi upungufu wa umeme nchini na kuimarisha uhusiano na nchi jirani hasa Umoja wa Afrika Mashariki na SADCC, kwa kuunganisha umeme tokea Zambia – Tanzania – Kenya na pia kuunganisha umeme wa Uganda uhudumie maeneo ya Ziwa Magharibi. Tanzania ina hazina kubwa ya nishati ya maji, jua, upepo, gesi, makaa ya mawe na hata *biofuels*. Kwa hiyo, natahadharisha kuwa mipango ya Wizara isitupeleke mahala ambapo miaka ijayo tutashindwa kuitumia hazina yetu ya nishati, kwa sababu tumezamia kwenye nishati toka nchi jirani.

Ugizaji mafuta kwa pamoja; mwaka uliopita, Bunge hili lilipitisha wazo la Serikali kuwa, mafuta hayo yaagizwe kwa pamoja kupitia TPDC na ikiwezekana washiriki wachache.

Sasa tunasikia kuwa, wafanyabiashara binafsi wameanza harakati za kupanga TPDC kuifanya kazi hii. Kwa bahati mbaya, tunasikia kuwa hata baadhi yetu Wabunge tumeanza kurubuniwa na tunawaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kuwa Wizara imeajiri mshauri wa kuliangalia hili. Hawa wafanyabiashara wanaziponda hata takwimu za TPDC na EWURA. Tafadhali, serikali iendelee kuwa na msimamo wake. Kama yatakuwepo mabadiliko, yatokane na ushauri wa huyo mtaalam.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FATMA ABDULHABIB FERREJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya njema na kuweza kuendelea na shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme katika maisha yetu ya sasa ni huduma ya lazima, ambayo inapaswa kila mwananchi iweze kumfikia ili aweze kuitumia na kunufaika na kuwepo kwake.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona kwamba, hata katika maeneo ambayo Serikali imejitahidi kufikisha umeme, bado ni wananchi wachache wanaofaidika na umeme

huo. Hii inatokana na gharama kubwa za kuunga umeme huo, ukilinganisha na hali halisi ya umaskini wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iandae Mkakati Maalum wa kuweza kupunguza gharama hizo za kuunganisha umeme au kufikiria kutoa ruzuku ili umeme uwafikie hawa wananchi tunaowalenga ili waweze kuwachangia katika maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, suala la uchanganywaji wa petroli na mafuta ya taa linalofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wenye tamaa ya kutajirika haraka, linatusumbua sana.

Mheshimiwa Spika, kasoro hii inasababisha uharibifu mkubwa kwa magari ya wananchi na kuwazidishia umaskini wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za haraka kulikomesha hili, badala ya kuiachia EWURA pekee ambayo inaonekana kushindwa na jukumu hilo. Inawezekana kwa kutegemea asilimia moja kutoka kwa makampuni hayo inayoyasimamia.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali iwawezeshe EWURA kutekeleza majukumu yake na iachane na mtindo wa kuwategemea wale wanaowasimamia.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko makubwa kutoka kwa Wananchi wa Kijiji cha Mgusu, kilichopo Kata ya Mtakuja, iliyoko kwenye Wilaya ya Geita, Mkoa wa Mwanza. Malalamiko hayo yanahusiana na wananchi, kijiji hicho kufungiwa mlima ambao walikuwa wanautumia katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, je, kwa nini mlima huo ulifungwa na badala yake unataka kupewa SHANTA? Je, wanakijiji hao wanachofanyiwa ni haki ndani ya nchi yao wenyewe?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpogeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, kwa Hotuba nzuri ya Bajeti. Pia nampongeza Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kusaidiana vizuri na Waziri wake, kuiongoza Wizara na kwa kazi nzuri. Nawapongeza Wataalam wote, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara wote, wakiongozwa na Katibu Mkuu wao.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inayoshugulika na masuala ya madini, mafuta ya petroli na umeme.

Mheshimiwa Spika, tunao utajiri mkubwa wa madini katika nchi yetu; ni rasilimali ya asili na ni bahati kubwa. Nchi yetu inashangaza kuwa maskini ndani/katikati ya utajiri mkubwa wa dhahabu, tanzanite, almasi na sasa uranium. Siyo tu tunashindwa kunufaika na rasilimali zetu hizi kushindwa ku-*export*, bali pia tunazipoteza na kuwaachia wageni wakijinufaisha kupita kiasi. Ni aibu kuona kwamba, baada ya miaka kumi ya uchimbaji mkubwa wa dhahabu, hatuwezi kuonesha barabara kilometa ngapi zimejengwa kwa fedha za dhahabu. Tuiondoe aibu hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahusika katika utafutaji wa mafuta ya petroli, kuchimbwa, uagizaji na udhibiti wa bei na thamani (*quality*). Ni dhahiri mpaka sasa upatikanaji wa mafuta yaliyoagizwa, yanaathiri bei/gharama za uendeshaji katika nyanja mbalimbali katika uzalishaji na utoaji huduma hasa za umma. EWURA itusaidie katika

kuleta nidhamu ya bei ya mafuta nchini, kwani kila bei ya mafuta ya diesel/petrol inapoongezeka, inaleta mtikisiko katika bei za bidhaa nyingine zote kutokana na kupanda gharama za uchukuzi (*transportation costs*).

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ni msingi mkubwa katika maendeleo ya kisasa. Hvyo basi, upatikanaji wa nishati ya kuaminika na nafuu kwa watumiaji ni mojawapo ya Malengo Makuu ya MKUKUTA. Umeme wa uhakika na wa kuaminika utawezesha uzalishaji viwandani, utasaidia kuboresha kilimo na utasaidia kutolewa vizuri huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, *value addition* ya mazao ya kilimo na hivyo *realization* ya Kilimo Kwanza; *value addition* ya madini tuseme chuma, kinatupatia mitambo ya mashine mbalimbali na huduma za upasuaji hospitalini, kwenye maabara na kadhalika na kwenye shule zote; msingi hadi vyuo vikuu ni kazi ya umeme. Hivyo, umeme ni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na umeme wa kuaminika, lazima kuwe na miundombinu ya uhakika. Hapa nchini, Watanzania wanaopata umeme ni asilimia kumi tu ya *population* ya watu 39.4 milioni. Sababu kubwa ya uchache huu ni kutegemea chanzo kikuu, ambacho ni maji (*Hydropower Generation*), 62.8% ya uzalishaji; (*Frost & Sullivan- the global growth consulting company*).

Mheshimiwa Spika, lazima kufikiria vyanzo vingine vya kuzalisha umeme kama inavyofanyika kwa Songas.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, aniambie kwa nini katika mipango yote hakuna linalozungumziwa juu ya *nuclear energy* ili kuzalisha umeme kama inavyofanyika kwingine? Japan wanazalisha umeme 80% kutoka au kutumia *nuclear power*. Tunayo uranium sasa; kazi yake ni nini kama siyo kutusaidia umeme?

Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu tunayo *substation* kubwa ya umeme wa Gridi ya Taifa, yenye ukubwa wa MW 35, inapeleka umeme Mbulu, Karatu, Kondoa na Kiteto; lakini Jimboni kwangu na Wilaya ya Babati kwa ujumla, tunatumia MW 5 tu.

Kwa nini umeme upo lakini usisambazwe? Pamoja na kwamba, nashukuru kupatiwa umeme Dareda Nashanet, Galapo, Magugu na kadhalika, bado hatujapata umeme sehemu nyingi zenye mahitaji makubwa. Serikali ilitenga Sh. 10 bilioni mwaka 2009/09, kwa ajili ya *Rural Electrification*. Babati hatupo. Mwaka 2009/10, zimetengwa Sh. 811.384 bilioni kwa ajili ya *Rural Electrification* na REA (Wakala), bado sioni katika kitabu chote hiki cha bajeti hata kijiji au mradi wowote kutoka Jimboni Babati Vijijini; kwa nini?

Sasa naomba umeme Riroda, Mamire, Magara, Njiapanda – Madunga, Utwari, Ufana, Loxmanda, Mandi, Gidas na Qash.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini niambiwe kwa nini Babati Vijijini hakuna hata kijiji kimoja kwenye REA Programme?

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa juhudi wanazozifanya kuendeleza Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la STAMICO lilianzishwa kwa madhumuni ya uchenguaji, utafutaji, uchimbaji madini na kadhalika. Shirika lilipowekwa kwenye orodha ya kubinafsishwa au kuuzwa, shughuli zote za maendeleo zilisimama. Miundombinu kama vile nyumba zilizohamishwa umiliki na kupewa TBA, kwa kuwa Shirika hili halibinafsishwi tena, STAMICO warudishiwe mali zao ili waweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi. STAMICO wamepewa jukumu la kutoa huduma za kiufundi kwa wachimbaji wadogo wadogo. Je, wamewezeshwa kiasi gain au ni maneno ya kulifurahisha Bunge lako Tukufu?

Mheshimiwa Spika, wananchi wangependa kujua uharibifu mkubwa wa mazingira uliofanywa na wawekezaji wa Buhemba Gold Mine; mashimo makubwa ya kutisha yaliyoachwa yatafukiwa na nani? Kwa nini Serikali imeshindwa kuwadhibiti wawekezaji wasiotaka kufuata Mkataba (EIA)?

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri Ripoti ya Tume iliyoundwa kuchunguza madhara yaliyowapata Wananchi wa Wilaya ya Tarime, yaliyotokana na kemikali inayotoka katika machimbo ya Barricks Gold Mine; naiomba Serikali iwapime afya zao wananchi wote wanaotumia maji yaliyo jirani na Mgodu, kujua athari zitakazowapata wananchi hao kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haijanufaika na madini tuliyonayo; Serikali inajua na wananchi wanajua. Wizara kuunda chombo mahususi cha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini mwaka 2010/11 ni kuchelewesha mapato kwa Serikali. Hiki ni chombo muhimu na ningetarajia kwa kuzingatia umuhimu wake, kingeundwa mwaka huu wa fedha. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ikaweka mikakati ya muda mfupi na mrefu, kukabiliana na tatizo la umeme ukame unapotokea. Mipango ya dharura imeingiza nchi yetu katika migogoro mikubwa na katika hasara isiyotarajiwa. Mfano, ukodishaji wa mitambo ya DOWANS, IPTL na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei za mafuta ya petrol kwa mikoani sio mzuri, kwani matajiri wenye vituo vya mafuta wanauza mafuta ya petroli wanavyopenda wao. Hii inatokana na EWURA kuwa na Ofisi Dar es Salaam tu. Ni lini EWURA watakuwa na ofisi mikoani ili kudhibiti upandaji holela wa bei ya bidhaa hiyo muhimu? EWURA wako wapi kudhibiti uchanganyaji wa mafuta ya taa na dizeli? Wamedhibiti kiasi gani mafuta ya dizeli yasiyolipiwa kodi kwa nia ya kusafirishwa nje ya nchi na wafanyabiashara wasio waaminifu huuza bidhaa hiyo nchini?

Mheshimiwa Spika, umeme ni nishati muhimu kwa matumizi katika shule zetu za Sekondari na pia vituo vya afya, lakini wananchi wanashindwa kutokana na bei kubwa ya kuweka umeme kwa Shule za Kata na Vituo vya Afya vya Kata.

Serikali ifikirie namna ya kupunguza bei ya umeme kwa Shule zetu za Kata na Vituo vya Afya vya kata pia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kuunga mkono hoja yake, naomba kuwasilisha mchango wangu, kwa niaba ya Wananchi wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nyingi na nzuri wanazozifanya katika Wizara ya Nishati na Madini. Pia, nampongeza Katibu Mkuu, kwa kuwapa ushirikiano na msaada ufaao, Viongozi wake hawa. Kazi za Wizara ni nyingi na ngumu, lakini wanazimudu. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba niishukuru Wizara, kupitia Wakala wa Umeme Vijijini, kwa kupitisha mradi wa kupeleka umeme kwenye vijiji vya Katunguru, Mwakata na Mpera, Wilayani Kahama.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba kuunga mkono hoja hii. Naomba Wizara katika utekelezaji wa bajeti yao, izingatie yafuatayo:-

1. Vijiji vya Lunguya, Ikinda, Shilela na Segese vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Umeme wa Ilogi – Bukombe. Mradi huu ulishapitishwa siku nyingi na pia tumeshawatangazia wananchi kuwa, utanza kutekelezwa mwezi Januari, 2010. Naomba sana, utekelezaji wa Mradi huu na hasa kuwasha umeme katika vijiji hivyo, ufanyike kama ilivyopangwa na kama tulivyokwisha kuwatangazia na kuwaahidi wananchi. Kwa kuwa tarehe hii ni ya makadirio, naomba kujua lini hasa utekelezaji wa Mradi huu utanza; ni hiyo Januari, 2010 au kuna mabadiliko na utaisha lini?

2. Vijiji vya Mpera, Mwakata na Ntunguru vitapatiwa umeme kupitia REA. Taarifa tulizonazo toka REA ni kuwa, Mradi huu ulipangwa kutekelezwa mwaka 2008/09, muda ambao umeshapita! Baada ya mawasiliano na REA na TANESCO, tuliambiwa na mimi kuwatangazia wananchi kuwa, Mradi ungeanza Juni, 2009. Napenda kujua kwa nini Mradi umechelewa kuanza wakati REA wanazo fedha? Naomba sana uishe mapema iwezekanavyo.

3. Maeneo ya wachimbaji wadogo – Mwazimba: kama inavyojulikana, toka 1996, Wananchi wa Kahama, waliokuwa wakifanya kazi za uchimbaji mdogo eneo la Bulyanhulu, walibaki bila eneo. Jitihada kubwa zimefanyika za kuwashawishi wajiunge katika ushirika ili Wizara iwapatie maeneo. Wananchi waliitikia na kuunda Kikundi cha KAGOMICO. Mapema mwezi Februari, 2009, kikundi hicho kiliomba eneo Mwanzimba na Wizara kuwapa leseni katika eneo hilo, hata hivyo, bado hawajaoneshwa rasmi eneo lao na mikapa yake. Naomba yafuatayo yafanyike kuhusu jambo hili:-

(a) Mheshimiwa Waziri kama alivyoahidi, aje Mwanzimba, atembelee eneo husika na aonane na wachimbaji wadogo na kuwaonesha mipaka ya eneo lao kama walivyoomba.

(b) Kuna mchezo mchafu hapo Wizarani wa kubadilisha *coordinates* ili kuwawezesha waombaji waliochelewa kupeleka maombi wapate sehemu na kuaacha waliowahi kuomba. Naomba sana. Kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Waziri hapo Wizarani, inaharibiwa na watu hao wasioelewa ugumu ambao CCM inaupata kutokana na tatizo la wachimbaji wadogo kutopatiwa maeneo. Naomba achunguze na kuchukua hatua.

(c) Wachimbaji Wadogo wa Msalala walioko Kakola ni zaidi ya 40,000. Naomba sana Wizara iharakishe mikakati yake ya kuwatafutia maeneo ya kufanyia kazi. Kujadiliana na wenye leseni ili waachie kwa hiari; ni njia mojawapo, lakini njia ya uhakika ni kubadili Sheria ya Madini kama Kamati ya Bomani ilivyopendekeza.

(d) Naomba wachimbaji wadogo waliopata eneo la Mwazimba, kwa kuwa ndilo eneo pekee rasmi la wachimbaji wadogo wa dhahabu Kahama, wasaidiwe vifaa na elimu ya uchimbaji wa kisasa kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya CCM 2005.



4. Malalamiko ya wananchi waishio jirani na migodi kutonufaika na madini, bado yapo sana. Naomba sana, mapendekezo ya Kamati ya Bomani kuhusu jambo hili yatekelezwe. Mapendekeo yafuatayo ni ya muhimu kuhusu jambo hili:-

(a) Mrabaha usiende asilimia mia moja Hazina. Kiwepo kiasi cha kubaki kwenye mamlaka za maeneo husika.

(b) Wanaohodhi maeneo makubwa bila kuyafanyia kazi kwa *speculative motive*, wadhhibitiwe kwa kuweka, pamoja na mambo mengine, *a minimum expenditure requirement per license*.

(c) Ili Waziri awe na mamlaka na uwezo wa kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo kadiri atakavyoona inafaa, Sheria ya Madini ibadilishwe, hususan kifungu kinachosema mwombaji wa kwanza lazima apewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba nisisitize kuwa, Kamisheni ya Madini ina Maafisa Madini ambao ni *corrupt*. Kama Kamishna na Waziri hawajui, naomba mljue hilo. Mfano, Mwazimba ni *clear evidence* ya hisia hizi. Naomba sana wapendwa ndugu zangu; Kamishna Kafumu na Mheshimiwa Waziri Ngeleja, lijueni hilo.

Baada ya kuwasilisha malalamiko na kero za wananchi wangu, ambazo wanapenda Wizara izifanyie kazi haraka baada ya bajeti kupitishwa, naunga mkono hoja. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwisho wa wachangiaji kwa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na mtakubaliana nami umeisha kwa kishindo kwa sababu Mheshimiwa John M. Cheyo amechomekea suala ambalo tunalielewa vizuri sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge, orodha ilikuwa bado ndefu tu lakini hatuwezi kuendelea zaidi kwa sababu ndiyo hali yenyewe.

Nimesimama ili nitimize lile nililosema asubuhi nalo ni kuwatambulisha wageni wa Wizara hii ambao ni kama ifuatavyo kwa Watendaji Wakuu, Ndugu Arthur Mwakapugi Katibu Mkuu, Ndugu Inovatus Swai, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ndugu Dr. Dalali Kafumu, Kamishna wa Madini, Ndugu Bashir Mrindoko, Kamishna wa Nishati na Maendeleo ya Petrol, Ndugu Said Msambachi, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Ndugu M. B. Machari, Mhasibu Mkuu, Ndugu Salome Makange, Mwanasheria wa Wizara, Ndugu Khamis Komba, Naibu Kamishna wa Madini na Ndugu Subira Wandiba, Mwanasheria wa *TANESCO*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika yaliyo chini ya Wizara ambao ni Ndugu Ramadhan Khatib, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Taifa la Madini yaani *STAMICO*, Ndugu Gen. Robert Mboma, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petrol, Bi. Ritta Akena, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini yaani *REA*. Karibuni sana na sana, ahsanteni. *(Makofi)*

Pia kuna Watendaji Wakuu wa Taasisi za Wizara kama ifuatavyo; Prof. A. H. Mruma, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Jiolojia yaani *GST*, Dr. L. Mwakahesya, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Umeme Vijijini yaani *REA*, Dr. Idris Rashid, Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO*, Ndugu Grey Mwakalukwa, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Madini na

Ndugu Yona Kilagane, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petrol. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katika majukwaa mengine, tunao Watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania yaani *TANESCO*, Shirika la Maendeleo ya Petrol (*TPDC*), Shirika la Madini la Taifa *STAMICO*, Wakala wa Jiolojia Tanzania *GST*, Kitengo cha Ukaguzi wa Dhahabu (*GAP*) na Wakala wa Nishati ya Umeme Vijiji yaani *REA*. Karibuni sana na ninashukuru sana Watendaji wote kuwepo hapa na kufuatilia mjadala huu wa Bunge. *(Makofi)*

Sasa kwa kuhitimisha hoja, atatangulia Naibu Waziri, Mheshimiwa Adamu K. Malima kwa dakika zisizozidi kumi na tano na baada ya hapo, Mtoa hoja kwa dakika zisizozidi thelathini.

Mheshimiwa Naibu Waziri karibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yote, kwa hakika sina sababu ya kukasirikia fadhila zote anazonitendea ikiwa ni pamoja na hii ya kusimamia mbele yenu kwa unyenyekevu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa dhamana hii kubwa aliyonipa na ninaomba pia nimshukuru Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, kwa uongozi wake mahiri ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru, Marehemu Mzee wangu, Kighoma Ali Malima, Mwenyezi Mungu amrehemu na Marehemu Mke wangu, Zinduna Ismail Mpenda, wazazi wangu na wazee wangu na wanangu Amina, Mariam, Ally, Abdallah, Adam, Abdul, Ranyam, Adam, Asina, Ayubu, Hawa na Khanifa na naomba pia niwashukuru ndugu zangu wote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru pia wapiga kura wangu na wananchi wote wa Mkuranga, Viongozi wote wa CCM, DC, Mkurugenzi wa Wilaya na mwisho siyo kwa umuhimu lakini naomba nimshukuru Mke wangu, Naima Mama Mbonde, Barafu wa Moyo wangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Na wakati huu unaihitaji sana barafu! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Sana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema na Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano na kazi nzuri anayoifanya na uongozi wake ndani ya Wizara yetu. Ninaomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kila mnalotuambia, mnatusaidia kuwa na ufanisi na utekelezaji wenye ubora zaidi wa majukumu ambayo tumepewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tumegawana baadhi ya mambo lakini naomba niyaseme machache na Mheshimiwa Waziri ataendelea na mengine ikiwa ni pamoja na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge. Lakini kwa wale waliochangia masuala ya madini, naomba nijibu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Somangafungu, hiki ni kituo cha umeme kipo Kilwa. Kimezungumzwa na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa na linamgusa pia Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Somangafungu, ni mradi ambao tangu mwanzo ulianza kwa matatizo kwa sababu ulipochorwa mara ya kwanza, Wakandarasi walipokwenda pale wakakuta hawawezi kuanza kuutekeleza mpaka wajaze udongo kwa sababu ulikuwa kama uko kwenye bonde kidogo. Sasa hiyo kazi ikachelewesha mradi mzima kwa zaidi ya miezi tisa. Lakini baada ya hapo tukawa na Mkandarasi mmoja ambaye kusema kweli aliuchelewesha ule mradi na wengine wote wakachelewa kuutekeleza baadaye, matokeo yake ni kwamba zile ahadi zote za utekelezaji zikawa zimechelewa kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa hivi tuna mambo mawili yaliyobaki, moja ni kwamba katika makampuni yote haya ile kampuni ya *Generation RENCO* na kampuni ya kusambaza nyaya kwenda Rufiji, *ELTEL* na kwenda Kilwa tumekubaliana kwamba yale mambo madogo madogo ambayo walikuwa wanasema hawawezi kuanza kufanya kazi mpaka walipwe, mengine yameshakulibaliwa na Benki ya Dunia kwamba watayalipa lakini kwa yale ambayo Benki ya Dunia hawatayatekeleza, tumekubaliana kwamba ili mradi usichelewe Serikali yenyewe ibebe dhamana hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwataarifu Wabunge husika na Watanzania wote wa maeneo hayo, kwa kusema kwamba, tumekubaliana ifikapo katikati ya mwezi wa tisa tuwe tumeshakutana na Wakandarasi wote na tuwe tumejiwekea *deadline* na haya masuala ya kusema nani analipwa nini yawe yamekwisha, watu warudi haraka kwenye maeneo ya kazi ili kazi hizo zianze na ikiwezekana hili suala la umeme wa Kilwa na umeme wa Rufiji uwe umekwisha ifikapo mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, tatizo dogo tulilokuwa nalo la kuvusha umeme kwenye daraja la Mkapu, mwanzoni Wataalamu wengine walikuwa wanasema labda umeme ukipita pale, daraja litaungua na kadhalika lakini tumempata mshauri na mshauri huyo anasema inawezekana kuweka nyaya pale juu kwa hiyo nalo hilo limeondoka, tunatarajia tutafanya kazi na wenzetu wa Miundombinu na tatizo hilo litakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa hapo hapo, naomba pia nizungumzie suala la mrahaba wa gesi. Suala la mrahaba kwa ujumla wake, linafanyiwa kazi ili kuangalia haki za wananchi na za jamii zilizo kwenye rasilimali husika. Kwa hiyo, ninaomba niseme tu kwamba, ni suala ambalo linafanyiwa kazi kwa pamoja na tunatarajia tuwe tumelipitia upya kwenye Sheria mpya ya Madini lakini pia kwenye Sheria mpya ya Gesi asilia na mafuta ambayo tunarajia kuleta hapa Bungeni mwezi wa kumi na moja, tukirudi, *Inshallah!*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la chumvi, limezungumzwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani. Lakini na mimi linanigusa kwa sababu ya wachimbaji wangu wa kule wa Kisiju na Shungubweni na Mafia pia nadhani wapo. Tumekubaliana na Kamishna wa Madini kwamba msisitizo uliokuwa unawekwa na Idara ya Madini kwenye masuala ya uchimbaji wa chumvi ulikuwa hautoshelezi kwa hiyo lazima tuweke mkazo zaidi kwa kutuma Wataalamu. Lakini pia tunataka tuangalie kwa sababu kama hii chumvi ambayo inasemekana ni chumvi nzuri tufanye nini ili chumvi hii ipate kuweza kuongezeka ubora zaidi kwa kuongezea utaalumu pia na kuwapatia mitaji hasa ikizingatiwa kwamba katika maeneo mengi wachimbaji wa chumvi ni akina mama na mara nyingi wanakuwa kwenye makundi ya ushirika kwa hiyo pia inaendana na Sera na Ilani za Chama cha Mapinduzi. Lakini pia hili jambo la kodi ya Madini

Joto, tunataka tuzungumze na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tuone tunafanyaje kwa sababu tukiliondoa tunaongeza ubora wa chumvi lakini pia tunaongeza na ushindani wa chumvi yetu na chumvi nyingine zinazotoka nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie masuala ya madini yafuatayo, kwanza naomba niseme tu kwamba kusema kweli mengine katika sekta hii yatajibiwa na Mheshimiwa Waziri. Lakini naomba niseme Serikali ya CCM ni Serikali sikivu na ni Serikali rahimu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye masuala matatu ambayo nimemwakilisha Mheshimiwa Waziri. Moja ni hili la Mgodu wa Buzwagi ambalo limeletwa na Mheshimiwa James Daudi Lembeli. Tulipokwenda Buzwagi, tulikuta kuna tatizo ambalo kimsingi lilikuwa limetengenezwa na watu ambao roho zao zilikuwa dhaifu kwa sababu mfumo wa kuwalipa wananchi ulikuwepo. Lakini tulipofuatilia, tulikuta pande nyingi kila mtu alikuwa ametia ujanja wa namna fulani kuliharibu zoezi lile. Kwa hiyo, tulichokubaliana pale ni kwamba lazima ule mfumo wa kuangalia fidia iliyolipwa kwa wananchi upitiwe upya lakini pia mfumo huo uwe shirikishi kwa namna ambayo wananchi wanakuwa na wawakilishi wao, mwekezaji anakuwa na mwakilishi wake, Halmashauri inakuwa na mwakilishi wake na Afisa Ardhi anakuwa na mwakilishi wake.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mambo madogo madogo ambayo yalikuwa yanavunja imani ya wananchi wa maeneo ya Mwendakulima na jirani zao, tukasema haya mambo ni lazima yaangaliwe upya. Huwezi kwenda kumsainisha mtu, ukasema mali zako ni hizi kwa penseli halafu unaporudi baada ya miezi mitatu unakuta karatasi ile ile imeandikwa na peni. Sasa haya ni mambo madogo madogo ambayo tumesema yanavunja imani lakini kwa kuwa wahusika walikuwa ni watu wa pande zote mbili, tumesema tupitie upya na tumeanza tangu huko ambako kulikuwa na malalamiko mpaka sasa hivi wananchi wanne hawajalipwa fidia wakiongozwa na Bwana Feros tunafahamiana vizuri, lakini tumekubaliana kwamba hili zoezi ni endelevu, Mbunge anahusika, Wizara inahusika na mimi mwenyewe tumekubaliana kwamba ninaendelea kulifuatilia na baada ya Bunge hili, tutarudi tena Buzwagi kuangalia utekelezaji wa jambo hili umefikia wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la *GGM*, kuna eneo linaloitwa Mainimpya, Mainimpya walihama pale halafu wakaenda kukaa katikati ya Geita lakini wanakaa kwenye mahema. Kwa kweli wanakaa kwenye mazingira ya hovyoya sana. Sasa tumesema kuna kesi inaendelea Mahakamani lakini masuala ya kibinadamu *not withstanding*, inabidi tupate ufumbuzi wa suala la Mainimpya. Tulipokwenda pale, tulizungumza na *DC* tukamwambia atutafutie maeneo ili tuanze ku-*mobilize funds* tuone kama tunaweza tukapata *low cost housing* ili tuwahamisha kutoka pale kwenye mahema na tuwapeleke kwenye mfumo wa maisha ambayo yana heshima zaidi kuliko yale waliyokaa nayo pale. Mpaka sasa hivi, Mheshimiwa *DC* ametuandikia, ameshapata viwanja 56 na sisi tunafanya utaratibu wa kushirikiana na wenzetu wetu yaani Halmashauri, *GGM* na Wizara kuangalia namna ambavyo tuta-*raise* hizo pesa zinazotakiwa kwa ajili ya kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Mererani na suala la mionzi. Juzi mimi nilikwenda pamoja na Kamati ya Madini, tulipata maelezo ya *Tanzania Atomic Energy Commission* kuhusu ufanisi wa zile mashine. Moja ambalo lilikuwa ni dhahiri ambalo tulilionga pale ni kwamba namna ambayo wachimbaji wale wanapitishwa kwenye zile mashine hazilingani na ustaarabu wetu sisi Watanzania. Kwa hiyo, tulikuwa pale na Waheshimiwa Wabunge tumewaambia *this must stop*, ukiniambia mimi huu ni utaratibu ambao uko kwenye nchi nyingine, sisi ustaarabu wetu huwezi kumpitisha mtu mzima pale wa miaka 60, unampitisha na kibukta kwenye mashine, haiwezekani! Kwa hiyo, tumesema hii lazima isimame na wakati

huo huo tumekubaliana kwamba zile mashine na mambo mengine yote pale tunaunda Tume ya kufuatilia mambo yote yanayopita pale ikiwa ni pamoja na kuangalia madhara haya ambayo wachimbaji wadogo wameyapata kama kuathirika katika zile sehemu nyingine na kadhalika. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba ikilazimu ni lazima waende wakafanyiwe *medical checkups* ili tupate ukweli wa kina na hatua stahili zitachukuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la *EWURA*. *EWURA* wamelalamikiwa kwa mambo matatu makubwa. Kwanza, wamelalamikiwa kwa sababu wanaadhibu watu kwenye vituo ambavyo viko Mikoa ya kati yaani Dodoma, Iringa, Singida, Tabora na Mbeya wakati uchekechuaji wote tunajua unafanyika baina ya Kibaha, Mlandizi na Mdaula. Sasa tumekubaliana na *EWURA* lakini lazima niseme pia kwamba hapo hapo wamefanya *random checks* kwenye vituo kama 17, sasa tumekubaliana kwamba *something is wrong* yaani lazima kuna tatizo kwa sababu kama hili zoezi linaendelea na pale ndipo wanapofanya uchekechuaji ni lazima tuchukue hatua za makusudi.

Mheshimiwa Spika, sasa tulichokubaliana wafanye, ni kwamba wanakuja na mitambo mipya ambayo yenyewe itanusa na kubaini uchekechuaji hata kwenye maeneo kabla mtu hajapewa yale mafuta kwenye kituo chake. Kwa namna hiyo, unamwepusha mtu na kumwadhibu kwa kumuonea kwa sababu kusema kweli imebaini kwamba wengine wanapokea mafuta haya lakini madereva wao na wasafirishaji wao kama alivyosema Mheshimiwa Shabiby wanakuwa wametengeneza *line* hapo katikati, kwa hiyo huko ni kumwonea mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumekubaliana kwamba yale Mahekalu yaliyopo pale Kibaha, Mlandizi mpaka Mdaula ni lazima tuyapatie utaratibu wa kuyashughulikia kwa sababu kusema kweli yana malengo gani yale mahekalu ya nyuma makubwa yale? Kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi na tunarajia kwamba Serikali itakuja na majibu na tulishakubaliana na Kamati ya Nishati na Madini kwamba *EWURA* watuletee tathmini yao ya namna ya kurekebisha hali ile.

Mheshimiwa Spika, umeme wa Kigoma. Kama tunavyofahamu, kuna tatizo kubwa la umeme Kigoma Ujiji lakini kwa hivi sasa tulichobaini ni kwamba ule mfumo wa *maintenance* yaani mfumo wa kurekebisha mashine zile kusema kweli haukidhi haja kwa sababu kinachotokea ni kwamba unatoa mashine moja iliyokufa unachukua spea unapeleka kwingine. Sasa mfumo ule unafanyika Kigoma, kwenye mashine za Mpanda, Songea na hata Masasi lakini hautusaidii. Kwa hiyo, tulichosema ni kwamba *TANESCO* lazima walete mashine na *spear* mpya lakini pia kuna matatizo yanayotokea pale *TRA* na Bandarini, huwa wakati mwingine spea zinakuja pale zinakaa mwezi mzima, watu wanapata shida ya umeme kule ninyi mnakaa mnatengeneza taratibu na kama Babu yangu alivyokuwa anasema kusema kweli busara inashinda taratibu. Kwa hiyo, hili jambo tumekubaliana kwamba ni lazima tulifanyie kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa haraka haraka nizungumzie suala la Kasulu na Kibondo. Kasulu, Kibondo na Mpanda kuna mashine zile zilizobaki 12 ambazo tunatarajia tunategea pesa zitoke Wizara ya Fedha. Lakini *in the mean time*, tumekubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo kwamba kuna vyanzo vya maji ambavyo vinaweza kuleta *megawatt* 1 au 1 ½ na hata mbili na ni umeme wa kutosha tu kwa maeneo hayo. Lakini pia kuna suala la umeme ule wa Rusumo wa nchi tatu ambao wenzetu hawahitaji umeme mwingi kama huo. Kwa sasa hivi jambo hilo la Rusumo liko kwa mshauri nadhani ni Mjerumani yule amesema kwamba yeye anataka umeme ule uzalishwe *megawatt* 80 lakini uharibifu wa mazingira utakuwa ni mkubwa zaidi, sisi wenyewe tumesema tuwe na umeme

wa *megawatt 60* ambao utagawanywa miongoni mwetu na sisi wengine tukiuhitaji tutaununua. Kwa hiyo, hilo linaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Masasi, tunapeleka umeme huu kutoka Ndanda - Nyangao, tunatarajia umeme huo utakamilika Novemba kama tulivyosema. Kwa hiyo, suala hili la Masasi kusema kweli litakwisha ifikapo Novemba na tunaamini hivyo kwa sababu tumeshakubaliana kwamba Novemba kiutaalamu jambo hili litakwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Songea, linahuzunisha kidogo, lakini nalo liko kwenye matatizo hayo ya mfumo wa *maintenance*. Lazima nitambue kwamba Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, amekuwa anakuja mara kwa mara ofisini kuhimiza suala hili na niseme tu kwamba liko katika utaratibu wa kubadilisha namna nzima ya kufanya *maintenance* ya mitambo ya *TANESCO*, hii ya kutoa mashine iliyoharibika huku na kufunga kwa gharama kubwa halafu baada ya siku mbili inaharibika. Tumekubaliana kwamba ni lazima tubadili mfumo wa kufanya *maintenance*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, naomba niseme yafuatayo:-

Naomba nizipongeze sana hizi taasisi mbili *GST* na *STAMICO*. Mwaka juzi zilikuwa ni taasisi ambazo zilikuwa zinagalagala kabisa zinaelekea *ICU*. Lakini kwa sasa hivi wamebuni wao wenyewe njia zao za kuzalisha pesa. Kusema kweli, Kamati ya Nishati juzi imekwenda na tumekuta mabadiliko makubwa katika kipindi cha miezi 12.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini, kama tulivyosema kwenye hotuba, kinafanyiwa utaratibu wa kuunganishwa na *UDOM*, kwa hiyo, nacho tunatarajia kwamba tutapata mabadiliko makubwa katika ufanisi, *intake* ya Chuo cha Madini, lakini pia na *quality* ya kozi zinazotolewa pale.

Mheshimiwa Spika, suala la *TPDC Retention* na *Bulk Procurement*, tumekubaliana kwamba Mheshimiwa Waziri atalizingumzia mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba niwaambie ndugu zangu kwamba, katika haya masuala tunayozungumzia, kila tunapotaka kupeleka umeme kuna ukweli wa...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Naibu Waziri ili umalizie vizuri tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuna ukweli wa *generation* (uzalishaji), usafirishaji na usambazaji. Kwa sasa hivi, pamoja na yote tunayotaka kufanya, tunaomba mtuunge mkono katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa umeme kwa sababu kwa hii miradi tuliyonayo ya kutaka kusafirisha umeme ili uende huko, uende Kaliua, uende Urambo, uende Bunda, uende wapi, ni *thousands of kilometers* kwa sababu ya ukubwa wa nchi yetu. Kwa kadri ya uzalishaji huu tulio, tukibaki hapa hapa tulipo, ule umeme kadri unavyozidi kuzalishwa, unazidi kupoteza nguvu. Kwa hiyo, tunakuombeni kwamba kuna miradi hii midogo midogo ambayo inalenga kuongeza nguvu kwenye gridi; mradi wa upepo wa Singida, ni muhimu sana, mradi wa *megawatt 60* wa *distribution* ya Mwanza, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ambayo tunatarajia itaongeza nguvu kwenye gridi upande wa Mbeya kule kuna *Geothermal*, kuna Kiwira, kuna Luhuji, ni miradi muhimu mno

au Kinyerezi ule wa *megawatt* 200 unaweza kuonekana labda ni mdogo, lakini unaongeza nguvu na *stabilization* kwenye gridi kwa kiasi ambacho sisi wote nchi nzima tunaweza tukadokoa kidogo kidogo kwa usambazaji huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nishukuru sana kwamba katika michango yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameleta, tumeona msisitizo huo wa kuongeza nguvu ya uzalishaji na kuongeza uwekezaji kwenye uzalishaji wa umeme ili kuboresha nguvu ya usafirishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia sisi sote kuiona siku ya leo na hatimaye kutufikisha hatua hii ya kuhitimisha mjadala kuhusu makadirio ya fedha ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini, kutoa pole kwa wale ambao wameguswa kutokana na ajali iliyotokea huko Mkoani Tanga ambapo Watanzania wenzetu wamepoteza maisha, kwa taarifa ambazo tumepewa asubuhi. Tunaendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu roho zao azilaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuhitimisha hoja hii ikiwa ni hoja ambayo imechangiwa na wachangiaji 201. Ninaamini, kwa utaratibu wa kawaida, nitakapokuwa nawatambua waliochangia, muda huo hautatumika kwa ajili ya kuhesabu dakika ambazo nimepewa. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwatambua waliochangia kuanzia kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi. Waliochangia kwenye Wizara hiyo katika hoja zilizohusu Wizara ya Nishati na Madini, kwanza alikuwa Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa *Archt.* Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Mhonga. S. Ruhwanya, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi pamoja na Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, waliochangia masuala yaliyohusu Wizara ya Nishati na Madini ni pamoja na Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Said A. Arfi pamoja na Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwenye mjadala huu kuanzia Jumamosi hadi leo, waliochangia kwa kuzungumza ni pamoja na Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Brigedia Generali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa *Arch.* Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Balozzi Dr. Gatrude I. Mongella, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Devolta M. Likokola, Mheshimiwa Joseph J. Mungai, Mheshimiwa *Eng.* Laus Mhina, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa John M. Cheyo pamoja na Mheshimiwa Adam K. Malima, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbod P. Slaa, Mheshimiwa *Eng.* Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Omar Shekha Mussa, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Balozzi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa, Mheshimiwa, Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa *Arch.* Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Fred T. Mpendazoe na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba, Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mheshimiwa *Capt.* John Z. Chiligati, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Dr. Emmanuel J. Nchimbi, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Dr. David M. David, Mheshimiwa Juma H. Killimbah na Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Salim



Hemed Khamis, Mheshimiwa Anna Maulida Komu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Lucas L. Seleli, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Eliatta N. Switi, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Al-Shymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Ussi Amme Pandu na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanry, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Fatuma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa John P. Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambao ametoa kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini zilizotokana na michango mingi iliyotolewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, nimekumbushwa kwamba kuna Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, tulimsahau, ni mmojawapo wa waliochangia kwa kuzungumza, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo amesaidia kuchangia na kwa kutoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema, hoja ni nyingi kweli na kwa utaratibu wa kawaida, nianze kusema kabla sijasahau ni kwamba, tutaendelea kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali kwa maandishi zile ambazo kwa muda huu hatutazifikia ili ziwafikie Waheshimiwa wote waliochangia kwa kuzungumza lakini pia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, pia nakumbushwa kuwa Mheshimiwa Castor Ligallama, ni mmojawapo wa waliochangia, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa nafasi hii ambayo nimeipata, naomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa kwa sababu nimesema muda hautatosha. Kwanza, nitaanza na Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge, kwa taarifa, maoni na ushauri yao ambayo iliwasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini, natumia fursa hii, kuwashukuru sana Wabunge wote kwa ujumla, kwa ushauri, maoni na changamoto

mlizotupa. Sisi tunaamini kwamba, changamoto mlizotupa, ni namna nzuri ya kutufanya sisi tuendelee kujipanga na kuboresha utekelezaji wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wenzangu, nawashukuru sana kwa pongezi ambazo mmetupa sisi na ninawashukuru sana. Kwa kweli, mengi ni ya kujenga, hatujaona hata moja ambalo limeelekezwa kuwa *personal*. Kwa hilo tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya Nishati na Madini, chini ya Mheshimiwa William Shellukindo, imekuwa ni Kamati ambayo imetushauri sisi kwa nafasi ya Wizara lakini ni Kamati ambayo inafanya mambo makubwa sana kwa mchango wa Taifa, imetoa maoni mbalimbali hatimaye ikatushauri kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hayo yaliyosemwa, nianze na suala la *retention* kwa ajili ya Shirika letu la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Kama ambavyo tumekwishasema kwenye kitabu cha hotuba, maamuzi ya msingi yalishafanywa na Serikali Kuu kwamba *retention* ya asilimia hamsini (50%), kwa Shirika letu la Maendeleo ya Petroli (TPDC), ifanyike na tunaamini kwamba, jambo hilo litatekelezeka ndani ya mwaka huu wa fedha. Katika hili, nisingependa kuongea mambo mengi na tunaamni baada ya kufanikisha hilo, yawezekana kukawa na mambo ya kiutaratibu ambayo tunayakamilisha sisi na Wizara ya Fedha na Uchumi lakini kimsingi maamuzi ya msingi yalishafanywa na tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo hatua kubwa itapigwa kwa ajili ya kuwezesha uwekezaji unaofanywa na TPDC ambayo ni mkono wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi ambayo yamesemwa. Mojawapo katika hili ambalo ushauri umetolewa na Kamati yetu lilikuwa ni kuhusu utekelezaji wa mapendekezo hasa ya Tume ya Bomani ambayo kimsingi sisi kama Serikali tumeanza kuyatekeleza. Yapo mambo ambayo yalishauriwa katika taarifa ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, yalianza kutekelezwa kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi na hatua zimeshachukuliwa. Lakini niseme kwamba yapo mambo ambayo utekelezaji wake utategemeana na mabadiliko ya Sheria. Sisi kwa nafasi yetu kama Wizara ya Nishati na Madini, tumeshasema mara kadhaa, tumeshaliarifu Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla kwamba tunakuja na Sera mpya ambayo tayari Serikali imeshairidhia na baadaye tutakuja na Sheria mpya ya Madini ambayo tunaamini itategemea ratiba ya Bunge mwezi wa Kumi au Kumi na Moja, tutawasilisha Muswada wa Sheria mpya ya Madini. Yako mambo mengi ya msingi ambayo utekelezaji wake unategemeana na mabadiliko ya sheria. Tunaamini kwamba kwa kufanya vile, itatusaidia sana kuttoa hapa tulipo na kutusogeza mbele.

Mheshimiwa Spika, kikubwa na miongoni mwa mambo ambayo yalipendekezwa katika Tume ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, ni pamoja na kuboreshwa kwa fidia kwa wananchi ambao wanapisha shughuli za uchimbaji madini, hili tumeliongelea kwa kina na niseme kwamba, kwa sasa litakuwa ni mkombozi kwa ajili ya sheria zilizopo kwa wananchi ambao wanapisha shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, tulishauriwa kuhusu masuala ya *Tanzinite*. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, yako mambo mengi kayafafanua lakini naomba niombe muda kidogo, nitalizungumzia hili la ushauri wa Kamati yetu ya Nishati na Madini pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusu suala la *Tanzanite*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu nimesema yako mambo mengi ambayo sisi tumejipanga kuyatolea ufafanuzi wa kina, naomba sasa nitoe ufafanuzi

kuhusu hoja kadhaa ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Waziri mwenzangu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mnyaa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja, kwa nini Wizara inaomba kiwango cha chini kuliko kile kilichopangwa na Serikali katika bajeti kuu. Kwa nini hii tofauti ya bajeti ya Serikali na Wizara ya shilingi milioni 58.5 isiende kwenye bajeti ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa asilimia 46.4 (46.4%) kwa kulinganisha na ya mwaka jana?

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wake ni kwamba, kwa mwaka wa 2009/2010 kiasi cha fedha kilichotengwa kwa Wizara cha shilingi bilioni 226.9 ni sahihi kwa sababu kulikuwa na hoja kwamba, mwaka jana ni tofauti na mwaka huu lakini pia kitabu cha Wizara ya Fedha na Uchumi kinaonyesha kwamba fedha iliyoombwa ni shilingi bilioni 285.

Mheshimiwa Spika, kiasi alichodai Mheshimiwa mtoa hoja cha shilingi bilioni 285.4, kinajumuisha shilingi bilioni 58.5 kwa ajili ya miradi ya nishati mitatu chini ya programu ya *Millenium Challenge Corporation - MCC* kwa mwaka 2009/2010. Aidha, tofauti ya kiasi cha fedha kinachoombwa na Wizara ya Nishati na Madini na kiasi kilichotengwa, kwa mujibu wa bajeti ya Serikali, ukurasa wa 41 na 42 kama ambavyo Mheshimiwa mtoa hoja alitoka, ya hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kimsingi ni shilingi 54, 528, 715,000 na sio shilingi 58, 773, 953,000 kama ambavyo mtoa hoja alikuwa anaelezea.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba iko miradi mingine ambayo imeonyeshwa kwenye Wizara ya Fedha na Uchumi lakini matumizi yake yako kwenye Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu miradi ya *MCC* kimsingi *contracting party* kwa sehemu ya Tanzania, aliyeingia mkataba ya *MCC* ni Wizara ya Fedha na Uchumi ambayo ndiyo mwakilishi wa Serikali, ndiyo maana kunaonekana fedha kule huku zimepungua lakini kimsingi ukizijumlisha matumizi yake yanakuwa ni yale yale.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba kwa nini matumizi ya kawaida yamezidi kwa asilimia 13.4 (13.4%) ikilinganishwa na mwaka uliopita? Ufafanuzi ni kwamba, matumizi ya kawaida kwa mwaka 2009/2010 yamezidi kwa asilimia 11.8 (11.8%) na siyo asilimia 13.4 (13.4%) kama ilivyoelezwa na mtoa hoja. Aidha, kiasi hicho kimeongezeka kutokana na sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu kama tatu kwa haraka haraka nitazipitia; kwanza ni kutengwa kwa bajeti ya Kitengo cha Ukaguzi wa Migodi, kazi ambayo ilikuwa inafanywa na Alex Stuart kifupi tunaita *GAP*, ya shilingi bilioni tano kwa mwaka 2009/2010 iliyojumishwa katika bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara ya Nishati na Madini tofauti na miaka iliyopita ambapo fedha hizo zilikuwa zinatengwa chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, mwaka huu tumeziweka chini ya Wizara yetu ndiyo maana inaonekana kama kuna ongezeko lakini mwaka jana zilikuwa zimetengwa kwenye wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ni kutengwa kwa kiasi cha shilingi bilioni moja ya Mfuko wa Kuwandleza Wachimbaji Wadogo. Tunakumbuka miaka mitatu tumekuwa tukiongelea dhamira ya Serikali ya kuanzisha Mfuko wa Wachimbaji Wadogo, hatimaye mwaka huu tumetenga fedha. Kwa hivyo, kwa mwaka huu wa fedha, jambo hili la kuanzisha mfuko kwa ajili ya wachimbaji wadogo, sio suala la nadharia tena, ni suala la kweli, ni suala la utekelezaji, ndiyo maana inaonekana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna sababu nyingine kwamba kiasi cha shilingi milioni 546,664,716, ni nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa Wizara waliopandishwa vyeo,

ajira mpya na kuongezeka kwa viwango vya posho na stahili za viongozi. Ukisoma hotuba yetu utaona kwamba mwaka jana kuna wafanyakazi wengi tumeongeza na mwaka huu tunategemea kuongeza wafanyakazi zaidi ya 100, ndiyo maana bajeti yake inaonekana kwamba imeongezeka kwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba katika mwaka huu, Wizara imetenga shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya mishahara na Mashirika yake ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilitengwa shilingi bilioni 3.3. Hivyo ziada ya shilingi bilioni 2.9 ni kwa ajili ya nini? Ufafanuzi ni kwamba, kiasi cha shilingi bilioni 3.3 kilichotengwa katika mwaka 2008/2009 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara tu kama ilivyoonyeshwa katika Ukurasa wa 64 wa hotuba yangu ya mwaka huo. Aidha, katika mwaka huo, shilingi bilioni 2.3 zilitengwa kwa ajili ya mishahara ya Mashirika ya *TPDC* na *REA*, hivyo katika mwaka wa 2008/2009 jumla ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya Wizara na Mashirika yake ni shilingi bilioni 5.6 na siyo shilingi bilioni 3.3 kama ilivyoielezwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie nafasi hii, kumkaribisha Mheshimiwa Mnyaa maana yake tunaongelea habari za namba hapa, yeye ni *Engineer*, wapo wataalam wengine lakini kimsingi tunaweza kumpa ufafanuzi wa kutosha kabisa tukiwa tumekaa pamoja na kumueleza na kwa sababu tumesema kwamba taarifa hizi zitatoka kwa maandishi pengine itarahisisha.

Mheshimiwa Spika, niseme moja lililotolewa kwenye mchango wa Mheshimiwa Mnyaa, ambalo lilikuwa ni la ujumla. Mheshimiwa Mnyaa alihoji baada ya kusema hizo taarifa ambazo zilikuwa zinaonekana kwamba mwaka huu kasma au makadirio ya Wizara ya Fedha yamepungua, alitoa hoja kwamba shilingi bilioni 320 zilizotengwa kwa Wizara hii mwaka uliopita, ni kutokana na miKataba ya kufilisi nchi zaidi kuliko shughuli za maendeleo na akasema Kambi ya Upinzani inahitaji ufafanuzi wa kina katika hili. Najaribu kuelezea ufafanuzi huu, lakini nimwombe Mheshimiwa Mnyaa kama bado, kwa sababu ya muda hataridhika na mambo, nimkaribishe ofisini tumpe ufafanuzi. Lakini kikubwa ni kwamba kwanza, hizo fedha hazikutengwa kwa ajili ya kufilisi nchi, hilo si kweli, hazikuwa kwa ajili ya miKataba ya kuifilisi nchi, bali ni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Tumesema mwaka jana tulivunja mkataba wa *Dowans*, lakini pia mkataba wa *Aggreco* ukaisha mwezi wa kumi na moja mwaka jana. Kwa kuondoa zile, ikatupunguzia gharama fulani na ndio maana ikaonekana kwamba bajeti imepungua. Kimsingi sisi Wizara yetu tungependa ipate fedha nyingi kama ambavyo Wizara zingine zingependa, lakini tunafahamu uwezo wa Serikali, tunafahamu kasma ya Serikali, tunafahamu makusanyo yetu, siku zote tumekuwa tukisema na hatimaye sasa hivi tunafanya vipaumbele na sisi Wizara yetu ni mojawapo ya vipaumbele katika mpangilio wa kiwizara lakini bado tunasema kwamba mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wetu. Kwa hiyo, ni mambo ambayo kwa kweli yanategemea uwezo wa nchi. Lakini niseme tu kwamba kuna hoja zingine kama ambavyo anaendelea kusema Mheshimiwa Mnyaa, tutazitolea ufafanuzi kwenye maandishi.

Mheshimiwa Spika, niseme la jumla moja lingine kuhusu umeme Vijijini au utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuhusu kusambaza umeme kwa kuanzia na hasa vipaumbele ambavyo tumejiwekea kwa Mikoa ambayo haijaunganishwa katika gridi, lakini pia katika Wilaya ambazo hazijaunganishwa wala hazijapata huduma ya umeme. Jambo hili limeongelewa niseme na Wabunge wote kwa sababu linatuhusu sote. Tunaheshimu sana maoni ya Waheshimiwa Wabunge, tunathamini michango yao. Lakini kama ninavyoweza kusema kwamba kwa sababu ya ufinyu wa bajeti zetu, tumekubaliana kwamba tuanze kwa vipaumbele, Mikoa ambayo haijaunganishwa kwenye gridi kwa sababu ya gharama za kuiunganisha ndio maana tumekuwa tukizishirikisha nchi wahisani, nchi washirika wetu wa

maendeleo kutusaidia na iko miradi mikubwa ambayo inatekelezwa. Lakini kwenye Wilaya, tumesema tuongeze kasi kwa kutumia pia mfuko wetu sisi wenyewe, Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo tumejipa kipaumbele, kwa mfano, Wilaya ambazo zilikuwa zimebaki hazijaunganishwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amezieleza. Tumishaagiza mitambo ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, lakini pia mashine za Wilaya ya Kibondo, Kasulu, Ngorongoro pale Loliondo pamoja na Sumbawanga, zimeishaagizwa. Ninapoongelea mashine ambazo zinakuja Mji wa Sumbawanga, zitakwenda mpaka Nkasi na kwa kufanya vile, tunaamini zitasaidia na maeneo mengine. Wataalam wetu wametuambia pale tuna-*extend* tu *line* kwa Mheshimiwa Nyami, kutoka Sumbawanga tutapeleka *line* ile ile moja kwa moja mpaka Nkasi. Huo ni mpango. Ninafahamu pia kwa kaka yangu Mheshimiwa Mpendazoe pale Kishapu ana maombi yale kwenye Wilaya ile. Lakini ni juhudi za Serikali kwamba tunaendelea kuzitengea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu, tunapoongelea masuala ya umeme Vijijini, wapo Waheshimiwa hapa tunafahamu kabisa kwamba wengine wanaomba maeneo ya Vijiji, wengine wanaomba maeneo ya Kata lakini kimsingi yako maeneo ya Wilaya na Mikoa ambayo hayajapata umeme. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wengi ambao wametupa changamoto na wameomba kwa dhati kwamba mwaka huu wasipona mpango wa kufikisha umeme maeneo yao ambayo wameyaomba, pengine mambo hayatokuwa mazuri na pengine hapa patachimbika. Lakini niseme tu kwamba kwa ufinyu wa bajeti hii, sioni sababu ya kuchimba huu ukumbi kwa sababu miradi hii ni yetu wote, uwezo wa kifedha tunaufahamu kama Taifa na Serikali inafanya juhudi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mungai ametusaidia kuainisha vipaumbele ambavyo tumevionyesha, lakini kwenye hotuba vinajieleza. Tungependa usambazaji wa umeme ufanyike kwa nchi nzima pengine kwa muda wa miaka miwili au mitatu lakini tunafahamu ukomo wa uwezo wetu wa kuwa na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, tunakuja na mpango kabambe wa kueneza umeme nchini kupitia ule Mpango wa *Power Master Plan* ambao unatuongoza, ni mwongozo. Ninakumbuka Waheshimiwa Wabunge wengine walikuwa wanahoji uwezekano wa kuutekeleza mpango huo kwa sababu unaonekana unakwenda mpaka mwaka 2033. Tulishafanua mpango ule ni mwongozo, lakini si Msaafu. Yako mambo ambayo sisi tutazidi kuyatekeleza kwa jinsi muda unavyokwenda na katika hili, tunashirikisha sana sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Gaudence Kayombo, umeongea kwa uchungu sana kuhusu mradi wa Ngaka, tunaufahamu na miongoni mwa wadau katika huo mradi wako hapa Bungeni. Lakini nataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia, ni mradi mmoja mzuri sana, tunautambua. Ni bahati mbaya kwamba isingewezekana kuweka mipango iliyopo na mipango ya utekelezaji ndani ya Wizara ya Nishati na Madini, tukaweka yote hapa. Lakini mradi wa Ngaka tunaufahamu vizuri, ni miongoni mwa miradi ambayo sisi tunaitekeleza ndani ya muda muda mfupi mpaka muda wa kati. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed unafahamu mradi huo, wapo Waheshimiwa wengi hapa, akina Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, wanaufahamu vizuri mradi huo. Lakini pia kama unavyosema, Serikali yetu kupitia Shirika letu la Maendeleo ya Taifa, ni sehemu ya wabia katika mradi ule. Lakini siyo miradi hiyo tu, iko miradi mingi ya nishati mbadala ambayo tunaitekeleza. Suala tu ni kwamba tusingeweza kuiweka yote hapa, lakini wakati mwingine inapotokea hoja kama hii, inakuwa fursa kwetu kufafanua.

Mheshimiwa Spika, katika kueneza huduma ya umeme nchini, nilisema kwamba tunasaidiwa pia na Wahisani wa Maendeleo. Iko miradi ya *MCC*, iko miradi ambayo inatekelezwa kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Nakumbuka Mheshimiwa Bujiku Sakila, juzi alichangia kwa uchungu sana na akatoa mifano mikali sana. Lakini nataka niwaambie ndugu zangu wa Wilaya ya Kwimba, wakati mwingine haya mambo Waheshimiwa Wabunge kama tunavyofahamu, ni suala la jinsi utaratibu utakavyokuwa. Mradi kama wa *MCC* ambao unatekelezwa katika Mikoa sita, Tanga, Mwanza, Mbeya, Iringa, Morogoro na Kigoma, miradi hii itatekelezwa kutokana na taratibu zilizopo. Ni kweli mwaka jana tulisema kwamba miradi hii ilitarajiwa kuanza na kwa kweli imeshaanza, miKataba imeshasainiwa, lakini utekelezaji wake unakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, pengine nitumie nafasi hii kusema, kama unaniruhusu sio kampeni, Meneja wa Waheshimiwa Wabunge hapa, lakini nataka niwaombe kwa wananchi, wananchi wasiwahukumu Waheshimiwa Wabunge waliopo hapa kwa ajili ya kuchelewa utekelezaji wa miradi ya *MCC*. Ninaomba wananchi wasiwahukumu Wabunge waliokuwa hapa kwa sababu ya kuchelewesha utekelezaji miradi ya inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Wananchi wasituhukumu sisi na hasa sisi wa Ukanda wa Kusini, mradi wa Makambako kwenda Songea ambao utakwenda mpaka Mbinga na Namtumbo utapitia pia kwa Prof. Mwalyosi, tunaomba tusihukumiwe kwa sababu hata kama angekuja nani kwa utaratibu uliopo hawezi kutekeleza nje ya utaratibu unaofanyika. Kwa hivi, naomba wananchi watuelewe hivyo, isiwe kwamba wananchi hapa Mbunge huyu ameshindwa kufanya kazi, Wabunge hawajashindwa kazi, wanafanya vizuri sana, naomba sana, tuna miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, inafanyika.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu nafahamu tuko kwenye kipindi cha hekaheka, wako watu wanapita, wanadhani, aah, Mbunge gani huyo, tungekuwa sisi tumeshaleta umeme, hizo ni ghiriba tu za kisiasa. Ukweli ni kwamba Waheshimiwa Wabunge hawa wanafanya kazi nzuri sana, lakini utekelezaji wake unafuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, juzi tumezindua hapa Dar es Salaam mradi ambao unafadhiliwa na Serikali ya Japan, tunasaidiwa hapa kuboresha miundombinu ya Dar es Salaam. Lakini watu wanapitapita wanasema wale Waheshimiwa Wabunge si lololote wale. Kwa hiyo, nasema tunaongea masuala mazito ya nchi. Nchi ni yetu na sisi hapa ni viongozi wa Kitaifa lazima tueleze ukweli na wananchi tusiwapotoshe, wananchi tunaomba wajue umakini uliopo, tumeahidiwa miradi ya *MCC*.

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, wananchi wa Busanda waelewe tu kwamba miradi inakuja na sasa hivi tumesema tumeweka programu kwenye hotuba yetu. Hii nasema tu, tumetoa mfano wa dada yangu Lolesia Bukwimba, iko miradi mingi ya *MCC* hapa inayotekelezwa na inatekelezeka, lakini hakutokuwa na maajabu zaidi ya utaratibu uliopo. Kwa hivyo, naomba sana wananchi waelewe hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusemea miradi hiyo, sasa niseme kuhusu wachimbaji wadogo, ni eneo ambalo linatusumbua. Nasema kwa masikitiko nikiwa miongoni mwa Watanzania tunaotoka kwenye wachimbaji wadogo, ninafahamu adha wanazozipata, lakini nafahamu pia uchungu wa wananchi walionao na matarajio waliyonayo. Lakini nataka nilishauri Bunge hili na niwashauri wananchi, watambue juhudi za Serikali ambazo zinafanyika. Ni miaka 12 iliyopita tu kwenye sekta hii ya wachimbaji wadogo, wachimbaji wadogo walikuwa hawafiki 2,000 kwa takwimu tu za mwaka jana tulikuwa na wachimbaji zaidi ya 13,000 tumewatambua. Lakini hatujaishia hapo tu, tumesema kwa sababu wamekuwa wakihangaika sana na kwa sababu sheria zipo, lakini wakati mwingine sheria

inaweza ikawepo lakini utekelezaji wake ni mgumu na wakati mwingine ni uharaka wa kutaka kufanikisha hilo mnalotaka kufanya, tukaamua mwaka juzi tuanze kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo na tumeanza, zoezi linaendelea.

Mheshimiwa Spika, nina orodha ya maeneo ambayo tumeshayatenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Tunafahamu kule Wilaya ya Geita, Rwamgwasi tumetenga hekta 710 kwa ajili ya wachimbaji wadogo na tumeshatoa leseni pale. Ukienda pale Nyarugusu na hivi bahati nzuri sana ni maeneo ya Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge mpya ndani ya nyumba hii, tumeshatenga maeneo ya hekta 510. Lakini nataka niwaambie wananchi wa Geita, mna maombi yenu kule Buziba, bado kuna maeneo ambayo mnadhani tunaweza kuwashirikisha kuwapa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za wachimbaji wadogo, tunasema kazi zinaendelea, haijaisha, lakini nataka niseme hatujaishia hapo kuna maeneo mengine tumeshatenga, Mererani pale tuna hekta 1,490 kwa ajili ya wachimbaji wadogo wapo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kasoro zipo na kwa sababu kama tunavyosema hata kwenye familia huwezi kuyamaliza yote, lakini juhudi za Serikali zinafanyika. Kule Kilindi, Mvomero tumetoa ekari 269,000 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Nataka kusema hili nikielezea juhudi ambazo zinafanywa na Serikali. Lakini pale Shinyanga, Kishapu kwa Mheshimiwa Mpendazoe, kule tuna hekta 14,870 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kule London na nimeona mchango wako Mheshimiwa Chiligati, unahoji kuhusu wachimbaji wadogo. Nataka kutambua hilo na wananchi wajue kwamba unalifuatilia, kule tumetenga hekta 76,600 kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Chegeni na Dr. Limbu mnafahamu vizuri. Kule Mabungasamo, tumetenga hekta 229 kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Nyasenderwa, Musoma Vijijini, kwa Mheshimiwa Mkonzo, sina hakika kama yuko hapa lakini Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mara wanafahamu, tumetenga kule eneo la hekta 172, Ruwabasi kule Musoma Mjini hekta 429 na kule Matabe Mheshimiwa Magufuli pamoja na Mheshimiwa Mukasa bado tunamalizia zoezi hilo na Wizara ya Maliasili na Utalii. Eneo la Matabe lile kuna hekta zaidi ya 880 kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya sio kwa sababu nataka bajeti hii ipite, kimsingi hilo ndilo la mwisho lakini tunaieleza ukweli wa mambo, juhudi zinazofanywa na Serikali. Sasa kwa sababu hii sifagilii, naelezea ukweli kwa sababu sisi hapa kazi yetu ni kueleza ukweli. Kwa hivyo, nasema haya kuonyesha msisitizo kwamba tunazingatia na tunawajali wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwashirikishe wananchi wa Tarime, Mheshimiwa Mwera, ni shahidi, Kata ya Kemambo, tumetenga maeneo kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi *Barrick*. Tumetenga kwa wachimbaji wadogo wadogo na kuna vikundi vinne vimeshajiunga na tumeshatoa leseni ambazo zina jumla ya watu 58 na mradi huo wa Kata ya Kemambo unafadhiliwa na *Barrick* thamani yake ni shilingi bilioni tatu. Naelezea kazi inayofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kazi haijaisha, tumesema mwaka huu kwa sababu tumekuwa tukijipanga, tunasema tunakuja na shilingi bilioni moja na shilingi bilioni moja haitoshi, lakini hatuna namna tumeanza sasa. Mwaka jana tulikuwa na mipango, mwaka juzi tulisema tuna nadharia, mwaka huu tunasema lazima itoke, Mheshimiwa Mkulo tunakuomba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shellukindo, ametoa ushauri na maoni hapa, nakushukuru sana. Ameomba sisi wa Nishati na Madini tuwe katika hatua ya orodha ya

Wizara nyingine ambazo zimekuwa zikipewa fedha *quarterly* kwa sababu ya mambo kama haya. Sisi tunahitaji fedha, wachimbaji wetu wanahangaika sana, tunataka tuanzishe mfuko utakaozungusha kama ule ambao ulikuwa unaitwa Mfuko wa Mheshimiwa Rais ule, sisi tunaanzisha mfuko wetu maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Nayasema haya ili kuelezea kwamba juhudi za Serikali zinaendelea katika kuboresha shughuli za wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, lipo swali la *Tanzanite*. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi alioutoa, lakini nataka niseme, hapa kuna hoja nzito na ya msingi, ni vyema tukaiweka wazi na ikaeleweka. Sheria yetu ya Madini ya sasa inaelekeza kwamba katika ushiriki wa uchimbaji wa vito walau Serikali iwe na asilimia sio chini ya 25, lakini kwenye suala la mgodi wa *Tanzanite*, jambo hilo halijafanyika pamoja na kwamba lilikuwa kwenye mchakato.

Mheshimiwa Spika, nataka niwapeni historia halisi, sasa hivi natoa taarifa ambayo ni taarifa rasmi ya Kiserikali. Mgodi wa *Tanzanite* ulivyoingizwa kwa wawekezaji binafsi haukuwa na utaratibu wa kawaida, ulitokana kwanza na Kampuni iliyokuwepo ambapo kulikuwa na Shirika la Umma la *TGI* ambalo lilikuwa ni Kampuni Tanzu ya *STAMICO* iliingia ubia na Kampuni zingine za uwekezaji za kigeni, ile Kampuni ikafilisika na naomba sana tusaidiane katika kulielewa suala hili. Ilivyofilisika ule mgodi ukaingia kwenye mnada wa zabuni ya kawaida. Sasa huu utaratibu wake ni tofauti kidogo na migodi kama ya Mwadui na mingine kwa sababu ule ubadilishaji wa umiliki pale haukuwa wa kawaida, huu mgodi umekuwa umefilisika, unauzwa sasa, wakaja wanunuzi na kwa utaratibu wa kisheria ulivyokuwa umekaa pale haukuwezesha kuingia *automic* ile asilimia 25 ya Serikali ama kwa Watanzania, ndiyo maana wakachukua, lakini baada ya kuuchukua juhudi zikaanza.

Mheshimiwa Spika, nataka kwa sababu ya kuzingatia muda, niseme kwamba hatua tuliyofikia mimi na wenzangu, tumekuta mambo haya yameshaanza na sisi tumeyaendeleza, tumeona njia bora ya sisi Watanzania kumiliki asilimia 25 ndani ya mgodi wa *Tanzanite* ni kuhakikisha kwamba tunapeleka kupitia soko la hisa. Tumeshaanza mwaka juzi na mwaka wa jana hiyo kazi na sasa hivi makabrasha ya Kampuni ya *Tanzanite* imeyachukua, yako kule, wameshachukua, walishapewa na Mamlaka husika wayafanyie kazi ili sisi baada ya hapo sasa tuwarajisi na mpango wetu ni kwamba nataka niweke wazi si kwamba jambo hili limefanyika jana ni suala ambalo limefanyika kwa miaka hatimaye tumefikia, wakaenda kuchukua, kulikuwa na taratibu pale za kikanuni zinarekebishwa, wanazikamilisha kwenye soko la hisa na ofisi yenye mamlaka ya mitaji lakini kimsingi tumeshakubaliana kwamba kufikia mwishoni mwa mwaka huu zoezi liwe limeshakamilika. Nilitaka nitoe taarifa hii ya Kiserikali kuhusu tuko wapi na tunaelekea wapi. Kwa hiyo, Serikali ina nia ya dhati, yale mengine Mheshimiwa Naibu Waziri ameshayasema.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, nakuomba Mheshimiwa Ole-Sendeka, mipango ipo na tunaendelea kufanya kazi. Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela, umetusaidia kwa ushauri mzuri sana. Haya madini ya *Tanzanite* na vito vingine kwa nini yasiwe ya Watanzania tu. Ilikuwa ni miongoni mwa mapendekezo ambayo tumepewa. Lakini kama nilivyosema yako ambayo tunaweza tukayatekeleza leo lakini yako ambayo yanategemea mabadiliko ya sheria. Kikubwa ni kwamba sisi kama Serikali, kiseru tumeshakubali kuzingatia kwenye madini lazima Serikali iwe na nafasi kubwa zaidi. Sera tumeshakubali kwamba Watanzania wapewe nafasi kubwa katika ushiriki wa hili jambo. Lakini tutakapokuja na sera na sheria mpya, mtaona tunataka kufika wapi, kimsingi tunataka kuvuka hapo tulipo kwenye asilimia 25. Kwa hiyo, jambo liwekwe kwenye *progress* na tutaendelea kulifanyia kazi.



Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Mwakyembe na Waheshimiwa wengine, mmeongelea habari ya unafuu wa kodi. Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, Mwalimu wangu, umetupa changamoto, ukatupa changamoto. Ukatuambia kwa nini mabadiliko haya tusitumie kile kipengele cha *force majeure*, ni bahati mbaya Mheshimiwa Dr. Mwakyembe ni Mwalimu wangu. Ni changamoto lakini nataka niliseme jambo hili kwa changamoto tuliopewa haliwezi kuisha leo. Bahati nzuri, naomba radhi sana Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, ni jambo ambalo hatuwezi kulimaliza leo kwa busara za Serikali na tafsiri yetu ya kisheria, tunadhani na tunafahamu kwamba kuna msingi ambao ni wa asili katika utunzi wa kisheria. Unapotunga sheria mpya inanzia hapo unapoitunga kwenda mbele, ukienda nyuma inakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, sisi Tanzania tuna Sheria ile ya Uwekezaji ya mwaka 1997, mnaifahamu vizuri sana. Lakini ndani yake, mojawapo ya masharti ambayo tumejifunga katika kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji, kuna kitu kinaitwa MIGA, mnaifahamu vizuri sana hii ni *guarantee* kwa wawekezaji, ukianza kubadilisha leo kwa kinyume hata misingi ya utungaji wa sheria inaweza kutuletea matatizo. Kwa hivyo, naomba Mheshimiwa Mwakyembe na Waheshimiwa wengine tupeni muda tulifanyie kazi lakini mtazamo wetu ni kwamba tulikuwa tunazingatia ile kanuni ya utungaji wa sheria kwamba sheria zinaanzia pale ilipotungiwa. Haya mambo ndiyo maana Mheshimiwa Rais alisema kwamba tunajipa muda wa kujadili na hawa wawekezaji wahame kutoka kwenye *regime* iliyopo sasa kuja kwenye *regime* mpya ambayo tunakuja nayo.

Mheshimiwa Spika, lingine lilikuwa ni suala la uagizaji wa mafuta ya jumla. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mliiongelea kwa uchungu sana. Natambua michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi sana, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Mwakyembe, Mheshimiwa Mama Malecela na wengine wengi, wengi mmesema jambo hili. Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Simbachawene, nafahamu Waheshimiwa wengi mmesema hapa kwa uchungu sana lakini kikubwa ambacho nilitaka niwaambie ni kwamba sisi utaratibu huo hatujauleta kwa bahati mbaya. Utaratibu huo wazo lilianza hapa Bungeni mwaka 2006, ikafanyiwa kazi, *EWURA* wakafanya kazi yao, wakawashirikisha wawekezaji hawa waliopo katika sekta ya mafuta. Ni bahati mbaya sana kwamba tunashughulika na suala ambalo pande mbili zina maslahi tofauti. Ni jambo la wazi, ni akili ya kawaida kwamba mfanyabiashara anaangalia kutengeneza fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili, naomba sana Mheshimiwa Shellukindo, Mwenyekiti wangu, nikushukuru kwa jinsi ambavyo ukiitisha vikao, tunashiriki kwa pamoja ingawaje unafahamu kwamba kuna hofu miongoni mwa wadau lakini nataka niwahakikishieni kwamba Serikali inaleta utaratibu bila ya kuathiri wawekezaji wetu. Tunajali maslahi yao, wametufikisha hapa, tutaheshimu sana biashara zao na hatutadiriki hata kidogo kuwa-*disturb*. Lakini kikubwa ni kwamba tunataka tufikie mahali ambapo wananchi wananufaika na wafanyabiashara wananufaika. Kwa hivyo, kusiwe na hofu, tunakwenda vizuri na utaratibu huu tunakwenda kuutekeleza, hatuna matatizo na hilo.

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo kuhusu masuala ya Muungano kuhusu mafuta. Bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliongelea wiki iliyopita, swali hili aliulizwa na Mheshimiwa Seleli kuhusu suala la mafuta ya Muungano. Suala la mafuta ya Muungano, nafahamu kuna utaratibu wake chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Makamu wa Rais, ndivyo tulivyokubaliana na Serikali za pande zote mbili sehemu ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini niliseme hili kwa sababu ni la kihistoria.

Mheshimiwa Spika, kwanza hakuna ubishi kwamba suala la mafuta na gesi ni la Muungano kutokana na makubaliano au mabadiliko yaliyokubalika kwenye Katiba mwaka 1968. Lakini pia mwaka jana mwezi Aprili, tuliweka utaratibu, pande zote mbili zilisaini makubaliano ya kumweka Mshauri Mwelekezi, tukakubaliana. Lakini tarehe 20 Juni, 2008, pande zote mbili zikaridhia mgawanyo wa gharama za kumgharamia huyo Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya Uingereza. Mwezi Julai 2008, rasimu ya kwanza iliwasilishwa na rasimu ya mwisho iliwasilishwa juzi, tarehe 23 Juni, 2009 kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naliongelea hili kwa masikitiko kwa sababu wakati mwingine kama taratibu ziko wazi mmekubaliana kwa pande zote mbili, inauma.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais, tarehe 26 Aprili, 2009, aliongelea wakati wa Maadhimisho ya Miaka 45 ya Muungano, alisema kwa kina na kwa dhati, sisi tunaamini kwamba suala hili mpaka sasa hivi lilipofika hakuna utata. Taarifa ya mwisho imeletwa tunaifanyia kazi pande zote mbili. Tuendelee kuwaomba wenzetu kwamba, kama ilitokea jambo fulani labda kwa sababu ya tafsiri lakini tumeshakubaliana tangu mwaka jana, tumesaini makubaliano, tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwa sababu kuna mapendekezo mengi na mojawapo ni hili la kuliweka Shirika la *TPDC* liwe la Muungano, sisi tunaamini, kwa utaratibu huo, kama jamii ambayo inaheshimu misingi ya sheria na utawala bora, tunaamini kwamba tutafika tunakokusudia.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitumie nafasi hii, kama alivyoomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wenzetu tuzidi kushirikiana, ni kwa nia njema na si jambo la kuanza kusemezana maneno makali na sitaki kurudia maneno aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu, yalikuwa wazi, lakini kweli leo tunaanza kuitana kwamba 'wezi wa mchana'! Si jambo la kurudia kwa kweli. Lakini niseme tu kwamba ni suala ambalo lina utaratibu wake, tumekubaliana vizuri na tunaamini kwamba kwenye safari yetu tutafika.

Mheshimiwa Spika, wako baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakati wanachangia waliyasema baadhi ya mambo hapa, mojawapo ni kuhusu urejeshwaji wa mazingira bora katika maeneo mbalimbali ambapo shughuli za uchimbaji migodi zinafanyika. Nataka nitumie nafasi hii, kuwahakikishia kwamba Sheria tuliyonayo leo, inatambua hilo hasa Sheria ya Mwaka 1998 lakini pia Kanuni zake na Sheria ya Mazingira, inatambua hilo ingawaje niseme tu kwamba inawapa uhuru viongozi wanapokuwa kwenye nafasi kulitekeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba, katika migodi mikubwa, kikubwa kinachofanyika, kuna kitu kinaitwa *self regulation* lakini hiyo haimaanishi kwamba Serikali isiweke mkono wake. Jambo hilo limekubalika kutekelezeka na sisi kama Serikali tumekuwa tukilifuatilia. Haya ni mambo Kiserikali yalikuwa yanafanywa na Kampuni ya *Rex Tours*. Ilipokuja, mojawapo ya mambo waliyokuwa wanafanya, ni kuangalia jinsi gani utaratibu umeandaliwa, migodi hii inapomaliza kuchimbwa, fursa yake inapoisha, mazingira yanarejeshwa vipi. Lakini baada ya kuondoka, kimeingia kitengo chetu cha *GAP*, kimefanya kazi nzuri sana na robo ya kwanza ya mwaka huu, tumekamilisha hiyo kazi. Sisi jambo hilo tumeshaanza kulifanyia kazi kwenye mgodi, *specifically* wa Tuyawaka, tayari fedha ilishatengwa na napenda kutumia nafasi hii, kutaja kiwango cha fedha ambacho kimeshatengwa kuyarejesha mazingira katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Mgodi huu unatarajiwa kufungwa mwaka 2012 na fedha iliyotengwa ni dola za Kimarekani 5,892,949.26 baada ya tathmini iliyofanywa na wataalam

wetu. Lakini niseme kwa migodi mingine iliyobaki nini kinaendelea. Sisi tangu mwaka jana tunaifanyia kazi kupitia kitengo chetu cha *GAP* na kufikia wiki iliyopita tulifanya kikao cha mwisho na haya Makampuni makubwa ya uchimbaji madini. Nashukuru, tumekubaliana kwamba miKataba kwa ajili ya uhuishaji wa mazingira, migodi inapofungwa rasmi, tutaifunga tarehe 30 Septemba na utekelezaji wake unaanza tarehe 1 Oktoba mwaka 2009. Hayo tumeshakubaliana kwa sababu tulikuwa tumeshayafanyia kazi kwa muda mrefu. Nataka nitoe taarifa hii kwa sababu ni kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nitumie nafasi hii, kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa jinsi ambavyo mmetusaidia kuchangia mawazo mbalimbali, kutushauri na kuturahisihia kazi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, lakini nitumie nafasi hii, kuwashukuru wataalam wangu, wanatusaidia sana, walikuwa wakikeshia pale ofisini kwangu, ukiondoa viongozi wakuu wa Wizara ambao tumewataja hapa kwa kuwatambua, nina mama zangu pale Makatibu Muhtasi, mama Senerwa na Kapota lakini pia nina Mama Mwamsaka, wanatusaidia sana. Waheshimiwa Wabunge wengi mnawafahamu. Tuna rubani wetu pale, Bwana Mturo lakini nina Katibu wa Waziri Bwana Masolla pamoja na wasaidizi wa Naibu Waziri, tunazitambua kazi zao, wamekuwa wakituwezesha, wakati mwingine wanafanya kazi mpaka usiku wa manane kwa sababu ya changamoto zilizoko ndani ya Wizara hii, sio wakati wa bajeti tu hata wakati kawaida. Tunawashukuru kwa kutambua hilo lakini niwashukuru sana kwa uvumilivu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, tunaomba mtukubalie, tukafanye kazi, tukakamilishe miradi iliyoainishwa na baada ya kusema haya naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa kujibu hoja zetu, kama kawaida yako, kwa ufasaha kabisa. Lakini hoja yako tutaiamua kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni 100 hadi 104. Kwa hiyo, namwita Katibu ili atufikishe kwenye hatua hiyo.

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... .. Shs. 2,442,704,000/=

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru programu namba 10, *subvote* 1001.

**MWENYEKITI:** Nendeni tu, kasma hii 1001 inajulikana sana.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi kwa Waziri, niliulizia juu ya mrahaba unaotolewa katika madini ya *copper* na *silver*. Katika kitabu cha Waziri, kinaonesha kwamba katika

kipindi cha miaka 2004 – 2008, ni wastani wa paundi, walivyoandika wao zaidi ya milioni 18 za *copper* zimesafirishwa. Bahati mbaya, sikupata maelezo juu ya mrahaba unaotozwa kwa thamani kubwa hii ya *copper*. Sasa nilitaka nipate maelezo kwamba, je, hii *copper* inayozalishwa ambayo kwa bei aliyoweka Waziri hapa ni senti 0.29 kwa paundi lakini hatuelezi mrahaba wake ni kiasi gani. Mrahaba mwingi tunaouona katika almasi na katika dhahabu, kwenye almasi mrahaba ni asilimia tano na kwenye dhahabu ni asilimia tatu lakini kwenye *copper* na *silver* ambazo Makampuni makubwa haya yanazalisha sana, hatuoni mrahaba wake wala hatujui thamani halisi ya kuuzwa mali hii, tunaomba ufafanuzi Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli tumeona mchango wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, lakini ufafanuzi wake ni kwamba, mrahaba kwa kiwango cha asilimia ni kama vilivyo kwenye dhahabu asilimia tatu na madini ya vito ni asilimia tano lakini kwa namba halisi hasa thamani yake, nilishamdokeza Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya ufafanuzi zaidi wa kina kuainisha hasa ni kiasi gani ambacho kinapatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, wanaohitaji ufafanuzi ni Waheshimiwa Wabunge 73, kwa dakika zilizopangwa, hawatazidi 27. Kwa hiyo, nitajaribu kuchanganya Vyama vya Siasa, pande za Muungano, jinsia na wengine mtaachwa tu.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba ufafanuzi kwenye kubadilisha magari kutumia gesi asilia. Katika kitabu chake Mheshimiwa Waziri, anasema anaanza na magari 200. Gesi tunayo nyingi, mahitaji yapo na teknolojia ile ni ndogo, tena rahisi sana kwa nini magari 200?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru sana Mheshimiwa Kaboyonga. Tumeona mchango wake lakini kama nilivyosema kwamba tumeanza hili, ukisoma kitabu changu, pale chini tumeelezea awamu ya pili tutakuwa na magari mengi zaidi, tunatarajia kuwa na magari 8,000 lakini kwa sababu awamu ya kwanza imeshaanza na tunatarajia awamu ya pili haitachelewa. Naomba Mheshimiwa Kaboyonga atuamini, tutakwenda zaidi ya hapo lakini kwa sasa ilikuwa inategemea na kasma iliyokuwepo ambayo ilikuwa ni ya shilingi bilioni tatu na tunaamini kwamba mbele ya safari tutakuwa na zaidi ya hapo kwa sababu tunatarajia kutumia shilingi bilioni 32 au zaidi kidogo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Nataka kupata ufafanuzi, kwa kuwa kazi ya kupeleka umeme Bukene, inaonekana imeanza na kuna nguzo zimemwagwa pale Ijanija kuelekea Bukene na kwa kuwa Bukene ni Makao Makuu ya Jimbo na vile vile tumefufua Igembesavo ambapo wananunua mpunga mwingi sana, vile vile tumepata bwawa kubwa sana ambalo linaanza kuchimbwa hivi sasa, kwa hiyo kutakuwa na ulimaji mkubwa sana wa mpunga. Tunashindwa kufanya kazi ya kutengeneza mchele kwa sababu hatuna umeme lakini tuna mashine za kusaga ambazo zinatumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Bukene utafika lini kwa sababu nguzo zipo tu pale siku nyingi na kama zingekuwa hazikuwekewa dawa, zingekuwa zimeshaanza kupata mchwa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na namshukuru sana dada yangu, kwa sababu mwaka jana walau hali haikuwa hii, leo tunaongea kwa *frequency* zinazolingana. Ni kweli, tumeshaanza kupeleka nguzo na utekelezaji wake unaendelea. Hii ni pamoja na mradi wa Mheshimiwa Seleli na miradi ya maeneo mengine kama Ihanja na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe jibu la jumla kwamba, miradi yote ambayo imepitishwa na *REA* ambayo mnaiona ipo kwenye vitabu vyetu, ambayo utekelezaji wake haujaanza lakini hapa inaonekana fedha imeshatengwa, zabuni za kuwapata Wakandarasi watakoingia maeneo ya utekelezaji wa miradi, zimefunguliwa wiki iliyopita, tunatarajia kufikia mwezi wa tisa, kazi zitakuwa zimeshaanza kwa sababu sasa hivi tunachambua hizo zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenye swali linalofanana na hili kwenye miradi inayoonekana kwenye jedwali, pengine idadi yao sasa inaweza kushuka chini kidogo kutoka 75. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nilitaka maelezo kwa Waziri kuhusu wachimbaji wadogo wadogo na wawekezaji wa Mererani kuhusu mipaka yao, Serikali itamaliza lini tatizo hilo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mererani tumekuwa tukiendelea nalo, nimeona mchango wa Mheshimiwa Mbunge, nadhani hoja pale ni kwamba kwa Jiolojia ya pale mwelekeo wa mlalo wa mashimo yale au uelekeo wa mwamba, unakuwa unaingiliana na maeneo mengine, kwa sababu leseni zinapotolewa zinazingatia *vertical inclination* lakini sasa inapokuja suala la *horizontal* wanakwenda mpaka mita kadhaa ndiyo matokeo ya ile mikwaruzano. Ni suala ambalo tumekuwa tunalifanyia kazi. Lakini suluhisho la hilo siyo kuweka mipaka tu, tumeshauri kwamba kwa sababu kwa asili ya Jiolojia ya pale, tunadhani kwamba ni vema wajiunde na tulishaanza kujadiliana na wachimbaji wadogo wa Mererani kuhusu suala hilo, ianzishwe kampuni moja kubwa kwa maeneo yote ambayo yamepewa vitalu ili wachimbe kwa ufanisi na kwa kutumia teknolojia ya kisasa zaidi ambayo itaondoa kabisa haya matatizo.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Uongozi ni kutoa maamuzi na wakati mwingine maamuzi magumu sana ambayo yataudhi wachache lakini yatafanya Taifa lineemeke kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wakati nilipokuwa nachangia, nilitoa mifano ya nchi nyingi sana zenye vito kama sisi na nchi zote ulimwenguni haziweki wawekezaji kwa sababu vito vinahitaji wachimbaji wadogo wadogo na havihitaji *heavy machinery*. Kwa kuwa mimi niliongea na Waziri, akaniambia *Tanzanite One*, leseni yao na kibali chao kinakwisha mwaka 2012 na akanikubalia kwamba wazawa wanauwezo wa kufanya kazi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *commitment* ya Serikali, je, *Tanzanite One* mwaka 2012 wakimaliza, kwa sababu Watanzania wote isipokuwa wale wanaofaidi kutoka *Tanzanite One*, wanataka hivi vito tuchimbe sisi wenyewe na tumuenzi Baba wa Taifa, unanipa *commitment* gani ili Watanzania wakusikilize. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mama Malecela, ni kweli juzi baada ya mchango na hata leo tumeonana, ni

kweli kwamba ni changamoto nzuri. Naomba tu nilieleze Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba tunaangalia *Tanzanite One* kama sehemu ya uwakilishi wa uwekezaji nchi hii na ni *commitment* ya Serikali kwamba tutaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kadri itakavyowezekana ili kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye sera inayokuja, tumezingatia hilo kwamba tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba Watanzania ama kupitia Serikali yenyewe ama Watanzania mmoja mmoja wanashiriki kwa kiwango kikubwa katika suala la umiliki wa rasilimali za Tanzania. Ni zoezi ambalo linaendelea na ninamwomba Mheshimiwa anielewe kama tulivyoongea kwa sababu ni suala ambalo ni Sera ya Taifa, lakini ni changamoto ambayo tunaendelea kuifanyia kazi na tunazidi kuboresha mazingira ya uwekezaji kadri siku zinavyokwenda sasa.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Tanzania nzima wananchi wana umeme kati ya asilimia 10 na 12 tu, katika mchango wangu wa maandishi, niliuliza ile Sheria tuliyoipitisha ya Mfuko wa Kusaidia Usambazaji umefikia hatua gani, Waziri hajazungumzia chochote. Ninapenda nipate ufafanuzi, Mfuko huu upo na kama upo una mkakati gani wa kupata fedha na fedha zake zinaelekezwa vipi katika maeneo ya Vijijini ambako ndiko zilikolengwa kuliko utaratibu wa sasa ambako unaelekea kwenye Makao Makuu ya Wilaya ambayo inategemea zaidi na bajeti kuu, utaratibu huo ukoje?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dokta Slaa, ni kweli niliona mchango ule lakini kwa sababu ya muda sikuweza kujibu. Ufafanuzi wake ni kwamba tuko katika hatua ya juu ya utekelezaji na tulipofikia ni kwamba kwa sababu ile tozo ya asilimia tatu tuliyoisema kwa sasa hivi wakala wetu atakuwa ni shirika la *TANESCO* kwa kuwasiliana na *REA*. Tumeshakamilisha taratibu zote na kuanzia mwezi wa tisa, makusanyo yanaanza kutoka shirika la *TANESCO* kuja *REA* ili tusaidie kueneza huduma za usambazaji umeme Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, naomba nichukue nafasi hii, kusema kwamba tumekuwa na takwimu za kusema sasa hivi tumefikia asilimia kati ya kumi na kumi na mbili kwa miaka miwili, ni bahati nzuri kusema japo kidogo, tumesogea mbele, sasa hivi ni asilimia 14 ya Watanzania ambao wana huduma ya umeme nchini.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi pia nilikuwa nasubiri majibu ambayo sikuyapata, nimeomba umeme wa Kagoma tangu mwaka 2000, mwaka jana nikaahidiwa kwamba utapatikana kutokana na *REA*, mwaka huu hata kwenye bajeti haumo. Lakini nilikuwa nimeomba pia Vijiji vya Kafunjo, Bushagara, Ruhanga, Shule ya Sekondari ya Izigo ambapo transifoma iko karibu, yote hakuna lililotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Waziri alipokuwa ananijibu, alisema kuna mpango mkakati wa Mkoa wa Kagera lakini leo sikusikia kabisa kitu chochote, ninaomba Waziri atusaidie, anatumfanyia lipi kati ya hayo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kweli Mheshimiwa Ruth Msafiri, hoja yake ninayo na nimekuwa tukibadilishana mawazo kila wakati. Changamoto ni ile niliyosema kwamba tumeanza na vipaumbele, maombi ya Mheshimiwa Ruth tunayo lakini sasa hivi yanafanyiwa kazi na Wakala wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho ninaomba, ni kwamba kulikuwa na mpango tulishausema miaka ya nyuma kwamba wadau wa maendeleo ya nchi yetu Sweden, walionesha nia ya kutusaidia kufadhili Mkoa wa Kagera. Walichokuwa wanasubiri sasa hivi, ni kuona commitment ya Serikali kwenye Mfuko huu ni kiasi gani halafu wao, kwa sababu zamani ule mradi ulikuwa utekelezwe pamoja na mradi wa kupeleka umeme Wilaya mpaya ya Bukembe, wakarudi nyuma wakasema waiangalie commitment ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ikipita, Sweden wako tayari kusaidia fedha na kimsingi ni nyingi kuliko ilivyokuwa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kusaidia uenezaji wa umeme Vijijini. Imani yetu ni kwamba tutakapopata fedha hizo, tukijumuisha na hizi tunazosema tozo asilimia tatu na tulikuwa tunafanya marekebisho ya sheria fulani ili tupate fedha zaidi, tukishafanikisha haya yatawezesha kukamilisha Mkoa wa Kagera lakini pia na maeneo mengine nchini.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa wenzetu wa Mtwara na wale wa Lindi Kusini, wanapata umeme kwa bei nafuu kutoka Artumas, je, sisi watu wa Songas tunaotegemea kupata umeme kutoka Songosongo, wananchi wangu wategemeo nini kwa mradi huo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Dr. Mpanda, ufafanuzi ni kwamba, kimsingi kama tunavyofahamu, masuala ya bei ya umeme yanadhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Umeme (*EWURA*). Kwa hiyo, wanachofanya wao *TANESCO* na wadau wengine wanaotaka kufanya shughuli hizi wanapeleka maombi yao. Lakini kikubwa kinachofanyika kule Mtwara kulikuwa na mfuko ambao ulianzishwa maalum kwa mazingira ya wakati ule kwa Mikoa ya Kusini Mtwara na Lindi ambao ulikuwa unapata ruzuku kwa ajili ya kuifanya sasa bei ije kama ile ambayo *EWURA* wameipitisha kwa maeneo mengine. Kwa hiyo, jambo hilo limezingatiwa na bei zake zinakuwa zinatumiwa kwa vigezo vile vile ambavyo vinatumika na maeneo mengine hivi sasa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la umeme Vijijini nitalifuatilia kwa utaratibu wa kusubiri majibu ya Waziri, kwa hiyo, naomba hilo niliache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie jambo la Kitaifa zaidi. Huu mtindo wa watu kuuza hisa zao nje halafu wanachukua mali ya Tanzania, Sheria hatuna? Tumeomba kwamba Sheria ibadilishwe, haijabadilishwa na tunaona Mwaui juzi imeuzwa hatujui tumepata kiasi gani! Tunajua kuna utaratibu wa kuuza gesi ya *Mnazi Bay*, hivi Mheshimiwa Waziri haoni labda ana uwezo kabisa wa kutumia hata *GN* kusimamisha mambo haya ya kuuza mali ya Tanzania Ughaibuni huku Sheria mpya ikiwa inatengenezwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli muda haukutosha kufikia hatua hiyo ya kumjibu Mheshimiwa Cheyo, lakini kwanza alichokisema kuhusu mauzo ya hisa za *ARTUMAS* ndani ya mradi wa *ARTUMAS*, kilichofanyika kwa taarifa ya awali, ni kwamba wao wamefanya majadiliano na wawekezaji wawili ambao wameshawania kuja kuwa wabia na hiyo kwetu nataka niliseme kwa mtazamo wa chanya zaidi, mtazamo wa kusonga mbele, mradi huu ulikuwa umekwama na umedorora sana sababu ya kushuka kwa zile hisa za *ARTUMAS* kwenye soko la hisa, kama tunavyofahamu zile hisa za *ARTUMAS* zilikuwa Kronor 55 na zilishuka mpaka chini ya Kronor 1- kwenye msukosuko huu wa uchumi na ndiyo maana ule mradi wetu wa *ARTUMAS* mkubwa wa kuzalisha *megawatt 300* ulisuasua na ndiyo maana tunasema sasa tunataka tuuharakishe baada ya kupata matumaini kwamba wawekezaji hawa sasa wanaleta fedha ipatikane fedha ya

kuchimba visima vinane pale Msimbati vitakavyoweza kutoa gesi zaidi. Gesi nyingi ndiyo itatusaidia kujenga hiyo *generation plant* kwa ajili ya kuzalisha *megawatt 300*. Lakini gesi hiyo itatusaidia kujenga kiwanda cha kisasa na kikubwa zaidi cha mbolea na kwa matumizi mengine na kulikuwa na viwanda vya chuma vilitakiwa kujengwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii, kufafanua kwa Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kwamba dhamira ya mauzo hayo si mbaya na nataka niseme Sheria zilivyosimama ile ya *TPDC* na Wawekezaji, iko vizuri. Wameonesha nia lakini kwa waliofuatilia kwenye *website* wamesema itategemea na ridhio la Serikali. Kama Serikali itaridhia mauzo hayo basi biashara hiyo itaendelea na niseme kwamba kwa hili tupo makini kuhakikisha maslahi ya Taifa yanalindwa.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Sina shida ya kutoa shilingi, ninaomba ufafanuzi. Kwa sababu Mji wa Songea umekumbwa na matatizo ya umeme kwa muda mrefu, naamini ikiwemo shule ya Luhila ya Wasioona, je, katika marekebisho hayo, shule hiyo nayo imo katika kupelekewa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana suala hili lilikuja Bungeni na tulilijibu, tayari *TANESCO* wakati huo walishafanya tathmini kwamba kulikuwa na vifaa na mahitaji ya jumla yalikuwa kama shilingi milioni 11 kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye shule hiyo ili kuwezesha matumizi ya vifaa hivyo ili kuwezesha kuboresha elimu inayotolewa kwa wanafunzi wasioona. Sasa tumekubaliana na wenzetu na tutatafuta namna kupitia *REA* au kupitia mfumo mwingine wowote ili zile gharama zinazotakiwa kuunganisha umeme zifanyike wakati tukitatu tatizo la la jumla la umeme wa Songea kwa ujumla.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika kuchangia kwa maandishi, nilitaka kujua hatma ama hali ikoje na hatua gani ya haraka itachukuliwa na Serikali kuhusu gesi ya *Helium* ambayo iko katika kijiji cha Nyamusi, Kata ya Goribe, Tarafa ya Girango Wilaya ya Rorya. Gesi hii iligunduliwa miaka kumi iliyopita na nimekuwa nikichangia mara kwa mara bila kupata majibu. Sasa naomba tamko la Serikali na jirani zetu wanaimzeza mate gesi hiyo. Naomba Serikali itoe tamko leo kuhusu gesi hiyo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza kuhusu utekelezaji wa suala hili la Mheshimiwa Prof. Sarungi na kwa kweli alitueleza kabla na tumekubaliana kwamba kwanza twende na wataalam wetu tuambatane na Mheshimiwa Sarungi. Baada ya hapo, wataalam watashauri jinsi ya kufanya lakini tuamini kwamba ni jambo ambalo tunalifanya kwa namna ambayo Taifa letu litanufaika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nimezungumzia suala la Mgodini wa Buhemba ambao Mheshimiwa Waziri hakupata nafasi ya kuweza kutoa ufafanuzi. Mgodini huu, wakati unaanza uzalishaji wa dhahabu mwaka 2003, ulikuwa na uwezo wa kuzalisha tani 65 za dhahabu kwa muda ambao ungeweza kuwepo. Mpaka ulipokuwa unafungwa ulikuwa umeshazalisha tani tano za dhahabu na baadaye Kampuni iliyokuwa inaendesha mgodi huu ya Meremeta ikawa imefilisika ikafutwa ikapewa kampuni ya Tangold. Hivi tunavyozungumza Kampuni ya Tangold inatakribani shilingi bilioni 10/- katika akaunti zake na hazijafanya kazi yoyote toka iliposimamisha uzalishaji kwenye mgodi huu. Sasa mapendekezo ambayo tuliyatoa na mgodi wa Buhemba katika Ripoti ya Bomani yanaendana na mapendekezo ya Kiwira. Lakini mpaka sasa linaloshughulikiwa ni la Kiwira, la Buhemba limesahaulika kabisa na mapendekezo mengine yamekuja kutoka baadaye, ni kwamba kwa kuwa bado kuna dhahabu pale na kwa



kuwa Kampuni ile inamiliki leseni mbili katika eneo lile, kwa nini leseni hizi wasipewe *STAMICO* kwa kupitia maamuzi ya Serikali ili waweze kuendeleza uchimbaji kama dhahabu ipo na kama dhahabu haipo taratibu za ufungaji wa mgodi ili kutoweza kuathiri mazingira ya wananchi ziweze kuchukuliwa? Sasa ndipo hapo suala la umakini wa Serikali kwa sababu ni *asset* ambayo ipo na umetoka kumjibu Mheshimiwa Cheyo kuhusiana na umakini kwenye Artumas wa kuuzwa kwa shilingi milioni 12 ambao sisi tumewapa shilingi milioni saba ambazo tungeweza kuzichukua sisi hizi hisa kwa kuongeza hela kidogo. Huu umakini kwenye Buhemba unakuaje? Serikali inachukua hatua gani kuhusiana na hii *asset* iliyopo na leseni iliyopo Benki katika Kampuni ya Tangold?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, bahati mbaya ama nzuri, mchango wake umetufikia hapa wakati mimi najiandaa kupanda kwenye podium. Kwa kweli tulikuwa hatujaufanyia maandalizi ya ufafanuzi na kama tunavyofahamu Kanuni haziruhusu hapa kutoa majibu ya juu juu. Lakini kikubwa ambacho tunafanya Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Shirika ambalo limekabidhiwa majukumu yaliyokuwa yanafanywa na *PSRC* la *CHC*, tunafanya kazi kwa pamoja ili tukubaliane utaratibu mzuri wa kusonga mbele. Lakini niseme tu kwamba tupo makini kama nilivyomjibu Mheshimiwa Cheyo na ndiyo maana nikasema hata huo uuzaji wa Artumas wameonesha nia lakini watakuja Serikalini, tutaangalia kipi kifanyike ili kuwezesha shughuli hiyo ifanyike. Kwa hiyo, tutaendelea kumjibu Mheshimiwa Zitto kwa kutumia utaratibu wetu wa maandishi baada ya kuifanyia kazi hoja yake.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali, kwa jitihada zake zinazoendelea kuboresha umeme kati ya Ndanda na Nyangau. Hata hivyo, pamoja na maendeleo hayo yanayoendelea kule, bado kutakuwa na tatizo la umeme kati ya Mtwara Nanguruwe, Nanyamba, Kitama hadi Tandahimba. Je, nini ahadi ya Serikali juu ya kuwapatia umeme eneo hili maana awali Mheshimiwa Waziri aliwahi kuahidi kwamba umeme ungeweza kupatikana eneo hili mwaka jana kwenye mazungumzo yangu na yeye lakini kwenye bajeti ya mwaka huu hakuna kinachoelezwa. Napenda kujua *commitment* ya Serikali kwenye hili.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ombi la Mheshimiwa Njwayo tunalo na nia yetu iko palepale, sema tu kama unavyosema rasilimali fedha iko pungufu. Lakini faraja iliyopo ni kwamba, tutakapounganisha Ndanda – Nyangao na umeme wa Artumas ili usambae maeneo haya kwa sababu tutakachofanya baada ya kuunganisha maeneo yote, tunasema maeneo yaliyobaki yaunganishwe na umeme wa gesi asilia. Tunaamini kwamba mipango sasa tutai-*adjust* kulingana na huduma ambayo tutakuwa tunapata yenye uwezo mkubwa ya kutufikisha katika maeneo mengi. Bado matumaini yapo ya kuweza kuhudumia maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayasemea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakati tunaendelea kusubiri suala zima la utekelezaji wa mradi wa Makambako Songea, leo nishukuru kwamba Mkurugenzi wa *REA*, ule mradi wa Madaba kule Mhanje ameshafanya kazi kubwa sana na nzuri na leo amenikabidhi ripoti na mradi ule utanza. Nampongeza sana Bwana Lutengano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo tunapoendelea kusubiri miradi mingine ya kule Magagula ifanyiwe utekelezaji mimi na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Bunge hili toka limeanza tumekuwa na vikao takribani kama sita na Mheshimiwa Waziri wa Nishati, kutaka kujua wakati tunasubiri umeme huo wa gridi, je, suala la kuwasha

*generator* katika mji wa Songea kama tulivyokutana kwenye vikao karibu sita na cha mwisho tumekifanya jana usiku, umeme Songea utawashwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na ule umeme wa Peramiho ambao Mheshimiwa Waziri mwaka jana nilizungumza na wewe kwa hasira sana lakini *installation* ya nyaya imeshafika katika kijiji cha Likuyufusi. Ni lini sasa utafika Peramiho kwa kuwa ulishaahidi mwezi wa sita utawaka na mwezi wa sita umeshapita. Sasa tujue *generator* ya Songea Mjini itawashwa lini ili nguvu ile ya *generator* ipelekwe mpaka Peramiho. Je, utawaka kwa kuzingatia vikao vyetu sita tulivyokaa na Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Mbunge wa Songea Mjini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kusema kwamba, Mheshimiwa Mhagama anamtaja Dr. Lutengano Mwakahesya Mkurugenzi wa *REA*. Kumtaja kwake hakuchukui nafasi yangu kama tulivyoahidi kwamba tunashughulikia Mbunge wa Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kusema kwa dhati kabisa ni kwamba tunachangamoto kubwa kweli Mkoani Ruvuma hasa Mji wa Songea. Ni kweli jana usiku tumefanya kikao kwa muda mrefu na Mheshimiwa Mhagama pamoja na Mheshimiwa Nchimbi ambaye alikuwepo kuondoa utata kwa yale ambayo tunakubaliana. Tunasikitika kwamba tulitarajia kufika tarehe 25 mwezi wa sita Songea Mjini na ile *generator* tuliyoitoa Mkoa wa Mtwara ingeanza kufanya kazi lakini baada ya kumaliza ufungaji wakaanza majaribio ya kuiwasha ikaonekana ina kasoro kwenye chombo fulani. Leo kabla ya kuja hapa tulikuwa tunaongea na wataalam wa *TANESCO* wametuambia kwamba kile chombo kitapatikana ndani ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwaambia na kuwaomba radhi wananchi wa Songea kwa sababu mimi nilikwenda pale tarehe 22 mwezi wa sita, tukaahidi kwamba kwa sababu ya taarifa tuliyokuwa tumepata ya kitaalam, umeme ungewaka tarehe 25 mwezi wa sita, haijawezekana lakini juhudi zinaendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Nchimbi, jana mmetumia muda mwingi kwenye kikao chetu cha usiku lakini tuliyoyasema pia yamejitokeza kwa aliyoyasema Mheshimiwa Likokola leo na nilishangaa kwamba kwa sababu Mheshimiwa Likokola hakuwepo kwenye kikao kile lakini ameyasema. Hata ile dhamira ya watu wa Peramiho kupata umeme mwezi wa 12 kwa jinsi ambavyo tuli ahidi mwaka jana na nashukuru kwamba Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wanaushirikiano kwa sababu limesemwa na mtu ambaye hakuwepo kwenye kikao. Lakini ahadi yetu iko palepale kufikia tarehe 25 mwezi wa 12 kwenye Christmas umeme utakuwa umeshafika.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia suala la *TANESCO* na wachimbaji wadogo wadogo. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali hii inawathamini sana wachimbaji wadogo wadogo, sitaki kuamini hivyo na wala wachimbaji wadogo wadogo wa Mpanda, hawawezi kuamini maneno ya Mheshimiwa Waziri labda Mheshimiwa Waziri atoe maelezo mengine ya ziada kwa nini mgogoro wao ambao kwa mara ya kwanza ulifikishwa kwa aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Ndugu Yona tarehe 5/2/2005 na baadaye mimi nikawa nafuatilia kwa Mheshimiwa Waziri kwa kumpelekea nyaraka na ujumbe wa wachimbaji wadogo wadogo waliokutana naye ofisini kwake hapa Dodoma na akatoa ahadi na mpaka leo mgogoro huu haujaisha. Nataka maelezo ya ziada kuhusu tatizo la mgogoro la wachimbaji wadogo wadogo kule Mpanda katika Kata ya Mchimboni. Hatua gani zinachukuliwa na Serikali ili wale wachimbaji waweze kuendeleza maeneo yao?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utata kwenye mgogoro anaousema Mheshimiwa Arfi, kwa kweli nikiri kwamba tumekuwa na mawasiliano ya karibuni sana na namshukuru sana kwa ufuatiliaji wa suala hilo. Ni utata wa kitaratibu unaotumika kwenye leseni hizi. Bado fursa ipo na tulikuwa tunaongea na wataalam wetu lakini nimekubali kwamba kabla ya mwezi wa tisa, nitakwenda Mpanda na wataalam wetu tukaongeele kule kule kwenye eneo la tukio ili tujue kinachoendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Arfi, pengine tutapata suluhu tukiwa huko. Ahsante sana.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Busanda, ninapenda kuomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Nishati na Madini ili na wananchi wasikie ya kwamba, ni lini hasa mradi wa *MCC* utaanza utekelezaji wake katika Vijiji vya Bukoli, Katoro, Rwamugasa na Nyarugusu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majumuisho nimesema kwamba, ni miradi ambayo inatekelezwa kwa utaratibu huu lakini kama alivyouliza Mheshimiwa Bukwimba, kutaka kujua ratiba kamili, tumesema kwamba zabuni zitatangazwa mwezi wa tisa baada ya hapo kufikia mwezi wa kumi na moja kuelekea mwezi wa kumi na mbili, Wakandarasi wa kuingia kwenye miradi inayotekelezwa kupitia *MCC*, watakuwa wanaingia *site* na hiyo haimaanishi ni kwa maeneo anayowakilisha Mheshimiwa Lolesia Bukwimba peke yake, kama nilivyosema ni kwa Mikoa yote sita pamoja na Mkoa wa Kigoma kwa maana ya uzalishaji wa umeme pale Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia, wakishapatikana, watafanya *mobilization* lakini kufikia mwezi wa kwanza na kuendelea, tunaamini kwamba, maKatapira yataanza kuvunja ardhi kwenye maeneo hayo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Niombe na nirudie tena kuwaomba wananchi, hakuna miujiza katika hilo, hakuna atakayeliharakisha na hakuna atakayelichelewesha kwa sababu ni suala la utaratibu. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge waliopo, wanaofuatilia mambo yao, wasiadhibiwe kwa miradi ya *MCC*.

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Wakati nachangia siku ya Jumamosi, nilikuwa nimeeleza kwamba, mradi wa kupeleka umeme Mlalo ulikuwa umekamilika *by fifty percent* (50%) ulikuwa haujafika katika maeneo ya Mtae na cha kushangaza ni kwamba zaidi ya miaka kumi sasa imepita na hauonekani kabisa kana kwamba umefutwa. Nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri anieleze mradi huu utakamilika lini, kwa sababu watu walikwishafanya *wiring* lakini sasa mradi ule wa umeme haujatekelezwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati Mheshimiwa Mbunge anachangia, alianisha Vijiji kadhaa na sisi tumeshaanza kulifanyia kazi. Naomba nitumie nafasi hii, kumwomba Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, atuvumilie na sisi tuwasiliane naye pengine kuanzia siku tatu zijazo, tujiweke sawa, tufanye tathimini na wataalam wetu, kwa sababu tunahitaji kujiridhisha juu ya gharama za maeneo yote aliyoyasema na tujue namna gani ya kuingiza miradi hiyo kwenye mpango wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kumpa taarifa na sisi kwa sababu ofisi yetu iko wazi, kwa kuzingatia mchango wake alioutoa juzi, anakaribishwa.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuomba ufafanuzi.

Katika mchango wangu wa maandishi na nadhani hata Mheshimiwa Waziri mwenyewe anajua, nimeelezea sana kuhusu tatizo sugu la umeme Mkoa wa Kigoma na nimeuliza maswali mengi sana na nimeishapewa majibu mengi na katika ukurasa wa 25 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameelezea mkakati uliopo. Nakubaliana na yote lakini sehemu yoyote ambayo hakuna umeme kuna matatizo mengi, tatizo mojawapo ni kukosekana kwa maji. Matanki yapo na pampu za kusukuma maji zipo, visima vya maji vipo na vyanzo vingine vingi vya maji vipo. Kwa hiyo, kwa Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake zote Kasulu, Kibondo na Kigoma Mjini, hakuna maji lakini vyanzo vya maji vipo. Nimemwomba Mheshimiwa Waziri, atununulie *generators* zifungwe katika visima mahali ambapo matanki yapo katika Wilaya zote ili wakati tukisubiri mpango huo wa muda mrefu wa kupata umeme, tuepuke tatizo hili la kukosa maji safi na salama ili tuweze kupona maradhi ambayo yanatokana na kukosekana kwa maji. Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hili la kununua jenereta kila mahali mantaki yalipo labda tumwachie Mheshimiwa Prof. Mwandosya na Mheshimiwa Eng. Chiza, kwa suala la maji maana nadhani wanaweza kulitolea majibu.

Lakini kwa ujumla, kuhusu mikakati ya kuboresha huduma ya umeme Mkoa wa Kigoma na tuseme Manispaa ya Kigoma Ujiji, kama ambavyo tumeshasema hapa mara kadhaa na kwa kweli Mheshimiwa Peter Serukamba, tunatambua jinsi ambavyo amekuwa na sisi bega kwa bega, niseme tu kwamba, hatua tuliyofikia ndiyo hiyo ya kuagiza mitambo ambayo tunatarajia nadhani ya miezi 15 kama tulivyosema katika hotuba yetu kuanzia mwezi wa sita itakuwa imefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa Mji wa Kigoma Ujiji, tumeuchukulia kwa namna yake, tumefanya juhudi za makusudi ambazo zitakuwa ni suluhu ya muda mfupi na itatekelezeka kwa muda mfupi kwa sababu tumeagiza mitambo mingine kutoka Kampuni ya *Perkins* ya Uingereza, mitambo ambayo tunaamini itakuwa imeishafika na kuanza kufungwa kufikia mwezi wa tisa kama tulivyosema kwenye hotuba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndiyo juhudi ambazo tunafanya na kwa kweli Mheshimiwa Peter Serukamba, katika hili niseme amekuwa halali na tunaamini Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma pia Mheshimiwa Kijiko wa Kibondo, Mheshimiwa Nsanzugwanko Kasulu tunafahamu na Mheshimiwa Mporogomyi pamoja na Waheshimiwa wengine, Mkoa wa Kigoma tunauangalia kwa macho mawili.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Umeme kwa Vijiji vya Jimbo la Kwimba ambavyo viko katika jedwali Na. 4, ukurasa wa 99 wa kitabu cha hotuba, utafadhiliwa na *ADB* chini ya Mpango wa *Electricity Fibres*. Katika mchango wangu wa maandishi pamoja na kuongea, nimemwomba Mheshimiwa Waziri, atuambie ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya Vijiji hivyo ili tuondoke kwenye ahadi za kwenye vitabu na wananchi wa Nyamirama, Ilula, Gungumalo mpaka Shirima, wanasubiri jibu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani. Kwa mujibu wa Kanuni ya 104, nalazimika niongeze kipindi cha Kamati ya Matumizi, kipindi kisichozidi dakika 30. Tunaendelea, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Bujiku Sakila, juzi wakati alipokuwa anachangia alisema kwa uchungu sana na niombe radhi kwamba, kuna changamoto alitupa jana na juzi kwenye kutambua Vijiji katika maeneo aliyokuwa anayaombea, hatukuweza kufanya marekebisho kwenye jedwali kama alivyokuwa ameshauri mwaka jana na makosa yale yakajirudia, tunaomba radhi sana kwa hilo, haikuwa makusudio yetu, tumeshaliona na tumefanya marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha zinazohitajika kwa kila kijiji, tumechukua changamoto lakini mpaka tunakuja hapa, tulikuwa hatujamaliza kwa sababu ni Vijiji vingi. Ukisoma pale kwenye jedwali lililosema miji na Vijiji vitakavyopata umeme Mwanza na kwa kuanzia na Wilaya yake ambayo imetajwa ya pili ni vingi na tukadhani kwamba, tusije tukatoa takwimu za haraka haraka hapa, tunaendelea kuzifanyia kazi lakini tutaziwasilisha kwa Mheshimiwa Mbunge ili ajiridhishe na kwa kweli apeleke ujumbe kwa wananchi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilipozungumza naye mara kadhaa kuhusiana na matatizo ya umeme katika Tarafa zangu tatu za Singida Kaskazini, Tarafa ya Mgori pamoja na Sekondari zake, Sekondari ya Mgori, Sekondari ya Ngimu na Sekondari ya Itaja pamoja na vile Vijiji ambavyo vinapitia katika maeneo hayo, ninaomba tena nimkumbushie Mheshimiwa Waziri na aweze kutoa *statement* ambayo wananchi wa Tarafa hiyo pamoja na Tarafa ya Ilongero na Mtinko watasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesisitiza juu ya umuhimu wa kupitisha umeme katika Sekondari zote ambazo zimeanzishwa na wananchi pamoja na zile za binafsi. Tuna Sekondari zaidi ya kumi (10) katika haya maeneo ambapo nisingependa kuzitaja zote lakini Tarafa ya Ilongero, Tarafa ya Mtinko na katika eneo la Kibaoni, kuna transfoma ambayo ingeweza ku-*serve* Vijiji vingi sana. Ninaomba tu Mheshimiwa Waziri awahakikishie hawa wananchi katika haya maeneo kwamba hili jambo linafikiriwa na linatekelezwa? Nashukuru sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Lazaro Nyalandu tumekuwa na mawasiliano ya karibu kwa maeneo yake ya Tarafa za Mtinko na Ilongero lakini tumeweka pamoja na maombi ya Mheshimiwa Missanga ya kule Sepuka, pia tumeweka pamoja na maombi ya Mheshimiwa Msindai pamoja na Mheshimiwa Killimbah kwa maeneo ya Wilaya ya Iramba kwa sababu yamekuwa yakija kwa pamoja, tunayafanyia kazi kwa pamoja na kupitia wenzetu wa Wakala wa Umeme Vijijini, tutawapa taarifa muda si mrefu mipango ya utekelezaji hasa baada ya kuzitambua gharama halisi ni kiasi gani ili tujue namna ya kujipanga na tutekeleze miradi hiyo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Moja katika hoja zangu na kwa kweli hoja nzito ya Kambi ya Upinzani ni kuwa, Tanzania ina mpango wa kununua umeme wa *Megawatt 200* kutoka Ethiopia kupitia Kenya ifikapo mwaka 2014 katika Mpango wa *Powers System Master Plan*. Kenya itakuwa inafanyabiashara na sisi kwa sababu sisi hatuna mkataba na Ethiopia lakini Ethiopia ina sera kabambe ya kuuza umeme kwa Sudan, Djibout, Misri na Kenya. Tanzania imejaliwa rasilimali muhimu sana ya *Uranium*, lakini hatujaitumia rasilimali hii kuzalisha umeme kibiashara, je, Mheshimiwa Waziri kuna mchakato gani wa kutumia *uranium* tuliyonayo ili na sisi tufanye biashara ya umeme? Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Hemed kwa sababu suala hili amekuwa akilifuatilia sana kwa kweli hata nje ya Bunge lako Tukufu. Lakini niseme tu kwamba, utekelezaji wa miradi kwa ajili ya kuboresha huduma ya nishati nchini, zoezi hili tunalifanya kwa kuzingatia mamabo mengi, iko miradi ambayo tunaifanya sisi wenyewe kama nchi, iko miradi ambayo inatekelezwa Kikanda na ndiyo maana utakuta kuna miradi ambayo iko ndani ya Mipango ya Nile *Basin Initiatives* na ndiyo hicho ambacho Mheshimiwa Hemed anakiongelea. Lakini kwa upande wa Kusini huku, kuna miradi ambayo tunaitekeleza kwa kupitia programu za *SADC* lakini pia kuna miradi ambayo tunaitekeleza kwa kutumia majirani zetu wa Kenya, kama tulivyowasha umeme kwa Mheshimiwa Michael Laizer Longido, na sasa tumewasha Namanga tunaeeleka Longido lakini pia tuna miradi kule Karagwe kwa mfano pale Mrongo tunashirikiana na wenzetu Waganda kujenga kituo cha uzalishaji wa umeme wa *megawatt 10*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la kwanza tunaangalia kwa mtazamo huo, lakini kuhusu matumizi ya madini ya *uranium* kama tulivyotoa taarifa, tumejipanga vizuri, sasa hivi tuna timu ya kitaifa ambayo inatengeneza Kanuni ambapo ziko katika hatua za mwisho ili zitusaide sasa kusimamia uchimbaji wa *uranium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa, ni kama tulivyosema kwamba, kampuni inayofanya utafiti Wilaya ya Manyoni na Bahi, kampuni ya *Ironex*, wanatarajia kuanza kuzalisha madini ya *uranium* mwaka 2011. Kampuni ya Mantra inayofanya kazi kule Mkuju kwenye Jimbo la Mheshimiwa Vita Kawawa, kule Namtumbo, wanatarajia kuanza kuzalisha mwaka 2012. Tumejipanga vizuri na tutatumia uzoefu wa nchi zingine ikiwemo nchi ya Malawi kama tulivyokuwa tunashauriwa asubuhi na nchi zingine na tunazingatia Itifaki za Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea vizuri, lengo likuwa ni kufikia hapa, kama tunaweza kuzalisha nishati ya umeme kwa kutumia madini yetu ya *uranium* kwa kushirikisha pia na sekta binafsi.

**MHE. BALOZI DKT. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nilitegemea katika ku-*wind up*, Waziri afanue na kuweka *commitement* kwa maeneo yale niliyoyaonyesha ambayo tumeyafanyia kazi Wilayani, tumeyafikisha *TANESCO* mkoani na tumefikisha mpaka kwenye mradi wenyewe ili waweze kuyatazama kwa sababu ni vitu tu vya utekelezaji na nilijua wazi kwamba, ningeweza kuendelea hata na awamu ya pili ambayo tunategemea pia kuipata kama watatelekeza zile ramani zilizoko Wizarani kwao zinazoonisha umeme kuvuka Irondo Bay kwenda kisiwa cha Swizu na Ukara. Kwa hiyo, mimi nataka tu ile *commitement* kuja kusahihisha hii awamu ya kwanza ili hizi sehemu ambazo tumezifanyia kazi na tumeshaziwasilisha Wizarani na zilikuwemo kwenye ramani, naomba *commitement* hiyo, Waziri nitakuachia ukinipa hiyo *commitement*.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nimwombe Mama Mongella aniachie kwa sababu ninaongea mbele yake na Blandina yuko hapa na mimi naweza kuingia matatani. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kikazi ni kweli kabisa kwamba, tumepata maombi yake tunayo na *commitement* yetu ipo kupitia Mameneja wetu wa Kanda na Mkoa wa Mwanza lakini pia kwa Ukerewe sasa kwa sababu baada ya kufikisha huduma hiyo tunapeleka msimamizi kwa ajili ya maeneo hayo. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mongella kwamba sisi tuko tayari na tulishaanza kwa kweli kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa niaba ya wenzangu, nimshukuru sana Mama Mongella, asubuhi ametuchangia na akatuomba umeme kufika maeneo yetu na akatuonya kwamba tutakuja kuhukumiwa kwa sababu unapoongelea maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na maeneo tunayowakilisha sisi tunaosimamia Wizara. Mheshimiwa Balozi, tunakushukuru sana Mama, kwa kutukumbuka sisi wanao, maeneo ya Kimanzichana kwa Mheshimiwa Malima, lakini pia na kule ulikosema maeneo ninakotoka mimi mwakilishi wa Jimbo la Sengerema. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba katika Kamati ya Matumizi, mnachotakiwa kuomba ni maelezo zaidi au ufafanuzi kwa mujibu wa Kanuni ya 101 (2) siyo *commitement*, atakayeomba sasa *commitement* atakuwa ameomba nje ya Kanuni kwa hiyo sitaruhusu, nadhani tumeelewana!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Vinginevyo tunawaweka Waheshimiwa Mawaziri katika nafasi ngumu sana, akifanya *commitement* 75 mwaka ujao nadhani sijui tutafanyaje.

Kwa hiyo, tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Lyamba tafadhali! Atafuatiwa na Mheshimiwa ngoja niende Kusini kabisa huku, Mtutura.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Ndani ya mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimemweleza Mheshimiwa Waziri kwamba, miradi karibu yote ambayo ina fedha, tayari *TANESCO* imepangiwa fedha katika Wilaya ya Kilosa katika Kata za Mabwerekwere, Masanze, Kilangali, Ruhembe na Mikumi, imesimama kwa sababu ya ukosefu wa nguzo, kuna uhaba kabisa wa nguzo miradi hii haiendelei na fedha zipo. Utafiti unaonesha kuna nguzo zinasafirishwa kwenda kuuzwa Kenya, hapo hapo sisi tunanunua nguzo kutoka Afrika Kusini, sasa hali hii inaleta mashaka na kufanya tuhoji, je, miradi iliyokwishaanza na fedha zipo itamalizika namna gani? Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi na maelezo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lakini kikubwa hapa ufafanuzi wake ni kwamba, suala la ununuzi ya nguzo unaofanywa na Shirika letu la *TANESCO*, ni suala la kibiashara. Ni kweli kwamba kuna nguzo ambazo zimekuwa zikuuzwa Kenya, lakini na sisi kuna nguzo ambazo tumekuwa tukinunua kutoka nje ya nchi lakini hata za hapa nchini *TANESCO* wananunua. Lakini kikubwa ni kwa sababu manunuzi yanafanyika kwa kutumia utaratibu wa kawaida wa zabuni ambapo anayeshinda na kuonekana ana nafuu ndiye wanayemchukua. Hata hivyo, nataka pia nimpe faraja Mheshimiwa Lyamba kwamba sio maeneo aliyoyasemea hayo tu, lakini pia Sekondari ya Msolwa tunapeleka umeme, asubuhi tulikuwa tunafanya mazungumzo na *REA* ili tufikishe umeme kwenye eneo lake.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, juu ya mradi wa umeme kutoka Ubungo kwenda Kigamboni na kabla sijapata maelezo hayo, naomba ni-*declare interest*, mimi ni miongoni mwa wale ambao wamepitiwa na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umeathiri takribani watu zaidi ya 1,800 na baada ya tathmini ya awali, wananchi wengi hawakuridhika na tathmini ile na wakapeleka malalamiko yao na tathmini ya awali ilifanywa mwaka 2005 na wananchi sisi tukaambiwa kwamba tusifanye maendeleo yoyote, ambaye hana choo abaki hivyo hivyo, wananchi wengi wanapata huduma ya vyoo kutoka nyumba za jirani. Je, baada ya mchango wangu ambao nilimwomba Waziri awasiliane na viongozi wa *TANESCO* ambao wako hapa, ni maelezo gani wanatoa viongozi hao wa *TANESCO* ili kuwakomboa wananchi hao ambao wako katika mateso kwa zaidi ya miaka minne sasa hivi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunajaribu ku-*reconcile* taarifa zetu za *TANESCO* na sisi wenyewe Serikali Kuu na nisema tu kwamba, jambo hili tumeamua kulifanyia kazi kwa kina kidogo, kuna mambo ambayo pengine hapa hatuwezi kuyaongea yakaisha hasa kuhusu fidia kwa maeneo ambayo wanaathirika na mradi alioutaja Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo nirudie kusema yale ambayo nilisema kwamba, katika majibu ambayo tutatoa kwa maandishi ama kwa sababu Mheshimiwa Mtutura tumekuwa tukiwasiliana kwa karibu, tutampa ufafanuzi wa hatua ambazo tutazichukua ili tufikie mahali ambapo kweli tunatoa jibu na yeye pia afikie mahali aridhike.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilipenda tu Serikali itupatie ufafanuzi kwamba, nini hatima ya wananchi wanaoishi jirani na Mgodhi wa Madini wa North Mara na hasa baada ya Watanzania wote kuona ni jinsi gani wananchi hawa wameathirika na kwamba, hata wale wawekezaji wamefikia hatua ya kumdanganya Mheshimiwa Waziri pale wanapomwaga maji machafu, kitu kinachoonsha kwamba hawana nia nzuri kabisa na wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kujua kwamba, baada ya Serikali kuona tatizo hili kwa nini isifunge ule mradi kwa muda, kwanza uchunguzi ufanyike na waweke miundombinu mizuri ya maji machafu au vinginevyo wawahamishie wananchi wale maeneo mengine ili waache kuathirika na wapishe mradi uendelee ili kuonyesha kwamba inajali wananchi wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Kwa taarifa tu ni kwamba, Mheshimiwa Spika, amekwishapokea taarifa ya Wabunge waliokwenda North Mara, nasubiri pia majumuisho ya Serikali na taarifa hiyo itatolewa kabla ya Mkutano wa Kumi na Sita kuisha. Kwa hiyo, tukijadili leo tutakuwa tunaathiri Kanuni, tutakuwa tunawahisha shughuli ambayo bado inafikiriwa na Bunge na itakuja. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

**MHE. DR. ANTHONY M. DIALO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimshukuru sana Waziri na Wizara yake, wanajitahidi sana kupeleka umeme maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mradi wa *MCC*, nataka tu anipe ufafanuzi kwa sababu maeneo ya Jimbo la Ilemela yaliyotajwa humu kwamba ni mradi wa *MCC*, ninavyofahamu mimi siyo kutokana na fedha za *MCC* ila ni fedha zetu za *TANESCO*. Sasa nataka anihakikishie kwamba, haya maeneo siyo kwamba yataondoa maeneo ambayo tunajua sisi kulingana na bajeti ya mwaka jana, yanayoingia kwenye *MCC* yaani umeme kutoka



Kisesa kwenda Kayenze na kupita Kata ya Sangabuye kuja kuunganisha Igombe? Ninataka nifahamu haya maeneo bado yako kama yalivyopangwa? Maana hapa inachanganya kidogo, naomba ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo. Miradi ya *MCC* haiathiriwi na miradi inayotekelezwa kwa kufadhiliwa ama na Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini ama *TANESCO* yenyewe kwa sababu na yenyewe ina miradi yake. Lakini hii tuliyoonyesha hapa, ni miradi ambayo inatakelezwa kutokana na fedha ya *MCC* lakini watekelezaji wake kwa sasa ni *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa maeneo ambayo ameyaulizia Mheshimiwa Mbunge na kimsingi hata mwaka jana alisisitiza, bado tunasema mipango iko pale pale, maeneo ya Kayenze yatakata hiyo huduma na kama litajitokeza jambo lingine na kama Mheshimiwa Diallo ana taarifa zingine, tutawasiliana, aniarifu ni wapi ambapo panamkwaza lakini imani yetu ni kwamba, utekelezaji unakwenda kama ambavyo inaonekana kwenye jedwali.

**MHE: BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu sikupata fursa ya kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nitoe shukrani za dhati kwa mengi ambayo tunafanyiwa na Wizara hii kwa upande wa umeme, nishati na kwa upande wa madini. Ila kuna moja ambalo tuliahidiwa, kwa sababu Kilindi inafahamika kwa ajili ya utajiri wa madini, tuliarifiwa mwaka jana kwamba taratibu zinaandaliwa ili tuweze kupatiwa Ofisi ya Madini katika Wilaya ya Kilindi, kwa hivi sasa tunatumia ya Handeni na kibaya zaidi ni kwamba kwa takribani kwa mwaka mzima kumekuwa hakuna Afisa Mkazi wa Madini pale Handeni, hali ambayo imetuathiri sana sisi wana Kilindi na taratibu nyingi zinakwenda ndivyo sivyo kutokana na kukosa Afisa kama huyo na Ofisi kama hiyo ndani ya Wilaya. Tunaomba ufafanuzi wa Waziri, safari hii ametufikiria?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ambayo yanapatikana madini, tunapenda kusogeza huduma za ushauri na usimamizi katika maeneo hayo. Dhamira ya Serikali bado iko pale pale kwamba, Kilindi lazima tufikie mahali tuwe na ofisi yetu lakini changamoto tuliyonayo ni kwa rasilimali watu kwanza, ndiyo maana kwenye maombi haya, tumeomba tuongezewe fedha ili tuajiri watu wengine ili tujipange vizuri zaidi kwa sababu pale Makao Makuu na maeneo mengine pia tunahitaji wafanyakazi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishie Mheshimiwa Shellukindo kwamba, dhamira yetu iko pale pale na kadri siku zinavyokwenda, tutakuwa tunakupa taarifa za utekelezaji wa azma yetu hiyo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES.** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hapa Jumamosi, sikuunga mkono hoja hii sasa naomba nichukue nafasi hii, kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kufahamu kwamba, ule Mradi wa Umeme Vijijini katika Jimbo la Karagwe kuanzia Bugene kwenda Nyaishozi, hadi Yembe, ni lini utaweza kukamilika? Kwa bahati nzuri, nimeona fedha zimetengwa shilingi milioni 200, si haba, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilitaka nifahamu mradi ambao umekuwa ukiahidiwa kwa siku nyingi sana, mradi wa umeme kuanzia Bugene-Iyanda –Kiruruma-Nyabionza hadi Nyakaiga katika Jimbo la Karagwe, ufafanuzi wake ukoje? Utaisha lini? Pia mradi wa umeme kuanzia Kayanga - Ndama -Kituntwa hadi Gulwa, ambao nguzo zimeanza kupelekwa, nataka nifahamu miradi hii kama itaweza kuisha kabla ya mwaka 2010?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana rafiki yetu Blandes kwa sababu alianza wakati wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, akatoa angalizo kubwa sana kwamba kama hataona mambo, kuna jambo litatokea hapa, lakini nakushukuru sana Mheshimiwa Blandes. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba baada ya hiyo miradi ambayo tumeishaitengea fedha, yale maeneo ambayo Mheshimiwa Blandes alichangia juzi, tunayafanyia kazi. Kikubwa cha kwanza, ni kujiridhisha kwanza kuhusu gharama zake lakini zaidi ni kwamba, tumezingatia na tumeshaanza kuyafanyia kazi. Huu mradi ambao tumeutengea fedha, utatekelezwa kabla ya mwaka 2010 na hasa kabla ya mwaka 2010 mwezi wa sita, maana ukisema tu mwaka 2010 pengine inawezakuwa mwezi wa kumi na mbili, tutajitahidi kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili pia linaendana na mchango wa Mheshimiwa George Simbachawene. Mheshimiwa Simbachawene nimesoma mchango wake wa maandishi, amesema huungi mkono hoja kwa sababu hujapata ufafanuzi wa miradi yakw. Naifanyia kazi, tunataka kujiridhisha kwanza kwa tathimini, tathimini iliyokuwepo zamani inahitaji kufanywa sasa hivi kwa gharama za sasa. Kwa hiyo, kwa mtindo ule ule, Mheshimiwa Simbachawene, utakapopata fursa, tuendele tu kuunga mkono hoja kwa sababu tutakwenda kurahisisha utekelezaji. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kibaha Mjini ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani na Makao Makuu ya *TANESCO* ya Mkoa wa Pwani. Wananchi wangu wanaona magari makubwa makubwa yanayoharibu mpaka barabara ya Kibaha Mjini, yakipeleka nguzo za *TANESCO* pale Makao Makuu. Nimejaribu mwaka jana na mwaka mwaka huu, kumwomba Waziri, kuna maeneo hayafiki hata Kilomita moja kutoka Barabara Kuu ulipo umeme, nikimuuliza Meneja wa *TANESCO* anasema kweli wamekubaliwa na wanaomba wapelekewe zaidi ya wateja elfu kumi (10,000) lakini nikimpelekea anasema hela hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimemwambia Mkuu wangu wa Mkoa, akamuagiza *RAS* na taarifa niliyopata ni kwamba, amempelekea makisio ofisini kwake. Naomba Waziri anisaidia, je, maeneo yale ambayo nimemwambia ya Mkuu kuelekea Nyumbu, eneo la Visiga ambalo ni barabarani kabisa anakaa Diwani na eneo la Mbwawa, anisaidie maana sioni hata katika maelezo yake, je, tutafanikiwa lini au ndiyo tulie tu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaandaa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge, ilifikia mahali tukawa tunasema tukiona maombi ya Mkoa mmoja, tunayashughulikia kwa pamoja. Ombi la Mheshimiwa Dr. Gama pamoja na ombi la Mheshimiwa Ramadhani Maneno pamoja na Mheshimiwa Mzee Janguo, tunayafanyia kazi, yako kwenye ofisi zetu na tutaendelea kuyafanyia kazi na tutaendelea kuwapa taarifa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli changamoto ni hiyo kwamba wakati mwingine kasi ya kutoa fedha inakuwa si kubwa kama tunavyotarajia kwa sababu ya mapato ambayo inawezekana yasipatikane kwa wakati. Kikubwa ni kwamba tunayafanyia kazi na Waheshimiwa Wananchi katika maeneo hayo, wazidi kupata taarifa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi kuhusu Z.T.K *Interconnector* ambayo inaanzia Serenje Zambia, kupitia Tanzania mpaka Nairobi Kenya, itakuwa ni wastani wa kilomita 1600. Kwa kuwa ni mradi wa Kikanda, hivyo ushirikishwaji wa nchi tatu hizi *financially* au kigharama utakuwa namna gani wakati tukijua kwamba sehemu kubwa, robo tatu, itakuwa ndani ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi huu wa *Interconnector* hii, wa mwanzo, utawafaidisha Kenya kwa sababu ndio wenye umeme kutoka huko. Lakini pia isitoshe, hii *Power System Master Plan* ambayo imetengenezwa kwa gharama kubwa ya shilingi za Kitanzania bilioni mbili milioni mia sita ambapo mpaka sasa hivi hakujawa na mradi hata mmoja ambao tumeutumia, mwaka mmoja haujatimia, unafanyiwa mapitio, tena na kampuni ile ile, kulikoni hapa? Ninapenda Mheshimiwa Waziri atufafanulie kuna matatizo gani baada ya gharama zote hizo halafu iwe kitu hiki hakijafaa kitengenezwe tena? Ni Watanzania wangapi walihusika katika kutengeneza *Master Plan* hii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Z.T.K *Interconnector* limejadiliwa Lusaka mwezi wa nne na Serikali tatu na mimi ndio niliwakilisha Serikali ya Tanzania. Wakati huo, ilijadiliwa kwamba, kwa tathimini ya awali iliyofanywa kama miaka miwili iliyopita na *ZTK Interconnector* ingetugharimu kama *dollar* milioni 800 lakini ilijitokeza hali kwamba wawekezaji wanautaka sana ule mradi, *simply* kwa sababu unaunganisha *power pool* mbili, *South African power pool* ambayo inaishia Zambia na *East African Power pool* ambayo inaishia Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ule ndio mradi ambao unaunganisha umeme kutoka Misri mpaka *South Africa*, kwa hiyo, wawekezaji wanautaka, wameonyesha ishara ya kusaidia kuulipia. Sasa tumebaki na hatua ambayo tunategemea tuitishe kikao cha Mawaziri wa nchi hizi tatu, kujadiliana, kama tulivyosema kuna kipande kinatoka Arusha mpaka Nairobi ambacho tayari kimeanza. Tunategemea kuwa, kila nchi itakuwa na sehemu yake, tutakubaliana kwenye kikao cha Mawaziri.

**MWENYEKITI:** Nadhani hakuna haja ya kuelezea tena Watanzania wangapi, nadhani ulikwenda na ujumbe fulani, kwa hiyo, nadhani ni sawasawa tu. Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa muda wenyewe hautoshi, nitashindwa kulalamika ila nitatoa maelezo yafuatayo:-

Mkoa wa Tabora, mimi naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri anisaidie kwenye kitabu chake hiki, ukurasa wa 64 – 65, hakuna maelezo yoyote ya kukamilisha umeme Wilaya ya Uyui, kwenye upande wa utekelezaji wa Serikali na upande wa miradi ya *MCC*, hakuna

chochote kinachozunguzumzia Mkoa wa Tabora au Tabora yenyewe kama yenyewe hata kwako Urambo Mheshimiwa Mwenyekiti umesema hapa mchana kwamba panasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi maendeleo haya kwa Mkoa wa Tabora tutayapataje kama umeme haukidhi? Urambo kwako hakuna, Kaliua hakuna, sasa Mheshimiwa Mwenyekiti hebu naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri hili ameliwekaje hili? Naomba anisaidie ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango iliyopo ni kwamba maeneo karibu yote kwa maeneo ya Mikoa na Wilaya, tuyaunganishe kwenye mfumo wa upatikanaji umeme. Maeneo anayoyasema Mheshimiwa Mbunge Mwanne Mchemba, tunayafahamu, mipango ya kupeleka umeme Uyui, Kaliua mpaka kwako Mheshimiwa Mwenyekiti inafahamika, lakini tatizo ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kama nilivyosema kwa mfano kwa upande wa Wilaya ya Urambo, zabuni ndio hizo zimefunguliwa, zinafanyiwa kazi. Tulikuwa na changamoto ya kuimarisha ile *transimition line* iwe na uwezo zaidi kuliko ilivyo sasa, juhudi zote hizo tumezingatia na tunaamini kwamba kufikia mwishoni mwa mwaka huu, wananchi watakuwa wameona utekelezaji wa miradi hii.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nilipokuwa nachangia, niliulizia wananchi wa Mgusu. Walipewa *deadline* ya siku 90 na mpaka sasa hivi hatujajua hatma yao na kazi yao kubwa ni uchimbaji! Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tunalifanyia kazi. Kikao cha mwisho tulifanya na Mheshimiwa Mabina, ninamshukuru sana kwa kufuatilia pia na ujumbe wa viongozi kutoka kijiji cha Mgusu. Ni kweli tulitoa ahadi ya siku 90 lakini zikawa zimeisha mwezi wa sita na hatujakamilisha kazi, changamoto tuliyonayo katika wale wamiliki wenye leseni yaani *Shanta Mining* ni kampuni ambayo imeandikishwa kwenye soko la Hisa Uingereza. Sasa kuna changamoto kwa sababu la kwanza tulidhani kwamba wao waachie ili liwe eneo la wachimbaji wadogo ama Kampuni ya *Geita Gold Mining* tuishawishi inunue lile eneo halafu wao wakishalichukua walifanye kuwa la wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya kuwa sikupata muda wa kufikia hatua hiyo ya ufafanuzi lakini kazi zinaendelea na niwape matumaini wananchi wa Mgusu kwamba tunafanya kazi kwa ukaribu na Mheshimiwa Mbunge kulifuatilia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi nimeshindwa kuzifikia ikiwemo ya Mheshimiwa Ndassa, ametupa changamoto kuhusu matumizi ya ukarabati wa nyumba za Shirika la *TANESCO*. Naomba nitumie nafasi hii, kuliambia Bunge lako Tukufu na Watanzania kuwa tumepata changamoto sisi wenyewe, upande ule pale, ni Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO*, inateuliwa na Waziri na tumeshaanza kulifanyia kazi na tutatoa taarifa kwa kadri siku zinavyokwenda lakini tutahakikisha kwamba jambo hili litakwisha vizuri kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na jitihada zote za Kiti, tumeweza kuwafikia Wabunge 30 tu kwa hiyo Wabunge 43 imeshindikana. Miongoni mwao wakiwa ni Wabunge ambao nawafahamu vizuri na ni wachangiaji wazuri lakini hali ndio hiyo sasa tutaigia katika *guillotine*, Katibu!

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> ... ..	Shs.2,442,704,000/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ... ..	Shs.1,297,391,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> ... ..	Shs. 574,051,000/=
Kif. 1004 - <i>Internal Audit</i> ... ..	Shs. 229,515,000/=
Kif. 1005 - <i>Legal Services</i> ... ..	Shs. 211,865,000/=
Kif. 1006 - <i>Information, Education and Communication</i> ... ..	Shs.345,602,000/=
Kif. 1007 - <i>Procurement Management Unity</i> ... ..	Shs.296, 504,000/=
Kif. 1008 - <i>Environment Management Unit</i> . ... ..	Shs.198,820,000/=
Kif. 2001 - <i>Minerals</i> ... ..	Shs.9,013,303,000/=
Kif. 2002 - <i>Madini Institute</i> ... ..	Shs.1,402,261,000/=
Kif. 2003 - <i>Research and Laboratory Services</i> ... ..	Shs.1,889,782,000/=
Kif. 2004 - <i>Tanzania Diamonds Sorting Agency (TANSORT)</i> ... ..	Shs.1,436,099,000/=
Kif. 2005 - <i>Eastern Zone</i> ... ..	Shs.589, 193,000/=
Kif. 2006 - <i>Western Zone</i> ... ..	Shs.292, 789,000/=
Kif. 2007 - <i>Lake Zone</i> ... ..	Shs. 492,558,000/=
Kif. 2008 - <i>Northern Zone</i> ... ..	Shs.365,493,000/=
Kif. 2009 - <i>Southern Zone</i> ... ..	Shs.349,644,000/=
Kif. 2010 - <i>Central Western Zone</i> ... ..	Shs.396,496,000/=
Kif. 2011 - <i>Central Zone</i> ... ..	Shs.316, 573,000/=
Kif. 2012 - <i>Southern Western Zone</i> ... ..	Shs.337,812,000/=
Kif. 3001 - <i>Energy and Development</i> ... ..	Shs.32,801,123,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **FUNGU 58 – WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> ... ..	Shs.169,500,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> ... ..	Shs.435,000,000/=
Kif. 2001 - <i>Minerals</i> ... ..	Shs.16,095,440,000/=
Kif. 2002 - <i>Madini Institute</i> ... ..	Shs.600,000,000/=
Kif. 2003 - <i>Research and Laboratory Services</i> ... ..	Shs.800,000,000/=
Kif. 3001- <i>Energy and Petroleum</i> ... ..	Shs.153,546,529,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na  
Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA :** Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, mtoa hoja kwa ajili ta taarifa ya Kamati.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Nimesikia Wabunge wakicheka uliposema kifungu kwa kifungu, hiyo ndiyo lugha ya Kikanuni. Kwa hiyo, hukuingia kwenye mtego wa kusema tu kuwa imepitiwa kwa ujumla, kwa mafungu, hapana!

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu, ni kukubali kupitisha makadirio ya matumizi ya mwaka 2009/2010 ya Wizara ya Nishati na Madini. Hoja ilitolewa na ikaungwa mkono sasa nafurahi kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na kwa kupitia Bunge hili kuwa makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2009/2010, yamepitishwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, wajibu wangu mwingine ni kuwaambia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara hii, nafasi yao katika Taifa, ni muhimu sana, naomba sana. Mmesikia hoja zote na Mheshimiwa Waziri ameahidi atatupa kwa maandishi zile ambazo hazikuweza kujibiwa basi tunawaomba tu mfanye kazi kwa kujituma kweli kweli katika mwaka 2009/2010 ili hoja mbalimbali ziweze kupungua.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo, Kaimu Katibu wa Bunge, ameomba niwatangazie kwamba, kesho Jumanne, tarehe 28/7/2009, saa saba mchana kutakuwa na Kamati ya Uongozi.

Baada ya maelezo hayo, nawashukuru kwa ushirikiano wenu, tumepita hata muda. Kesho asubuhi tutaingia kwenye kujadili Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Nawatakia jioni njema na usiku wenye utulivu ili tuweze kuonana kesho.

Kwa hiyo, naahirisha sasa Bunge hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 28 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.11 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Tarehe 28/7/2009 Saa 3.00 asubuhi)*